**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Arobaini na Moja – Tarehe 11 Agosti, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Benki ya Uwekezaji Tanzania kwa Mwaka ulioishia Tarehe 31 Desemba, 2005 (*The Annual Report and Accounts of the Tanzania Investment Bank Limited for the Year ended 31st December, 2005)*

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MHE. ADAM K. A. MALIMA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI):** Maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa Mwaka wa Fedha Uliopita pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI:** Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, pamoja na Maoni kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**SPIKA:** Kabla ya kumwita mwuliza swali la kwanza kwa leo natangaza tu kwamba kama ilivyo kawaida wageni tutawatangaza mara baada ya kipindi cha maswali .

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 385

**Kuboresha Hospitali ya Mkoa wa Morogoro**

**MHE. DR. OMARI M. NIBUKA** aliuliza: -

Kwa kuwa Hospitali ya Mkoa wa Morogoro ilijengwa wakati wa Mkoloni kwa kukarabati na kuboresha majengo yaliyokuwa ya kituo cha Jeshi wakati huo na kwa kuwa idadi ya vitanda hospitalini hapo ni ndogo kulinganisha na idadi ya wagonjwa wanaolazwa hapo na wakati mwingine hospitali hupokea majeruhi wa ajali za barabarani zinazotokea mara kwa mara: -

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuiboresha hospitali hiyo ili ilingane na wakati wa sasa?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta Daktari Bingwa wa Mifupa ili wananchi wapate huduma ya kufaa na ya haraka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiboresha majengo ya Hospitali ya Mkoa wa Morogoro kwa muda mrefu ikiwa ni pamoja na vifaa vya kutolea huduma mwaka 2004/2005 na 2005/2006 kama ifuatavyo:-

(i) Kitengo cha Watoto: Serikali ilikarabati wodi ya watoto na kuweka vitanda 40 na kufanya idadi ya vitanda kuongezeka ikilinganishwa na ilivyokuwa hapo awali. Wodi hiyo imekarabatiwa kwa jumla ya Sh.30,000,000/= na vyumba vya Wauguzi na Madaktari vimeongezwa.

(ii) Kitengo cha Wagonjwa wa Akili:Kwa mwaka 2005/2006 ukarabati ulifanywa katika jengo hili kwa kuweka paa jipya na marekebisho haya yamefanywa kwa jumla ya Sh.32,000,000/= . Aidha, kwa mwaka wa fedha 2006/2007 Awamu ya Pili ya ukarabati itahusisha kuweka umeme, kupaka rangi na ununuzi wa samani na vifaa kwa gharama ya Sh.28,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia wahisani wa *AXIOS Foundation* chini ya Mpango wa Udhibiti wa UKIMWI, hospitali imekarabati kitengo cha wagonjwa wa nje kwa jumla ya Sh.11,000,000/=, kitengo cha maabara kwa jumla ya Sh.17,000,000/= pamoja na kufunga viyoyozi. Ukarabati wa kliniki ya mama na mtoto unaendelea kwa

gharama ya Sh.10,000,000/=. Pia, vimenunuliwa vifaa vya maabara vyenye thamani ya Sh.10,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, kupitia wahisani wa *Elizabeth Glacier Paediatric Aids Foundation (EGPAF)* hospitali imeongeza ukubwa wa kitengo cha wagonjwa wa nje kwa gharama ya Sh.70,000,000/= kazi hiyo bado inaendelea. Hivi sasa Serikali inaendelea kuwasiliana na wafadhili wa *Sight Savers International* kwa ajili ya kujenga kliniki ya macho. Vile vile, Serikali inafanya juhudi za kupata fedha za ujenzi wa chumba cha upasuaji cha kisasa kitakachokidhi mahitaji ya kuhudumia wagonjwa na majeruhi.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Hospitali ya Mkoa wa Morogoro haina Daktari Bingwa wa Mifupa. Hivyo, Serikali inajitahidi kutafuta Daktari wa fani hiyo ili asaidiane na Daktari Bingwa wa Upasuaji aliyepo. Tatizo hilo ni la nchi nzima kulingana na ufinyu wa Madaktari wa fani hiyo.

**MHE. DR. OMARI M. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Lakini pia ningependa nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na yenye kuleta faraja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza kwamba hospitali ile imefanyiwa ukarabati wa wakati kwa wakati. Lakini kama unavyofahamu, suala la ukarabati maana yake haligeuzi miundombinu ya majengo.

Kwa ukubwa wa hospitali ile vitanda havitoshi kulingana na idadi ya wagonjwa katika hospitali ile na kwa kufahamu kwamba Hospitali ya Mkoa wa Morogoro hakuna Hospitali ya Wilaya, hospitali ile inatumiwa kama Hospitali ya Rufaa na Hospitali ya Mkoa kwa hiyo itakuwa ina wagonjwa wengi kiasi ambacho haiwezi kukidhi haja.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba ni wakati muafaka kwa kujenga majengo mapya kwa sababu eneo bado lipo ili angalau kuiongeza Hospitali ya Mkoa wa Morogoro iendane na wakati uliopo sasa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. SELINA O. KOMBANI):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba ni kweli Hospitali ya Morogoro ni finyu na eneo lake ni dogo. Lakini kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba, Serikali kwa kutambua hilo ndiyo maana inatenga fedha kila mwaka ili kukarabati na kuongeza majengo katika eneo hilo.

Kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, wafadhili mbalimbali wanatafutwa ili kuboresha hospitali hii mara kwa mara na kwa mwaka huu Serikali imetenga pia Sh.75,000,000/= kwa ajili ya ukarabati na matengenezo madogo madogo na kuongeza vitanda katika hospitali hiyo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Uongozi wa Mkoa kuhakikisha kwamba zile fedha ambazo zimetengwa na

Serikali zifanye yale mambo muhimu ambayo yataiwezesha Hospitali ya Morogoro kukidhi au kupunguza matatizo yaliyopo katika hospitali hiyo. *(Makofi)*

Na. 386

**Huduma za Benki – Itigi**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mji wa Itigi una wafanyakazi wengi kwa mfano katika Taasisi kama *St. Gasper Hospital,* Sekondari, Reli Shule za Msingi, Misitu na kwa kuwa kuna wakulima na wafanyakazi katika maeneo mbalimbali ya Tarafa ya Itigi wenye vipato vizuri vya fedha kutokana na Mifugo, Alizeti, Tumbaku, Mbao, Asali, Nta na Machimbo ya Gesi:-

Je, ni lini Serikali itaweka huduma za benki Itigi Mjini ili kuokoa muda na gharama za usafiri wa kwenda Manyoni Mjini kila siku kufuata huduma za Benki kitu ambacho pia kinavutia majambazi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Sera ya Serikali ni kujiondoa katika shughuli za kibiashara. Hivyo, haiwezekani kwa Serikali kutoa ahadi ya lini huduma za Benki zitafikishwa Itigi. Serikali inachofanya ni kuweka mazingira muafaka kwa Sekta Binafsi kufanya shughuli hizo. Hivyo, wananchi wote wakiwemo wale wa Itigi wanahamasishwa kujiunga pamoja na kuanzisha Benki au Taasisi ya Fedha. Benki Kuu iko tayari kupokea ombi la kuanzishwa Benki au Taasisi ya Fedha kutoka kwa wananchi wa Mji wa Itigi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu inayohitajika katika kuweka mazingira ya kiuchumi, sheria na miongozo imara itakayowawezesha wananchi kuungana na kuanzisha Benki au Taasisi za Fedha katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, wakati Bunge lako Tukufu likipitisha Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 swali kama hili lilijitokeza. Tuliahidi kufanya kikao na Benki Kuu na Mabenki. Kikao hiki kilifanyika mwishoni mwa Mei, Mabenki yote yamekubali kutazama suala hili na wataleta taarifa yao kwa Waziri wa Fedha mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2006. Ni mategemeo yangu kwamba kutakuwepo na pendekezo la kuweza kusaidia sehemu ambazo hazina Benki.

**MHE. JOHN P. LWANJI**: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, napenda kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa miaka michache iliyopita *CRDB* iliwahi kufika Itigi na kuangalia hali ya uchumi ya wananchi wa Itigi na Tarafa nzima ya Itigi na wakaona kwamba wana uwezo mzuri wa kiuchumi na wakaona kwamba kuna uwezekano wa kufungua Benki,

lakini mpaka leo hawajafanya hivyo. Je, Wizara iko tayari kutusaidia kuwashawishi hawa watu wakafungua Benki?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi, *CRDB* ni mojawapo ya Benki 30 ambazo tulikutana nazo pamoja na Wizara ya Fedha na Benki Kuu na *CRDB* pia iliahidi kuangalia, si sehemu ya Itigi tu, lakini kuna maeneo mengi ambayo wameomba wapelekewe huduma za Benki. Ni matumaini ya Serikali kwamba ifikapo tarehe 31 Oktoba, 2006 Benki Kuu itakuja na taarifa Serikalini ya kuonyesha jinsi gani Mabenki yanaweza kujiandaa kushiriki sehemu ambazo pengine hakuna faida kama vile wanavyopata sehemu ambazo sasa hivi wapo.

Na. 387

**Mahitaji ya Benki Simanjiro**

**MHE. DORAH H. MUSHI** aliuliza: -

Kwa kuwa Mji wa Mererani una wakazi wengi wakiwemo wachimbaji wakubwa *(Tanzania One)* na wachimbaji wadogo wadogo, *Tanzania Africa Ltd,* wafanya biashara wa madini ya *Tanzanite*, vikundi vya uzalishaji vya akinamama kama *SACCOS, CEDHA* na *Pride Tanzania,* lakini hakuna huduma ya Benki na vikundi vyote hivyo vinahitaji huduma hiyo na kwa sababu huduma hiyo haipo hivyo hulazimika kuifuata Arusha Mjini ambapo ni mbali sana: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka huduma ya Benki katika eneo hilo haraka iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo taarifa kuwa Mji wa Mererani hauna Benki pamoja na mchango mkubwa wa kiuchumi unaotolewa na wachimbaji wakubwa na wadogo wa madini ya *Tanzanite*, wafanyabiashara na vikundi mbalimbali vya uzalishaji vilivyopo mjini hapo. Aidha, jukumu la Serikali katika uanzishaji wa Mabenki kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla ni kuweka mazingira ya kiuchumi yanayoiwezesha jamii na wananchi katika maeneo mbalimbali na kuwahamasisha kuungana pamoja ili kuanzisha Benki au Taasisi ndogo ndogo za fedha mahali walipo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sera ya sasa ya Tanzania, huduma ya Mabenki iko katika Sekta Binafsi. Kwa mantiki hiyo, Waheshimiwa Wabunge wa eneo husika wanaweza kushirikiana na Serikali katika kuwahamasisha wananchi wajiunge na kuanzisha Benki za Jamii *(Community Banks)* zinazozingatia mazingira ya mahali husika pamoja na kuzihamasisha Benki zilizopo nchini kufungua matawi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Benki Kuu, imeweka sheria na taratibu za kusaidia nguvu na juhudi za jamii na wananchi katika kuanzisha Mabenki na Taasisi za Fedha katika maeneo yao, zikiwemo *National Banks* na *Microfinance Banks.*

Aidha, Serikali inayo Sera ya Taifa inayolenga kuhamasisha uanzishwaji wa Mabenki kwa ajili ya wateja wadogo wadogo *(National Microfinance Policy)* inayosimamiwa na Benki Kuu. Kupitia Sera hii Serikali imeweka miongozo na taratibu za kusimamia uanzishwaji na uendeshwaji wa Benki hizi *(Microfinance and Micro Credit Regulations, 2005).*

Pia, Serikali kupitia Benki Kuu iko njiani kutunga mwongozo utakaoweka taratibu za uanzishwaji na uendeshwaji wa Taasisi za Fedha za wananchi zenye viwango cha chini. Taratibu hizi zinajulikana kama *Member Based Savings and Credit Associations (Licensing and Supervision) Regulations*. Sheria na miongozo hii itaweka viwango nafuu vya mitaji *(Capital Requirements)* na gharama nafuu za maombi ya leseni (*Application Fees)* ili kuhamasisha jamii na wananchi katika maeneo mbalimbali kuungana pamoja na kuanzisha Benki au Taasisi za Fedha katika maeneo yao. Aidha, Benki Kuu hutoa ushauri kwa wananchi ambao wana mipango ya kuanzisha Benki au Taasisi za Fedha ili kuhakikisha kuwa Taasisi hizi zinaanzishwa kwa misingi mizuri.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ningeomba Serikali sasa ione ni muda muafaka wa kupeleka huduma hii kule kwa sababu mara nyingi kumekuwa na vitendo viovu kama vya ujambazi na watu wanaibiwa na kunyang'anywa mali zao na hata pia kuuliwa.

Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka kuhamasisha hata kama ni *Microfinance* au watu binafsi ili waweze kufungua hizo Benki haraka iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kwanza swali lake linafanana na swali nililojibu awali la Mheshimiwa Lwanji. Jibu ni kwamba, ifikapo tarehe 31 Oktoba, Benki Kuu itakuja na mapendekezo ya jinsi gani Vyombo vya Fedha vinaweza vikasaidia sehemu ambazo kwa sasa hakuna Mabenki.

Namwomba Mheshimiwa Dorah Mushi, tushirikiane kuhamasisha wananchi wa Mererani ili kuhakikisha kwamba Vyombo vya Fedha vya Jumuiya ambavyo kwa sasa hivi ni pamoja na *SACCOS* vinaanzishwa katika eneo hilo.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa Wanawake wa Mkoa wa Ruvuma wameanzisha *SACCOS* nyingi, wameanzisha vikundi vingi vya *VICOBA* na vile vile Vikundi vya Uzalishaji Mali vya *DMI* ambavyo vina mtaji mkubwa sasa hivi na vile vile kwa kuwa *BOT* imeshakuja kutembelea vikundi hivyo na kuona umahiri wa vikundi hivyo.

Je, Serikali iko tayari sasa hivi kushirikiana na Wanawake wa Mkoa wa Ruvuma ili waweze kuanzisha *Community Bank? (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Serikali itakuwa tayari kushirikiana na akinamama hao pamoja na Taasisi yetu ya Benki Kuu kuhakikisha kwamba wanafanikiwa katika kuwa na *hizo SACCOS* na kuwa *Community Banks.(Makofi)*

Na. 388

**Mafao kwa Familia za Wastaafu Waliofariki**

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL** aliuliza: -

Kwa kuwa wapo wastaafu waliofariki dunia wakiwa bado wanafuatilia malipo ya uzeeni bila mafanikio na kuacha familia zao katika hali ya shida. Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha familia hizo zinapatiwa mafao hayo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Ni kweli kunatokea wakati mwingine mstaafu anafariki kabla ya malipo yake kukamilika, hivyo ni jukumu la wategemezi kuiarifu Hazina kuhusu kifo cha mstaafu ili malipo hayo yasiweze kuendelea yasubiri nyaraka za mirathi. Hata hivyo, uharaka wa malipo ya mirathi hutegemea uwasilishaji wa nyaraka za mirathi Hazina. Hazina mara baada ya kupokea nyaraka za mirathi huandaa malipo mapema na kuyatuma Hazina Ndogo. Uzoefu unaonyesha kuwa mara nyingi baada ya mtumishi au mstaafu kufariki inachukua muda mrefu sana kuwasilisha nyaraka za mirathi Hazina hasa kutokana na sababu zifuatazo: -

(i) Ucheleweshaji wa wana ndugu kukubaliana kufungua mirathi mahakamani.
(ii) Uletaji wa nyaraka pungufu.
(iii) Malumbano kati ya wana ndugu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hata kwa upande wa mwajiri inamwia vigumu kufahamu kama mstaafu wake amekufa kabla ya kupata malipo yake ili ataarifu Hazina. Hivyo, ili kuisaidia Serikali, ni jukumu la wana ndugu kutekeleza hayo niliyoyaeleza hapo juu mapema na Serikali itashughulikia mapema. *(Makofi)*

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa mara nyingi mara marehemu anapokuwa amefariki wanafamilia hukaa na kuandaa mambo ya mirathi na mara moja hupelekwa mahakamani na kwa kuwa Serikali imekuwa na uzoefu mkubwa sana wa kuchelewesha malipo haya. Je, kwa utawala huu wa Awamu ya Nne wa Kasi Mpya na Ari Mpya, Serikali inasemaje juu ya kubadilisha malipo haya?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi sana katika kuhakikisha kwamba wastaafu au watu wa mirathi wanapata malipo yao mapema kama inavyowezekana. Kama nilivyosema ikiwa *records* zao zote ziko sahihi na hali ya sasa si sawa kabisa na hali ilivyokuwa zamani kwa sababu hizo Hazina Ndogo tulizokuwa nazo zinasaidia kupeleka malipo kule kule mikoani kwa wale wahusika ambao wanatarajiwa wapate mafao yao. Kwa hiyo, ukiangalia historia ya hapo nyuma, Serikali imeendelea sana na bado tutaendelea kuhakikisha kwamba taratibu zinakuwa nyepesi zaidi na malipo ya wastaafu pamoja na mirathi yanakuwa kwa siku chache kabisa.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa haki halisi ya kupata mafao ni ya mstaafu mwenyewe na siyo mtu mwingine na kwa kuwa hufikia hadi watu kufa hawajapatiwa mafao yao kutokana na urasimu mkubwa uliopo. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kubadilisha kutayarisha mafao ya wafanyakazi mwaka mmoja kabla ya kustaafu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo mwanzo, Serikali imejitahidi kuhakikisha kwamba wastaafu hawapati shida. Hapo zamani ilikuwa ni Wizara ya Fedha na pengine *NSSF* na *PPF*. Wastaafu hasa wanaoanza sasa hivi *records* zao zote zimewekwa katika kompyuta na hawapati shida kama hao waliokuwa wanapata zamani kwa sababu hali imekuwa inaboreshwa kila tunavyoendelea siku za mbele na bado tunaziboresha. Wastaafu wa zamani ndiyo ambao walikuwa na matatizo kwa sababu wengi wao *records* zao hazipo, lakini kwa wastaafu wote sasa hivi *records* zao zipo kwenye kompyuta hakuna tabu ya kuwalipa kwa wakati.

Na. 389

**Mahitaji ya Umeme – Ukanda wa Mwambao wa Kigamboni**

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI** aliuliza:-

Kwa kuwa maeneo ya Ukanda wa Mwambao kutoka Kigamboni hadi Kata ya Pemba Mnazi ni Ukanda unaoendelea kwa ujenzi wa Hoteli za Kitalii, lakini mpaka sasa hakuna huduma ya umeme hasa katika maeneo ya Kibugumo, Kata ya Mjimwema hadi Pemba Mnazi, Kata ya Pemba Mnazi na kwa kuwa Watalii hufika katika maeneo hayo kupumzika, lakini pia wananchi wanahitaji kupatiwa umeme:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme Kibugumo, Mjimwema, Pemba Mnazi, Kanda ya Pemba Mnazi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kufikisha umeme katika Kata ya Chamazi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a) na b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu kwa ajili ya kupeleka umeme maeneo ya Kibugumo, Mjimwema, Pemba Mnazi, Kanda ya Pemba Mnazi hadi Ras Kutani umeshafanyika na gharama za mradi huo zimekadiriwa kufikia Shilingi milioni 380 na Serikali inatafuta pesa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

(b) Mheshimiwa Spika, vijiji vya Chamazi na vitapatiwa umeme chini ya mradi wa kuvipatia umeme vijiji vilivyoko kando ya mkuza wa bomba la Songosongo unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Mradi huu unaendelea kutekelezwa na ujenzi wa njia kubwa ya umeme na usimikaji wa nguzo umekamilika. Mradi unategemewa kukamilika mwezi Agosti, 2006. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika maeneo ya Hoteli za Kitali katika fukwe za bahari ni muhimu kuweko na umeme kwa sababu ya kuibua uchumi wa nchi hii. Je, Serikali ina mikakati gani ya kusambaza umeme katika maeneo kama hayo ambayo Pangani yanahusika kutoka Mkwaja kupitia Buyuni hadi Sadani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina mradi kabambe wa *Energizing Rural Transformation (ERT)* ambayo lengo lake kuu ni kuhakikisha kwamba maeneo mengi hapa nchini ambayo hayana umeme hivi sasa yanapata umeme. Ningependa kumhakikisha Mheshimiwa Rished kwamba katika kupanga vijiji na maeneo ambayo yatapata umeme Wizara yangu inazingatia maeneo ambayo yana mvuto wa kibiashara kwa ajili ya mahoteli kama yale ambayo aliyoyataja. Ningependa kumhakikishia kwamba Wizara yangu itajitahidi kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanapata umeme kadri fedha zinakavyopatikana ili kuhakikisha kwamba mahoteli ya kitalii na biashara zingine zinapata umeme kama zilivyopangwa.

Na. 390

**Mradi wa Gesi wa Kampuni ya Tanzania Oxygen**

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa miaka ya nyuma kampuni ya *Tanzania Oxygen* ilikuwa ikijishughulisha na biashara ya uuzaji wa gesi kutumika ndani ya nchi na nyingine kusafirishwa nchi za Zambia, Zimbabwe na Malawi hali iliyosababisha Serikali kujipatia fedha za kigeni:-

(a) Je, ni nini kilisababisha kampuni hiyo kusitisha shughuli zake za uzalishaji wa gesi hiyo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua upya mradi huo wa gesi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-
Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba katika miaka ya nyuma kampuni ya *Tanzania Oxygen* ilikuwa ikijishughulisha na biashara ya uuzaji wa gesi inayopatikana Wilayani Rungwe kwa matumizi ya ndani na nyingine kusafirishwa nje katika nchi za Zambia, Zimbabwe na Malawi. Kampuni ya *Tanzania Oxygen.* Bado inazalisha gesi huko Wilayani Rungwe, Mkoani Mbeya, kwa sasa kampuni hii imesitisha kusafirisha gesi kwenda nje kwa sababu mahitaji ya ndani ya nchi ni makubwa na mtambo uliopo sasa unatosheleza mahitaji hayo tu.

(b) Kwa kuzingatia ongezeko la mahitaji ya gesi ndani na nje ya nchi, kampuni imeagiza mtambo mkubwa zaidi wa kuzalisha gesi hiyo toka Denmark ili kukidhi mahitaji hayo. Mtambo huo unategemewa kuwasili nchini mwezi Septemba yaani mwezi ujayo, 2006. Mazungumzo ya awali ya kibiashara yamekwishafanyika ili mara mtambo utakapofungwa, gesi hiyo iweze kusafirishwa tena kwenda Zambia, Malawi na hatimaye Zimbabwe.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Watanzania wengi walinunua hisa za *TOL* na kwa miaka mingi sana hawajapewa gawio lolote na kwa kuwa hivi sasa *TOL* imepata wawekezaji wapya wakiwemo wazalendo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuipa *TOL* msukumo mpya ili kujenga matumaini na imani ya Watanzania juu ya hatma ya fedha zao? (*Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba sasa hivi tunaanza kuona kwamba Kampuni ya *Tanzania Oxygen* ambayo ndiyo iliyokuwa kampuni ya kwanza kuwa *listed* katika *Dar es Salaam Stock Exchange* inaanza kuonyesha mafanikio. Palikuwepo na matatizo hapo mwanzoni ya mtambo huo pamoja na mtambo huo ulikuwa mkubwa sana ambao ulikuwa hauwezi kuendeshwa kibiashara na ndiyo sababu palikuwepo na matatizo na mpaka wakaingia katika mchakato wa kuweza kuwapata wabia. Mwanzoni ilikuwa wawe wabia wa nje lakini ikaona kwa sababu wanaweza wakatuchezea kwa sababu wale wabia ambao walikuwa wanataka kuingia walikuwa na masoko jirani na wangeweza kuingia wakaifunga hiyo *Tanzania Oxygen* tukaanza kupata matatizo kama viwanda vingine mlivyokuwa mnavizungumzia ndiyo wakaingia wazalendo pamoja na kampuni ya nje ambayo sasa hivi imeanza kuonyesha mafanikio. Nafikiri kama mtakuwa mnaangalia kwenye ubao wa biashara mnaweza kuona kwamba zile hisa ambazo nyuma ziliweza kufikia mpaka shilingi 180 kwa hisa moja jana ilikuwa imefikia hisa kwa bei ya shilingi 295 hayo ni matokeo mazuri na tunafikiri kwamba hapo baadaye wataweza kutoa gawio kwa wale wana hisa ambao wako hapa.

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea swali linalofuata la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi nilikuwa naangalia nikaona kwamba Naibu Spika, hayumo ukumbini, Wenyeviti wote wawili hawamo ukumbini.

**MBUNGE FULANI:** Mwenyekiti yupo.

**SPIKA:** Mmoja yupo samahani sikukuona mahali pako. Nilitaka kumalizia kama hivyo ndivyo basi tungeendelea tuombeane dua kwa sababu lingempata jambo lolote Spika hivi sasa kikao kingekwisha katika hali isiyokuwa ya kawaida. (*Makofi*)

Na. 391

**Ukosefu wa Gari Sekondari ya Kibiti**

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA** aliuliza:-

Kwa kuwa shule ya sekondari Kibiti ndiyo shule pekee ya bweni katika Wilaya ya Rufiji na ina jumla ya wanafunzi na watumishi zaidi 650 na mara kwa mara, wanafunzi huwabeba wenzao kwenye machela kuwapeleka katika Kituo cha Afya Kibiti kutokana na kukosekana kwa gari la kutoa huduma katika shule hiyo:-

(a) Je, Serikali ina mpango wowote wa kuipatia shule hiyo gari?

(b) Kama Serikali inao mpango huo. Je, ni lini gari hilo litapatikana?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mbunge wa Kibiti, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kila shule kuwa na chombo cha usafiri hasa sekondari za bweni na za wasichana. Serikali itaangalia uwezekano wa kuipatia shule ya sekondari Kibiti gari litakalokuwa likitoa huduma pia shule za jirani pale uwezo kifedha utakapopatikana.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Rufiji ina shule za sekondari 9 na shule zote za sekondari katika Wilaya ya Rufiji hazina hata gari moja, shule zote 9. Je, Serikali ina mpango wowote wa dharura wa kusaidia walau magari ambayo yanawekwa pale Wizarani kwa ajili ya kuuza pengine baada ya kutumika muda mrefu ili yaweze kutumika baada ya kupelekwa kwenye shule zile za sekondari? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Wilaya ya Rufiji, ina shule nyingi za sekondari na kwamba hazina usafiri. Ushauri wake alioutoa Mheshimiwa Mbunge naupokea nitaufanyia kazi na *inshallah*

tutakwenda kuangalia kama kuna gari ambalo liko katika kuwa-*phased out* tutawapelekea. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu lililo safi.

Na. 392

**Barabara itokayo Mikoa ya Kanda ya Kaskazini**

**MHE. NURU AWADH BAFADHILI** aliuliza**:-**

Kwa kuwa barabara itokayo Mikoa ya Kanda ya Kaskazini na nchi jirani ya Kenya kupitia Segera hadi Dar es Salaam imekuwa na msongamano mkubwa wa mizigo ambao mara nyingi husababisha ajali:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara toka Tanga hadi Dar es Salaam kupitia Pangani, Sadani, Bagamoyo ili kupunguza tatizo hilo la msongamano wa magari na ajali za mara kwa mara?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninatofautiana na Mheshimiwa Mbunge kuwa barabara hii ina msongamano wa magari ya mizigo. Takwimu tulizonazo zimethitisha kuwa ajali nyingi kwenye barabara hii hazitokani na msongamano wa magari yenye mizigo bali ni kwa sababu ya mwendo wa kasi wa madereva ambao mara wanapokutana na vikwazo hushindwa kulidhibiti magari na kupata ajali.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ya Denmark imekubali kugharimia ukarabati wa barabara ya Chalinze – Segera – Tanga kwa mara ya pili kama ilivyofanya mwaka 1989/1999. Katika awamu hii ya ukarabati, suala la usalama litazingatiwa hususan kwenye maeneo ya vijiji lakini barabara haitapanuliwa.

Mheshimiwa Spika, barabara mbadala kutokea Dar es Salaam kwenda Kaskazini, Kusini, Magharibi na Kaskazini Mashariki mwa nchi yetu ukiacha ile ya Dar es Salaam – Kibaha – Chalinze, ni ile Dar es Saalam – Bagamoyo – Msata - Segera Mikoa ya Kaskazini Dar es Salaam – Bagamoyo – Msata – Chalinze kuelekea kuelekea Mikoa ya Kusini na Kati na Dar es Salaam – Bagamoyo – Sadani – Pangani – Tanga kuelekea Kaskazini Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Bagamoyo – Sadani - Pangani – Tanga Serikali ina mpango wa kuifanyia upembuzi yakinifu (*feasibility study*) katika mwaka wa fedha 2006/2007. Aidha, tutafanya pia upembuzi yakinifu barabara ya Bagamoyo – Msata nia ikiwa ni kuzijenga barabara hizo kwa kiwango cha lami.

**MHE. NURU AWADH BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa magari yaliwekewa vidhibiti mwendo na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, alisema kuwa ajali nyingi zinasababishwa madereva kwa mwendo kasi wa magari. Je, vidhibiti mwendo vile viliishia wapi na wakati magari yote yalikuwa yamewekewa vidhibiti mwendo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba magari hasa mabasi ya abiria yaliwekewa vidhibiti mwendo lakini tumekuwa tukishuhudia jinsi ambavyo madereva wamekuwa waki-*temper* na hivi vidhibiti mwendo na magari kuendelea kwenda kwa kasi. Pamoja na hatua ambazo zimekuwa zikichukuliwa na Serikali imeonekana kwamba kwa kweli suala hili la vidhibiti mwendo limekuwa likiwa linafanyiwa mzaha na hawa madereva. Serikali inaangalia namna gani itaweza kudhibiti mwendo na kuwadhibiti hawa madereva ambao kwa kweli wanahatarisha sana usalama wa raia wa Tanzania. Niseme kwamba kwa kweli katika hotuba za Mheshimiwa Rais na viongozi wa kitaifa wamekuwa wakikemea sana madereva kwenda kwa kasi. Jambo hili ni jambo la kitaifa na mimi nina hakika Serikali ya Awamu ya Nne itaangalia namna gani ya kudhibiti ili ajali zisiendelee kutokea.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuongezea jibu zuri sana la Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa ajali za barabarani kama tulivyosema na kama mwuliza swali alivyosema zinatokana na madereva. Uko mpango ambao unashughulikiwa sasa na Wizara ya Fedha kwa kutumia chombo chake cha mamlaka ya Mapato Tanzania na sisi wa Miundombinu tumeshirikishwa ambao kwao utahakikisha kwamba leseni bandia za madereva au madereva wenye leseni lakini hawakufuzu sawa sawa watadhibitiwa. Mpango huu tunatumaini utaanza kabla ya mwisho wa mwaka na utashughulikia suala la leseni bandia na madereva bandia wenye leseni halali, ili kwanza tuweze kuhakikisha kwamba anayeingia barabarani ni madhubuti kwa kila hali.

La pili, ambalo Serikali inafikiria sasa hivi ni lile la kutumia teknolojia nyingine za kudhibiti magari mabovu kwa sababu vidhibiti mwendo vya sasa vimeonyesha haviwezi kufanya kazi. Tutatafuta teknolojia nyingine tunazungumza na watu tofauti sasa ili tuweze kuwa na utaratibu mzuri wa kudhibiti magari mabovu barabarani kwa njia ya kisayansi. Mpango huu utakapofanikiwa yote miwili tumaini letu ni kwamba itapunguza sana ajali za barabarani.

**SPIKA:** Naona pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, bado Mheshimiwa Rished analo swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze Serikali kwa kuona kwamba barabara ya kutoka Tanga – Pangani hadi Bagamoyo ni barabara mbadala na ni muhimu kiusalama na kiuchumi katika nchi yetu. Je, Serikali haioni umuhimu kwa hali ya dharura hivi sasa kuanza mikakati ya kuimarisha madaraja ya Makurunge na Daraja la Mto Wami kwa maeneo ya Kitami pamoja na kivuko cha Pangani japokuwa kinakuja kipya lakini cha hivi sasa kina miezi miwili hakifanyi kazi. Je, Serikali iko tayari kuimarisha maeneo haya ili kuwa na urahisi wa kupitika barabara hii kwa wakati wote wa mwaka mzima? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kweli madaraja hayo aliyozungumzia ni muhimu wakati tuendelea na *visibility study* ili barabara hiyo ije ijengwe kwa lami kuna umuhimu kweli wa kuweza kuimarisha madaraja hayo. Vile vile kuhusu Kivuko cha Pangani yeye mwenyewe tumekuwa tukiwasiliananaye juu ya juhudi zinazofanyika kwanza za kukarabati kilichopo, lakini kuagiza kivuko kipya ambacho kitaingia mwezi wa nne mwakani. Juhudi zote hizi kwa kweli ni za kuweza kuhakikisha kwamba njia hii inaendelea kupitika wakati tunangojea hiyo lami. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba madaraja hayo yataimarishwa kama tulivyokuwa tumeongea naye ni kwamba tutawasiliana na Meneja wa Mkoa na mimi mwenyewe niliahidi kwamba tutatembelea maeneo hayo ili madaraja haya yaweze kuimarishwa. (*Makofi*)

Na. 393

**Ujenzi wa Mto Kilombero na la Mto Mwatisi**

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kampeni za uchaguzi wa mwaka 2005, Rais wa Awamu ya Nne aliahidi kujenga daraja la mto Kilombero na Mto Mwatisi kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi na kwa kuwa azma ya daraja hilo ni kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Ruvuma kibiashara:-

Je, Serikali haioni kuwa wakati umefika wa kuingiza barabara ya kuanzia Kidatu hadi Ifakara, Lupiro, Malinyi hadi Mwatisi kwenye mpango wa kitaifa ili madaraja hayo yakikamilika na barabara hiyo iwe imekamilika kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mto Kilombero kwa sasa unavukwa kwa kutumia kivuko kilichopo katika barabara kuu ya Mikumi – Kidatu – Ifakara – Lupiro hadi Mahenge yenye urefu wa kilometa 178.14. Kivuko hiki kipo umbali wa kilometa 6 kutoka Mji wa Ifakara katika

Wilaya ya Kilombero. Daraja la mto Mwatisi liko mwisho wa barabara ya Mkoa ya kutoka Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo yenye urefu wa kilometa 164.

Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 50 kwa ajili ya kufanyia upembuzi wa awali wa daraja la Mto Kilombero na pia katika mwaka wa fedha 2006/2007 jumla ya shilingi 70 zimetengwa kwa ajili ya upembuzi na usanifu. Baada ya kazi hizi za awali, Serikali itaendelea na juhudi zake za kupata fedha za ujenzi wa daraja hilo kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais.

Kwa upande mwingine juhudi zinafanywa na Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Maliasili na Utalii na Halmashauri za Wilaya ya Ulanga Mkoani Morogoro na Namtumbo Mkoani Ruvuma na wananchi za kufungua barabara kati ya Kilosa kwa Mpepo Mkoani Morogoro na Kitanda Mkoani Ruvuma. Hadi mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara ya Miundombinu imechangia jumla ya shilingi 750 milioni katika ujenzi wa madaraja ya Furua na Mwatisi Mkoani Morogoro na Daraja la Londo Mkoani Ruvuma, pamoja na ujenzi wa barabara kati ya Kilosa kwa Mpepo na Kitanda. Kwa kuwa kazi hizo zinaendelea, katika mwaka huu wa fedha, Wizara imetenga tena shilingi milioni 170 kwa ajili ya kuendeleza kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, Mbunge wa Kilombero kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kidatu – Ifakara – Mahenge ni sehemu ya barabara kuu ya Mikumi – Kidatu – Ifakara – Mahenge yenye urefu wa kilometa 175. Sehemu ya Mikumi hadi Kidatu kilometa 35 ilishajengwa na kukamilisha kwa kiwango cha lami. Aidha sehemu ya barabara hiyo kutoka Kidatu – Ifakara – Mahenge ni mojawapo ya barabara iliyopo kwenye mpango kabambe wa *transport sector investment programme* wa kuijenga kwa kiwango cha lami kuanzia kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007 hadi 2010/2011. Hata hivyo utekelezaji wa mradi huu utategemea upatikanaji wa fedha katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa haina mpango wa kuijenga barabara ya Mkoa Lupiro – Kilosa kwa Mpepo kwa kiwango cha lami ila itaendelea kupata matengenezo ya kawaida na maalum ili iweze kupitika na kutumika muda wote wa mwaka.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nilivyoangalia katika miradi mingi ya miundombinu mingi inapelekwa kuanzia mwaka 2007/2008 na tuna muda kama wa miaka miwili na miezi minne.

Je, haoni kwamba itafika wakati tutakuwa na viporo vingi vya ahadi hizi bila kutekelezeka kama isivyotawanywa kuanzia mwaka huo wa kwanza wa Ilani yetu ya Uchaguzi 2006/2007?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba miradi mingi inaanza

kutekelezwa mwaka 2007/2008 katika mwaka huu wa fedha tayari mipango ipo ya kuanza kutekelezwa ahadi zilizotolewa kwenye Ilani ya Uchaguzi na zile ambazo Mheshimiwa Rais aliziahidi na ndiyo maana tarehe 4 mwezi uliopita Bunge lako Tukufu liliidhinisha mabilioni ya fedha katika Wizara hii kuanza kutekeleza ilani ya uchaguzi ni zile ahadi za Rais. Kwa sababu ahadi hizi ni nyingi zote haziwezi kuanza kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha, ndiyo maana miradi mingine itaanza kutekelezwa mwaka kesho, mingine mwaka unaofuatia lakini nia ya Serikali ni kutekeleza ahadi zote ambazo zipo katika Ilani pamoja na zile ambazo Rais aliahidi. (*Makofi*)

Na. 394

**Ruzuku kwenye Pembejeo**

**MHE. AZIZA S. ALLY (K.n.y. MHE. SAID J. NKUMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakulima wa tumbaku na mahindi wa Mkoa wa Tabora bado wanazalisha mazao hayo kwa kukopeshwa au kununua kwa bei ya juu na kwa kuwa Serikali ya awamu ya Nne imedhamiria kuwapa wakulima hao kwa kutoa unafuu katika bei ya pembejeo ili waweze kuzalisha mazao hayo kwa faida:-

(a) Je, ni nini mikakati ya Serikali katika kuhakikisha utoaji wa ruzuku kwa pembejeo za kilimo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani katika kujibu hoja iliyo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM juu ya kuanzisha na kufufua viwanda vya mbolea hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Tamko la Serikali, kuhusu kutoa unafuu katika bei ya pembejeo kwa wakulima mwaka wa 2005/2006 Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 7,486 kwa ajili ya ruzuku kwa tani 63,840 za mbolea.

Aidha, Serikali ya Awamu ya Nne, imedhamiria kuendeleza utaratibu huo. Katika mwaka wa 2006/2007 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 21 kwa ajili ya ruzuku ya mbolea na mbegu bora, kwa ajili ya tani 129,000 za mbolea ambazo ni sawa na asilimia 33 ya mahitaji nchini na tani 2,000 za mbegu bora ambayo ni asilimia 10 ya mahitaji.

Katika kuhakikisha kuwa pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati muafaka, Serikali inaendelea kuyahamasisha makampuni makubwa duniani yaendelee kuleta mbolea hizo kwa wingi ili kuleta unafuu wa bei. Kwa kuanzia, Serikali imekubaliana na kampuni ya Yara kufungua Ofisi yake hapa nchini na imefanya hivyo kwa jina la Chapa Meli.

Aidha, majadiliano na wahisani na wadau wa ndani na nje yanaendelea katika kuandaa utaratibu wa kuwafikishia pembejeo wakulima vijijiji kupitia *DADPs* kwa kuwapatia mikopo kupitia katika Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) kwa ajili ya kununulia pembejeo.

Halmashauri za Wilaya zinahimizwa kuandaa *DADPs* ili kuhakikisha wananchi wanafaidika na mipango hiyo ya Serikali ya kuendeleza kilimo nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, Sura Na. 3 Ibara Na. 31 (d) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka wa 2005 inaeleza kwamba: "CCM katika kipindi cha Ilani hii itazitaka Serikali kuchukua hatua za dhati za kuweka utaratibu wenye uhakika wa upatikanaji wa mbegu bora na mbolea".

Kama sehemu ya utekelezaji wa agizo hilo Serikali inafanya jitihada za kuwahamasisha wawekezaji kujenga viwanda vya mbolea nchini hususan kwa kutumia malighafi zilizopo hapa nchini. Serikali pia inaendelea kuwahamasisha wenye kiwanda cha Minjingu ili kiongeze uzalishaji na usambazaji wa mbolea hiyo nchini. Aidha, juhudi zinafanywa ili kuhakikisha mbolea inafungwa katika mifuko midogo midogo ili kurahisisha ununuzi kulingana na mahitaji ya wakulima.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zao la tumbaku hulimwa sana katika Mkoa wa Tabora, Mkoa wa Rukwa na Wilaya ya Kahama:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa umuhimu wa kuhamasisha wawekezaji kuja kuanzisha kiwanda katika Mkoa wa Tabora cha Tumbaku? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, wakati wa Bajeti yake alisema kuna mkakati kabambe wa kuweza kuhamasisha na kuweza kuwasaidia wakulima wa tumbaku waweze kupata mbolea ya pembejeo kwa bei nafuu zaidi.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri anaweza mkakati huo Kabambe mpaka sasa tunamaliza Bunge mbona haujaja na mkakati huo unasubiri mvua zianze kunyesha wakulima waanze kulima ndiyo mkakati huo uje? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali yake mawili kama ifuatavyo, la kwanza kuhusu kiwanda ni wazo ambalo tungependa litekelezwe lakini namna pekee ya kuvutia kiwanda kiwepo Mkoa wa Tabora ni kuongeza sana uzalishaji kwa sababu sasa hivi nafasi katika viwanda vya Morogoro *Capacity* bado inatosheleza.

Kwa hiyo, nawashauri wananchi wa Mkoa wa Tabora tuongeze juhudi na tuangalie mikakati mingine kwa mfano yale maeneo yanayoweza kufunguliwa kwa mashamba makubwa ya kibiashara kama nilivyoshauri tuyafanyie kazi ili tuongeze uzalishaji kuweza ku-*justify* kuwepo kwa kiwanda.

Kuhusu suala la pili, kwamba niliahidi mpango kabambe wa mbolea mbona haupo napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba mkakati ambao nilikuwa nimeahidi matokeo yake ndiyo kuongezwa kwa ruzuku ya mbolea kutoka bilioni 7 mpaka bilioni 21 zikiwemo mbolea kwa ajili ya zao la tumbaku. Kwa hiyo, mkakati huo ni tayari umo ndani ya utekelezaji. (*Makofi*)

**MHE. BENITO MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jibu lake zuri.

Lakini nina swali moja kwamba Mkoa wa Ruvuma wana utaratibu mzuri sana katika huduma za maduka ya dawa, wameandika vibao kila duka kwamba duka na dawa muhimu. Sasa Serikali ina mpango gani wa kuelekeza watu wanaopata mbolea za ruzuku na wauzaji wa mbolea za ruzuku kuandika duka la mbolea ya ruzuku?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, katika utaratibu ambao umeandaliwa na Wizara wa usambazaji wa mbolea mwaka huu, tutaimarisha na tutachukua yale mambo mazuri yaliyofanywa katika baadhi ya Mikoa kuyasambaza nchi nzima. Kwa mfano hilo alilopendekeza la kuweka matangazo kwamba duka la mbolea tutafanya hivyo.

Lakini pia tutaongeza tumeamua safari hii kuongeza kigezo kingine ili kuepusha mbolea yenye ruzuku kuuzwa kwa bei zisizo na ruzuku. Tumeamua kwamba mwaka huu ile mifuko ya mbolea ya ruzuku itachpishwa maandiko yasiyofutika kwamba mbolea ya ruzuku. *(Makofi)*

Na pia bei katika vituo vile vikuu ambako mbolea ya ruzuku inafikishwa nayo itatangazwa katika mabango pale mahali ambapo inauzwa. Na Mawakala watakaoteuliwa haitakuwa tu kuteuliwa kuwa Wakala wa kuza mbolea wataingia pia mikataba na mamlaka za Wilaya na Mikoa ambamo wanathibitisha kwamba watachukua kiasi kile cha mbolea na kuifikisha katika maeneo.

` Kwa hiyo, hizo ni sehemu ya juhudi ambazo tumezifanya ili kuhakikisha kwamba mbolea ya ruzuku ambayo tumeiongeza maradufu mwaka huu kweli inafika kwa walengwa kwa bei tuliyoilenga ambayo ina ruzuku karibu asilimia 30. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wa Spika.

**Mhe. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, alipokuwa anajibu swali Na. 390 alijibu kwamba gesi inapatikana Wilaya ya Tukuyu. Sasa nilikuwa naomba mwongozo wako kwamba sidhani kama tuna Wilaya ya Tukuyu kwa ajili pengine ya kumbukumbu ya *Hansard* ni vizuri hilo likasahihishwa kwamba tuna Wilaya ya Rungwe siyo Tukuyu. Ahsante Mheshimiwa.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa ni sahihi kabisa. Hatuna Wilaya ya Tukuyu ni Wilaya ya Rungwe. Ahsante sana. Naona yatarekebishwa kama inavyopasa. Nilikuwa nimesimama kutangaza kwamba muda wa maswali umekwisha na maswali yenyewe pia ya leo yameisha.

Kwa hiyo, ninayo matangazo Waheshimiwa Wabunge mnivumilie ni mengi kidogo leo. Sijui kwa nini Kamati zote zimetaka leo zikutane. Lakini basi, kwanza nafurahi kutangaza kwa utaratibu ule ule ambao Waheshimiwa Mawaziri hususan wanaume na Naibu Mawaziri wanaume wameendeleza utamaduni mzuri ambao hauelekei pamoja na wito wa Spika haiungwi kabisa na Mawaziri na Naibu Mawaziri wanawake.

Leo kwenye *Speaker's Gallery* tunaye mke wa Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa. Yeye ni mama Azana. Yule pale. Pamoja na Binti yao Hawa ambaye yuko mwaka wa pili Chuo Kikuu cha Nanjin Uchina. Ahsante. Anasomea Udaktari. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Haroub Kiaratu, Mjumbe katika Kamati ya Kampeni ya Ulanga Magharibi. Yeye anatoka Tawi la CCM Mji mdogo wa Mtimbira karibu sana. Karibuni sana familia ya Mheshimiwa Waziri, kipekee tunapenda kumkaribisha binti aliyetoka Uchina kuja Tanzanika **k**umsikia baba yake ambaye ni Waziri wetu akifanya shughuli zake hapa Bungeni. Karibu sana. *(Makofi)*

Upande wangu wa kushoto katika *Public Gallery* wapo wanafunzi na walimu wa shule za msingi za Mnadani na *Holly Trinity* za Dodoma Mjini, naomba wasimame. Karibuni sana vijana wetu. Ahsante sana Walimu wa Mnadani na *Holly Trinity* kwa kuwaleta vijana wetu hapa ili wapate mafunzo mapema kabisa tena *live* ya jinsi demokrasia inavyoendeshwa ndani ya nchi yao. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Halima Mamuya ana wageni wake kama ifuatavyo:- Wapo Wajumbe 21 kutoka Mkoa wa Arusha ambao ni Wajumbe wa Umoja wa Wanawake wa Tanzania na Makatibu wa UWT Mkoa na Wilaya kutoka huko huko na Madiwani wanawake. Naomba tafadhali wasimame. Wale pale. Karibuni sana Waheshimiwa. Karibu sana. Na kweli ni Arusha naona baadhi yao wana vazi rasmi la Kimasai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Galinoma ameniomba nitangaze wageni wake kama ifuatavyo:- Mkewe Bibi Amelia Galinoma, ni Diwani, siyo tu yuko hapa kama mke wa Mheshimiwa Galinoma lakini Diwani Kata ya Kalenga. Yule pale. Na pia yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Halmashauri ya Wilaya. Mtoto wao Selina Galinoma, imeandikwa ana miaka 7. Kumbe Mheshimiwa Galinoma ana mtoto wa miaka 7. *(Kicheko/Makofi)*

Pia yupo Katibu wa Mbunge anaitwa Juma Mkombozi. Ahsante sana. Wapo wageni wa Mheshimiwa Balozi Hamis Sued Kagasheki, Mbunge wa Bukoba Mjini, nao ni Bwana Kobianda, Meneja Mkuu wa *Euro African Bank* yule pale. Pia Bwana Wasia

Mushi, Meneja wa Masoko yule na Bi. Lite Kisuda, ambaye ni *Marketing Executive* yule pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wa Dar es Salaam, wameomba nitambulishe viongozi wa vibarua wa Mamlaka ya Bandari Dar es Salaam, Viongozi wa Vibarua. Mmoja anaitwa Mputa Zeno yule pale amenyoosha mkono. Na mwingine Bwana E.P. Siafu. Karibuni sana, karibuni sana. Na poleni na kazi ngumu mnayoifanya pale Bandarini. *(Makofi)*

Halafu Mheshimiwa Devota Likokola, ameniomba nitambulishe wageni wake ambao ni kama ifuatavyo wanatoka Songea. Bwana Samwel Mbano, Bi. Zuhura Msengi, Bwana Noel Mwigane, Asumtha Mwamtende, ni mama huyo. Kipande Ali, sina hakika Kipande ni mwanamme au mwanamke labda akisimama. Ah! Ni mwanamme. Na Bi. Marieta Msembele. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Halima Mamuya pamoja na Mheshimiwa Batilda Burian naona wageni wao hawa nimekwishawatambulisha ndiyo wale wageni kutoka Arusha. Tayari nimeshawatambulisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lembeli, Mbunge wa Kahama na Mheshimiwa Maige wa Msalala, wanao wageni wao ambao ni Madiwani wanne kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kahama, wanaongozwa na Mheshimiwa Diwani Josephine Balanoga, wale pale. Ahsanteni sana. Karibuni sana Waheshimiwa. *(Makofi)*

Wageni ambao sikuwataja inawezekana karatasi zimekuja zimechelewa sana, kwa sababu niliona vikaratasi vilikuwa vinaendelea kuja hadi sasa. Siyo rahisi wakati naendesha kikao kuweza kuwa nasoma tena matangazo kama hayo. Kwa hiyo, mniwie radhi Waheshimiwa mliochelewa kuleta taarifa zenu kuhusu wageni.

Waheshimiwa Wabunge kesho Jumamosi tarehe 12 kutakuwapo na Kongamano/Semina ya UKIMWI kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Semina hiyo imeandaliwa kwa maombi mahsusi ya sisi Wabunge kutokana na ile Semina ya awali tuliyokuwanayo mapema kabla ya mkutano huu. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa zamani wa Bunge na itaanza saa 3.30 na nusu asubuhi.

Mada zenyewe zinatokana na utafiti halisi uliofanywa na *REDET* wakati wa Uchaguzi. Kwa hiyo, zimelenga hali ya UKIMWI katika majimbo ya Uchaguzi. Ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge tuwepo ili tuweze kusikia hali halisi ilivyo hivi sasa katika vita ya Taifa dhidi ya balaa hili. Ni saa 3.30 asubuhi kesho katika Ukumbi wa Bunge wa zamani.

Waheshimiwa Wabunge kesho pia baada ya hiyo semina kutakuwa na uchaguzi wa viongozi wa *Commonwealth Parliamentary Association* ngazi ya Tawi letu la Bunge la Tanzania. Mnafahamu kwamba uongozi wa *CPA* Tawi la Tanzania ulikuwa umemaliza muda wake na tulikuwa hatujafanya uchaguzi. Sasa tunaenda kwenye Mkutano Mkuu Ghana wa *CPA* mwezi ujao tarehe 14 Septemba, 2006. Ni muhimu sana tuweze kupata uongozi ili wakashiriki kikamilifu na kihalali katika huo Mkutano.

Nafasi ambazo zitagombewa ni Mwenyekiti, Makamu wa Mwenyekiti, Wajumbe 10 wa Kamati Kuu kwa mpangilio ufuatao:- Wawili kutoka Chama Tawala, wawili kutoka Kambi ya Upinzani. Wawili wanawake. Na mjumbe mmoja mmoja kutoka katika Kambi zote hizo wa ziada. Kwa hiyo inakuwa jumla 10. Nawasihi sana kesho tuwe na subira mara baada ya semina tubaki ili tuweze kufanya uchaguzi.

Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati Bunge ya Huduma za Jamii, anawaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Huduma za Jamii wakutane saa 5 leo Ukumbi Na. 219 ghorofa ya pili, jengo la Utawala, saa 5 asubuhi ya leo Ukumbi Na. 219 Kamati ya Huduma za Jamii. *(Makofi)*

Mhesihmiwa Anna Abdallah, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, anatangaza kwamba leo saa 5 asubuhi Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje wakutane katika chumba Namba 133. Kamati ya Mambo ya Nje wakutane Chumba Namba 133.

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti, Kamati ya Uwekezaji na Biashara, anawaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara wakutane Ukumbi Na. 231 ghorofa ya pili, jengo la Utawala saa 6 mchana. Saa 6 mchana Kamati ya Uwekezaji na Biashara chumba Namba 231.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anatangaza kuwa tarehe 13 yaani Jumapili ijayo kutakuwa na kikao cha Wajumbe wa Kamati hiyo, saa 5 asubuhi chumba Namba 231. Kamati ya Maendeleo ya Jamii saa 5 asubuhi Jumapili tarehe 13 mwezi wa nane.

Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira wafanye mkutano leo saa 5 asubuhi chumba Namba 428. Kamati ya Maliasili na Mazingira saa 5 asubuhi leo chumba Namba 428.

Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, anakumbusha kwamba Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali na za Serikali za Mitaa, yaani *PAC* na *LAAC* watakuwa na mkutano katika chumba Namba 431 saa 5 asubuhi. *PAC* na *LAAC* saa 5 asubuhi chumba Namba 431.

Timu zetu za mpira wa miguu na netiboli kesho zitakuwa na michezo ya kirafiki baina ya timu zetu hizo na timu za viongozi wa Dini wa Dodoma. Michezo yote hiyo itachezwa uwanja wa Jamhuri saa 10 jioni. Waheshimiwa Wabunge itakuwa ni baada ya Semina na nadhani baada ya uchaguzi wa *CPA* tukazishangilie timu zetu na wafuasi wetu tuwakaribishe ili tuone pengine tunaweza kurejea yale yaliyotokea kule Kongwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, anaomba tutangaze kwamba Wajumbe wale wanaokwenda Dar es Salaam wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Huduma za Jamii na Mambo ya Nje, kutakuwa na Warsha itakayofanyika *Hotel* ya Kilimanjaro na kwamba kutakuwa na kikao saa 11.00 jioni kujadili safari hiyo.

Saa 11 jioni leo katika Ukumbi wa zamani wa Bunge, Wajumbe wa Kamati hizo tatu ambao wanajiandaa kwenda Dar es Salaam. Nitoe tu taarifa tumepanga utaratibu ili waende kwa awamu, wengine wanahitajika hapa Jumatatu. Nusu watakwenda mapema na nusu watafuata baadaye. Lakini maelezo ya ziada yatapatikana saa 11.00 jioni katika Ukumbi wa zamani wa Bunge.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Kikao tunakiomba saa 10.00 jioni na siyo saa 11.00 jioni, Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Sawa, Saa 10.00 jioni imesikika.

**Mhe. MBARUK K. MWANDORO:** Ndiyo, Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Vema saa 10.00 jioni, Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge jana nilipokea mbele yenu hapa hoja kutoka kwa Mheshimiwa Mudhihir Mohamede Mudhihir ambayo ilikuwa inapendekeza kuleta jambo Bungeni kama jambo la dharura na muhimu lijadiliwe chini ya Kanuni 45, Kanuni ndogo 3(f). *(Makofi)*

Kwa kutumia Kanuni ya 55 Kanuni ndogo ya 2 ya Kanuni hiyo ambayo nitaisoma hapa ambayo inasema: "Spika, anaweza ama papo hapo kutoa uamuzi wake juu ya jambo la utaratibu lililotajwa au kuahirisha uamuzi ili alifikirie zaidi jambo hilo na kutoa uamuzi wake baadaye".

Waheshimiwa Wabunge, nimetafakari kwa muda huu wa saa 24 nimeona jambo alililoleta Mheshimiwa Mudhihir ni jambo la dharura na la haraka na lina haja ya kujadiliwa na Bunge hili. Kwa hiyo, nimemkubalia ombi lake na namwomba sasa aendelee na alielezee hilo jambo kama mtoa hoja. *(Makofi)*

## AZIMIO BINAFSI KUHUSU FILAMU YA DARWIN'S NIGHTMARE

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kwa mujibu wa Kanuni ya 45, Kanuni ya 3(f) Bunge lako Tukufu lipitishe hoja ya dharura kuhusu filamu iitwayo *Darwin's Nightmare.*

Mheshimiwa Spika, mtengenezaji wa *Darwin's Nightmare*, Bwana Hurbert Saoper ni Mwandishi wa kujitegemea, mkazi wa Ufaransa aliye raia wa Australia. Alipokuja nchini Tanzania aliomba kibali cha kupiga picha kwa ajili ya kutengeneza d*ocumentary* kuhusu aina mbali mbali za samaki wanaopatikana katika Ziwa Victoria. Alifuata taratibu zinazotakiwa katika kupata kibali cha kupiga picha katika Jiji la Mwanza. *(Makofi)*

Shughuli ya upigaji picha kati ya mwezi Februari, 2003 na mwezi Mei, 2003. Lakini badala ya kupiga picha kama alivyoomba, amepiga picha ambayo maudhui yake ni tofauti kabisa na madhumuni ya kibali alichopata. Filamu ya *Darmin's Nightmare* kwa mtazamo wake inatoa taswira kuwa Tanzania ni jinamizi la kiza la zama za kale. Mambo yaliyokusudiwa katika filamu hiyo ni kuonyesha umaskini uliokithiri, ukahaba na ulevi, uchafuzi wa mazingira uliopindukia mipaka, njaa, uingizwaji haramu wa silaha kupitia kiwanja cha ndege cha Mwanza, ndege mbovu zinatumika kusafirisha samaki kwenda soko la Ulaya na usalama mdogo uliopo katika kiwanja cha ndege cha Mwanza. Mambo yaliyoonyeshwa ni uongo, uzandiki, mambo ya kupanga na ya kubuni. *(Makofi)*

Ipo mifano mingi inayodhihirisha nia mbaya ya mwandishi wa filamu hiyo, miongoni mwa hayo ni kama yafuatayo:- Umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, katika kujenga taswira ya umaskini uliokithiri mwandishi amechagua makambi ya wavuvi ambayo siyo makazi ya kudumu na kuonyesha kuwa ndiyo makazi na maisha halisi ya wakazi wa Mwanza. Kundi la watoto wa mitaani walioonyeshwa, ni dhahiri walichukuliwa baada ya kuandaliwa kwa ajili ya kujenga taswira iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Wahusika waliochaguliwa, walichaguliwa mahususi kwa kukamilisha dhamira yake na hivyo kuonekana katika matukio mbalimbali. Kwa mfano, mtu yule yule mmoja ameonekana akiwa mlinzi na mishale yake. Mvuvi akisukuma kafi. Msimulizi wa kadhia zilizopo Mwanza na msomaji wa makala ya gazeti la *The East African* linalozungumzia uingizaji wa silaha.

Mheshimiwa Spika, ukahaba na ulevi. Wanawake walioonyeshwa kuhusika na ukahaba ni wanne na marubani wawili. Wao wamerudiwa hao hao katika maeneo mengi ya filamu. Watoto walioonyeshwa kuvuta sigara na kunusa gundi au petroli ni wachache na ni wale wale katika filamu mzima.

Mheshimiwa Spika, usafirishaji wa silaha, hakuna ushahidi kuwa ndege zilizoonyeshwa zilibeba silaha badala yake yupo mtu mmoja aliyesoma habari za kwenye gazeti la *The East African.* Taarifa hizo ziliwahi kukanushwa humu Bungeni na Serikali na Waziri wa Mambo ya Ndani, tarehe 25 mwezi wa saba mwaka 2002 na kwa ruksa yako naomba kunukuu sehemu ya *Hansard* hiyo.

Hoja hii ilikuwa imetolewa na Mheshimiwa Derefa aliyekuwa Mbunge wa Shinyanga Mjini. Na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib, alijibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lakini watu wa Mkoani wanatuambia kwamba jambo hili lilitokea zamani, yaani tuhuma hizi si za leo ni za toka mwaka 2000 na wakawa na kikao tarehe 20 Septemba mwaka 2000 chini ya *RPC, RAO, TRA, RCO* na kadhalika.

Walikutana pale Mwanza katika kikao chao wakaenda kwenye viwanda vya samaki, wakaenda kwenye viwanja vya ndege kuangalia, wakahakikisha kwa kweli

hakuna mtu yeyote awezaye kuja nchini kuleta silaha kwa sababu wanachunguza kila kitu. Kwa hiyo jambo hili si jipya kwa Mkoa wa Mwanza.

Lakini nashukuru kwamba ametuzindua, tutajitahidi kuongeza nguvu zaidi. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, hata mwanamke aliyeulizwa kuhusu silaha hizo hakuthibitisha kuwepo kwa silaha. Badala yake zilionekana picha za bunduki zilizokuwa ukutani. Ukweli kuhusu hali ya uvuvi wa samaki. Kiwango cha samaki wanaouzwa katika soko la Ulaya hakiwezi kuathiri samaki wanaoliwa ndani ya nchi na kusababisha njaa kwa sababu takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba samaki wanaouzwa nje ya nchi ni kidogo ukilinganisha na wanaotumika hapa nchini.

Kwa wastani samaki aina ya sangara wanaovuliwa nchini ni tani laki moja ishirini na tano. Kati ya hao ni tani themani elfu tu ndiyo wanaopasuliwa na kuuzwa nchi za nje. Kwa kweli samaki wa aina ya sangara hawapendwi sana na wenyeji wanaozunguka Ziwa Victoria. Wapo aina ya samaki wengine zaidi ya 17. Kwa ruksa yako ningependa niwataje badhi yao: Wapo sato wa rangi ya udongo. Katika jamii ya sato wapo njusi, wenyewe ni wekundu na wakubwa. Wapo nembe, wapo ningu, na katika jamii ya ningu wako mhuyu, wenyewe ni wakubwa. Wapo gogogo, wana miba mbavuni, wanatumia kama *defense* wako njegele, kuna fulu, kuna mumi, ni aina ya kambale, wana sharubu, lakini katika aina hiyo ya mumi wako mbofu wana minofu mikubwa. Wako salali, ni vidogo vidogo lakini wana mayai. Wapo wa aina ya mamba. Wapo mbese, wapo ngele, wapo soga, wapo pongwe, kuna dagaa watamu, wapo kamongo na hawo sangara.

Kwa hiyo, si kweli kwamba kutoka kwa sangara hawa ndiyo wananchi mpaka wanakwenda kunyang'anyana samaki na ndege na mafunza. Serikai imepiga marufuku mauzo ya nje ya samaki wa aina yoyote zaidi ya sangara. Uvuvi wa aina zote za samaki ni tani 475,400 ambayo ni tani 80,000 wa aina ya sangara wanaouzwa katika soko la Ulaya. Tani 395,400 ni kwa matumizi ya ndani.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya kusindika sangara zimeongeza sana ajira katika muda mfupi. Wapo wavuvi 98,015 walioajiriwa na kujiajiri katika uvuvi. Wapo wafanyakazi 3,947 ambao wameajiriwa na viwanda vya minofu ya samaki. Wapo watu wengine wengi walioajiriwa katika uuzaji wa samaki, utengenezaji wa mazao ya samaki, kama vile chakula cha kuku. Utengenezaji wa maboti na kadhalika.

Ukweli ni kwamba maisha ya wavuvi katika ukanda wa Ziwa yameboreshwa kutokana na biashara ya sangara. Kuhusu ukahaba hili ni tatizo la ulimwengu wote. Na msingi wake ni mmomonyoko wa maadili na si sahihi kuihusisha na biashara ya minofu ya sangara peke yake. Hata hivyo, sio kweli kwamba ukahaba umekithiri kwa kiasi kile kikubwa jijini Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Filamu ya *Darwin's Nightmare* imejaa uzushi na uwongo wenye lengo la kupaka matope Tanzania na kuhujumu biashara ya samaki katika Ziwa Victoria kwa upande wa Tanzania.

Alipokuja Tanzania Bwana Hurbert Saoper, alitumia njia zisizokubalika kitaalam ikiwa ni pamoja na kuhonga, kubadilisha jina, taaluma na madhumuni ya safari yake nchini mwetu. Yeye mwenyewe amekiri katika *website* yake *www.darwin'snightmare.com* Utumiaji wa njia hizo haramu katika ukusanyaji wa habari na kupiga picha. Hiki ni kielelezo cha uovu wa dhamira yake ya matumizi ya picha kama ilivyodhihirishwa na filamu yake iliyokithi uwongo na uzushi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, mbali na itikadi zetu tofauti waniunge mkono.

Baada ya kutoa maelezo hayo, sasa naomba kulisoma azimio lifuatalo ambalo ndilo ninalowaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waniunge mkono. Azimio la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu filamu iitwayo *Darwin's Nightmare:*

KWA KUWA wakati akilihutubia Taifa tarehe 31 Julai, 2006 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alizungumzia pamoja na mambo mengine filamu iitwayo *Darwin's Nightmare* iliyotengenezwa na mwandishi wa habari anayeitwa Hurbert Saoper, anayeishi Ufaransa; na

KWA KUWA maudhui ya filamu hiyo ya *Darwin's Nightmare* yamelenga kuonyesha kwamba uvuvi wa samaki aina sangara katika Ziwa Victoria unafanyika kwa njia isiyo salama na uuzwaji na usafirishaji wa minofu yake kwenda katika soko za nchi ya Ulaya kumesababisha majanga mbalimbali kwa wananchi waishio katika Ukanda wa Ziwa Victoria; na

KWA KUWA filamu hiyo inaonyesha kwamba wananchi waishio Ukanda wa Ziwa Victoria hawafaidiki na biashara hiyo ya samaki na badala yake wanaambulia mabaki ya samaki hao maarufu kwa jina la mapanki;

NA KWA KUWA filamu hiyo imekusudia kuonyesha taswira ya Jiji la Mwanza, kwa kutumia makambi ya uvuvi, pamoja na vijiji kadhaa, ili kubainisha umaskini uliokithiri na uchafuzi wa mazingira uliopindukia katika ziwa Victoria.

NA KWA KUWA filamu hiyo, inajenga dhana isiyokuwa na ukweli ya kuoanisha biashara hiyo ya minofu ya samaki na kuwepo kwa ulevi na ukahaba uliosababisha kuenea kwa ugonjwa hatari wa UKIMWI Katika eneo hilo.

NA KWA KUWA filamu hii imetamka kwamba ndege zinazohusika na ubebaji wa minofu, kutoka Mwanza, huwa zinaleta silaha hapo Mwanza, kwenda katika nchi za Maziwa Makuu, kuchochea vurugu na vita, jambo ambalo ni la uzushi na uzandiki.

NA KWA KUWA takwimu zilizopo, zinaonyesha kwamba minofu ya samaki inayouzwa katika soko la Ulaya ni samaki wa aina ya Sangara pekee ambao ni asilimia 17 ya samaki wote wanaovuliwa katika ziwa Victoria upande wa Tanzania.

NA KWA KUWA zipo hatua madhubuti zinazochukuliwa, na zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali, kwa ajili ya kuweka mazingira bora ya uvuvi katika Ziwa Victoria. Kuhifadhi mazingira na kuendeleza wananchi kiuchumi na kijamii.

NA KWA KUWA maudhui ya filamu ya *Darwin's Nightmare* yana nia mbaya kwa nchi yetu na watu wake na kwamba yanalenga kuharibu soko la minofu ya samaki aina ya Sangara lililoshamiri katika nchi za Ulaya na hivyo kuathiri uchumi na ajira ya Watanzania.

KWA KUWA, lengo jingine la filamu hii ni kutia dosari jina nzuri la Tanzania katika Afrika na Jumuiya za Kimataifa kuhusu nafasi yake ya usuluhishi, wa migogoro na kutetea amani Afrika na duniani kote kwa kudai kuwa Mwanza ni kituo cha kueneza silaha katika nchi za maziwa makuu, zinazoletwa na ndege zinazokuja kuchukua minofu ya samaki.

KWA KUWA kwa ujumla filamu hiyo inawadhalilisha Watanzania katika macho ya ulimwengu na kuharibu sifa na jina nzuri la nchi yetu, hivyo basi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika mkutano wa nne kwa mujibu wa kanuni ndogo ya pili ya kanuni ya 43 ya kanuni za Bunge, toleo la mwaka 2004, linaazimia kama ifuatavyo;

1.Tunampongeza na kumuunga mkono Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ujasiri aliouonyesha wa kueleza ukweli wa uzandiki na upotoshaji uliofanywa na filamu hiyo. (*Makofi*)

2.Kumkaripia mtunzi na mwandishi wa filamu ya *Darwin's Nightmare* kwa kutumia vibaya uhuru wake na kukiuka miiko ya uandishi wa habari. (*Makofi*)

3.Kumkaripia Mwandishi wa filamu ya *Darwin's Nightmare*, kwa njama zake za kutaka kuharibu fursa ya Tanzania katika biashara ya minofu ya samaki katika soko la Ulaya. (*Makofi*)

4.Kumkaripia Mwandishi wa filamu ya *Darwin's Nightmare,* kwa kutoa taarifa za uwongo, uchonganishi na uzandiki kwa nchi yetu kwamba biashara ya minofu ya samaki, inauhusiano na uingizwaji wa silaha katika nchi za maziwa makuu kupitia jiji la Mwanza isivyo halali. (*Makofi*)

5.Kumkaripia Mwandishi wa filamu ya *Darwin's Nightmare* kwa kueneza uwongo na kuharibu sifa ya nchi yetu na watu wake kwa mambo yasiyo ya ukweli. (*Makofi*)

6.Kuvitanabaisha vyombo vya habari, vya nchini na wananchi kuweka mbele uzalendo na maslahi ya kitaifa wanapotumia uhuru wao wa kutoa maoni yao. (*Makofi*)

7.Tunaomba Watanzania wawe macho wakati wote, kwani katika mazingira ya leo watatokea watu wasioitakia mema nchi yetu, watakaojaribu kupiga vita jitihada zetu za kujenga taifa letu, watakaotaka kudhoofisha maslahi ya taifa letu na kwamba tukiwa macho tutaweza kuzifichua njama hizo kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. FAIDA M. BAKAR:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iliotolewa iamuliwe)*

**SPIKA**: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo iko mbele na imeungwa mkono lakini itabidi ijadiliwe, na nitoe tu sahihisho, sio kwa mujibu wa Kanuni ya 45(2) ambayo ingenilazimisha mimi niipeleke kwenye Kamati huu ni mjadala wa kawaida. Hoja hii iko mbele ya Bunge sasa kwa mujibu wa kanuni 38 kanuni ndogu (1) ndivyo inavyozungumza jambo la dharura linatolewa, halafu kwa kanuni, kanuni ndogo ya (4) ya kanuni hiyo ya 38 muda wa kuijadili ni nusu saa tu. Sasa nimepima hali yenyewe na kwa sababu lazima tutoe pande zote za uwakilishi ndani ya Bunge hili kuweza kupata muda wa kutosha wa kuijadili, nusu saa haitatosha ambayo iko kwenye 38(4). Kwa hiyo napenda nimwombe Mheshimiwa Waziri wan chi Ofisi ya Waziri Mkuu, masuala ya Bunge atoe hoja, ili tutengue kanuni ya 38(4) tupate muda ulio zaidi ya nusu saa kujadili hoja hii. (*Makofi*)

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, kwa mujibu kama ulivyosema kanuni ya 38(4) ambayo inatutaka baada ya kusikiliza hoja iliyotolewa na wewe kuridhika kwamba ni jambo la dharura lazima lijadiliwe linatutaka upitishe, uliruhusu hili kwa muda wa nusu saa.

Sasa mimi baada ya kusikiliza kwa makini sana aliyoyasema Mheshimiwa Mudhihir, naridhika na kukubaliana na wewe sana, kwamba jambo hili ni nzito la kitaifa ambalo Watanzania wenye uchungu na taifa lao wenye upendo na wazalendo halisi, wangependa kabisa kushiriki katika mjadala na kumuunga mkono Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, ni kweli nusu saa haitoshi.

Sasa naomba kutoa hoja kwamba kifungu hicho cha nne kinachokutaka iwe nusu saa kitenguliwe ili kuwapa Waheshimiwa Wabunge muda wa kutosha kujadiliwa na muda ambao wewe mwenyewe utaona unatosha kuweza kulijadili jambo hili kwa uzito ambao Watanzania wanatutegemea Bunge letu tufanye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyo mbele yetu ni ya Bunge kutakiwa kutengua kanuni ya 38(4) ili kutoa muda wa kutosha kujadili suala hili lililo la dharura na muhimu kwa taifa letu, na nimeamua kutoa nafasi ya kutosha kama kawaida yetu ya robo saa isiyozidi robo saa kwa kila mchangiaji, na kwa maana hiyo sasa nitamwita msemaji kutoka kambi ya upinzani Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nashukuru sana kwa fursa hii uliyonipa ya kuwa msemaji wa kwanza katika jambo hili zito, ambalo kila Mtanzania halisi anaona kuwa hili ni jambo zito. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la kulinda hadhi ya nchi yetu, labda mimi niseme halina mchezo, ni suala linahitaji umoja wa kweli wa sisi Wabunge na Watanzania kwa jumla na kwa msingi huo basi kabla ya kusema yale ambayo ninayo ningependa niweke malalamiko machache juu ya jambo hili kwa wenzangu walio wengi katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge letu sasa ni kipindi cha tatu cha mfumo wa Vyama Vingi, mimi kwa mawazo yangu nilidhani kuwa sasa tumefika wakati wa kubadilika katika kukubiliana na mambo hasa yakiwa ya kitaifa, na tukaweka mbali ushabiki wa kambi, au ushabiki wa itikadi, tukashirikiana katika kujadili jambo ambalo linatuhusu wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni majuzi tu tulionyeshwa kanda hii na wengine sisi ilikuwa mara ya kwanza kuiona kwa macho, ingawa habari zake tumeshazisikia. Mimi nilifikiri kuwa baada ya kuonyeshwa jambo lile sote tungepaswa kukaa sote kama Wabunge tukajadili tufanye nini na tutoe Azimio gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana hilo halikufanyika, kundi moja lilikaa peke yake likajadili jambo hili, sasa ni vizuri basi tunaposema tunajadili jambo la kitaifa, tuache kubaguana tushirikiane kujadili jambo kama hili. (*Makofi*)

Ushahidi upo, jana kuna baadhi ya mikoa ilikaa, kujadili jambo hili, nasikitika sana kukuambia kuwa wajumbe Wabunge wa Upinzani waliotoka ndani ya mikoa hiyo, wengine hawakualikwa na wengine walitolewa nje ya mlango ati watu wanakikao maalumu cha chama, hivi katika jambo hili tuna kikao cha chama kweli? (*Makofi*)

Hii ni tahadhari naitoa, nafikiri tumeisikia sitaki niendelee sana.

Mheshimiwa Spika, filamu hii sio mpya, Watanzania ni vizuri wakaelewa kuwa hii filamu sio mpya kama alivyosema mtoa hoja imeandaliwa mwaka 2003 na ilitolewa rasmi na kuanza kutizamwa huko ilikotizamwa mwezi Septemba, 2004.

Serikali kwa wakati ule ilichukua hatua zinazofaa iliwatumia mabalozi, wakakanusha, mimi nina uhakika aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, alifanya jambo kubwa kumwarifu Rais juu ya jambo hili, na Rais wa awamu ya tatu yeye alifikiria kuwa kwa wakati ule ni bora kuliacha kwanza na liliachwa kwanza halikusemwa.

Likaendelea kuoneshwa huko lilikooneshwa, likaibuka tena katika mwaka 2005, Mheshimiwa Rais vilevile akaamua kuwa liachwe, lakini inaonekana mtu aliyezoea kukupaka matope, hasiti ataendelea, kwa vile inaonekana imeendelea kuoneshwa huko ilikooneshwa, na ndio sasa leo tupo katika ukumbi huu tunajadili au tunajadili hoja hii ya kumuunga mkono Mheshimiwa Rais ambao sisi upande wa upinzani tunaiunga mkono sana.

Lakini sasa kama ilivyo kawaida, mtu anapokupiga yai viza juu ya bega lako inabidi uangalie mambo mawili, kwanza uangalie lile yai limekuumiza halikuumiza lakini pili je, limekuharibia nguo au halikukuharibia. Kama limekuumiza au halikukuumiiza ni hatua ya kwanza lakini kama nguo imeharibika, basi unapaswa kuisafisha, huwezi kuiacha ikakaa, na mambo ya ajabu ajabu, na ukaweza kutembea nayo nguo ile.

Mheshimiwa Spika, huyu ametuambia jambo baya sana, lakini sisi kama Watanzania tunapaswa kutizama na mimi ningeiomba sana Serikali itizame basi katika haya yaliyosemwa, yamo ya uwongo, lakini yale yaliyo ya kweli je, yameshafanyiwa marekebisho? (*Makofi*)

Umetajwa ukahaba, imetajwa ulaji wa mapanki, imetajwa uvutaji wa gundi, nasema niyaseme haya matatu kwanza. Je, haya tunayafanyaje? Serikali inapaswa iangalie imechukua hatua gani kurekebisha masuala haya, imetajwa njaa mimi sidhani kama njaa tunaweza tukasema moja kwa moja kwamba nchi haijawahi kukabiliana. Ingawa huyu mwandishi anazungumza njaa ya samaki, kwetu sisi katika Tanzania sisi hatuli samaki kama chakula, hii ni mboga tu, lazima tuangalie hatujawahi kukabiliana na mambo haya, tukiwa hapa ndani wenyewe. Tungejitizama na tukaona tunafanyaje au tunaamini vipi katika jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini baya zaidi alilolisema ni hili la silaha, Tanzania imekuwa *foforant* katika historia yake, sio tu katika kusuluhisha matatizo ya maziwa mkuu, lakini hata kuzikomboa nchi zilizokuwa kwenye ukoloni, ni nani asiyejua hilo. Sasa anapotokea mtu akasema kuwa sisi ati tunatumia nchi yetu kupitisha silaha kuongeza vurugu katika nchi tunazozisuluhisha kwa kweli huu ni uzalilishaji mkubwa sana ambao napenda sana Watanzania waone juu ya jambo hili. (*Makofi*)

Lakini katika hotuba ya Mheshimiwa mtoa hoja, alisema kuwa hapa huyu mwandishi aliingia alipewa vibali vyote halali vya kufanya kazi, kwa mawazo yangu mimi na kwa mawazo ya kambi ya upinzani, mtu anapopewa vibali halali, akafanya kazi, halafu mwisho huku wanasema alipomalizia kuwa alikuwa anafanya udanganyifu, kweli hii pia peke yake inaleta hali ya wasiwasi, vibali halali au alikuwa mdanganyifu, *anyway* hiyo *is not* sio hoja. Lakini hoja yangu hapa na hoja ya kambi ya upinzani, hawa watu vyombo vya dola vilivyompa kibali, kufanya kazi kama hii, hivi baadaye hawakumweka kitako wakaangalia hii kanda ina uhalali gani?

Mheshimiwa Spika, huo ni udhaifu na tusihuru tena, hapa vyombo vyetu vya dola vimeteleza na lazima tuviwajibishe kwa jambo hili, sisemi kwamba kuwa tuwafukuze, lakini angalau tukiwaambia kuwa hapa mlikosea wakubali kuwa walikosea na waiombe

radhi Serikali kwa jambo hili. Kwa sababu wametuambisha, asingeweza kufikia kote huko kama vyombo vya dola vilichukua hatua inayofaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikirudi mwanzo, tulinyimwa fursa muhimu sana ya kushiriki katika jambo hili. Sasa kwa sababu tulinyimwa fursa ya kushiriki jambo hili, sisi kambi ya upinzani tunaomba sasa basi, tutumie kanuni ya 47(c) ili tushauri baadhi ya mabadiliko, ili tuwe pamoja katika jambo hili zito, kwa sababu fursa hii mlitunyima ya kuwa pamoja na ninyi. (*Makofi*)

Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda sasa kuwasilisha mapendekezo ya mabadiliko kama ifuatavyo;

Mapendekezo ya Kambi ya Upinzani Bungeni juu ya Azimio la Bunge, kuhusu filamu itwayo *Darwin's Nightmare*, kambi ya upinzani inawahakikishia Watanzania wote kwamba, siku zote itakuwa mstari wa mbele katika kutetea maslahi ya taifa letu na kwa hiyo basi tunapenda kufanya marekebisho yafuatayo katika Azimio hilo. (*Makofi*)

Kwanza kwamba tunamwunga mkono Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, na Watanzania wote katika kulinda hadhi, heshima, uhuru wa taifa letu na utu wa Watanzani, dhidi ya uzalilishaji wa aina yoyote ile. (*Makofi*)

Pili, kwamba tunavitaka vyombo vya habari kuendelea kuwaelimisha wananchi na kufichua ukweli bila woga upendeleo au vishawishi vya aina yoyote kwa maslahi ya taifa letu.

Tatu, kwamba tunampongeza Rais wetu kwa kuunda Kamati ya Uchunguzi, ili kupata taarifa zaidi juu ya ukweli na athari zinazotokana na filamu hii.

Nne, kwamba baada ya uchanguzi kukamilika, hatua zichukuliwe kuwaelezea Watanzania na watu wengine kwa ujumla, kuhusiana na maelezo aliyotoa mwandishi huyu, ikiwa ni ya kweli au la.

Tano, kwamba hatua madhubuti na muafaka zichukuliwe dhidi ya mwandishi huyu baada ya uchunguzi wa kina kukamilika na matokeo yake kutangazwa. (*Makofi*)

Sita, kwamba pamoja na uchunguzi unaoendelea kufanyika ni ukweli usiopingika kuwa mwandishi wa filamu hii amewazalilisha Watanzania kwa kutumia vibaya uhuru wake. (*Makofi*)

Saba, kwamba Tanzania inarekodi nzuri duniani katika kusuruhisha migogoro ya nchi za jirani kuhifadhi wakimbizi na kushiriki katika kuleta amani ya kuudumu katika Maziwa Makuu. Hivyo basi tunaitaka Serikali ichukue hatua muafaka, dhidi ya vyombo vyote vya Serikali vilivyohusika kwa kuzembea, hadi nchi yetu ikafikia katika hali hii ya udhalilishwaji na kuhatarisha maslahi ya uchumi na kiusalama ya nchi yetu. (*Makofi*)

Nane, kwamba tunaitaka Serikali itengeneze filamu mbadala *Counter Documentary*, ya kuonyesha ukweli dhidi ya filamu ya *Darwin's Nightmare*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maazimio haya yanalenga kurekebisha maazimio yanayopendekezwa na Mheshimiwa Mudhihir Mohammed Mudhihir, ambaye nampongeza sana kwa kazi aliyofanya na hasa katika maazimio nambari moja hadi saba. Ili kufanya maazimio ya Bunge hili yawe mazito zaidi, tunapendekeza mapendekezo yetu, namba moja mpaka nane yachukue nafasi ya maazimio moja mpaka saba, yanayosomeka katika hoja ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kitendo kilichofanyika sisi hatudhani kuwa suala la kumkaripia tu litatosha, tunapaswa tuchukue hatua za muafaka ili yeye pamoja na wengine wote wanaokusudia kuichezea Tanzania, wasidhanie kuwa Tanzania inaweza kuchezewa kama kitambaa cha kupangusia mafua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, ahsante. (*Makofi*)

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu, kanuni hiyo hiyo 47 amesoma moja, mimi ningeomba iongezwe na Kanuni Namba 47(2) ambayo inasomeka hivi: Isipokuwa kama taarifa imetolewa mapema mtoa hoja ya kubadilisha hoja kabla ya kutoa hoja hiyo, atakmkabidhi, kwa maandishi yenye saini yake na yanayoonyesha mabadiliko anayotaka afanye.

Lakini Spika, anaweza kulegeza sharti hili kama mabadiliko yanayokusudiwa ni madogo au ni ya uhariri.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko yaliyotolewa hapa sio madogo sio ya uhariri, ni kwamba ametoka Azimio jingine jipya kabisa, ningeomba katika hali kama hii mwongozo wako unasemaje.

**MBUNGE FULANI**: Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilisimama kabla hajasimama Mheshimiwa Mudhihiri, ili kuweza kutoa mwongozo. Kwa hiyo, pia ameniomba ni sahihi tu. Nadhani kwanza nalegeza sharti la kuhitaji nipewe kwa maandishi kabla, kulingana na suala lenyewe hili nadhani kambi ya upinzani wanayo haki ya kuweza kuleta masahihisho.

Tatizo masahihisho hayo, kama ilivyo kwa Miswada yote, hoja zote yasiwe makubwa, kiasi cha kuipindisha hoja yenyewe tena, au Azimio au kubomoa kabisa. Kwa hiyo, ningeomba wakati tunaendelea na mjadala kwa sababu ninao wachangiaji kiasi cha 20 basi ufanyike ukarabati, jambo hili ni la Kitaifa, ni letu kwa pamoja jamani, tufikie mwisho vizuri.

Ufanyike ukarabati kwa hoja ya mabadiliko ya Mheshimiwa Khalifa, ili yale yanayosaidia kujenga umoja wetu, yaweze kuongezwa yajadiliwe na tuweze kuyapitisha.

Kwa hiyo tunaendelea, nilikuwa nashauri, kwanza kabla hatujaendelea Mheshimiwa Mbunge mwenye gari *T837AMK,* limewekewa ile tahadhari ya *alarm* na linaendelea kupiga kelele sasa wakati wote, tunamwomba akarekebishe hali hiyo. Inakuwa ni kero huko nje, akafanye utaratibu wa kurekebisha hali hiyo. Gari *T837AMK,* hawakusema ni la aina gani, lakini nadhani mhusika atagundua hilo.

Baada ya hayo naomba sasa tuendelee, ningeomba sio lazima kurudia rudia jamani ili tuweze kuokoa muda na sio lazima wote, ukiona *point* yako imeshasemwa, basi unaweza kutulia. Sasa namwita Mheshimiwa Job Ndugai, marekebisho tutayasubiri kwa wakati wake, kadri mjadala unavyokwenda, kwa sababu tutalipitia Azimio hapo mwisho.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyo mbele, kwanza nianze kwa kuiunga mkono na kumshukuru sana kipekee Mheshimiwa Mudhihir kwa kuleta hoja hii. Kuhusiana na filamu ya Bwana Hubert Sopers, ya *Darwin's Nightmare*. (*Makofi*)

Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo ameilinda nchi yetu dhidi ya mashambulizi yasiyokuwa na nia nzuri. Hasa kuhusiana na masuala ya silaha kwamba zinapitishwa katika nchi yetu, hili limetuuma sote kabisa, jambo ambalo si kweli kabisa.

Lakini la pili msisitizo mkubwa sana kwenye filamu ile kwamba katika nchi yetu karibu watu wote wagonjwa wa UKIMWI, limerudiwa sana hili.

Mheshimiwa Spika, Ziwa Victoria sisi Tanzania tuna nusu ya ziwa lile kwa ujumla wake. Huyu samaki aliyetuletea mgogoro, anayeitwa Sangara, kiingereza wanamwita *Nile Page* alipandikizwa kwenye lile ziwa miaka 60, na mtu mmoja sijawahi kupata jina lake. Nikikumbuka enzi hizo wakati niko chuo, zamani hizo katika wana mazingira ulikuwa ni mjadala mkubwa kuhusiana na suala la huyu samaki, kwamba pamepandikizwa kitu ambacho ni tatizo katika ziwa. Samaki huyu anaongezeka kwa haraka sana, kuzaana kwake ni kukubwa sana. Samaki huyu…

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa. Kwa kuwa jambo linalojadiliwa ni la Kitaifa na la maana sana, nilikuwa nashauri kuwa mikutano ambayo tumeipanga saa tano, iahirishwe mpaka hapo jambo hili litakapomalizika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa John Cheyo, mimi nakubaliana na wewe, naona hatuwezi kuwa tumekutana kwa dharura kwa jambo zito la kitaifa halafu Kamati zote wajumbe wanatoka hatima yake itaonekana kwamba tunalokusudia na vitendo vyetu havilingani hata kidogo. Nakubaliana na wewe nawaomba Wenyeviti waahirishe kidogo ili tulimalize jambo hili, ahsante sana, endelea Mheshimiwa Ndugai.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheahimiwa Spika, nakushukuru sana. Samaki huyu ni mkubwa sana, zaidi ya futi sita na kilo nyingi. Samaki huyu anakula samaki wenzake ndani ya ziwa, anakula mpaka watoto wake mwenyewe huyu samaki. Kiasi kwamba samaki wale ambao ndio wenyeji wa ziwa Victoria kwa kiwango kikubwa wamepungua sana na kuonekana kwao ni kwa tabu sana.

Samaki huyu kwa kiasi kikubwa *echo system* ya ziwa ameivuruga walifikia mahali wamepunguza hata *level* ya *oxygen* ya ziwa Victoria, miaka ile ya 1970, walifikia mahali wakawa wanakufa tu wenyewe kwa wingi unakuta wana-*float* tu, samaki hawa ilikuwa ni tatizo miaka ya 1970 hadi 1980. Ikawa ni mjadala ya kwamba tunafanyaje, ziwa linaharibika, masamaki haya, masangara yameingia yamevuruga ziwa, wamkula samaki wengine huyu samaki kwa neno rahisi ukichukulia kama shamba hivi huyu ni gugu, ni kama una shamba lako la mahindi halafu kuna magugu yameingia kwenye shamba la mahindi, kwenye ziwa lile huyu ni gugu amepandikizwa huyu samaki.

Lakini cha ajabu sasa katika mambo haya yote, huyu gugu huyu, hili gugu limekuja kuwa na soko kubwa sana, hasa nje ya nchi yetu, kitu ambacho kilikuwa ni tatizo lakini sasa hivi ni baraka kubwa sana kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Hata *IUSN* ambao wao ndio *World Conservation Union* wamemworodhesha *Nile Page* katika viumbe 100 ambao ni waharibifu wakubwa wanaosambaa kwa haraka, anafahamika kabisa kwamba ni *ecological disaster* huyu samaki.

Kwa hiyo, hata ikitokea tuseme kwamba haya, kutokana na matatizo haya kwa hiyo sasa Sangara asivunwe, ukiweka *burn* labda miaka 10, utakachoishia ni kuua ziwa Victoria, kwa sababu huyu sangara, pale sio eneo lake amepandikizwa, ni samaki mwenye matatizo kweli kweli katika uhai wa ziwa letu Victoria. Lakini kama nilivyosema bahati nzuri, hilo gugu sasa limepata soko lina bei nzuri kweli kweli kuliko mahindi, katika shamba lako.

Sasa nitashangaa kama mtu analalamikia tena kuuza magugu, samaki huyu ni tatizo, lakini bahati nzuri amepata soko nzuri, huko nje, matokeo yake tutafaidika nini? Tumepata kitu cha kuuza nje tunapata hela za kigeni, ukiangalia idara ya uvuvi ya miaka ya 70 ya Wizara ya Maliasili ya Utalii na Idara ya uvuvi ya leo, Idara ya Uvuvi ya leo ina fedha nyingi sana kiwango kikubwa kutokana na biashara ya huyu samaki.

Tunapata fedha za maendeleo, viwanda vimejengwa, watu wamepata ajira, na kadhalika. Biashara imekua, tumeonyeshwa *flights* pale za ndege kuingia Mwanza na kutoka, biashara za *bar,* biashara ya hoteli, ma-*watch man of course* pamoja na matokeo mengine ya dada zetu na kadhalika. Lakini ni gugu hili kubwa ambalo limeleta na biashara hii ya samaki anayeitwa sangara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kilichonifanya nisimame kuzungumza kwanza ni kuungana mkono na kilicholetwa hapa mbele kupinga sana suala la silaha na kupinga sana suala la UKIMWI kwamba umezagaa. Lengo lilikuwa ni kuua soko la samaki. Ukiua soko la samaki huyu kama nilivyokwisha elezea hulitakii mema Ziwa Victoria

kwa sababu wanaongezeka kwa haraka sana ndani ya miaka 10 yataanza kufa yenyewe tu na ku - *float* kwa kukosa chakula anakula chakula kingi kuliko samaki wenzake, anakula samaki wenzake, anakula mpaka watoto wake kwa kweli ni tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nilitaka kumalizia ili nitoe nafasi kwa wenzangu kwa kusema kwamba kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira na wenzangu tutakwenda kukaa na tutapenda kutembelea Mwanza kabla ya mwezi wa Oktoba, 2006 kuviona viwanda na watueleze namna ambavyo wameweka mipango yao katika suala zima la *disposal mechanism* ya Mapanki. (*Makofi*)

Lakini pia ningependa kupendekeza kwamba wale wote ambao katika filamu ile wameonekana wazi kabisa wakisema kwamba silaha zinateremka au yule mlinzi wetu Bwana Raphael anayesema kwamba anatamani vita ije ili wapate cha kufanya, ningependekeza kwa Serikali watu kama wale tafadhali watafutwe ili wachukuliwe hatua kali kabisa. *(Makofi)*

Lakini la mwisho ni kuhusiana na suala la vibali kwa wageni wanaokuja kufanya kazi kama hizi za *filamu* katika nchi yetu, pawe na ufuatiliaji wa karibu ili kuona kwamba maudhui aliyoyaweka katika kuomba kibali chake ndiyo hayo ambayo anayafanyia kazi. Kinyume na Bwana Sopa huyu ambaye aliomba kufanya *filamu* kwa ajili ya aina ya samaki na mazingira yao katika Ziwa Victoria lakini akaishia kutuletea tatizo kubwa sana la kuipaka matope nchi yetu katika uso wa dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa Waheshimiwa Wabunge maombi yameendelea kumiminika hapa ya kuchangia hoja hii kiasi kwamba hata ile dhana kwamba tumeungana pamoja kwenye hili itapotea kwa sababu si lazima tu kila Mbunge aseme.

Sasa basi, Majina niliyonayo hapa ni 25 ambayo hata kwa dakika 10 tu ni kwamba tutazungumza hadi tuanze tena saa 11 baada ya kuahirisha na mimi lengo langu na kwa ratiba ilivyo nilipenda jambo hili tulimalize saa 7:00 mchana tuwe tumemaliza kwa hiyo nitajaribu kwa mchanganyiko ambao nitatumia hekima tupate maoni mbalimbali halafu nasihi kwamba Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa *Mover* wa *Amendments* aendelee kuwasiliana na mtoa hoja ili kije kitu ambacho hakituweki katika hali tofauti na kwa maana hiyo kabla ya saa 7:00 mchana tuweze kupitisha Azimio ambalo inaelekea kabisa kwamba kwa mwelekeo hata wa mazungumzo kwenye lengo tuko pamoja na Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa nitawatamka watakao changia katika muda mfupi ujao sasa hivi atafuatia Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Jackson Muvangila Makwetta, Mheshimiwa John Momose Cheyo, na baada ya hapo nitamwita Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa.

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kuniita niweze kuchangia katika hoja hii muhimu sana ambayo sasa imekuwa ni mjadala wa kitaifa na ningependa pia nizungumze kwa muda mfupi sana.

Mheshimiwa Spika, wakati sote tumekula kiapo hapa Bungeni, tulikula kiapo cha kuilinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na ningependa ninukuu sehemu ya Katiba Ibara ya 28 Namba (1) ambayo inasema kwamba:

"Kila raia anawajibu wa kulinda, kuhifadhi na kudumisha Uhuru, Mamlaka, Ardhi na Umoja wa Taifa letu".

Mheshimiwa Spika, kwa kunukuu kipengele hicho cha Katiba ambacho sote tuliapa kwa kuilinda hii Katiba napenda niseme kwamba itakuwa ni jambo la ajabu sana kama kuna Mtanzania yeyote atakayetokea ambaye kwa vyovyote vile hatasimama pamoja na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Watanzania wengine katika kuhakikisha kwamba hadhi na sifa ya Taifa letu inalindwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi wengine tulisoma siyo zamani sana lakini nakumbuka tulikuwa na kitabu cha lugha Darasa la III ambacho tulikuwa tunafundishwa imani 10 za Mwana *TANU* inasema kwamba: "Nitasema kweli daima na uongo kwangu mwiko." (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningependa katika mjadala wangu tuelezane tu kuhusiana na masuala mazima ya ukweli na baadaye kuweza kuhakikisha kwamba Azimio linalotoka Bungeni ni Azimio ambalo linalinda Hadhi na Maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kama jinsi ambavyo imeelezwa na Mtoa Hoja na ninampongeza sana kwa kuleta hoja yake hapa na vilevile *Mover* wa *Amendment* na ninampongeza sana kwa kuleta hoja yake hapa.

Vilevile *Mover* wa *Amendment* za hoja ya Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani ni kwamba filamu hii ilitengenezwa toka mwaka 2003 na ilianza kurushwa tarehe 1 Septemba, 2004 na kama jinsi ambavyo ilielezwa kwamba kulikuwa na juhudi kadha wa kadha zilikuwa zinafanyika kuhakikisha kwamba Taifa linatoa kauli kuhusiana na filamu hii.

Ninakumbuka mwanzoni mwa mwaka 2005 Mwandishi wa Habari wa Gazeti la Rai Bwana Johnson Mbwambo aliwahi kuandika makala kuhusiana na filamu hii lakini bahati mbaya ni kwamba hatukuweza kuijadili kwa kina.

Mheshimiwa Spika, Sasa filamu hii ina athari kadhaa na mimi ningependa nijikite katika athari mbili. Athari ya kwanza ni ya suala zima la kuathiri biashara yetu ya minofu ya samaki ambayo kwa sasa hivi imekuwa ni biashara ambayo inaliingizia Taifa fedha nyingi sana.

La pili ambalo nitalizungumzia pia kidogo ni suala zima la Silaha na kwamba nchi yetu inatumika kama ni sehemu ya kupitishia silaya na la tatu la kumalizia nitazungumzia matatizo ambayo kweli ndani ya nchi yapo na ni lazima tuweze kuyaangalia.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa kweli kushukuru sana kwa kuonyesha ni jinsi gani ambavyo sisi kama Wabunge tunakuwa kitu kimoja tunajiunga pamoja kujadili masuala ya kitaifa. Mimi binafsi na pia wenzangu kama ambavyo Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa amesema tulifadhaishwa sana tena sana napenda tu niweke wazi kwa sababu ni suala ambalo tunakosoana ili baadaye yasije yakatokea matatizo.

Mara baada ya filamu ile kuonyeshwa kitendo cha Waziri Mkuu kuwaita Wabunge wa CCM peke yake kukaa na kujadili kwa kweli ni kitu ambacho hakikuwa kizuri, na ninaamini kabisa kwamba Waziri Mkuu ambaye ninamheshimu na kumwanini sana hataweza kurudia, kwa sababu ujumbe mmoja tu ambao ningependa kuwaeleza Wabunge wenzangu ni kwamba sisi tuko wachache lakini sauti yetu inasikika na mawazo yetu wakati mwingine ni mawazo mazuri. Kwa hiyo si kila wakati tupime mambo kutokana na uwingi wa watu, kambi nyingine inaweza ikawa wako wengi wanaweza wakatushinda kwa kura lakini bado sauti yetu Watanzania wataisikia na kuna Watanzania ambao wataendana hiyo sauti yetu. Kwa hiyo nadhani kuanzia sasa tuanze kuweka utamaduni wa kuwa na wajibu wa kushirikiana pale ambapo mambo ya kimsingi yanapokuwa yanatokea.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Maliasili na Utalii amesema katika baadhi ya majibu yake kwa Waandishi wa Habari kwamba filamu hii mpaka sasa haijawa na athari kwa biashara yetu. Haikuwa na athari kwa sababu bado haikuwa *popular* sana tena sana lakini hivi sasa imekuwa ni mjadala mkubwa sana ukifungua kwenye *internet*, magazeti mbalimbali duniani yanajadili mara baada ya kauli ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, *in one way or the other* ni kama tumeianzisha upya na ninaamini kabisa kwamba filamu hii kwa siku chache zijazo inaweza ikapelekea bei ya samaki wetu katika soko la Ulaya ikaanza kupungua na hasa ukizingatia kwamba hatuko peke yetu ambao tuna *export* hawa samaki kwani wapo Wakenya, Waganda na wanaweza wakatumia *opportunity* hii kuhakikisha kwamba wanaiathiri nchi yetu kiuchumi.

Kwa maana hiyo wazo ambalo limetolewa la kuiomba Serikali itengeneze *Counter Documentary film* na kuhakikisha kwamba *Counter Documentary film* hii inasambazwa kwa wingi iwezekanavyo lifanyike haraka ili kuweza kulinda maslahi ya kiuchumi ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili suala la silaha kwa kweli ni kitu cha ajabu sana, mimi hata siku moja na hata ingekuwa ni kweli kama Mtanzania siwezi kukubali kamwe mtu na hasa Mzungu naomba nisisitize hili mtu na hasa mzungu aje aseme kwamba eti nchi yetu inapeleka silaha kwa waasi wa nchi nyingine. Katika hali ya kawaida huyu mtu angekuwa ni Mtanzania *this is a treason case* katika hali ya kawaida, lakini kwa sababu siyo Mtanzania na ndiyo maana inabidi tuanze baadhi ya marekebisho kwa sababu neno kumkaripia tu mtu halitoshi inabidi tuwe na neno gumu zaidi kwa sababu *as a country,* kama nchi tunapolinda maslahi ya nchi yetu nchi ambayo ina majeshi, nchi ambayo

tulimpiga Idd Amin Dada wa Uganda tukamshinda lakini mtu mmoja tukisema tukaripie tu haisaidii na tena haisaidii ndiyo maana watakapokwenda kufanya *amendment* wajaribu kuhakikisha kwamba wanaweka maneno ambayo ni *very strong* kuhakikisha kwamba hatua muafaka za kisheria zinachukuliwa dhidi ya mtu yeyote ambaye anataka kuchafua sifa nzuri ya nchi yetu ya kuleta amani katika eneo la Maziwa Makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ni suala hili la uwezo wa Serikali yetu kulinda hadhi ya nchi yetu. Jana mara baada ya mjadala huu kuwa mkali kidogo nilijaribu kwenda kuangalia kwenye *internet* kwenda kuona watu wengine wanasema nini kuhusu hi filamu, nikapata barua ya kutoka *The World Conservation Union* ambao walimwandikia huyu Bwana H. Sopa tarehe 8 Desemba, 2005 kuelezea ni jinsi gani ambavyo filamu yake imechukua *negative sights alone.* Yaani imechukua tu *negatives* imeacha *positives* na wala haina *balance.*

Barua hii kwa kweli ningependa kuiwasilisha mezani kama sehemu ya *reference* kwani ni barua ambayo ni muhimu sana kwa sababu hoja nyingi ambazo Mheshimiwa Rais alizungumzia pia katika barua hii ya *World Conservation Union* walizizungumzia. *(Makofi)*

Vilevile tulipata *document* kutoka *Colombia University* ambao nao pia walikuwa wanafanya *criticism* ya filamu ya *Darwin's Night Mare* toka mwaka jana lakini sisi tulichelewa na wala siyo kipindi cha kuanza kulaumiana ni kipindi cha kuanza kuelimishana kwamba inapofikia maslahi ya Taifa na tupo kwenye mtego tuwe mstari wa mbele sana kulinda, tusisubiri na ni mbaya zaidi kusubiri mpaka Rais aseme kwa sababu hiki kitu kilikuwa kinafahamika hakuna mtu aliyekuwa anaizungumzia mpaka baada ya Rais kuongea ndiyo imekuwa ni *hot case* kila mtu anaizungumzia. Rais ana mambo mengi sana ya kushughulikia katika nchi hii, ana Mawaziri 30, Mawaziri wanasubiri Rais aseme ndiyo wenyewe waanze ku – *act,* Wabunge wanasubiri pia Rais aseme ndiyo na wenyewe waanze ku - act. Mkoa wa Mwanza una Majimbo takriban 12, Wabunge wa Mwanza wa mwaka jana na mwaka huu walikuwa kimya wanasubiri Rais aseme, hii hali ni lazima ibadilike nchi haiwezi kuongozwa na mtu mmoja na ninaomba hili Mawaziri mliangalie.

Kila wakati utasikia Rais kasema hiki Mawaziri mnafuata nyuma wakati mwingine mpaka wengine muitwe, naomba mbadilike, mnapokuja kutetea maslahi ya nchi yetu muwe mstari wa mbele mhakikishe kwamba mnailinda nchi yetu kwa hali yoyote ile.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto ni lazima tujali Kanuni za Mjadala unachokisema si sahihi hakuna anayesubiri Rais afanye kitu chochote. Rais anaweza kuwa na habari ambazo Mbunge wa kawaida huna. Kwa hiyo, kuchelewa kwa sisi wengine Wabunge kusema chochote juu ya kitu haitokani na kutokuwa wazalendo au kutokujua, wengine hapa filamu ndiyo juzi wameiona, maudhui ndiyo wameyaona. Kwa hiyo, ningeomba ufute usemi wako huo wa kusema kila kitu Wabunge na Mawaziri wanasubiri Rais aseme. Nchi haiendi hivyo. (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Taarifa ya nyongeza.

**SPIKA:** Taarifa ya nyongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Taariaf ya nyongeza.

Kwa heshima zote kwa Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, kama ungetazama vizuri zaidi mwezi wa Nane mwaka jana, 2005 kwenye *internet* yapo majibu ya *Cinema* hiyo ikijibiwa na Ubalozi wetu kule Ufaransa. Kwa hiyo, tulijibu wakati huo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Zitto kwa tahadhari hiyo.

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maelezo yako na pia maelezo ya Waziri Mkuu. Naomba tu nisisitize kwamba sikusema kwa nia mbaya kwamba tunasubiri mpaka Rais aseme lakini nilisema katika hali ya tahadhari.

Tafadhali nalindwa na Katiba. Nilisema katika hali ya kuhakikisha kwamba tunakuwa mstari wa mbele sote kwa pamoja bila kusubiri viongozi wetu wa juu na ninafahamu kwamba Ubalozi wetu mwaka jana ulijibu filamu hiyo nafahamu. Lakini majibu kama jinsi ambavyo filamu ilikuwa haifahamiki hata majibu pia yalikuwa hayafahamiki, kwa hiyo ni katika kushauriana tu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ni hili suala la matatizo ambayo yameelezwa katika …

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika!

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, umeelekeza kwamba Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, afute usemi wake na mpaka sasa sijasikia kama amefuta bali amezungukazunguka tu. Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge hatujasikia kama akifuta au hafuti usemi wake.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Nashukuru umenikumbusha na mimi nilighafilika kidogo ni muhimu kwa mjadala huu kama wowote ndani ya Bunge tufuate kweli Mwongozo wa Spika, niliyaona maneno hayo ya kusema kuwa: "Kila kitu tunamsubiri Rais ndiyo wengine wanafuata." Hilo ndilo ambalo ulilitamka lifutwe ili tuendelee kwa amani.

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nilifuta labda tu Mheshimiwa Job Ndugai hakuweza kuelewa lugha niliyoitumia.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kusema kwamba si kweli kwamba kwa kila kitu mpaka Rais afanye ndiyo wengine wanafuata ingawa *trend* imeonekana kwamba ni kwa mambo mengi. Kwa hiyo, ningependa kuchukua ushauri wako wa kufuta hilo eneo.

Mheshimiwa Spika, naomba tu nichukue tu dakika mbili ….

**MHE. KABUZI FAUSTINE RWILOMBA:** Mwongozo wa Spika!
**SPIKA:** Mwongozo wa Spika kuhusu hilohilo?

**MHE. KABUZI FAUSTINE RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

Mheshimiwa Spika, mimi natoka Mkoa wa Mwanza na si lazima nione kila filamu kwa jinsi alivyozungumza kwa wananchi wangu wa Mwanza wanaona kwamba mimi sifuatilii hata vitu ambavyo wakati mwingine ni kuletewa.

Naomba azungumze wazi kwamba kwa Wabunge wa Mwanza hawaangalii kila kitu naomba afute usemi wake. (*Makofi*)
**SPIKA:** Sasa mimi nadhani ili mradi Mheshimiwa Kabwe Zitto amefuta sehemu ile iliyokuwa inawagusa basi tumwachie ili amalize hoja yake vizuri. (*Makofi*)

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie tu kwa kusema kwamba naomba niiombe Serikali ihakikishe kwamba baadhi ya matatizo ambayo wageni wanayatumia kuielezea nchi yetu yaweze kutatuliwa ili kuweza kuondoa aibu ya nchi yetu.

Kwa mfano ni kweli kabisa kwamba suala la umaskini katika nchi yetu lipo si kweli kwamba Watanzania wanakula mapanki yaliyooza hilo siyo kweli lakini Watanzania wanakula mapanki hili ni jambo ambalo lipo kwa sababu yale mapanki ni chakula yakitengenezwa vizuri yanaweza kuwa chakula cha mifugo. Lakini cha msingi hapa ni tuhakikishe kwamba yale mazingira ambayo yaliyopo katika mchakato yaani ile *process* ya utengenezaji wa samaki yaweze kuangaliwa.

Pili, tatizo la watoto wa mitaani limezungumziwa sana na Wabunge wameuliza maswali mengi sana. Mawaziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, wamejibu maswali ya watoto wa mitaani kwa hiyo pia filamu hii itufumbue macho tuweze kuangalia ni jinsi gani ya kuweza kutatua haya matatizo ambayo nchi yetu inayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na kufuatia marekebisho ambayo Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa ameyapendekeza, pamoja na kazi ambayo Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa na Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir walikwenda kuifanya nitaunga mkono hoja ya kuhakikisha kwamba tunalinda hadhi na sifa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON MUVANGILA MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Nimesimama hapa kwanza kabisa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuliweka suala hili hadharani kwa sababu sisi wengine hatukuwa tumejua hili licha ya ukweli kwamba filamu ilishatolewa siku nyingi.

La pili kumpongeza Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir kwa kuleta hoja hii mbele yetu ili tuweze kuchangia mawazo yetu na mimi naunga mkono kwamba haya ndiyo yawe maazimio yetu.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa busara yako umeamua kwamba yale mawazo ya wenzetu wa upande mwingine tunaweza tukayachukua na kutazama wapi yanaweza ku-*fit* katika lile azimio kwa ujumla ili tuonekane tu wamoja maana nchi hii ni yetu wote kwa pamoja. Baada ya kusema hivyo mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa hiyo ningependa kusema kwamba katika mazingira haya ya utandawazi na uchumi wa soko ni rahisi maadui sasa kupenya au ku – *penetrate* katika nchi yetu kuliko ilivyokuwa kabla. Kwa hiyo, malipo ya uhuru wetu ni kujitahadhari wakati wote na huu ndiyo upande mbaya wa upande wa soko na utandawazi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa filamu hii mimi kama ulivyosema ningependa kufupisha mambo kwa kusema kwamba tumejifunza nini katika filamu hii. Huyu mwandishi au aliyetoa filamu hii inasemekana ni miongoni mwa wale ambao wanapiga vita madhara ya *globalization* na katika barua yake ile kama mkifuatilia anasema eti hakuwa na nia mbaya lakini alitaka atume hii kuelezea walimwengu waone huruma kwa sisi masikini.

Mheshimiwa Spika, hawa mamluki wa aina hiii katika dunia wanamadhara makubwa sana, wenye mwelekeo wa kutafuta fedha hasa wapiga picha kama unapatwa na ajali unakaribia kufa hatahangaika kukuchukua akupeleke hospitali atahangaika kukupiga picha aone unavyokufa ile dakika ya mwisho ili ile picha yake ipate soko kwamba yeye alikuwa ndiye pekee aliyeona unakufa. Kwa hiyo, haya ndiyo madhara ya mtu ambaye akili yake ni *money* imeelekezwa katika kutafuta fedha bila ubinadamu ndani yake.

Sasa mimi hapa nimejifunza mambo machache kwamba moja itabidi lazima tuangalie suala la ulinzi, ulinzi wa sasa si kuangalia maadui wa kiwiliwili tu kuongeza akili na kutazama na kuwa na mashaka na *everybody* vinginevyo hili tunashukuru kwamba limetokea kwa upande fulani kwamba kwa kuwa hatukufa tunashukuru kwamba limetokea kwamba sasa huenda yapo mengi ya aina hii ambayo hayaonekani na katika mazingira yetu hawa mamluki na watu masikini ni rahisi kununuliwa na kuwa vibaraka wa maadui zetu.

Nilidhani kwa kweli hili liwe ni somo la kuzidi kuimarisha ulinzi na maeneo haya mengine ya udhaifu kwa sababu kwa mfano katika ile filamu unamkuta hata Mkuu wa Mkoa alipigwa picha bila kujijua. Wale wengine walikuwa *condition* tu sasa kuna mapendekezo haya kwamba tufanye *counter film* huenda katika saikolojia ikawa ni

*endless exercise* mimi nadhani wenzetu mtatafakari kama Serikali na Rais amesema aachie vyombo vya Ulinzi na Usalama tuishie hapo.

Lakini tukisema kwamba na sisi tukapige nadhani Serikali itatumia busara yake kutazama ni namna gani inaweza ku – *react* ili kulifanya jambo hili liende chini zaidi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasoma kitabu kimoja kimeandikwa na Mwamerika mmoja kinasema *how to live with shacks without being eaten* kwa Kiswahili labda ningesema namna ya kuishi na papa ndani ya Bahari huku ukiepuka usimezwe. Hii ndiyo dunia tuliyonayo sasa maana papa wapo na sisi tunaishi bahari ileile na unawezaje kuogelea ndani ya Bahari ile usimezwe na nyangumi, ndiyo mikakati unayotakiwa kuishi.

Hawa wanakuja kwa jina la misaada, kwa jina la kutusaidia na kwa sababu hizo ndiyo wanatumia nafasi ya udhaifu wetu na umaskini wetu kufanya maovu ya aina hii.

Ameshatuchafua na kututangaza kote duniani nadhani mnajua aliingia kwenye mashindano fulani ya wapiga filamu na bahati nzuri alikuwa wa mwisho. Lakini aliruhusiwa kuingia kwenye mashindano akawa wa mwisho huyu katika mashindano hayo lakini madhara amekwisha fanya na kwa miaka hii mitatu ambayo sisi wengine hatukuwa na habari madhara yalikuwa ni makubwa zaidi.

Hivi ukinyolewa nywele halafu zikasambazwa nchi nzima wakazitafuta wazirudishe waziweke kichwani nadhani inakuwa ni kazi ngumu lakini unajaribu kukarabati hali yetu na *image* yetu kusudi iwe nzuri zaidi.

Ninachopendekeza hapa njia za kurekebisha tatizo hili tutumie busara zaidi na akili zaidi kuliko tukafanye tu kwa ghaflaghafla tupige picha nyingine tena sasa hiyo inawezekana isisomwe na haohao ambao wanatutakia mabaya.

Sasa hivi ni lazima tuwe wazi kwamba wenzetu hawa wakubwa na hasa wa hii dunia ya kwanza hawatupendi, kuna *blanket* na ukuta kati yao na sisi ingawa hawasemi waziwazi. Wakikuona wewe kidogo unazungumza lugha ya kingereza na unachangamka na hujambo la kiuchumi wanasema wewe ni tofauti na hao wengine yaani *you are different you don't look like them*. Wanasema wewe ni Mwafrika siyo mtu mweuzi ni *highbred* wewe haiwezekani mtu mweusi awe na akili kama ya kwako. *(Makofi)*

Kwa hivi vitendo vinafanywa ukitazama kwenye filamu zote za ulaya hali, dalili na mwelekeo ni kumdhalilisha mtu mweusi na hii yote unakuta hata wanavyochagua zile picha za filamu ya juzi wanachagua wale wanyonge na hali ile hawawezi kutafuta mtu aliyepiga suti, *smart* na anaweza kusimama vizuri, hawezi kwa sababu *mission* ni kuonyesha sisi ni nusu binadamu na si binadamu tunaishi tu kwa sababu tunaishi.

Kuna wakati mimi nilikuwa nafikiria vibaya nikafikiria kwamba hata huu UKIMWI kama ungegunduliwa dawa na wakubwa huenda wangezima tu kusudi hii *pigment* ya watu weusi itoweke.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo, katika hili mimi nilikuwa nakwenda kwenye Azimio kwamba kwa kuwa sasa tumekutana pamoja hapa tusipuuze yale mambo ambayo yanatutenganisha tugange yajayo inawezekana hapa na hapa tulighafilika lakini sasa nia ni nzuri kwamba tumelenga tujadili jambo ambalo linatuhusu wote na kama kuna kasoro ya hapa na hapa turekebishe lakini tuwe kitu kimoja. Kuendeleza mjadala wa tofauti na kwa nini ulifanya hivi kwa kweli haisaidii.

Hivi Ndugu yako akipata ugonjwa wa UKIMWI unapokwenda kumwangalia utaseme kwa nini ulitembea na wanawake Malaya wakati anakaribia kufa kwa kweli haisaidii kwa sasa ni kutazama tatizo hili na kuzuia lisitokee tena kwa namna gani huu ni wajibu wa kila mmoja, *good ideas are not a monopoly* ya CCM peke yake.

Mawazo mazuri yatatoka Upinzani, pande zote, yatatoka kwa vijana na hata wazee lakini hili la kufanya tufanye pamoja itatokea tu kama kuna *mutual respects*.

Kwa hiyo, *to compromise on principle is to betray the principle* hapa tumeungana kutetea nchi yetu kwa pamoja kwa hiyo nilikuwa napendekeza kwamba lile Azimio ambalo limetolewa kwa pamoja tuliunge mkono kama kuna urahisi wa hapa na pale kuliboresha halafu kwa pamoja tujenge nchi yetu, twende pamoja tushirikiane kujenga Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja hii muhimu wa Taifa letu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa nitamwita Mheshimiwa John Momose Cheyo atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nyawazwa. Waheshimiwa Wabunge naomba tupunguze usemaji kwa kweli kama nilivyosema lengo ni kwamba tu pamoja na ndiyo maana Mtoa hoja kutoka chama tawala na aliyependekeza mabadiliko kutoka Kambi ya Upinzani sasa hivi wako pamoja wanafanya kazi. Sasa hakuna haja tena ya mjadala mrefu nakusudia kufunga mjadala saa 6.30 ili tulipitie sasa Azimio. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nitajitahidi kutokuchukua dakika zote ambazo ni haki yangu.

Mheshimiwa Spika, lakini kwanza kabisa nashindwa kujizuia kusema kwamba leo ni mojawapo ya siku nyingi ambazo nimeona ni kwa nini tunahitaji Spika kama wewe. Leo umeonyesha busara kabisa na hekima ambapo kwamba kwa mambo ambayo ni ya Kitaifa uwingi usiwe ndiyo unatawala lakini upendo na uzalengo wa nchi yetu ndiyo uwe msingi wa kuweza kutoa maamuzi. Nakupongeza sana kwa maamuzi yako kwamba haya maazimio yote mawili yawekwe pamoja ili tupate jambo ambalo kweli ni la kitaifa. Kwa kweli pongezi nyingi sana. *(Makofi)*

La pili nataka kusema kwamba haiwezekani Mtanzania yeyote akakubali kutukanwa na mzungu kwa sababu yoyote ile. Tunaweza tukawa na udhaifu wa Serikali lakini anayetutukana anapaswa kupigwa. Tunaweza tukawa kweli maandalizi yetu ya mapanki siyo mazuri, lakini hiyo ukija na ukayaona na ukayatumia yale kunitukana mimi, mimi nikikasirika na mimi nitakupiga. *(Makofi)*

Alichofanya Mheshimiwa Rais ni jambo la kawaida kabisa la kibinadamu. Ukimtukana mtu, hatafurahi na yule uliyemtukana akicheka sio binadamu wa kawaida. Anayetusimamia katika nchi hii sisi ni Mheshimiwa Rais wa Tanzania, ameona nchi inatukanwa. Kama yeye ndiye Rais wa Tanzania alifanya vyema kabisa kusimama aidha hata kama kuna matatizo ya mapanki kana kwamba watu wenyewe hali ni chafu, kuna ukahaba na kama kuna lingine lolote ambalo hatujalifanya sawasawa.

Mheshimiwa Spika, lakini Rais alichofanya, kukasirika na kuonyesha hasira yake na kutoa maneno ya kuweza kumkashifu huyo bwana kwamba hafai, jambo hili ni la kibinadamu kabisa na anapaswa kuungwa mkono na kila mmoja wetu ambaye ni Mtanzania na anapenda nchi. Kwa hiyo, mimi namuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa alichokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kuna mengi ambayo baada ya kuwasikia wengi wameyasemea, sitaki kuyarudia, basi na Serikali na yenyewe iamke. Baadhi ya mambo ambayo mimi ningependa yangefuatiliwa la kwanza kabisa hebu sasa Serikali tangu leo ifuatilie mlolongo mzima wa namna samaki wanavyotengenezwa ili tusiwe katika mahali ambako kama huyo samaki ambaye kichwa chake ndiyo kinabaki na watu wanasema kuwa ni mapanki, kile kichwa ni kitamu kama ukiweza kukitayarisha vizuri na mkia wake ule ni mtamu kama ukiweza kuutayarisha vizuri na sio hivyo tu. Tujue kwamba watu wengi kusema kweli hawana mboga.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sisi Wakusuma kwamba tuna ng'ombe wengi, lakini hatuwachinji wale ng'ombe, tunaolea ng'ombe, lakini hatuwachinji ng'ombe kwa sababu hatuna mboga. Pamoja na kwamba tuna mbuzi, tunangoja mgeni aje ndiyo tuchinje Mbuzi, pamoja na kwamba tuna kuku, tunagojea mtu labda aje kushinda pale nyumbani ndiyo tunachinja.

Kwa hiyo, kuna tatizo kwamba hakuna mboga ya kutosha. Kwa kuwa hakuna mboga ya kutosha, mimi nina hakika sangara badala ya kuondolewa ule mnofu ambao unapelekwa Ulaya, akiandaliwa vizuri, katika mazingira mazuri anaweza kabisa akatumika kama mboga ya watu ambao wanataka kula samaki huyo na inafanyika. Kitu kilichopo sasa ni kwamba, Serikali yetu imelala juu ya kuangalia usafi wa mazingira na matayarisho ya huyo samaki. Hili ndio tatizo.

Kwa hiyo, wito wangu, tuamke. Yale ambayo tunaona yanaweza kutusaidia kuweza kusafisha, tuyasafishe, lakini hatuwezi kukubali mtu kutumia udhaifu huo kututukana. Huyo ametutukana, tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais na yeye tumtukane na kama angekuwa hapa karibu na mimi ningempiga ngumi kidogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi sitaki kuchukua muda mrefu, mengi yamezungumzwa, Serikali imesikia na ushauri wao umepokelewa vizuri. Ombi langu tu, tukae pamoja kwa mambo ya Kitaifa na tutengeneze Azimio ambalo ni zuri kwa sisi wote.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa John Cheyo, ahsante sana. Sasa tunajifunza kwamba hata Mheshimiwa John Cheyo anaweza kuonja mapanki yakiwa yameandaliwa vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja iliyoko mbele yetu nzito.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu aliyekaa Mwanza kwa wiki nzima na kulikemea jambo hili zito la kuidhalilisha Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naungana na wananchi wa Mwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais na kumuunga mkono na hatimaye na sisi Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mwanza tuungane naye kwa kutoa tamko la kulaani kitendo cha kutengeneza filamu ya kuidhalilisha Tanzania kwa kupitia Mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaungana na hoja iliyoletwa mbele yetu kwa sababu amewatumia wanawake na watoto ambao ni Taifa kubwa linalotegemewa na Watanzania sana katika maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alijaribu kuchukua wanawake wanne, ambapo hapa Tanzania tuko wanawake wengi sana tunajishughulisha na mambo yetu ya maendeleo ya kusomesha watoto wetu, tunaanzisha *SACCOS*, tunalima, tunaendeleza miradi yetu sisi wenyewe kwa kujitegemea. Amechukua picha kwa watoto. Mimi nilitegemea kwamba, kama kweli alikuwa anataka kuielezea vizuri Tanzania asingewachukua watoto ambao ni wa Mitaani ambao hata nchi za jirani zina watoto wa Mitaani.

Mheshimiwa Spika, lakini kama angetaka kuwasaidia hawa watoto, nilitegemea angejaribu basi kuona maendeleo yetu sisi Watanzania katika kuimarisha Shule za Msingi ili watoto wetu wasome, lakini hakuweza kwenda kwenye maeneo ya shule nzuri ambazo zimejengwa Tanzania nzima kwa kutumia mradi wa *MMEM* ili kuonyesha kwamba sisi tuna juhudi ya kuwasomesha hawa watoto, lakini yeye aliona tu kulenga katika kuchukua watoto hao kwamba wana dhiki sana Tanzania.

Mheshimiwa Spika, amelichukulia suala la ukahaba, amewachukua wale wanawake wanne kwa kuwadanganya danganya na kufundisha Kiingereza. Wale wanawake wanne wa nchi hii: Je, ukabaha ni Tanzania tu? Mbona hata huko Ulaya ni biashara ya watu. Kwa nini sasa inafikia hapa Tanzania amewachukulia hawa wanawake wanne kuidhalilisha Tanzania ili kutupunguzia soko la kuuza minofu yetu ya samaki

huko nchi za nje kwa kutumia wanawake wanne kwa ajili ya ukabaha. Ukabaha uko katika Jiji la Mwanza tu! Ukahaba uko Tanzania tu!

Mheshimiwa Spika, mbona ukahaba uko Ufaransa, uko Denmark, uko Canada, kwa nini aichukulie Tanzania tu ndiyo hao wanawake wanne wanaowakilisha wanawake wa Tanzania? Nalaani sana. Mimi kama Mbunge wa Mkoa wa Mwanza, hao wanawake ambao walichukuliwa kwa kulipwa fedha kidogo, nawalaani sana na wasitumie tena Mkoa wa Mwanza kupigwa picha za aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba basi, kwa sababu nilikuwa na uchungu sana wa kulaani vitu hivyo kwa kutumia wanawake, wanawake wa Mkoa wa Mwanza tulishazungumza kwamba sisi hatuchagui kazi, tunavua samaki, tunalima, tuna biashara zetu, tunaendesha miradi yetu vizuri. Kwa hiyo, naomba watu wa aina hiyo wanaokuja katika nchi yetu katika kutafuta biashara zao za kudhalilisha nchi yetu wasitutumie sisi wanawake wa Tanzania. Niwaombe sasa wanawake wa Tanzania tuwe macho na watu wa aina hii. Wanakuja tu ili wachukue picha zao waweze kuuza kule kwenye nchi zao na kutuharibia sisi sifa zetu Watanzania.

Mheshimiwa Spika, wanawake wa Tanzania ndio wahimili wakuu katika maendeleo ya nchi hii. Ninaomba sasa tusitumiwe wanawake kupitia Bunge lako Tukufu, tuungane wanawake wote kulisemea hili, kila mwanamke alipo kulaani kitendo cha sisi wanawake kutumiwa katika kudhalilishwa kiasi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kwa sababu sitaki kusema sana, niiombe Serikali kwamba, hili lisije likatokea tena, iwe macho sana na watu wa namna hii. Vibali hivyo tunavyovitoa tuangalie ni watu gani wanaokuja nchini kwetu, wana nia gani na nchi yetu. Hili la kuja kupiga picha vitu vya namna hiyo lidhibitiwe.

Mheshimiwa Spika, ninaomba basi vyombo vyetu vya Tanzania kama ninavyojua ni Watanzania halisi, tusaidiane tuungane pamoja, vyombo vyetu vya Tanzania kulaani huyo aliyetoa filamu, tumlaani wote tushirikiane na kama hao Waandishi wa Habari walione hili ni letu na ni la Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo machache, basi niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir kuleta hili jambo zito na sisi hatukubali na hatutakubali.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nataka niungane na wenzangu kwanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kututanabahisha kama wenzangu wengine walivyoeleza. Wengi wetu tulikuwa hatujaiona hiyo filamu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, tumeiona na nataka niseme kwamba kwa kweli imetudhalilisha sana Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka niunge mkono hoja na ninataka nimshukuru sana ndugu pale Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir kwa kuileta hoja hii ndani ya Bunge letu hili.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mengi ambayo nilitaka kuongea wenzangu wameshayazungumza, mimi nitasema machache tu ambayo yamesalia.

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nieleze kwamba filamu hii imewatumia watoto. Kwa kweli watoto hawa ni *innocent* na walikuwa hawaelewi hasa kitakachofuata. Nataka Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote tupige vita hatua hii ya kuwatumia watoto ambao kwa kweli ni *innocent. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka niungane na Mbunge mwenzangu aliyemaliza kuzungumza sasa hivi, kuelezea akina mama waliotumiwa katika filamu hiyo. Kwa kweli amewadhalilisha sana akinamama na ninataka akinamama wa Tanzania waungane mkono na Mheshimiwa Rais kupiga vita filamu hii. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, kama mimi ni Mtanzania na nina uzalendo, kwa kweli filamu hii imenisikitisha na imenisononesha. Kwanza, ninaamini kwamba, kuna baadhi ya Watanzania ambao hawaitakii mema nchi hii, wamempa msaada wa kutosha huyo Mzungu kutengeneza filamu hii.

Mheshimiwa Spika, ninataka niwaombe wenzangu wenye dhamana kwamba watu hawa watafutwe ili tuweze kuelewa ukweli wao ni nini hasa nia ya kutengeneza filamu hii. Hao Watanzania wenzetu waliomo ndani ya filamu hii. Naomba sana tuwatafute ili watupe ukweli hasa na ikidhihirika, sheria ichukue mkondo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nieleze kwamba, ukahaba sio sifa ya Watanzania. Watanzania hawana sifa ya ukahaba. Sisi tuliotembea katika dunia hii tunazijua nchi zenye sifa ya ukahaba.

Mheshimiwa Spika, tunaelewa kuna baadhi ya nchi makahaba wamepewa leseni, wamekuwa *registered.* M tanzania gani aliyepewa leseni katika suala hili? Kwa hiyo, hili ni kutudhalilisha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nieleze kwamba, mtu huyo basi aitwe, aeleze hasa wapi alipoona kwamba hii biashara ya ukahaba kama ni sifa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la silaha. Tanzania ni nchi ya amani sana. Sisi ndiyo tunaoonesha mfano nchi majirani kuwaweka pamoja wasikilizane. Tanzania haiwezi kusafirisha silaha kupeleka katika nchi za jirani. Hiki ni kitu kimetungwa na kimepangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni dhahiri kwamba hao waliotengeneza filamu hii wameitengeneza kwa nia ya kutaka kuifuja nchi yetu. Nataka tupige vita sana hatua hii ya kutengeneza filamu hii.

Mheshimiwa Spika, nataka nimalizie kwa kusema kwamba, tumeiona filamu hii na hatua ya kwanza ambayo wenzetu waliyochukua ni kutualika Waheshimiwa Wabunge wote kuangalia ile filamu. Tumeitazama siku ya Jumapili na wengi wetu ilitusononesha. Nadhani haikuwa kosa. Nataka niseme hivyo, haikuwa kosa kwa Chama cha Mapinduzi kuwaita Waheshimiwa Wabunge wake na kulizungumza suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ndani ya Bunge kuna *caucus* za Vyama, kwa hiyo, isionekane kama ni kosa kwa kutokuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge kwa hatua hii. Hapa sasa ndiyo Waheshimiwa Wabunge wote tumeshirikishwa. Mimi ninadhani wenzetu wangeliona hili kwamba Chama cha Mapinduzi kimeona hatua hii sasa isiwe ni kosa. Hapa ndipo Waheshimiwa Wabunge wote wanapaswa kushirikishwa na tayari tumeshashirikishwa na tumeanza kushiriki sote kwa kuangalia hiyo filamu, tumeshirikishwa kwa pamoja sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nieleze kwamba, la msingi ni hili la kwamba, sote tulaani hii filamu na sote sasa hivi tunatengeneza hoja ya pamoja ili kulaani hii filamu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa ajili ya kuendelea mbele kwa umoja, napenda tu kwa baadaye hata kunapokuwa na Kikao cha Chama cha Mapinduzi wanakutana kwenye jambo la Kitaifa, hiyo iwe ni njia ya kukutana tena wote kabla hata hatujaingia humu Bungeni baadaye. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru pia kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nami naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete kulaani vikali kitendo kilichofanywa na mtengeneza filamu huyo ambaye kwa kweli ameidhalilisha nchi yetu, ametuharibia sifa ambayo ilikuwepo kwenye Mataifa ya nje, wanapata taswira tofauti tuliyokuwa nayo sisi. Kwa kweli kitendo hiki mimi mwenyewe binafsi nakipiga vita na nimekilaani vikali na kwa sababu mengi yamezungumzwa na wenzangu nisingependa kuyarudia.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu ambayo kwa sehemu nyingine ni ya simanzi na masikitiko makubwa kwa watu wa Mwanza.

Mheshimiwa Spika, napenda nikiri, nadhani na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba filamu hii kwetu kama ni Mkoani Mwanza au kwenye eneo langu ilikuwa haijaonyeshwa. Naamini na kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu ilikuwa ni hivyo. Tulikuwa tunasikia tu, lakini tulisikia tu ni kitu kimekwisha.

Mheshimiwa Spika, sio kwamba tulikuwa tumekaa. Nimeiona juzi ambapo tumeshirikishwa wote na wenzetu wa Kambi ya Upinzani, nafikiri waliruhusiwa kuingia sidhani kama walizuiliwa. Hata Mikutano ya Chama, hiyo ni ya Chama. Lakini walishirikishwa Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani na sisi wote Waheshimiwa Wabunge wa CCM tukaenda kuiangalia hiyo filamu. Nadhani Mheshimiwa Waziri Mkuu alitumia hekima na busara akatuambia nadhani tutaijadili baadaye. Sasa leo tunaijadili.

Mheshimiwa Spika, mimi sioni tatizo kwamba wenzetu hawakushirikishwa na ninaomba ndugu Kabwe Zitto asifikiri Waheshimiwa Wabunge wa Mwanza, tumelala, tuko macho. Tulipoiona ile filamu juzi tulianza kuumia kuliko mtu yeyote. Mimi ni msanii kwa kiwango mpaka cha Chuo Kikuu, nimesomea mambo ya *film production.* Nimefanya *analysis* ya filamu ile. Ile filamu nilikuwa najaribu kuiangalia kama iko *balanced.* Ile filamu haikuwa *balanced* na haiku-*depict*, kuonyesha picha ya Mwanza, ilikwenda kutafuta maovu na ikaongezea maovu zaidi ndiyo yaonekane.

Mheshimiwa Spika, ni masikitiko makubwa kwa watu wa Mwanza kuonyesha kwamba watu wa Mwanza, kama alitaka kuonyesha Mwanza, haiwezi kuonyesha walevi tu, kwamba Mkoa mzima wa Mwanza ni walevi, ndiyo aliona kwamba achukue. Hawezi kuonyesha kwamba vijana au watoto wa Mkoa wa Mwanza wote ni wavuta bangi na wavuta petroli, sio hivyo Mwanza. Hata kwenye mapanki yale aliyoonyesha ame-*portray* picha tofauti.

Mheshimiwa Spika, mimi nawaambia mkifuatilia zile nguo zilizokuwa zimevaliwa na wale wauza mapanki, siyo zile za watu halisi katika utendaji. Hapakuwa na uhalisi wowote ule. Kama angetaka kuonyesha watu wa Mwanza, jinsi samaki zinavyopatikana, angeweza kuonyesha hata Soko Kuu la Mwanza samaki wanaouzwa pale, angeweza kuonyesha Kamanga, kama alitaka kuonyesha angeweza kuonyesha maeneo ya wavuvi ambao ni wavuvi kweli. Pale ni kwamba, ame-*model* majengo ambayo sio kweli kwa wavuvi. Angekwenda Mwalo wa Bukondo**,** angekwenda Mwalo wa Kagehe, Mwalo wa Nkome aone jinsi walivyo wasafi na jinsi wanavyojiongoza na wanavyosimamiana kutengeneza vyoo.

Mheshimiwa Spika, hicho alichokileta, kwa kweli mimi natoka Mwanza, nimekulia Mwanza, nimesomea Mwanza na nimefanya kazi Mwanza, ameleta picha ambayo nadhani hata kama anasema anataka kuwatafutia msaada, hakuna msaada wowote. Nani atakupa msaada wakati huna uwezo wa kufikiria? Nani atapewa msaada pale! Pale hakuna mtu wa kupewa fedha akazitumia vizuri! Alitaka kueleza kwamba Serikali ya Tanzania haiwaangalii watu wa Mwanza. Mimi nasema kwa kweli hii filamu laiti ingeonwa na watu wa Mwanza, nadhani Wazungu wale wangeanza kupigwa kwa sababu ya matendo waliyowafanyia watu wa Mwanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la silaha mimi kwangu naona mpaka sasa hivi sidhiriki ya yule kijana aliyekuwa anasema kwamba silaha zinaingilia hapa. Kwanza, ni tatizo. Amejenga picha kwa nchi jirani kutaka kutugonganisha, watushambulie, wakipata

matatizo waone Tanzania ndio inayowaletea matatizo. Kwa nini silaha hizo ziteremkie Mwanza? Mimi Mwanza naamini kuna *control,* wakifika ni mwendo mrefu kama ni kupitisha silaha. Ina maana Askari wote hawafanyi kazi? Huu ni udhalilishaji mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba, Serikali kama walivyoshauri wenzangu, itayarishe *count film* na mimi niko tayari kujitolea muda wangu tutengeneza *count film* ya kueleza Mwanza ikoje? Sisemi Mwanza ni matajiri wa kila kitu, lakini kuna mambo mazuri ya Mwanza, kuna Bugando, kuna Mji, kuna wavuvi wanaohitaji msaada wa Serikali. Wavuvi walioonyeshwa wale huwezi kuwapelekea fedha, ni wale wauza mapanki pale. Kuna mapanki yanauzwa, lakini ni sehemu ya minofu inayobakia na sisi tunaokula samaki, kichwa ndicho kitamu na ndicho huwa kinaliwa na mwanaume. Wenzetu wanachukua mkia. *(Makofi)*

Familia zinazokula samaki, ukienda kula nao, kimila hutakiwi kuanza kula kwenye kichwa, unaanzia kwenye mkia. Ukianzia kwenye kichwa, wanakwambia chukua yote, kwa sababu umeshakula utamu wote. Sasa ule utamu unabakia na wale watu wako *organized.* Sasa ile filamu kwangu mimi nilivyokuwa naiona sikuamini macho yangu. Mimi nilikuja nikakuta imeshafika katikati. Wale watani zangu Wagogo walikuwa wananiambia: "Ona kwenu!" nikasema hii siyo Mwanza. Mwanza haiko hivi. Ni tofauti! Kweli tunahitaji msaada, tunahitaji maendeleo, tunahitaji Serikali itusaidie, lakini siyo wajinga kiasi kile walivyokuwa wamechukuliwa. Wale vijana machokora, wameumbwa. Mimi ni msanii na ni muigizaji. Wameumbwa kuweza kuharibu sifa ya Mwanza na kuweza kuharibu sifa ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kuweza kuliona na kwa sababu anasafiri sana, nadhani aliliona kule, ikamtia uchungu sana, akaamua kufanyia likizo Mwanza na kwenda kuyasema maneno hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninamuunga mkono Rais kwa uamuzi wake na ninaomba Serikali yetu iangalie watu kama wale wanapoingia ni vyema wawekewe watu wa kuwafuatilia hata *researchers* wawekewe watu wa kuwafuatilia, ikiwezekana wa kuwasaidia ili waone kama kweli wanafanya kazi waliyokusudia. Huyo alidanganya, hakufanya kazi aliyokusudia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Lakini naomba watu wa Mwanza wawe wajasiri kwa watu hawa wanaokuja (Wazungu) wanaanza kuleta tatizo. Sio wote, lakini kuna ambao wanaanza kuleta zile picha za zamani kwamba Mwafrika bado akili yake ni sawasawa na mnyama kwa picha iliyoonyeshwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kweli msema ukweli ni mpenzi wa Mungu. Mimi nilikuwa sikuomba kuongea. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Niliyapokea majina haya kutoka Kambi ya Upinzani kwa orodha. Ndiyo maana nayafuatilia.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii nichangie hoja hii. Kwanza, kabisa, nimshukuru na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kukemea na kuweza kuhakikisha kwamba uovu huo unakemewa na watu wote wanaoipendea nchi yetu amani na wanaoipendea mema nchi yetu.

Lakini vilevile, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mudhihiri Mudhihir kwa kufikisha hoja hii mbele ya Bunge hili Tukufu na niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuunga mkono hoja hii bila kujali itikadi za Vyama vyetu. Kwa hiyo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninasema hapa kama Naibu Waziri mwenye dhamana ya watoto. Waheshimiwa Wabunge, walionitangulia wamezungumzia suala hili la watoto. Lakini nataka tu niliweke sawa ili watu wote na wananchi wajue kwamba Serikali hii inawapenda watoto na inawajali sana na kuna mengi ambayo tunayafanya kwa ajili ya watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakumbuka Mheshimiwa Rais alipokuwa anazindua Bunge letu Tukufu tarehe 30 Desemba, 2005, naomba ninukuu sehemu tu ya hotuba ya Mheshimiwa Rais.

"Mheshimiwa Spika, katika jamii yetu, yapo makundi maalum ambayo Serikali inayo wajibu wa kuwasaidia. Kundi la kwanza ni la watoto yatima. Hivi sasa kutokana na athari ya UKIMWI, idadi hii imeongezeka. Kwa hiyo, tutahitaji wadau mbalimbali wakae pamoja na kuandaa mpango endelevu wa kuwalea na kuwasaidia watoto hawa. Watoto yatima wanahitaji elimu, lishe bora, afya, makazi na upendo sawa na watoto wengine wa Kitanzania."

Mheshimiwa Rais akaagiza kwamba, nitataka Wizara nitakayounda kusimamia masuala ya watoto, wawasilishe Serikalini katika muda mfupi Mpango Endelevu wa kuweza kushughulikia mahitaji ya kundi hili linaloongezeka katika jamii."

Mheshimiwa Spika, naomba tu nieleze kwamba Wizara yetu tumekuwa tukikaa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika kuandaa Mpango huu. Tuna msaada kutoka Benki ya Dunia ambayo tayari wanasaidia, kuna *Clinton Foundation* na Taasisi mbalimbali ili kuhakikisha kwamba tunakuja na mpango thabiti wa kuweza kuwa na kinga ya jamii hasa kwa watoto hawa wanaoishi katika mazingira magumu na watoto wa Mitaani.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nieleze tu kwamba, suala hili la watoto wanaoishi katika mazingira magumu kwa upande wa nchi zinazozunguka Ziwa Victoria Tanzania, huwezi ikatiwa katika mfano kwa sababu ya athari ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu, haiwezi ikalinganishwa na nchi zinazozunguka Ziwa Victoria.

Watoto wa Tanzania wapo, wana matatizo, lakini wapo wengi katika nchi za jirani zetu na wanajulikana kwa uchokoraa na kwa matatizo yote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niseme kwamba mtunzi wa filamu hii alikuwa na lengo la makusudi la kuweza kuichafua nchi yetu. Tatizo la njaa limejionyesha katika filamu yake, lakini niseme tu kwamba, tatizo hili la njaa linaonekana kama vile Serikali inazembea na haikufanya makusudi na haikuonekana ile hali ya kimazingira au ya *climatic condition* ya ukame iliyoathiri hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme kwamba, wenzetu pia walipata tatizo la njaa na ilikuwa njaa mbaya kiasi kwamba watoto waliletewa biskuti zile za chakula cha mbwa. Sasa hili ni tatizo ambalo lilikuwa kubwa, kama lingeweza likazungumzwa, basi hiyo ilikuwa ni kashfa ambayo ingeweza ikawekwa kama kweli walikuwa na nia nzuri ya kuweza kuiweka Tanzania katika hali nzuri kama anavyodai yeye mwenyewe mtengenezaji filamu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninaliona na nakubaliana na mtoa hoja ni kwamba, huu ni uzandiki na ni nia mbaya ya mwonyesha filamu vilevile kuibeza nchi yetu. Kwa jinsi alivyoweza kutumia wimbo wetu, naweza nikasema ni wimbo wa Utaifa, wimbo ule wa Tanzania, Tanzania nakupenda kwa moyo wote, ametumia wimbo ule kwa makusudi kabisa kwa kutia maneno ambayo hayamo katika ule wimbo ili kuudhi na kukejeli Watanzania. Wote tumesikia.

Mheshimiwa Spika, wimbo huo wa Utaifa ni wimbo ambao wote tunaupenda, watoto kwa wakubwa. Mimi mtoto wangu ana mwaka mmoja na miezi sita anauimba huo wimbo wa Tanzania Tanzania nakupenda kwa moyo wote. Mashahidi wengi ni wazazi, wanajua watoto wanavyokua wanaanza kuimba nyimbo za Mungu ibariki Tanzania na wimbo huu wa Tanzania Tanzania nakupenda kwa moyo wote. Kwa hiyo, sasa watu wakianza kutuchafulia wanataka kufanya watoto wetu wasikue katika maadili ya uzalendo wa kupenda nchi yao. Kwa hiyo, hayo yote yanaonesha nia mbaya ya huyu muigizaji na mtayarisha filamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ambalo nataka nieleze ni kwamba, huu unaonyesha ni ushahidi tosha kwamba ni jinsi gani teknolojia ya habari na mawasiliano ambayo ni teknolojia muhimu kwa kuchochea maendeleo inavyoweza ikatumika vibaya na kuleta madhara. Tunaona jinsi gani wameweza kutumia hii teknolojia ya *ICT* kuleta madhara makubwa na kwa kipindi kifupi tu na kuenea dunia nzima na kuweza kutuletea athari mbaya.

Mheshimiwa Spika, lakini wenzetu wanasema ukianguka, uokote kitu; yaani *if you fall down pick up something*. Sisi tumeanguka, tumechukua kitu. Mimi ninachopenda kuwaasa wenzangu, ni vizuri basi sisi wenyewe tukaona kwamba tukapata ile *big picture.* Tusiangalie picha ndogo ndogo, tuangalie sisi mchango wetu katika kipande kidogo *at the end of the day* mkanda ukiunganishwa kutatoka picha gani?

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi waliotumika katika filamu naweza kusema wengi hawakujua kwamba walikuwa wanatumiwa kwa nia mbaya. Wengi walikuwa wanatoa taarifa na kushiriki bila ya kujua kwamba mwisho wa filamu hiyo, mikanda ikiunganishwa itatoka kitu gani. Nakubaliana kwamba kuna wachache walifanya makusudi kwa nia mbaya. Hao na mimi naungana na Wabunge wenzangu kwamba wale waliofanya kwa nia mbaya waweze wakafikishwa katika vyombo vya sheria wakapata adhabu inayostahili.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naomba kusema kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii nzito ya Taifa.

Pili, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake iliyoonyesha uzalendo wa kukaripia na kupinga kashfa iliyotolewa na mpiga picha huyu na kutaka kuibanika nchi yetu katika Jumuiya ya Kimataifa ionekane kwamba ina matatizo ambayo hayawezi yakatatulika hata kwa karne moja ijayo.

Pili, napenda kumpongeza ndugu yangu Mudhihir kwa kuonyesha uzalendo mkubwa wa kuileta hoja hii mbele yetu na kuizungumza ili tuweze kuitolea maamuzi na kulinda heshima ya nchi yetu.

Tatu, napenda kuwapongeza Wabunge wa Mkoa wa Mwanza kwa kumuunga mkono Mheshimiwa Rais baada ya hotuba ya kutanabaisha kwamba nchi yetu imevamiwa na yule mtu mkorofi mkubwa na pia napenda niwapongeze Wabunge wote waliounga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia eneo moja tu. Yote yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge hapa ya kulinda heshima na hadhi ya nchi yetu nayaunga mkono. Napenda nizungumzie upande wa uzalendo wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna haja kubwa ya kuzungumza neno hili la uzalendo katika nchi yetu ili kuweza kulinda nchi yetu. Hakuna kitu kikubwa katika nchi kama uzalendo. Sinema hii inaonyesha kwamba baadhi ya wenzetu wamekosa uzalendo na ndiyo maana wamekubali kutumiwa na huyu adui mkubwa katika nchi yetu. Tusicheze na suala la uchumi.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma tulikotoka, mambo kama haya ilikuwa ni nadra kuyaona kwa sababu zifuatazo: Tumekuwa tukijenga uzalendo mkubwa kwa kutumia Jeshi letu la Kujenga Taifa. Vijana walipokuwa wanakutana katika Jeshi la Kujenga Taifa, lugha, mtazamo na maudhui yote yalikuwa ni kujenga Utaifa. Wakitoka pale, wanatoka na Utanzania na ukereketwa wa nchi yao. Hivi sasa tunalo Jeshi la Kujenga Taifa, lakini halibebi dhana hii. Ni hatari kubwa! Ndiyo maana anaweza akaja mtu

kutoka nje ya nchi yetu akaomba kibali akapewa, akafanya maovu kwa sababu hatuna mwamko wa uzalendo hata kidogo. Uzalendo unapungua.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mfano. Bahati mbaya mfano huu utanihusu mimi mwenyewe, naomba Waheshimiwa Wabunge mnisamehe. Lakini nia yangu ni kutaka kusisitiza uzalendo.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana pale Redio Tanzania wakati bado ninatangaza. Tulikwenda kufanya kipindi Isansa katika Mkoa wa Mbeya. Tumefika Isansa tukamkuta Mjerumani anafanana na huyu Sampa, sijui nani. Tumekaa naye tunazungumza naye, akaanza kuzungumza maneno ya kashfa dhidi ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea. Siku ile tulikuwa na kipindi cha kurekodi nyimbo za makabila ya Wanyia. Mimi kwa kutumia ukereketwa wangu wa Uenyekiti wa Umoja wa Vijana, kwa uzalendo wa Tanzania, nilimkatalia yule Mzungu, nikamwambia hapa hurekodi, ondoka! Nimekuona hufanani na ukweli wa kuja kwako hapa. Yule Mzungu hakurekodi kile kipindi, aliondoka. Akauliza, hivi huyu ni nani katika Tanzania? Akaambiwa huyo ni kijana tu wa Tanzania, hana cheo chochote!

Mheshimiwa Spika, nilifanya hivyo kwa sababu ya maandalizi wakati ule wa Chama kimoja, ya Umoja wa Vijana. Tulikuwa tunajazwa uzalendo kuipenda nchi yetu. Huo mfano wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, mfano wa pili, niko Redio Tanzania tena. Alikuja Mzungu kutaka habari kuhusu utamaduni wa nchi yetu, ameweka nyani begani, ni mchafu ili tumkubali kwamba ni mtu wa kawaida. Lakini kwa sababu ya kujazwa uzalendo, tulianza kumfanyia wasiwasi pale pale. Ametoka pale akaenda *Daily News*. Tukawasiliana na wenzetu kule, alikamatwa yule Mzungu, ikafahamika kwamba kumbe alikuwa ni adui.

Mheshimiwa Spika, nimeitoa mifano hiyo kwa sababu, sasa hivi kuna hatari kwamba uzalendo haujengeki katika nchi yetu na ndiyo maana anaweza kuja mtu kama huyu akapata kibali tena Mzungu, anataka kufuatilia samaki wetu katika Ziwa letu, samaki wanaotuletea uchumi, hatuna wasiwasi tunamwachia. Hatumfuatilii, leo anakuja kutuadhiri katika dunia hii.

Mheshimiwa Spika, lazima tukumbuke tulikotoka. Tumewaondoa Wazungu hapa, hawakupenda. Nchi hii ni tajiri, wanaitaka na tumeshaonekana kwamba tunaanza kusimama kwa mbawa zetu, wanataka kuturudisha nyuma. Tuwazuie kwa kujaza uzalendo hasa sisi tuliokaa Ofisini tusimwone kila mtu ni rafiki yetu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, suala la *JKT* litazamwe kwa upana wake ili uzalendo uendelee kujengeka. Suala la kuelimishana juu ya kuipenda nchi yetu tusilifanyie masihara katika vyombo vyetu vya habari, magazeti, televisheni, Redio, tuzungumze uzalendo, vijana wetu wasije wakafika mahali wakataka kuiuza nchi hii kwa kukosa uzalendo.

Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema, mengi yamezungumzwa na mimi naomba nisiendelee sana, naunga mkono hoja hii na hawa watu ambao wameshirikishwa katika kutuaibisha, wachunguzwe, wachukuliwe hatua ili iwe ni mfano katika nchi yetu hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BERNARD K. MEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Hoja ya Azimio lililopo mbele yetu na ningependa nianze moja kwa moja. Kwanza nimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa. Mahali penyewe Mwanza panapohusika na jambo hili na maudhui pamoja na mambo aliyoyazugumza kwa kweli ni mazuri na ni ya Kitaifa na nawapongeza Watanzania wote na Bunge kwa kuungana naye kumpongeza kwa hatua na karipio alilolitoa dhidi ya maadui wanaoiangalia nchi yetu kwa jicho la husuda. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina mambo mawili makubwa ya kuyazungumza. La kwanza ni lalamiko la wenzetu wa Upinzani ambalo ndugu yangu Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, amelizungumza pia. Mimi niliangalia mjadala wa kwenye Bunge la Ottawa lililokuwa linaamua umuhimu wa kupeleka Majeshi ya Canada Iraq kwenda kupigana baada ya kuombwa hivyo na Serikali ya Marekani. Katika mjadala ule kulikuwa na vyama vitatu, *Liberal party* cha *Jean Clision, Lucian Bushee* na Chama chake pamoja na *the Conservatives* cha Priston Man.

Waziri Mkuu alipofikia uamuzi huo, Bunge lilipojadili, kila Chama kiljiadili chenyewe. Baada ya uamuzi wa kila Chama, ndipo walipokutana ndani ya Bunge kujadili sasa msimamo na wakafanya hivi hivi tunavyofanya hapa leo. Haiwezekani Vyama vyote vitatu vikutane nje ya Bunge kuweka msimamo wenye maslahi ya Taifa. *That is un-Parlimentary. Parliamentary democracy* inataka vyama vyote vikutane nje kwanza kwenye *caucus* halafu vikiwa na hoja ama ya kuunga mkono Serikali au ya kutofautiana, nafasi peke yake na sehemu pekee inayoruhusu mjadala huu ni humu ndani na hivi tunavyofanya *this is a pure parliamentary democracy* na tusiache huu utaratibu.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Mapinduzi kama Chama Tawala hakikukosea wala vyama vingine navyo vilivyokaa na kuweka *counter speech* havikukosea. Tunavyokutana hivi ndivyo wenzetu kwenye demokrasia zilizokuwa zinavyofanya hakuna kosa. *By partisan agreement* inayoitwa *by partisanship* inatokana humu ndani kwenye *by partisan discussions*. Ya kule nje tusingeweza kuyachambua.

Hatuwezi kukaa na *CUF, CHADEMA* kujadili, tunasemaje kwa sababu ni suala la Kimataifa. Hata tutakapolazimika kumuunga mkono katika kutangaza vita tunatakiwa tufanye hivi hivi. Chama Tawala na vyama vingine vya Upinzani vitakaa halafu tunakuja humu ndani kuweka msimamo wa pamoja. Hatujakosea kabisa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nimesoma kitabu kinaitwa "*The Lords of War,"* Wababe wa Vita. Kitabu kile kinaeleza nani anatengeneza silaha, nani anasambaza silaha katika Afrika na zinakwenda nchi gani na nani ana-*supply*. Yaani anayepeleka zile na

ma-*agents* wanaokwenda kufanya kazi hiyo na *mercenaries* wanaotumwa kuigombanisha na kuipiganisha Afrika kwa manufaa ya kutengeneza fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa furaha, naomba niliarifu Bunge lako Tukufu katika orodha yote ya watu wanaotengeneza silaha, watu wanao-*supply* silaha nchi zinazopitisha silaha hizi na *mercenaries* wanaokwenda kupiganisha watu hao Tanzania haimo katika orodha hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo ni jambo la uongo usiopingika kwamba mtu anaposimama na kuzua kwamba eti ndege zinazokwenda Mwanza zinabeba silaha. Yeye anajua wanaotengeneza silaha na hiyo nchi anayoishi imetamkwa kwamba inahusika na usambazaji wa silaha, awaulize vizuri. Akitaka kufanya utafiti mzuri, zipo nchi zinazofanya biashara hiyo na Tanzania sio miongoni mwa nchi zinazofanya biashara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo nchi Afrika zina umaskini uliokithiri, zina njaa iliyokithiri, zina vita vya wenyewe kwa wenyewe na zina ukahaba uliokithiri, Tanzania sio nchi inayoweza kutolewa mfano katika Afrika eti kwa kuandamwa na matatizo ya aina hiyo. Nchi yetu pamoja na matatizo yake mengine tuliyonayo sio nchi ambayo inaweza ikaruhusu mtu aje atengeneze filamu za uongo halafu akatengenezee mabilioni ya fedha. Aende Somalia mahali ambako mpaka sasa *officially* hakuna Serikali, mahali ambapo kuna njaa iliyokithiri, mahali ambapo kuna vita vya wenyewe kwa wenyewe na kila aina ya uovu kama angetaka kweli kuionyesha dunia mfano wa kufanya vile. Lakini sio kuichukua nchi yetu ambayo sasa inafanya kazi nzuri imeshayaona matatizo yake vizuri iko chini ya uongozi mzuri wa Awamu ya Nne, umechambua matatizo yako na tuko katika miezi sita au saba tunafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, lawama zimetolewa kwamba tulikuwa wapi? Lakini miezi 6, 7, 8, 9, 10, 11, 12 iliyopita tulikuwa kwenye vita na tulikuwa kwenye kazi ya kuunda Serikali ya Awamu ya Nne. Maadui zetu wanatumia mwanya huo wa uundaji na tunapokuwa katika mikiki mikiki ya kisiasa kuanza kupenyesha filamu hizo na kuzionyesha sehemu nyingine kwa ku-*take advantage* au kutumia nafasi ambayo sisi tulikuwa tunashughulikia kuunda Serikali ya Awamu ya Nne. Kwa hiyo, hata zile lawama kwa kweli sio nzito sana, lakini cha muhimu ni kuhakikisha kwamba nchi yetu haitumiwi tena na maadui zetu au watu wenye uroho wa kutafuta fedha kwa kuangalia matatizo madogo madogo na hivyo kulifadhaisha Taifa letu.

Namalizia kuunga mkono Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, namuunga mkono kaka yangu Mudhihir Mohamed Mudhihir na naunga mkono pia Wapinzani na Bunge zima kwa msimamo wa aina yake. Tusikubali kuwaruhusu Waandishi wa Habari uchwara wanaotafuta utajiri wa haraka haraka kuharibu sifa nzuri ya nchi yetu. Tunafanya vizuri na tunakwenda vizuri, tusirudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono tena Azimio hilo.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nami napenda nikushukuuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie kidogo Azimio hili la Bunge.

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali kwa hatua hizi ambazo zimekwishachukuliwa na napenda kusema kwamba mimi nilivyoona ni kwamba, Serikali imefanya kazi yake vizuri na haikuchelewa. Kwa sababu huwezi kuchukua hatua kama hujui inakubidi ujifunze kwanza, uelewe maudhui, ndio utoe kama ni tamko. Kwa hiyo, kwa kweli imefanyika, ni hatua nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilifanya kazi Mkoa wa Mwanza mwaka 1981 mpaka 1983, miaka mitatu. Napenda kusema kwamba nilivyowaelewa mimi wananchi wa Mkoa wa Mwanza na hasa Mji wa Mwanza mapanki sio mboga yao. Walikuwa wanavua wenyewe samaki na viwanda vilivyokuja ndiyo wakajitokeza mapanki.

Mheshimiwa Spika, mapanki yamekuja baada ya kuanzishwa viwanda vya Sangara. Kwa hiyo, sio kweli kusema wananchi hawana mboga. Wananchi wa Mwanza wana mboga. Kabla ya viwanda hivi walikuwa wanakula vyakula vyao na mboga zilikuwepo. Lakini yametokea mapanki.

Sasa mimi ushauri wangu, mapanki yale ni mazuri, supu nzuri. Sasa nadhani Serikali ingeagiza mazingira ya kuyaweka mapanki yawe mazingira ambayo yanalinda afya. Kwa hiyo, tujifunze kutokana na hilo kwamba wasije watu tu wakapiga mainzi yanazunguka, wakasema hayo ndiyo mazingira ya Kitanzania. Wananchi waendelee kutumia mapanki na hii kama ni biashara, basi hiyo biashara itengenezewe mazingira mazuri kwa sababu yakitupwa hivi hivi, nayo yatakuwa ni uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, mimi nilivyotazama suala hili, nadhani kwa kweli nimeshauri Serikali isilitazame juu juu. Huyu aliyetengeneza filamu hii, mimi nahesabu kwamba anatumia ujasusi wa kutumia teknohama, Ujasusi wa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano. Anakaa kando halafu anawaachieni mnapata matatizo. Hii ni kuvuruga uchumi wetu kwa sababu samaki hizi zina soko. Kwa hiyo filamu hiyo inayoonyeshwa huko, watu wanaweza kuamua kwamba tunasusa kwa sababu wananchi wanadhalilishwa, kumbe zinatolewa kule, wanakwenda kula Ulaya huko, lakini wananchi wanapata matatizo.

Mheshimiwa Spika, sangara sio mboga ya wananchi wa Mwanza. Kwanza sangara hapendwi sana. Mimi nimekaa pale, sijala sangara. Nilikuwa nakula sato zaidi. Lakini tumepata soko nje, sasa inapigwa vita hii. Kwa kweli sio jambo dogo, ni vita ya uchumi hii na pengine hayupo peke yake huyu, huenda kuna nchi zinamuunga mkono.

Kwa hiyo, tufanye uchunguzi wa kina kuelewa ameanza anzaje. Huyu mtu peke yake kweli anaweza kuwa na akili peke yake akakaa akasema nikapige filamu hii! Hilo ni moja nadhani lingeangaliwa.

Halafu kuna Watanzania ambao wamehusika. Nadhani wanaosema kwamba pengine hawakujua, sio kweli. Wewe mtu anakuja nyumbani kwako anasema anataka kukusaidia na unamwitikia tu, humwulizi unataka kunisaidia, nani amekwambia nataka msaada? Nadhani kuna kazi imefanyika hapo. Kwa hiyo, tusidhani yuko peke yake,

pengine kuna watu wazito huko. Kama kweli watakuwepo Viongozi wa Vyama vya Siasa, maana leo tumeungana wote, ambao wataonekana wamehusika huko Vyama vyao vielekezwe wawashughulikie na wananchi wajue kwamba hawa ni wasaliti, kwanza wa Chama chao na nchi kwa ujumla. Tusiwaachie tu hivi hivi. Kwa mfano kama yuko Kiongozi wa CCM amehusika, kwa kweli anafukuzwa uanachama wa CCM. Eeh! Kwa sababu anaanza vurugu ambazo kwa kweli zinaturudisha nyuma.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilitaka kulisema hapa ni kuhusu vyombo vya habari. Nilisoma kwenye gazeti moja juzi, linasema kwamba, tunalaumiwa sisi Bunge, kwa nini wakati wa Hoja ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo hatukumuunga Rais mkono? Bunge halirukiruki, kuna taratibu zake na kanuzi zake. Tunapitisha mambo kwa Maazimio. Lazima tuelewe suala, ndiyo tufanye kazi.

Kwa hiyo, sio kweli kwamba Bunge hatukuzungumzia suala hili wakati wa Hotuba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. Leo ndiyo siku yake ambayo imepangwa na Bunge. Bunge haliamki tu likajifanyia tu mambo. Kwa hiyo wasiliendeshe Bunge kutoka nje. Tuna mipango yetu na kanuni zinazotuongoza na leo ndiyo siku yetu ambayo Bunge linatoa tamko na kuiachia Serikali ichukue hatua na baadaye tuelezwe kama kuna hatua ambazo zinachukuliwa na sisi tufahamishwe ili na wananchi wote kwa jumla wajue.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono azimio hili, mia kwa mia. Ahsante sana.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niongee kidogo kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, napenda tu niseme kwamba nimewahi kufanya kazi nyingi pamoja na Mheshimiwa Kingunge-Ngombale Mwiru na wakati mmoja tulitumwa mimi na yeye na kutoa Semina kuhusu Umoja wa Kitaifa. Hiyo ndiyo iliyokuwa *topic.* Sasa Mzee Kingunge alisema wakati huo katika *paper* yake akasema kwamba, suala la Umoja wa Kitaifa tunachotazama ni *National Interests,* sio *interest* ya Vyama. Kwanza unazungumzia suala la *National Interests* na baadaye *Interest* ya vyama inakuja namba mbili. Sasa mimi nitazungumzia kwa mantiki hiyo kwamba, hili ni suala la Kitaifa. Kwa hiyo, tunazungumzia tatizo la Kitaifa na matatizo au *interests* za Vyama zitakuja baadaye.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mawili ambayo nahisi ni muhimu yazungumzwe na mimi nilikuwa sipendi nizungumzie, naweza nikasema malumbano ambayo hayana maana ya kusema nani kama *CCM* walikuwa wakosa, kama *CUF* walikuwa wakosa katika suala zima na baada ya kuangalia ile Kanda tena kila mtu, wakaitana peke yao. Nafikiri hayo tuyaache. Kwa sababu tukianza kuyazungumza hayo, mimi sitakubaliana na kusema kwamba kwa sababu tu Wazungu wa Canada waliitana katika Vyama tofauti tofauti na sisi tuige. Nafikiri hiyo sio kigezo kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba, kuna makosa mawili ambayo lazima tuyakubali na tuyarekebishe. La kwanza, mimi nina wasiwasi kidogo kwamba vyombo vyetu vinavyohusika vilikuwa kidogo havikufanya kazi yake. Kwa

sababu tokea mwaka 2002 mpaka leo vyombo hivi vinavyohusika, vyote hasa katika eneo lile la Mwanza, basi navyo vingelipaswa kueleza na kujua hasa kilichofanywa na Mwandishi huyu. Sasa hilo ni kosa moja kubwa ambalo Kitaifa lazima tulitazame. Kuna matatizo gani katika vyombo vyetu hivi? Vinginevyo, vyombo hivi vinaweza vikatuletea majanga mengi zaidi na makubwa ambayo hatukuyatarajia.

Mheshimiwa Spika, la pili, ninachosema ni kwamba hili ni suala kubwa na zito. Maana yake mtu anapokwambia kwamba Tanzania inapitisha silaha kwa kweli ni *crime* kubwa sana.

Sasa ikiwa hili ni suala zito ambalo sote tunakubaliana, sote Wabunge tuliomo humu tunakubaliana sasa, mimi nahisi kwamba lile Azimio lililotolewa na Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Mudhihir ni jepesi. Kwa sababu unaposema kukaripia, mimi nafikiria kwa mfano katika *GO's* kuna mtu au mfanyakazi wa kawaida akikosa jambo dogo ndiyo anakaripiwa.

Mheshimiwa Spika, kwanza anakaripiwa, halafu kuna karipio kali, halafu kuna kukatwa mishahara, halafu baadaye ndio kufukuzwa kazi. Sasa mnaposema mtu kama huyu tumkaripie, mimi nahisi kwamba *we are not serious*. Ndiyo maana tukasema lazima katika Azimio hili iwepo maelezo ambayo ni mazito zaidi kuonyesha kwamba sisi Watanzania tumekasirika sana na vitendo vibaya vya mtu huyu ambaye jina lake, *anyway* kwamba tumekasirishwa sana na vitendo alivyofanya vya mtangazaji huyu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba sana kwamba tusitumie maneno kukaripia. Kukaripia ni *very light*. Kukaripia haioneshi kwamba sisi Watanzania tumekerwa sana na mambo haya aliyoyafanya. Lazima tuchukue hatua muhimu na madhubuti ambazo zitaonesha kwamba Watanzania tumekasirika na kwamba mtu yeyote mwingine aogope kuja kufanya vitendo kama hivi. Lakini tukisema karipia tu, hata mtu mwingine anaweza akaja akasema Watanzania wamezoea. Tutafanya hili, kesho tutakaripiwa pengine tutakaripiwa mara ya pili itakuwa kwa ukali zaidi. Lakini hayo siyo. Kwa hiyo, hilo ni la pili ambalo ningelipenda tulizungumze.

Mheshimiwa Spika, la tatu napenda pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuandaa au kwa kufanya ile Kamati ambayo tunasikia kwamba ameiunda ili kujadili au kulitazama suala hili in *details.* Sasa katika Kamati hii naamini kwamba yatatokea mambo mengine mengi ambayo yatajionyesha na ambayo pia yataweza kusaidia Bunge lako hili Tukufu kuonyesha kwamba huyu mtu kwa kweli ametudhalilisha au amewadhalilisha Watanzania.

Sasa baada ya kupata taarifa ya Kamati hiyo, mimi nahisi ndiyo hapo tunaweza tukachukua hatua nzito sana na ikiwezekana hata kumshtaki kwa kutuvunjia jina au kutuvunjia hadhi ya nchi yetu ya Tanzania. *Now of course* katika Kamati kama hii ambayo imeundwa naamini kwamba ile *right of hearing* bila shaka anaweza akapewa ili kujua na kupata maelezo zaidi kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, ninachopenda kumalizia ni kusema kwamba, kwa kweli suala hili ni baya na sisi Watanzania tumekasirishwa sana kwa vitendo kama hivi na kwa kweli tunaunga mkono kwamba haya ni mambo ambayo hayatakiwi na lazima tuyapige vita kwa hali yoyote ile. Kwa maana hiyo, ni lazima Azimio letu lioneshe kukasirishwa kwetu kwa nguvu zote zile ambazo tunaweza kuziandika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii na mimi kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba ambayo aliitoa tarehe 31 Julai, 2006 Jijini Mwanza wakati anaongea na Taifa kupitia Wazee wa Mkoa wa Mwanza. Lakini pia nitoe pongezi kwa mtoa hoja, Mheshimiwa Mudhihir na pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Chama cha Mapinduzi kwa kuitisha Kikao kile cha Wabunge wa CCM kujadili jambo hili. Lakini pia nimpongeze sana Kiongozi wa Kambi ya Upinzani naye kwa kuitisha Kikao ambacho wao walijadili na kuweka msimamo wa mambo ambayo tunajadili kwa pamoja. *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa umoja wetu, tupo hapa kama Bunge na leo tunaonyesha msimamo wa pamoja katika suala hili ambalo ni la kitaifa zaidi. Nawapongeza sana Wabunge wenzangu na mwisho kabisa kwa umuhimu ule ule nawapongeza sana wananchi wa Mkoa wa Mwanza na majirani wa Mkoa wa Mwanza ambao tarehe 5 Agosti, 2006 walifanya maandamano kuunga mkono hotuba ya Rais aliyoitoa tarehe 31 Julai, 2006. Nawapongeza sana. Mimi kama Katibu wa Wabunge wa Mkoa wa Mwanza na kwa niaba na wenzangu pia tunasema tuko pamoja na tunaendelea kuwa pamoja kumsaidia Mheshimiwa Rais. Lakini cha msingi ni kupigania maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja. Kwanza kabisa, niseme kwa dhati kwamba naunga mkono hoja hii iliyoko mbele yetu. Lakini kwa kweli ninaguswa sana na mimi nasema, awali ya yote tumlaani sana mtayarishaji wa filamu hii.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi yamesemwa na tumepata nafasi ya kuiona hii filamu, tukaona maudhui yake. Yapo mengi yaliyosemwa, lakini naomba niongelee masuala matatu, manne.

La kwaza ni msisitizo wa ulaji wa mapanki kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa na hususan Mkoa wa Mwanza kama kielelezo cha umaskini walionao wananchi wa Mkoa wa Mwanza. Niseme ya kwamba, hapa tunaongea kama Bunge, kama Taifa, lakini jambo hili kwa sisi tunaotoka Kanda ya Ziwa na hasa Mkoa wa Mwanza uchungu tulionao inawezekana ukawa ni mkubwa kuliko uchungu wa wengine ambao wanatoka nje ya Kanda ya Ziwa. Mandhari na picha iliyoonyeshwa kwenye filamu ile nadhani inatudhalilisha kiasi ambacho hakivumiliki. *(Makofi)*

Kwa wale wenzangu waliosoma gazeti la tarehe 9, siku ya Jumatano ukurasa wa 12, kuna makala ambayo gazeti la Mwananchi limefanya mahojiano na mtayarishaji wa filamu. Kuna mambo ameyasema pale na hayo ndiyo yanayonifanya nichangie hoja.

Naomba niyaseme machache aliyoyasema akijenga hoja kutetea filamu ile kwamba ina maslahi kwa Watanzania na mbele ya safari, itakuja isaidie Taifa hili. Nakanusha hili. Haikuwa nia yake. Nia yake ni kuharibu ni kudhalilisha na kutufanya sisi tuonekane ni watu ambao hatutumii akili ambazo Mwenyezi Mungu katujalia.

Mheshimiwa Spika, kasema mambo kadhaa, anasema kwa kujiamini, eti akisisitiza ukweli anaousema katika maudhui ya filamu ile kwamba wananchi wa Mkoa wa Mwanza hawali samaki, bali wamekuwa wakila tu mapanki ama mabaki ya vichwa vya sangara. Lakini pia anaendelea, anasema hakuna mtu wa kawaida pale Mwanza ambaye ana maisha bora yaliyotokana na shughuli za uvuvi wa samaki. Inauma sana.

Mheshimiwa Spika, wapo pia wazandiki wengine katika nchi hii ambao wameshirikiana na huyu Bwana. Inasikitisha sana, kweli leo watu wanaoifahamu Mwanza kwa dhati wanaweza kusema kwamba biashara ya samaki haijawasaidia wananchi wa Tanzania na hasa wakazi wa Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa kwa ujumla. Anaongea kitu ambacho ni uongo ambao ni *obvious*, sijui tuseme kitu gani. Ni uzushi, ni uzandiki na tunaomba hawa ambao ameshirikiana nao, naomba walaaniwe sana. Lakini kwa sababu kitu ambacho naweza kusema ni kulaaniwa, hatuwezi kuvuka mipaka ya Mwenyezi Mungu.

Lakini ambacho naweza kusema ni kwamba, hii filamu haikuwa na nia nzuri kwa nchi yetu. Naomba tuwalaani na wajue kwamba msimamo wetu kama Taifa, tuko pamoja na Mheshimiwa Rais na tunaungana na wananchi wa Mkoa wa Mwanza na sio kweli wananchi wa Mkoa wa Mwanza wamekuwa kimya kwa muda wote huu, hapana. Wananchi wa Mkoa wa Mwanza na wa Kanda ya Ziwa ni sehemu ya Taifa hili na Taifa hili kwa muda wote halijawahi kukumbana na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naungana na wengine waliolaani na mimi naendelea kusisitiza kwamba tunalaani kwa nguvu zote kwamba filamu hii haikuwa na mandhari nzuri. Huwezi kuchukua picha zile za watoto kwa kuwadhalilisha kuonyesha hali halisi ya maisha ya Mwanza, ukasema eti wananchi wa Mwanza hawali vitoweo vya samaki eti kwa sababu tu ya biashara ya samaki inayofanywa katika Ziwa Victoria, inahusisha samaki aina ya sangara. Lakini tunafahamu tunaotoka kule na Taifa linafahamu kwa kumbukumbu zilizopo, Ziwa Victoria na hapa tumekumbushwa na asubuhi ya leo na Mheshimiwa mtoa hoja lina aina zaidi ya 17 ya samaki. Sisi kule Kanda ya Ziwa na hasa Mwanza kitoweo ambacho kinathaminika sana na ambacho wanachi wanakipenda ni sato. *(Makofi)*

Lakini pia katika viwango vya samaki zinazopatikana ziwani, viwango vinatofautiana bei kulingana na *size* ya samaki. Wapo samaki wadogo wadogo aina ya dagaa pamoja na fulu. Hawa wanaweza kutumiwa na wananchi wa kawaida. Leo tunaambiwa kwamba hakuna mwananchi anayekula samaki kama kitoweo, eti kwa

sababu biashara ya samaki inahusisha sangara. Ni kashfa kwa nchi yetu na naomba wachache wetu wanaotumiwa kueneza kwa sababu wanadhani kwamba kwa kusema vile watakuwa wanajenga hoja kutetea ulaji wa mapanki yaliyooza Mkoani Mwanza, naomba tuwalaani sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni zito na lazima tulikemee kama Watanzania. Tulikemee na pengine kama ilivyopendekezwa, hatua kali zaidi za kisheria zichukuliwe kwa wale ambao wameshirikiana na huyu Hubert Suoper kutayarisha hii filamu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka niliseme ni hizi tuhuma kwamba baadhi ya viwanja vya ndege vinavyozunguka Ziwa Victoria na kwa mandhari ya filamu ile huwezi kukiacha pembeni kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Mwanza. Sio kweli kwamba vinatumika kwa kuleta silaha. Huyu mtayarishaji, ukisoma hili gazeti ukurasa huu wa 12, alivyokuwa anahojiwa anasema kuna nyakati ililazimika kujifanya kama Rubani ama msimamizi wa upakuaji wa ndege na akaanzisha urafiki na hawa marubani wa hizi ndege.

Sasa katika mazingira hayo, unashindwa kuelewa kwamba hivi si kweli kwamba huyu bwana ametumiwa! Lakini kama alikuwa ana nia njema kwa sababu kwa kipindi cha miezi sita ambayo amekuwa akitayarisha hii filamu, basi yawezekana alizipata hizo dodoso pembeni akiwa anaongea na hawa ma-*pilot*. Kwanini asije akaongea na Serikali akaishauri kama kweli alikuwa na nia njema? Haya mambo ameyasikia, kama yapo ingawaje tunaamini kwamba hayapo. Lakini kama yapo, kwanini asubiri kutayarisha hii filamu ambayo kimsingi inakuja kuharibu sifa ya Tanzania ndani na nje ya Tanzania? Huyu hakuwa na nia njema hata kidogo. Kwa hiyo, lazima tumlaani na tumlaani sana. Kama walivyopendekeza wenzangu, sheria kali zichukuliwe dhidi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naungana na wenzangu kusema kwamba, hapana, huyu lazima alaaniwe sana. Lakini lingine ni hili suala la ukahaba. Tunafahamu wengi sana hapa wamefika Ulaya. Hivi jamani, biashara ya ukahaba inayofanyika kule kwenye nchi za Magharibi hasa zilizoendelea, unaweza ukalinganisha na haya mambo yanayosemwa Mkoani Mwanza pamoja na Tanzania kwa ujumla? Tunafahamu wengi wamefika Nice Ufaransa, mambo gani yanafanyika?

Mheshimiwa Spika, hata ukienda Cape Town, hapa Afrika Kusini, waliofika *Hollywood* watasemaji? Sasa haya mambo nadhani ni katika kuonyesha nia yake mbaya ambayo anadhani kwamba sisi ni wajinga sana, wachache wetu wanaweza kumuunga mkono kwa sababu ya hoja anazozitoa. Lakini kimsingi ni mtu ambaye hakuwa na nia njema.

Mheshimiwa Spika, la msingi, naomba kusisitiza tuendelee kuishukuru na kuipongeza Serikali na tuiombe tu iendelee kuimarisha uwanja wa ndege wa Mwanza kwa sababu kwa kweli kwa hali ya mazingira ya sasa yalivyo na itakavyokuwa mbele ya safari, ni kwamba Mwanza inastahili kuwa *hub* kama ambavyo nia njema ya Serikali Ilivyo. Tukiimarishe hiki kiwanja. Tunafahamu kweli biashara ya minofu ya samaki imeshuka kwa mwaka uliopita, lakini sio kwa sababu ya makosa ambayo tunayafanya

kama ambavyo tunajaribu kutuhumiwa katika filamu hii. Ninadhani Serikali ina nia njema na itaendelea kulinda uwanja wa ndege wa Mwanza na viwanja vingine. Lakini la msingi, tuimarishe utaifa na tusikubali kuchezewa kwa kiwango ambacho kimeonyeshwa katika filamu hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme kwa mara nyingine kwamba tunaungana na Mheshimiwa Rais, naungana na mtoa hoja, Waheshimiwa Wabunge na naungana na wananchi wa Mkoa wa Mwanza na tusimame kidete kuhakikisha kwamba tunapigania uzalendo na utu wa nchi yetu. Ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uamuzi wake sahihi wa kutoa tamko la kulaani kwa nguvu zote kuhusu upotoshaji wa filamu hii yenye kuidhalilisha nchi yetu kwa Mataifa yote duniani.

Aidha, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mudhihir Mohammed Mudhihir (Mbunge), kwa uamuzi wake wa kuleta hoja hii mbele yetu kwa uchungu wa kukerwa na filamu hii yenye wingi wa upotoshaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukahaba, Tanzania ni nchi mojawapo isiyokubali wananchi wake kuwa makahaba, kwani kama ni nchi inayokubali wananchi wake wawe na vitendo vya ukahaba, basi ingekuwa tayari kutokukemea na kuruhusu hata Vyombo vya Habari viwe huru kuonyesha hata filamu zenye kuvunja maadili ya Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi za Ulaya zimeweka bayana ukahaba na kutoa leseni ili ukahaba uendelee na kutambuliwa rasmi ndani ya nchi zao.

Mheshimiwa Spika, kweli Tanzania tulikumbwa na baa la njaa, lakini samaki ni kitoweo tu na sio chakula kama wenzetu wanavyotathmini, kwani utamu wa samaki uko kichwani zaidi kuliko sehemu nyingine na samaki nchi hii wako wa aina nyingi, sio hao tu wanaouzwa minofu yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwatumia watoto katika vitendo vya ajira na kuwarubuni, hicho ni kitendo kibaya sana na hayo ni matumizi mabaya ya kuwatumikisha watoto na kuwaingiza katika shughuli wasiyoifahamu. Naiomba Wizara husika ichukue hatua muafaka kuhusu mtu huyu kwa kuwatumikisha watoto kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, iko haja pia kuangalia vyombo vyetu vya ulinzi kuwa macho zaidi kwa watu kama hawa ili waweze kuwadhibiti mapema zaidi kabla madhara makubwa hayajatokea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, mimi naomba kuchangia jambo hili kwa kutoa maoni yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, muandaji wa filamu hii amekiuka mkataba wa kibali chake, yeye aliomba kupiga picha za aina mbalimbali za samaki, lakini haikuwa kupiga picha za maisha ya watu. Hata kama maisha ya watu yangekuwa vile, haikuwa kibali chake kile.

Mheshimiwa Spika, kama nia ya mpigapicha huyu ingekuwa ni kuisaidia nchi yetu katika soko la/au na kuonyesha ni jinsi gani tunavyodhulumiwa kwa bei na kadhalika, asingetoa pia hii.

Mpiga picha alikiuka mkataba wake kwa kutafuta waigizaji na kuwapandikiza yale aliyoyakusudia ili wayafanye. Hivyo, amewadhulumu hata wale waigizaji pamoja na watoto aliowatumia, hata kama amelipa bado hakishiriki, inawalinda. Je, wamefaidika nini?

Mheshimiwa Spika, maoni yangu ni kama ifuatavyo:-

(a) Mwandishi huyu Hurbert Sauper awaombe msamaha wananchi wote ambao ni wakazi wa Mkoa wa Mwanza ambao ndio waliohusika na filamu hii kwa kutumia uvuvi wa Ziwa Victoria;

(b) Aiombe nchi yetu ya Tanzania msamaha kwa kuidhalilisha kiasi kile;

(c) Jitihada za kimataifa zifanyike ili picha hii inayoendelea kuonyeshwa ipigwe marufuku; na

(d) Nchi yake ijulishwe na suala la kidemokrasia lichukuliwe ili itoe tamko kwa kulinda maslahi ya uhusiano wa nchi yetu na nchi yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba kujua *Tanzania Film Censorship* wanasemaje? Pamoja na kwamba, mkataba uliwekwa, sasa tuwe macho na wageni wanaokuja hapa nchini, hasa wanapopiga picha ovyo. Wasitoke nazo mpaka ziwe zimehakikiwa.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri Tanzania tuingie gharama ya kutengeneza filamu nyingine itakayoonyesha uhalisi wa ukweli wa aina na uvuvi wa samaki Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, namuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu. Naunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake aliyoitoa Mkoani Mwanza inayohusu filamu ya *Darwins Nightmare.*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Mzungu huyu ametudhalilisha kiasi kikubwa na Taifa zima kwa ujumla. Lakini ningependa kujiuliza: Je, wakati wote yote yanafanyika, hapakuwepo na vyombo vya ulinzi na usalama katika maeneo yote hayo? Ukianzia Serikali ya Kijiji au Mtaa, Afisa Mtendaji wa Kata, Mkuu wa Wilaya, Maafisa Usalama na vyombo vingine vinavyohusika na masuala ya ulinzi, vyote hivi vilikuwa wapi? Kibaya zaidi, mtu huyu akaruhusiwa kuingia katika chumba cha kuongozea ndege. Swali au changamoto kwa vyombo vyetu vya ulinzi, vimejifunza nini? Hasa Usalama wa Taifa kwa ngazi zote, maana usalama au *information* huanzia ngazi za chini, *ma-informer* wako wapi? Hivi sasa kuna Warundi wengi wamejaa lakini hakuna hatua za makusudi zinazochukuliwa. Naishauri Serikali iongeze *ma-informer* wengi waenee kila Kitongoji kwa lengo la kuimarisha ulinzi wa nchi ili tatizo hili la kila mtu kufanya atakalo katika nchi yetu lisitokee tena.

Mwisho, wale wote wasiojua wajibu wao katika masuala ya ulinzi waonywe vikali na wale vijana wenye tamaa ya vita wachukuliwe hatua kali kwa kuzingatia Tanzania imekuwa siku zote msuluhishi wa migogoro katika maziwa makuu na mwenyeji wa kubeba mzigo wa wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa asilimia mia moja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu kuhusu filamu hii, kwanza namuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa kulaani kazi isiyo na maadili iliyofanyika katika filamu hii pamoja na mtengenezaji na mmiliki wa filamu hii. Lakini pia naomba kutoa tahadhari kwa Watanzania wengine ambao pia wanadhalilisha Watanzania kwa kuchukua picha mbaya zinazoielezea jamii ya Tanzania kwa ajili ya kujipatia misaada kutoka nje kwa faida yao.

**MHE. IDD MOHAMED AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir kwa hoja yake aliyowasilishwa hapa Bungeni. Naunga mkono yote aliyoyaelezea pamoja na Maazimio yake.

Kwanza, naomba katika maazimio yake tuangalie ni jinsi gani tutamchukulia hatua za kisheria kwa maelezo yake ya uongo katika filamu ile mbali na kumkaripia tu.

Pili, tuwatafute wale Watanzania ambao wameshiriki katika filamu ile ili watueleze ukweli ni kwa nini walishiriki katika uongo uliomo ndani ya filamu ile na ikibidi wachukuliwe hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshmiwa Mudhihir kwa kuileta hoja hii hapa Bungeni. Kwa masikitiko makubwa, napenda nitoe maoni yangu juu ya filamu hiyo ambayo imetoa taswira ambayo imepotosha hali halisi ya nchi yetu. Nchi yetu inathamini utu wa kila mtu na inahakikisha anapata haki zake za msingi.

Lakini mwandishi na mtayarishaji wa filamu hiyo amepotosha umma kwa kuchukua waigizaji hao hao na kuwafundisha waonyeshe kama alivyotaka mtayarishaji huyo kwa maslahi yake. Isitoshe, amechagua maeneo ambayo hayaoneshi mandhari nzuri ya Mji wa Mwanza, hatimaye kuchagua baadhi ya watu ambao wengi wao wameonekana walemavu kama vile nchi hii imekumbwa na vita au kukosa matunzo bora.

Mheshimiwa Spika, suala la kutumia watoto na kuwadhalilisha katika kuwataka waonyeshe kwamba wanaishi kwenye mazingira magumu na kuwapanga waonekane wana dhiki kubwa sana kiasi cha kugombea chakula kuwavutisha sigara, gundi na petroli, huu ni udhalilishaji kwa watoto hao. Yeye kwa kuwa ni mwandishi kwa taaluma, anayaelewa yote hayo, iweje adhalilishe watoto hao na hata wanawake walioonekana wakifanya ukahaba?

Natoa wito kwa kuunga mkono hoja hii ambayo imeletwa na Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir na pia napendekeza wahusika wakuu wote waliohusika wachuliwe hatua zinazostahili. Naunga mkono hoja.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii. Naomba kutoa wito kwa Watanzania wenzangu kuunga mkono hoja hii na kuendeleza usahihi wa tamko la Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete la kuipinga Filamu hii kwa kuwa haina maudhui halisi ya mazingira ya Tanzania na Watanzania wenyewe kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi ya amani na ni nchi inayotetea na kuongeza mazungumzo ya amani katika Afrika yetu mbali ya kushiriki bega kwa bega katika ukombozi wa nchi za Afrika kwa njia nyingi za kiufundi na hatimaye nchi kadhaa zimepata uhuru wake kwa kutokana na mchango mkubwa wa Tanzania kwa uongozi wa Marehemu J. K. Nyerere. Leo iweje Tanzania hii iingize silaha kuchochea vita vya wenyewe kwa wenyewe katika nchi jirani?

Mheshimiwa Spika, samaki ni kitoweo kwa Watanzania, sio chakula. Watanzania wanaweza kuishi bila ya kula samaki, kwani vitoweo viko vya ana nyingi na Watanzania wanao uwezo wa kutumia vitoweo hivyo mbadala. Huu ni upotoshaji. Kuna mengi ya kasoro/sio sahihi katika filamu hiyo. Hivyo, naishauri Serikali kufanya mambo yafuatayo:-

(1) Kuwahoji wote walioshiriki (Watanzania) katika filamu hiyo kujua kulikoni ili kujenga msingi wa kuwachukulia hatua za kisheria watengenezaji wa filamu hii;

(2) Kwa nini muda mrefu umepita bila ya Wizara ya Utalii na Maliasili kulishughulikia hili?

(3) Hatua za kuwashitaki kimataifa zichukuliwe ili Mataifa mengine wajue kwamba Tanzania sio jalala/jaa la biashara za maovu na kuchezewa.

(4) Ukiacha sisi wenyewe, Watanzania tuandae filamu ya Ukweli kuhusu Mwanza na uvuvi. Watafutwe pia waandaaji wa filamu na kutoka nje ya nchi ambazo watakuwa tayari kuonyesha hali halisi ya maisha ya Watanzania kwa Ukweli kwa kuandaa au kama zipo zilizokwishaandaliwa zinazofanana na tatizo hili, iwe kigezo cha kukanusha *story* ya filamu ya *Darwin's Nightmare.* Ahsante.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii tena na kwa kweli sikusudii kujibu hoja ya kila mmoja kwa sababu wote wamezungumzia jambo lile lile kwa ufundi tofauti. Ningependa niwatambue waliochangia kwa kuzungumza ambao ni Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Esther Nyawazwa. Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Dr. Batilda Buriani, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary na Mheshimiwa William Ngeleja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu napenda pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuandaa au kwa kufanya ile Kamati ambayo tunasikia kwamba ameiunda ili kujadili au kulitazama suala hili in *details.* Sasa katika Kamati hii naamini kwamba yatatokea mambo mengine mengi ambayo yatajionyesha na ambayo pia yataweza kusaidia Bunge lako hili Tukufu kuonyesha kwamba huyu mtu kwa kweli ametudhalilisha au amewadhalilisha Watanzania.

Sasa baada ya kupata taarifa ya Kamati hiyo, mimi nahisi ndiyo hapo tunaweza tukachukua hatua nzito sana na ikiwezekana hata kumshtaki kwa kutuvunjia jina au kutuvunjia hadhi ya nchi yetu ya Tanzania. *Now of course* katika Kamati kama hii ambayo imeundwa naamini kwamba ile *right of hearing* bila shaka anaweza akapewa ili kujua na kupata maelezo zaidi kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, ninachopenda kumalizia ni kusema kwamba, kwa kweli suala hili ni baya na sisi Watanzania tumekasirishwa sana kwa vitendo kama hivi na kwa kweli tunaunga mkono kwamba haya ni mambo ambayo hayatakiwi na lazima tuyapige vita kwa hali yoyote ile. Kwa maana hiyo, ni lazima Azimio letu lioneshe kukasirishwa kwetu kwa nguvu zote zile ambazo tunaweza kuziandika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii na mimi kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba ambayo aliitoa tarehe 31 Julai, 2006 Jijini Mwanza wakati anaongea na Taifa kupitia Wazee wa Mkoa wa Mwanza. Lakini pia nitoe pongezi kwa mtoa hoja, Mheshimiwa Mudhihir na pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Chama cha Mapinduzi kwa kuitisha Kikao kile cha Wabunge wa CCM kujadili jambo hili. Lakini pia nimpongeze sana Kiongozi wa Kambi ya Upinzani naye kwa kuitisha Kikao ambacho wao walijadili na kuweka msimamo wa mambo ambayo tunajadili kwa pamoja. *(Makofi).*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa umoja wetu, tupo hapa kama Bunge na leo tunaonyesha msimamo wa pamoja katika suala hili ambalo ni la kitaifa zaidi. Nawapongeza sana Wabunge wenzangu na mwisho kabisa kwa umuhimu ule ule nawapongeza sana wananchi wa Mkoa wa Mwanza na majirani wa Mkoa wa Mwanza ambao tarehe 5 Agosti, 2006 walifanya maandamano kuunga mkono hotuba ya Rais aliyoitoa tarehe 31 Julai, 2006. Nawapongeza sana. Mimi kama Katibu wa Wabunge wa Mkoa wa Mwanza na kwa niaba na wenzangu pia tunasema tuko pamoja na tunaendelea kuwa pamoja kumsaidia Mheshimiwa Rais. Lakini cha msingi ni kupigania maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja. Kwanza kabisa, niseme kwa dhati kwamba naunga mkono hoja hii iliyoko mbele yetu. Lakini kwa kweli ninaguswa sana na mimi nasema, awali ya yote tumlaani sana mtayarishaji wa filamu hii.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi yamesemwa na tumepata nafasi ya kuiona hii filamu, tukaona maudhui yake. Yapo mengi yaliyosemwa, lakini naomba niongelee masuala matatu, manne.

La kwaza ni msisitizo wa ulaji wa mapanki kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa na hususan Mkoa wa Mwanza kama kielelezo cha umaskini walionao wananchi wa Mkoa wa Mwanza. Niseme ya kwamba, hapa tunaongea kama Bunge, kama Taifa, lakini jambo hili kwa sisi tunaotoka Kanda ya Ziwa na hasa Mkoa wa Mwanza uchungu tulionao inawezekana ukawa ni mkubwa kuliko uchungu wa wengine ambao wanatoka nje ya Kanda ya Ziwa. Mandhari na picha iliyoonyeshwa kwenye filamu ile nadhani inatudhalilisha kiasi ambacho hakivumiliki. *(Makofi)*

Kwa wale wenzangu waliosoma gazeti la tarehe 9, siku ya Jumatano ukurasa wa 12, kuna makala ambayo gazeti la Mwananchi limefanya mahojiano na mtayarishaji wa filamu. Kuna mambo ameyasema pale na hayo ndiyo yanayonifanya nichangie hoja.

Naomba niyaseme machache aliyoyasema akijenga hoja kutetea filamu ile kwamba ina maslahi kwa Watanzania na mbele ya safari, itakuja isaidie Taifa hili.

Nakanusha hili. Haikuwa nia yake. Nia yake ni kuharibu ni kudhalilisha na kutufanya sisi tuonekane ni watu ambao hatutumii akili ambazo Mwenyezi Mungu katujalia.

Mheshimiwa Spika, kasema mambo kadhaa, anasema kwa kujiamini, eti akisisitiza ukweli anaousema katika maudhui ya filamu ile kwamba wananchi wa Mkoa wa Mwanza hawali samaki, bali wamekuwa wakila tu mapanki ama mabaki ya vichwa vya sangara. Lakini pia anaendelea, anasema hakuna mtu wa kawaida pale Mwanza ambaye ana maisha bora yaliyotokana na shughuli za uvuvi wa samaki. Inauma sana.

Mheshimiwa Spika, wapo pia wazandiki wengine katika nchi hii ambao wameshirikiana na huyu Bwana. Inasikitisha sana, kweli leo watu wanaoifahamu Mwanza kwa dhati wanaweza kusema kwamba biashara ya samaki haijawasaidia wananchi wa Tanzania na hasa wakazi wa Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa kwa ujumla. Anaongea kitu ambacho ni uongo ambao ni *obvious*, sijui tuseme kitu gani. Ni uzushi, ni uzandiki na tunaomba hawa ambao ameshirikiana nao, naomba walaaniwe sana. Lakini kwa sababu kitu ambacho naweza kusema ni kulaaniwa, hatuwezi kuvuka mipaka ya Mwenyezi Mungu.

Lakini ambacho naweza kusema ni kwamba, hii filamu haikuwa na nia nzuri kwa nchi yetu. Naomba tuwalaani na wajue kwamba msimamo wetu kama Taifa, tuko pamoja na Mheshimiwa Rais na tunaungana na wananchi wa Mkoa wa Mwanza na sio kweli wananchi wa Mkoa wa Mwanza wamekuwa kimya kwa muda wote huu, hapana. Wananchi wa Mkoa wa Mwanza na wa Kanda ya Ziwa ni sehemu ya Taifa hili na Taifa hili kwa muda wote halijawahi kukumbana na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naungana na wengine waliolaani na mimi naendelea kusisitiza kwamba tunalaani kwa nguvu zote kwamba filamu hii haikuwa na mandhari nzuri. Huwezi kuchukua picha zile za watoto kwa kuwadhalilisha kuonyesha hali halisi ya maisha ya Mwanza, ukasema eti wananchi wa Mwanza hawali vitoweo vya samaki eti kwa sababu tu ya biashara ya samaki inayofanywa katika Ziwa Victoria, inahusisha samaki aina ya sangara. Lakini tunafahamu tunaotoka kule na Taifa linafahamu kwa kumbukumbu zilizopo, Ziwa Victoria na hapa tumekumbushwa na asubuhi ya leo na Mheshimiwa mtoa hoja lina aina zaidi ya 17 ya samaki. Sisi kule Kanda ya Ziwa na hasa Mwanza kitoweo ambacho kinathaminika sana na ambacho wanachi wanakipenda ni sato. *(Makofi)*

Lakini pia katika viwango vya samaki zinazopatikana ziwani, viwango vinatofautiana bei kulingana na *size* ya samaki. Wapo samaki wadogo wadogo aina ya dagaa pamoja na fulu. Hawa wanaweza kutumiwa na wananchi wa kawaida. Leo tunaambiwa kwamba hakuna mwananchi anayekula samaki kama kitoweo, eti kwa sababu biashara ya samaki inahusisha sangara. Ni kashfa kwa nchi yetu na naomba wachache wetu wanaotumiwa kueneza kwa sababu wanadhani kwamba kwa kusema vile watakuwa wanajenga hoja kutetea ulaji wa mapanki yaliyooza Mkoani Mwanza, naomba tuwalaani sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni zito na lazima tulikemee kama Watanzania. Tulikemee na pengine kama ilivyopendekezwa, hatua kali zaidi za kisheria zichukuliwe kwa wale ambao wameshirikiana na huyu Hubert Suoper kutayarisha hii filamu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka niliseme ni hizi tuhuma kwamba baadhi ya viwanja vya ndege vinavyozunguka Ziwa Victoria na kwa mandhari ya filamu ile huwezi kukiacha pembeni kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Mwanza. Sio kweli kwamba vinatumika kwa kuleta silaha. Huyu mtayarishaji, ukisoma hili gazeti ukurasa huu wa 12, alivyokuwa anahojiwa anasema kuna nyakati ililazimika kujifanya kama Rubani ama msimamizi wa upakuaji wa ndege na akaanzisha urafiki na hawa marubani wa hizi ndege.

Sasa katika mazingira hayo, unashindwa kuelewa kwamba hivi si kweli kwamba huyu bwana ametumiwa! Lakini kama alikuwa ana nia njema kwa sababu kwa kipindi cha miezi sita ambayo amekuwa akitayarisha hii filamu, basi yawezekana alizipata hizo dodoso pembeni akiwa anaongea na hawa ma-*pilot*. Kwanini asije akaongea na Serikali akaishauri kama kweli alikuwa na nia njema? Haya mambo ameyasikia, kama yapo ingawaje tunaamini kwamba hayapo. Lakini kama yapo, kwanini asubiri kutayarisha hii filamu ambayo kimsingi inakuja kuharibu sifa ya Tanzania ndani na nje ya Tanzania? Huyu hakuwa na nia njema hata kidogo. Kwa hiyo, lazima tumlaani na tumlaani sana. Kama walivyopendekeza wenzangu, sheria kali zichukuliwe dhidi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naungana na wenzangu kusema kwamba, hapana, huyu lazima alaaniwe sana. Lakini lingine ni hili suala la ukahaba. Tunafahamu wengi sana hapa wamefika Ulaya. Hivi jamani, biashara ya ukahaba inayofanyika kule kwenye nchi za Magharibi hasa zilizoendelea, unaweza ukalinganisha na haya mambo yanayosemwa Mkoani Mwanza pamoja na Tanzania kwa ujumla? Tunafahamu wengi wamefika Nice Ufaransa, mambo gani yanafanyika?

Mheshimiwa Spika, hata ukienda Cape Town, hapa Afrika Kusini, waliofika *Hollywood* watasemaji? Sasa haya mambo nadhani ni katika kuonyesha nia yake mbaya ambayo anadhani kwamba sisi ni wajinga sana, wachache wetu wanaweza kumuunga mkono kwa sababu ya hoja anazozitoa. Lakini kimsingi ni mtu ambaye hakuwa na nia njema.

Mheshimiwa Spika, la msingi, naomba kusisitiza tuendelee kuishukuru na kuipongeza Serikali na tuiombe tu iendelee kuimarisha uwanja wa ndege wa Mwanza kwa sababu kwa kweli kwa hali ya mazingira ya sasa yalivyo na itakavyokuwa mbele ya safari, ni kwamba Mwanza inastahili kuwa *hub* kama ambavyo nia njema ya Serikali Ilivyo. Tukiimarishe hiki kiwanja. Tunafahamu kweli biashara ya minofu ya samaki imeshuka kwa mwaka uliopita, lakini sio kwa sababu ya makosa ambayo tunayafanya kama ambavyo tunajaribu kutuhumiwa katika filamu hii. Ninadhani Serikali ina nia njema na itaendelea kulinda uwanja wa ndege wa Mwanza na viwanja vingine. Lakini la msingi, tuimarishe utaifa na tusikubali kuchezewa kwa kiwango ambacho kimeonyeshwa katika filamu hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme kwa mara nyingine kwamba tunaungana na Mheshimiwa Rais, naungana na mtoa hoja, Waheshimiwa Wabunge na naungana na wananchi wa Mkoa wa Mwanza na tusimame kidete kuhakikisha kwamba tunapigania uzalendo na utu wa nchi yetu. Ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uamuzi wake sahihi wa kutoa tamko la kulaani kwa nguvu zote kuhusu upotoshaji wa filamu hii yenye kuidhalilisha nchi yetu kwa Mataifa yote duniani.

Aidha, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mudhihir Mohammed Mudhihir (Mbunge), kwa uamuzi wake wa kuleta hoja hii mbele yetu kwa uchungu wa kukerwa na filamu hii yenye wingi wa upotoshaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukahaba, Tanzania ni nchi mojawapo isiyokubali wananchi wake kuwa makahaba, kwani kama ni nchi inayokubali wananchi wake wawe na vitendo vya ukahaba, basi ingekuwa tayari kutokukemea na kuruhusu hata Vyombo vya Habari viwe huru kuonyesha hata filamu zenye kuvunja maadili ya Mtanzania.

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Zaynab Vullu na Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote kwa ujumla tumekuwa tukizungumzia mambo makubwa manne.

(i) Filamu hii inatuchafua;

(ii) Filamu hii ina dhamira mbaya dhidi ya nchi yetu;

(iii) Umo uzushi mkubwa; na

(iv) Kuna vitimbakwiri humu ndani.

Mheshimiwa Spika, wasaliti ndani ya nchi yetu wanaotumiwa kwa namna moja au nyingine, Waswahili wanawaita vitimbakwiri. Sasa mimi napenda kuzungumza maeneo makubwa yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, kwa kweli naungana na Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia na ambao hamkuchangia kwamba tunamuunga mkono Rais kwa hotuba

yake dhidi ya jambo hili. Lakini naomba niwapongeze sana Wabunge wenzangu kutoka Kambi ya Upinzani kwa hoja waliyoiona ya kufanya marekebisho katika azimio na mimi kama mtoa hoja, kwa kweli sikuona ubaya wowote katika marekebisho. Nilisimama kwa sababu tu ya taratibu za Kanuni kwamba marekebisho yasibadili sura ya hoja iliyoletwa. Sasa kama azimio langu lilikuwa na vipengele saba, Mheshimiwa Khalifa akaleta vinane na pale ni lazima kwamba masikio yalitaka kuzidi kichwa na hii haiwezekani kwa mwanadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la ukahaba. Mimi ningeomba, tunaopenda kuzungumzia kwa maana ya kumuunga mkono Bwana Sauper tuwe na hadhari na uzalendo. Kuna nchi huko Ulaya Magharibi wana *Square* yao fulani hivi sitaki kuitaja jina, kila siku ya Mungu, kuna malori mawili yanakusanya kondomu hapo. Kuna vijana hawana mahali pa kwenda kufanyia ukahaba, wanafanyia kwenye ile *Square*. Tulitegemea huyu aandike, maana yuko pua na mdomo zaidi kuliko Mwanza.

Lakini Mheshimiwa mwingine amezungumza hapa kwamba, Ulaya kunatolewa leseni za ukahaba na wanapimwa na Madaktari, kana kwamba hiyo haitoshi, hivi sasa Ulaya kuna ndoa za wasagaji. Mwanamke kwa mwanamke wanafungishwa ndoa Mahakamani, wanafungishwa Kanisani. Lakini hivi punde tumeshuhudia Maaskofu wakifungishwa ndoa wanaume kwa wanaume Kanisani. Haya ndiyo mambo tulitegemea yaandikwe. Lakini hayo kwao wameyaweka kando. Sisi tusishabikie mambo ambayo hayana manufaa kwetu.

Mheshimiwa Spika, mapanki, wala sio jambo geni. Kwa kawaida katika biashara, mali nzuri yoyote inakuwa *for export*. Ujerumani wanaongoza kwa ku-*export* nguruwe, lakini ukienda wewe kwenye ile migahawa unakuta kwato na miguu. Ukienda nchi za Ulaya kwenye migahawa, kwa kawaida unakuta kuna vitu vinaitwa shingo, vipapatio wanaviita *chicken wings* na filigisi. Kuku huwezi kula wewe mtu wa kawaida. Hata kwenye viwanda, *rejects* ndizo zinazovaliwa ndani ya nchi zile, zinazotoka vizuri ndiyo zinakuwa *exported.*

Sasa sisi tunashangaa! Kwanza mapanki yenyewe watu wa Mwanza hawayapendi, sio asili yao. Yamekuja kumaliza samaki wao waliokuwa wanawapenda. Kwa hiyo, Mwanza hawali mapanki kwa sababu ya njaa, hawali mapanki kwa sababu ya kukosa samaki, nimetaja asubuhi aina 18 ya samaki wanaopatikana katika Ziwa Victoria.

Suala la silaha limesemwa lakini hakuna ushahidi. Lakini angalieni vyombo vyetu vya habari. Marekani ikitawala, *Republican* kunakuwa na kitu kinaitwa *United States Information Services* (*USIS*). Ikija ikitawala *Democrat* inakuwa *United States Information Agency* (*USIA*), chombo kile kile kinabadilika kutoka *USIS* kuwa *USIA* na kazi kubwa ni kuvitawala vyombo vikubwa vya habari, *CNN*, *Sky News*, *BBC,* kazi yao kubwa ni hiyo, kuvitawala. Ndiyo maana leo watu wanakufa kweli kweli Mashariki ya Kati. Vyombo vile vinaonyesha ubaya wa *Hezbollah*. Havizungumzii ubaya wa wanaotengeneza silaha wala wale ambao wanawasaidia wanaowaua Waarabu, wanaowaua wananchi wa Afghanistan, vimekaa kimya. Lakini hapa kwetu likitokea

jambo dogo, wao ndio wa kwanza kushika bango. Uzalendo kwanza, baadaye pesa. *(Makofi)*

Tuna *CNN*, *Sky News*, *BBC*, *Deutch Velle*, hakuna hata siku moja wanaandika maovu ya nchini kwao. Hata hiyo *BBC* ambayo inawasikizaji wengi Tanzania kwa Sauti ya Kiswahili, habari wanazotangaza ni za Afrika, sio za kwao na ukimwona adui yako anakupigia makofi katika jambo lako, hilo jambo liache. Sio zuri, halina manufaa kwako. Raha ya adui yako anune kwa jambo lako, unajua jambo langu mimi zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwape pongezi wananchi wa Mwanza kwa maandamano waliyoyafanya tarehe 5/8/2006 kumuunga mkono Rais. Nitumie njia hii kuwakumbusha Watanzania kwamba, ingawa picha ile imechukuliwa katika mandhari ya Mwanza, lakini tumedhalilishwa Watanzania, sote Bara na Tanzania Zanzibar.

Kwa hiyo, wananchi wa Mwanza hawakujifanyia jambo lile wao wenyewe tu, wamelifanya kwa niaba ya Watanzania wote na kwa kweli kama kuna Watanzania wawe ni jumuiya ya chama au nini, wakijisikia kufanya jambo hili wala hawajachelewa, ni haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tumekubaliana kwamba yanapotokea masuala haya ya kitaifa tuwe tunashirikiana, ningeomba nilizungumzie kidogo. Mimi nakubaliana sana na jambo hili kwamba sisi wote ni watu wa Taifa moja, ni lazima tukutane. Mimi nafikiri kwa bahati mbaya tulimwelewa vibaya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Yeye hakuwaita Wabunge wa CCM kwa nafasi yake kama Waziri Mkuu. Aliita kama Mwenyekiti wa Chama kwa Kamati ya Wabunge wa CCM. Sasa hii kofia nyingine ndiyo imeharibu ikaleta mazingira haya. Kama asingekuwa Waziri Mkuu asingepata matatizo haya kwa sababu na wenzetu nao wanaitana vile vile.

Sasa mimi naomba, kama lilikuwa linaeleweka vibaya hili la Waziri Mkuu, hili alituita sisi kama wananchama wa Chama cha Mapinduzi na yeye kama Mwenyekiti wetu. Lakini nashukuru kwamba baada ya Kambi ya Upinzani nayo kukaa, CCM wamekaa kuonesha kwamba Wabunge sisi ni watu wenye busara, tumekubaliana na azimio litakalotoka hapa ni la Wabunge wote bila kujali itikadi zetu za Chama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, unajua wakati umetupa kazi mimi na Mheshimiwa Khalifa tukalipitie lile azimio, mimi nililazimika kukaa pale niendelee kusikiliza, lakini nimelipitia na nimekubaliana na Mheshimiwa Khalifa kwamba linakidhi hoja ya Bunge linaloongozwa na Spika mwenye viwango na kasi. Sasa kwa sababu sikuwepo katika kuliandaa kwa dakika ya mwisho, nimelisoma tu kwa haraka haraka, sikujiandaa, ili nisipoteze kiwango cha Bunge, azimio hili ninaomba lisomwe na *Attorney General* ambaye alikuwa ananiwakilisha kule.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa mtoa hoja. Namwita sasa Mwanasheria Mkuu ambaye yeye ndiyo alikuwa anaratibu mazungumzo ya pande mbili kufikia azimio hilo.

**MWANASHERIA MKUU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi hii ili kuweza kutoa Azimio la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu filamu iitwayo *Darwin's Nightmare*.

KWA KUWA wakati akilihutubia Taifa mnamo tarehe 31 Julai, 2006 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete alizungumzia pamoja na mambo mengine, filamu iitwayo *Darwin's Nightmare,* iliyotengenezwa na Mwandishi wa Habari anayeitwa Hubert Sauper anayeishi Ufaransa;

NA KWA KUWA maudhui ya filamu hiyo ya *Darwin's Nightmare* yamelenga kuonesha kwamba uvuvi wa samaki aina ya sangara katika Ziwa Victoria unafanyika kwa njia isiyo salama na uuzwaji na usafirishwaji wa minofu yake kwenda katika Soko la nchi za Ulaya kumesababisha majanga mbambali kwa wananchi waishio katika Ukanda wa Ziwa Victoria;

NA KWA KUWA filamu hiyo inaonyesha kwamba wananchi waishio Ukanda wa Ziwa Victoria hawafaidiki na biashara hiyo ya samaki na badala yake wanaambulia mabaki ya samaki hao maarufu kwa jina la mapanki;

NA KWA KUWA filamu hiyo inakusudia kuonyesha taswira ya Jiji la Mwanza kwa kutumia makambi ya uvuvi pamoja na vijiji kadhaa ili kubainisha umaskini uliokithiri na uchafuzi wa mazingira uliopindukia katika Ziwa Victoria;

NA KWA KUWA filamu hiyo inajenga dhana isiyokuwa na ukweli ya kuoanisha ishara hiyo ya minofu ya samaki na kuwepo kwa ulevi na ukahaba uliosababisha kuenea kwa ugonjwa hatari wa UKIMWI katika eneo hilo;

NA KWA KUWA filamu hiyo imetamka kwamba ndege zinazohusika na ubebaji wa minofu kutoka Mwanza huwa zinaleta silaha hapo Mwanza na kwenda kwenye Nchi za Maziwa Mkuu kuchochea vurugu na vita, jambo ambalo ni la uzushi na uzandiki;

NA KWA KUWA takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba minofu ya samaki iliyouzwa katika Soko la Ulaya ni samaki wa aina ya sangara pekee ambao ni asilimi 17 ya samaki wote wanaovuliwa katika Ziwa Victoria upande wa Tanzania;

NA KWA KUWA zipo hatua madhubuti zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kwa ajili ya kuweka mazingira bora ya uvuvi katika Ziwa Victoria, kuhifadhi mazingira au kuwaendeleza wananchi kiuchumi na kijamii;

NA KWA KUWA maudhui ya filamu ya *Darwin's Nightmare* yana nia mbaya kwa nchi yetu na watu wake na kwamba yanalenga kuharibu Soko la Minofu ya Samaki

aina ya Sangara iliyoshamiri katika nchi za Ulaya na hivyo kuathiri uchumi na ajira ya Watanzania;

NA KWA KUWA lengo lingine la filamu hii ni kutia dosari jina zuri la Tanzania katika Afrika na Jumuiya ya Kimataifa kuhusu nafasi yake ya usuluhishi wa migogoro na kuleta amani Afrika na Duniani kote kwa kudai kwamba eti Mwanza ni Kituo cha kueneza silaha katika nchi za Maziwa Makuu zinazoletwa na ndege zinazokuja kuchukua minofu ya samaki;

NA KWA KUWA kwa ujumla filamu hiyo inawadhalilisha Watanzania katika macho ya ulimwengu na kuharibu sifa na jina zuri la nchi yetu.

HIVYO BASI, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Nne kwa mujibu wa kanuni ndogo ya pili ya kanuni ya 43 ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004 linaazimia kwamba:-

(i) Tunaungana na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Watanzania wote katika kulinda hadhi, heshima uhuru wa Taifa letu na utu wa Watanzania dhidi ya uzalilishaji wa aina yoyote ile; *(Makofi)*

(ii) Tunaomba Serikali iendelee kufuatilia tuhuma zilizotolewa hasa kuhusu uingizwaji wa silaha nchini;

(iii) Tunaiomba Serikali ichukue hatua muafaka ya kuweka masharti yaliyo bayana ya utengenezaji wa kazi kama hizi ili isiwe rahisi kwa wale wenye nia mbaya kuweza kuhatarisha usalama wa nchi yetu na ichukue hatua ya kinidhamu endapo kuna watumishi waliozembea katika suala hili; *(Makofi)*

(iv) Kumkaripia mtunzi na mwandishi wa filamu ya *Darwin's Nightmare* kwa kutumia vibaya uhuru wake na kukiuka miiko ya Uandishi wa Habari;

(v) Kumkaripia mwandishi wa filamu wa *Darwin's Nightmare* kwa njama zake kutaka kuharibu fursa ya Tanzania katika biashara ya minofu ya samaki katika soko la Ulaya;

(vi) Kumkaripia mwandishi wa filamu ya *Darwin's Nightmare* kwa kutoa taarifa za uongo, uchonganishi na uzandiki kwa nchi yetu kwamba biashara ya minofu ya samaki ina uhusiano na uingizwaji wa silaha katika nchi za Maziwa Makuu kupitia Jiji la Mwanza isivyo halali;

(vii) Kumkaripia mwandishi wa filamu ya *Darwin's Nightmare* kwa kueneza uongo na kuharibu sifa ya nchi yetu na watu wake kwa mambo yasiyo ya ukweli;

(viii) Kuvitabainisha Vyombo vya Habari vya nchini na wananchi kwa ujumla kuweka mbele uzalendo na maslahi ya kitaifa wanapotumia uhuru wao wa kutoa maoni yao na kwa upande wa Vyombo vya Habari tunasisitiza viendelee kuwaelimisha wananchi kuzingatia uhuru na maadili ya kazi zao;

(ix) Tunashauri Serikali ione uwezekano wa kutengeneza filamu mbadala kuhusu hali halisi ya biashara ya minofu ya samaki katika Ziwa Victoria upande wa Tanzania; na

(x) Mwisho tunaomba Watanzania wawe macho wakati wote, kwani katika mazingira ya leo, watatokea watu wasioitakia mema nchi yetu, watakaojaribu kupiga vita jitihada zetu za kujenga Taifa letu, watakaotaka kudhoofisha maslahi ya Taifa letu na kwamba tukiwa macho tutaweza kuzifichua njama hizo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitoliwa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio Binafsi kuhusu Filamu ya Darwin's Nightmare lilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninashukuru sana, Azimio limepitishwa kwa kauli moja. Ninayo mambo machache ya kusema. Kwanza, ningependa nieleweke kwamba, nilipozungumzia juu ya kazi za pamoja za Vyama vya Siasa nje ya Bunge, sikuwa nahoji uhalali wa *caucus* za Vyama. Lakini sisi ni nchi ambayo sijui nani amesema, hatuhitaji kuiga kila kitu bila kuboresha. Kwa hiyo, ikubalike *caucas* zipo, lakini pia isikataliwe pale inapobidi, vyama vyote vikae pamoja nje ya Bunge. Ndio ninachosema tu na hii haiathiri kitu chochote, wala haitupunguzii chochote kabisa kwenye masuala ya msingi. *(Makofi)*

La pili, ni kwamba, sasa hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, itawasilishwa saa 11.00 na itaendelea hadi Jumatatu Saa 7.00 mchana, kwa maana ya kuipitisha. Kwa hiyo, ukijumlisha jioni ya leo na nusu siku ya Jumatatu, ndio naye amepata siku moja.

Tunaposambaa, walioomba kuchangia wapo wanane wajijue tu; Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi na Mheshimiwa Raynald A. Mrope. Nimeona niwataje kwa sababu tunaanza saa 11.00 na wasingeweza kujiandaa. Nimewataja kwa mtiririko huo.

La tatu, ninalotaka kusema ni kutangaza tu kwamba, kulikuwa na Vikao vya Kamati vilitakiwa vifanyike Saa 5.00, Wenyeviti waliitikia wito wa Spika, wameahirisha. Kwa hiyo, Kamati ya Uwekezaji na Biashara, sasa itakutana saa 7.00 mchana Chumba Namba 231, mara baada ya kuaahirisha. Kamati zile mbili za *PAC* na *LAAC*, nazo zitakutana chumba namba 431 kwa mchana huu.

Waheshimiwa Wabunge, nataka nimalizie jambo moja, ambalo lilinisikitisha sana, nilitaka niliandikie Waraka niusome hapa, lakini naomba nilieleze tu. Moja ya makundi rasmi ya Waheshimiwa Wabunge, walipokutana katika kikao chao ambacho mimi sikuwepo, kwenye mengineyo, walihoji hatua ya Spika kulipeleka suala la Mheshimiwa Adam K. A. Malima, Mbunge wa Mkuranga na *IPP Media* kwenye Kamati ya Maadili.

Kwanza, nadhani niseme tu, mimi nilivyo, ni vizuri kama kuna jambo linazungumzwa na linanihusu mimi binafsi au kama Spika, chama chochote, waniite ili niweze kuwepo na kuweza kuchangia. Vinginevyo, Mamlaka ya Spika ndio yanawezesha kuendesha vikao humu. Yakimong'onyolewa au yakianza kutafunwa tafunwa, itakuwa ni tabu sana katika kuendesha shughuli zetu. Kibaya zaidi, baadhi ya watu ambao nawafahamu na mahiri sana, walifikia hatua ya kusema Spika kavunja Katiba. Sasa, naomba niwasomee Ibara inayolinda uhuru wa mawazo ndani ya Bunge. Kuwasaidia tu, Waheshimiwa Wabunge, Ibara hii ya 100, inasema hivi: "Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano au katika Mahakama au mahali penginepo…" Nadhani hawa waliishia hapo, wakayaacha maneno matatu muhimu: "Penginepo nje ya Bunge." Tofauti ni kubwa sana hii.

Waheshimiwa, tukichukua tafsiri kwamba tunayoyasema humu, tunalindwa dhidi ya sheria yoyote, ni makosa. Si kweli, hakuna uhuru wa mawazo usio na mipaka chini ya Katiba. Sisi ni wananchi wa Tanzania, hatuko juu ya wananchi. Tusichukulie kwamba, kuchaguliwa kwetu hapa, sasa sisi tumekuwa juu ya wananchi. Mamlaka yetu kwa Ibara nyingine ya Katiba, yanatokana na wananchi. Kwa hiyo, hatuna haki inayowazidi wananchi. Natoa maelekezo haya, ambayo mtu anayetaka kuya-*challenge*, ziko taratibu kwenye Kanuni.

*Ruling* yangu ni kwamba, mwananchi yeyote au mkaazi wa Tanzania au Taasisi ya Tanzania, ikiona haikutendewa haki na matamshi yoyote ya Mheshimiwa Mbunge humu ndani, mwananchi huyo mkazi au Taasisi, wana haki ya kuleta malalamiko yao kwa Spika. Ndio maana basi tuna utaratibu ndani ya Kanuni wa kushughulikia malalamiko kama haya. Kwa hiyo, tofauti tu na watu wengine ni kwamba, Mbunge hawezi kushtakiwa mahakamani kwa yale aliyoyasema Bungeni. Hawezi kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Lakini, Katiba imeweka utaratibu ambao umechukuliwa ndani ya Kanuni kwamba, kwa hayo anayoyasema, anawajibika kwa Spika, kwa utaratibu wa ndani ya Bunge. Kwa hiyo basi, vinginevyo hata zile taratibu za ndani ya Kanuni, zitakuwa hazina maana. Ndio maana Spika, anaweza kumtaja na Mbunge yeyote anaweza kumwomba Mbunge athibitishe lile analosema.

Sasa uhuru huu ungekuwa asilimia mia moja, ingekuwa unaruhusiwa kusema uongo, Mbunge unaruhusiwa kutukana, Mbunge unaruhusiwa kuwasema walio nje ya Bunge hili, hawawezi kujitetea. Haiwezekani hivyo. Kwa hiyo, uamuzi wangu wa kulipeleka suala la Mheshimiwa Adam K. A. Malima, si kwamba nimemhukumu. Nimetimiza wajibu wangu kwa nchi yangu kama Spika kwamba, mwananchi au Taasisi imelalamika, Mbunge naye kalalamika, mahali pazuri na wengi wanadhani eti Kamati ya Maadili maana yake ni kudhibitiwa.

Kamati ya Maadili sio kudhibiti tu, kwa Kanuni za Bunge, Mheshimiwa Spika amepewa Mamlaka ya kulipeleka jambo kwenye Kamati yoyote, anayoona inafaa, ili liweze kupatiwa ufumbuzi, uchunguzi ufanyike na mambo yote yataletwa na uamuzi ndio utachukuliwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hatuna uhuru wa mawazo ambao haudhibitiki kwa namna yoyote. Hata Spika, haruhusiwi hivyo, ndio maana kwenye Kanuni, unaweza kum-*challenge* Spika mwenyewe wa Bunge hili na akizidi, upo utaratibu wa kumtoa madarakani, kwa sababu anaharibu haribu mambo. Kuvunja Katiba ni kosa la kuweza kumtoa Spika kwenye Kiti.

Niseme tu, nimesononeshwa sana. Naomba sana watu wanapotaka kujaribu kujadili mambo yanapomhusu Spika, basi kama ilivyo kwa kikao kinachotaka kutenda haki, asijadiliwe mtu wakati hayupo. *(Makofi)*

Baada ya hayo, nilikuwa nataka kusema tu sasa huo ndio mwongozo wangu. Suala la Mheshimiwa Adam K. A. Malima liko mbele ya Kamati ya Maadili, litashughulikiwa. *IPP Media* hawakukosea kuleta malalamiko ya kile walichoona wamekosewa. Yote yatashughulikiwa na taaraifa tutapewa mbele ya Bunge.

Nashukuru sana, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.10 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa tulikuwa na ile kazi muhimu sana, ambayo tumeimalizia katika kile kipindi cha asubuhi, sasa ninayo heshima kumwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri, ili atoe hotuba yake ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Mheshimiwa Waziri, karibu. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007 – Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuwasilishwa leo asubuhi kwa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, iliyochambua makadirio ya matumizi ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa mwaka 2006/2007, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu, lijadili na hatimaye kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, pamoja na Asasi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuishukuru kwa dhati, Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, chini ya Mwenyekiti wake, mwenye uzoefu mkubwa, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa mchango wake mkubwa ilioutoa wakati ikijadili na kuchambua kwa kina, kwa umakini na kwa umahiri na mwishowe kupitisha makadirio haya. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu imezingatia vilivyo, mapendekezo ya Kamati na inaahidi kuyatekeleza. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda, kwa msingi imara aliouweka na kwa kuiongoza Wizara hii, wakati huo ikiitwa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwekezaji, kwa ufanisi na mafanikio makubwa kwa kipindi chote cha uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii, kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Mwenyekiti Mwenza, Mheshimiwa Job Y. Ndugai na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa umakini na umahiri mlioonesha kwa kazi hii muhimu ya kupitia, kujadili na kupitisha makadirio ya bajeti za Wizara mbalimbali tangu kuanza kwa Mkutano huu wa Bunge la Bajeti, tarehe 13 Juni, 2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, napenda kutoa shukrani zangu nyingi kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, akiwakilisha Mkoa wa Kilimanjaro, kwa mchango wake mkubwa katika maandalizi ya bajeti. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu kwa Katibu Mkuu, Dr. Enos S. Bukuku na Naibu Katibu Mkuu wake, Dr. Stergomena Tax-Bamwenda, Wakurugenzi, Viongozi wa Asasi na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kwa juhudi na ushirikiano wao, uliowezesha kutekeleza malengo tuliyojiwekea kwa ufanisi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2005/2006 na pia kukamilisha kwa wakati, maandalizi ya makadirio ya mwaka 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza kwa dhati, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kwake kwa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, hapo tarehe 25 Juni, 2006. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Yusuf R. Makamba, kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na Katibu Mkuu wa CCM na wote walioteuliwa kuunda Sekretarieti ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mwisho, napenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza kwa mara nyingine, Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa wawakilishi wa wananchi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kufuatia Uchaguzi Mkuu

wa mwaka 2005. Hii inatokana na imani waliyonayo wananchi, juu ya uwezo wenu wa uwakilishi kwao. Kutokana na ushirikiano mzuri uliopo miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge na kutokana na dhamira ya Serikali ya Awamu ya Nne ya kushughulikia kero za wananchi kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya, nina matumaini makubwa kwamba, Bunge hili litatimiza matarajio ya wapiga kura na wananchi wote kwa kiwango cha hali ya juu. Aidha, napenda kuwashukuru kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu, wapigakura na wananchi wa Jimbo la Ulanga Magharibi, kwa kunipa heshima ya kunichagua kuwa Mbunge wao, kwa mara ya tatu mfululizo. Nawaahidi utumishi makini na mahiri kwa kadri ya uwezo wangu wote. *(Makofi)*

Aidha, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa imani yake kwangu kwa kunipa fursa ya kuiongoza Wizara hii. Namuahidi utumishi uliotukuka, makini na wenye unyenyekevu na heshima. Vile vile, napenda kumshukuru mke wangu na watoto wangu, kwa kuniunga mkono kwa saa zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne, ilifanya marekebisho makubwa katika Muundo wa Serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa majukumu yaliyo mbele yake na pia kuharakisha upatikanaji wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Kutokana na marekebisho hayo, Muundo wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji umepanuka na kuwa na idara na majukumu mengi zaidi kuliko hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ni pamoja na kuishauri Serikali na Taasisi zake juu ya masuala ya kiuchumi na kijamii; kuandaa Miongozo ya Mpango na Bajeti; kutayarisha Taarifa za Hali ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii; kusimamia na kuweka mazingira bora ya kisera ili kuwezesha Sekta Binafsi kushamiri na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii; na kuratibu mipango ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kwa lengo la kujiletea maendeleo. Majukumu hayo yanatekelezwa kama ilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, MKUKUTA na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Katika kufanikisha majukumu haya, Idara na Asasi zilizoko chini ya Wizara hii, zinashirikiana katika kusimamia utekelezaji wa kazi zifuatazo: -

(i) Kuchambua na kubuni sera za uchumi jumla, kuratibu na kusimamia shughuli za kiuchumi, pamoja na kuandaa miongozo ya uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji;

(ii) Kuchambua na kuandaa sera na mikakati ya sekta ya nje;

(iii) Kuibua na kubainisha fursa kwa ajili ya kuvutia uwekezaji;

(iv) Kuchambua na kufafanua sera na mikakati ya kiuchumi na kijamii kwa ajili ya maendeleo ya kisekta;

(v) Kubuni na kufanya utafiti na uchambuzi wa masuala muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

(vi) Kuchambua na kubuni sera za kuendeleza rasilimali watu;

(vii) Kuchambua, kubuni na kuratibu mikakati na programu za kuongeza ajira;

(viii) Kuweka mazingira bora ili kuwezesha Sekta Binafsi kushamiri na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii;

(ix) Kuchambua sera na mikakati ya maendeleo vijijini;

(x) Kukusanya, kuchambua, kutunza na kusambaza taarifa na takwimu za kiuchumi na kijamii;

(xi) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na kuratibu shughuli za uwezeshaji;

(xii) Kuratibu, kuhimiza na kufuatilia masuala ya kuondoa umaskini; na

(xiii) Kujenga uwezo wa Wachumi, Watakwimu na Maofisa Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo kuhusu majukumu ya Wizara yangu, pamoja na Asasi zake, sasa naomba kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa malengo ya mwaka 2005/06 kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, mafunzo yalitolewa kwa wadau mbalimbali ili kuelimisha jamii kuhusu MKUKUTA. Warsha za kikanda kwa ajili ya kuelimisha Wataalam wa Uchumi na Mipango, pamoja na Maofisa wa Bajeti kutoka Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara, ziliendeshwa ili kuhakikisha kuwa, Mikoa na Halmashauri zinaandaa mipango yake kwa kuzingatia malengo na falsafa ya MKUKUTA. Mafunzo pia yalijumuisha namna ya kuoanisha mfumo wa upangaji mipango kwa kuzingatia malengo ya MKUKUTA katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia ilifanya mapitio ya Mfumo wa Ufuatiliaji wa Hali ya Umaskini *(Poverty Monitoring System)* kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Mapitio hayo yalilenga kuuboresha mfumo huo ili uweze kwenda sambamba na malengo ya MKUKUTA, ambayo ni mapana na ni mengi zaidi. Matokeo ya mchakato huo ni kuandaliwa kwa Mpango Kabambe wa Kufuatilia Hali ya Umaskini *(MKUKUTA Monitoring Master Plan).* Kazi hii ilijumuisha mapitio ya viashiria ili vitumike kupima mafanikio yanayopatikana katika utekelezaji wa MKUKUTA na kurekebisha pale inapobidi. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kukamilika kwa Ripoti ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu *(Poverty and Human Development Report)* ya mwaka 2005, inayoonesha hali halisi ya umaskini nchini. Ripoti hii imewekwa kwenye Tovuti ya Taifa na imesambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge na kwa wadau mbalimbali. Aidha, taarifa mbalimbali zimetafsiriwa kwa Kiswahili na kuchapishwa katika majarida ili kuongeza uelewa wa taarifa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuoanisha Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo *(Opportunities and Obstacles to Development – O&OD)* na MKUKUTA. Kupitia mfumo huu, wananchi katika ngazi za Vijiji hadi Wilaya, wanaweka bayana mipango yakinifu ya utekelezaji wa MKUKUTA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa, bado kuna changamoto nyingi katika juhudi za kuondoa umaskini. Changamoto hizo ni pamoja na upatikanaji wa fedha za kutosha za kugharamia hatua mbalimbali za utekelezaji, zilizoainishwa katika malengo mahsusi ya MKUKUTA, hususan Sekta Binafsi. Sekta Binafsi ina nafasi kubwa katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Wizara imeendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii ili kukuza uelewa wa dhana nzima ya ushirikishwaji wa wananchi katika kubuni mipango na kuitekeleza ili kuboresha hali zao za maisha. Aidha, mifumo bora ya ufuatiliaji katika ngazi ya Mtaa na Kijiji, haijaimarika vya kutosha kuwezesha upatikanaji wa takwimu sahihi za utekelezaji wa MKUKUTA kuanzia ngazi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu ilianza kutekeleza Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania *(Tanzania Mini–Tiger Plan 2020)* ili kuleta msukumo mpya wa kuongeza ukuaji wa Pato la Taifa, kuongeza mauzo ya bidhaa nje, kuongeza ajira na kupunguza umaskini nchini kwa kuzingatia uzoefu wa nchi zilizoko Kusini Mashariki mwa Asia. Shughuli zilizotekelezwa katika mpango huu ni pamoja na kuzinduliwa kwa kampuni ya kuagiza na kukarabati magari, mashine na vipuri mbalimbali *(Tsubasa Renewcar E.A. Ltd.)* na kuanza kwa ujenzi wa eneo maalumu la uwekezaji lililopo Mabibo, Dar es Salaam, linalojulikana kama *The Benjamin William Mkapa Special Economic Zone (BWM -SEZ)*. Aidha, Kamati ya kuanzisha eneo maalum la uwekezaji rasilimali ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT-SEZ),* imeundwa na Serikali chini ya uratibu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Vile vile, Timu ya Wataalam ilitembelea India mwezi Oktoba, 2005 na Mauritius mwezi Mei, 2006 ili kujifunza na kupata uzoefu wa namna ya kuanzisha na kuendesha *ICT-SEZs*. Sheria ya kuanzisha Maeneo Maalum ya Uwekezaji Raslimali *(SEZ Act),* imeanza kutumika baada ya kupitishwa na Bunge lako Tukufu tarehe 18 Februari, 2006 na kuridhiwa na Mheshimiwa Rais mwezi Machi, 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuutangaza mpango huo, semina kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge, ilifanyika tarehe 9 Julai, 2005, kwa lengo la kuwaelimisha juu ya maudhui ya mpango. Kwa pamoja, Waheshimiwa Wabunge, walikubaliana kuwa mpango huo ni muhimu na utachangia kwa kiasi kikubwa, kasi ya ukuaji wa uchumi na kuondoa umaskini. Vilevile, vitabu vya Mpango Maalumu wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania, vimeendelea kugawiwa kwa wadau mbalimbali kwa lengo la kuutangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliendelea na kazi za kuratibu juhudi za kuimarisha mazingira ya kufanyia biashara na uwekezaji, kushiriki katika kufanya mapitio ya sheria na kanuni mbalimbali chini ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA); kuratibu utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji Rasilimali nchini; kuratibu utekelezaji wa Sera ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma; kuwezesha

kufanyika mikutano ya Baraza la Taifa la Biashara *(TNBC),* kwa lengo la kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuratibu jitihada za kukuza Sekta Binafsi; kuandaa utafiti unaolenga kubainisha fursa zilizopo na vikwazo vinavyozuia ukuaji wa Sekta Binafsi na kufanya maandalizi ya kutayarisha Mkakati wa Kuendeleza Sekta Binafsi nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia na wadau wengine, imekamilisha maandalizi ya Mradi wa Biashara Ndogo na za Kati *(Micro, Small and Medium Enterprises Competitiveness Project - MSMEs),* wenye lengo la kuimarisha ushindani wa Sekta Binafsi, kuongeza upatikanaji wa mitaji na kuimarisha mazingira ya kufanyia biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC),* iliendelea kutoa huduma mbalimbali za uwekezaji na kuzitangaza fursa mbalimbali za uwekezaji ndani na nje ya nchi yetu. Katika mwaka 2005/2006, Kituo kilisajili jumla ya miradi 643, yenye thamani ya Sh.1,913,342/=. Kati ya miradi hiyo, 437 ilikuwa mipya na miradi 206 ilikuwa ya ukarabati na upanuzi wa shughuli zilizopo. Mchanganuo wa umiliki wa miradi hii unaonesha kuwa, miradi 330 ilikuwa ya wawekezaji wa ndani, miradi 146 ya wawekezaji wa nje na miradi 167 ya ubia. Miradi hii inatarajiwa kutoa fursa za ajira kwa watu 607,922 baada ya kuanza uzalishaji. Aidha, Kituo kilipokea maombi ya ajira za wageni 1,845, vibali vya uhamiaji 2,087, masuala ya kodi 3,486, uandikishwaji wa makampuni 138, leseni za biashara 157 na maombi ya ardhi 296. Ili kuvutia wawekezaji kutoka nje, Kituo kilifanya semina za uhamasishaji katika nchi za Falme za Kiarabu, Urusi, Singapore, Indonesia, Jamhuri ya Korea, Ujerumani na Sweden. Juhudi hizi zililenga katika kutekeleza mkakati wa kumlenga mwekezaji *(Investor Targeting).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendeleza miradi ya Watanzania na kutoa huduma kwa karibu zaidi kwa wateja, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Kituo cha Uwekezaji Tanzania, kimefungua Ofisi ya Kanda Jijini Mwanza, ambayo itahudumia Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara na Kagera. Ofisi hiyo, kama ile ya Kilimanjaro, itatoa huduma kwa wawekezaji wa nje kwa ajili ya ubia *(Joint Venture);* kuwasaidia katika utayarishaji wa michanganuo inayokubalika ya miradi ili kusaidia upatikanaji wa mikopo kutoka Taasisi za Fedha; kufanya semina na mikutano mbalimbali kwa wawekezaji wa ndani na wananchi kwa ajili ya kukuza ujasiriamali na kuwaelimisha juu ya fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo vile vile kimeendelea kufanya na kusimamia tafiti mbalimbali zenye lengo la kuishauri Serikali na vyombo vya umma, juu ya njia bora za kuboresha hali ya uwekezaji, kukuza uchumi na kuondoa umaskini nchini. Vile vile, Kituo kiliainisha maeneo yenye fursa za uwekezaji nchini ili kuwezesha ubunifu wa mikakati ya kuvutia wawekezaji kwenye maeneo hayo na kuendeleza ujasiriamali nchini. Baadhi ya tafiti hizo ni Utafiti wa Soko la Ajira nchini *(Labour Market Survey),* Utafiti wa Matatizo ya Nishati na Madhara yake katika Uwekezaji na Utafiti wa Uwekezaji Nchini kwa mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2005/2006, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kupitia Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma

*(PSRC),* iliendelea kuratibu zoezi la ubinafsishaji na urekebishaji wa Mashirika ya Umma. Jumla ya mashirika saba, ambayo ni *NMB, Celtel, Tunduru Cashewnuts Processing Co. Ltd., Pugu Kaolin, Light Source Manufacturing Co. Ltd., NAFCO Matadi Farm* na *Tanzania Legal Corporation,* yalibinafsishwa na kufanya jumla ya Mashirika yaliyobinafsishwa kufikia 322 na mali zilizouzwa 647, tangu utekelezaji wa sera hii uanze miaka 13 iliyopita. Zoezi hili limeipatia Serikali jumla ya Sh.88,014,008,264/= na Dola za Kimarekani 291,426,028/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu urekebishaji wa Shirika la Reli Tanzania *(TRC),* mkakati wa Serikali ni ukodishaji wa miundombinu na huduma za reli katika mtandao wa *TRC,* kwa mwendeshaji binafsi kwa miaka 25. Kati ya wazabuni watatu waliowasilisha zabuni zao kukodisha *TRC,* zabuni kutoka Kampuni ya *RITES* ya India, ilitimiza masharti yote na hivyo kushinda. Kupitia ukodishaji huo, mwendeshaji binafsi, atapewa haki za kutoa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo katika mtandao wa *TRC* uliopo hivi sasa. *TRC* inatarajiwa kurekebishwa na mali zilizopo katika miundombinu yake, ikiwa ni pamoja na injini na mabehewa, zitahamishiwa katika kampuni mpya itakayojulikana kama *Railway Assets Holding Company - RAHCO.* Kampuni hii itashughulikia uuzaji wa mali zisizo za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2005/2006, Serikali kwa kupitia Baraza la Taifa la Biashara *(Tanzania National Business Council - TNBC),* imeanzisha Mabaraza ya Biashara ya Mikoa, kwa lengo la kupanua wigo wa mashirikiano na mashauriano kati ya Serikali na Sekta Binafsi ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara katika Mikoa na Wilaya. Mabaraza hayo yameanzishwa katika mikoa 14 ifuatayo: Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Tanga, Kigoma, Mwanza, Kagera, Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Mtwara, Pwani na Dodoma. Aidha, Baraza la Biashara la Zanzibar limeanzishwa chini ya Uenyekiti wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza MKUMBITA kwa lengo la kupunguza gharama za uanzishwaji na uendeshaji wa biashara, kwa kuondoa vikwazo vikiwemo vya kisera, kisheria, kanuni, kiutaratibu na kitaasisi, ambavyo vinakwamisha ukuaji wa Sekta Binafsi. Katika mwaka 2005/2006, MKUMBITA uliendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini ikiwa ni pamoja na: -

(i) Kukamilisha mapitio ya sheria na kanuni mbalimbali kwa lengo la kuimarisha mazingira ya biashara nchini. Sheria na kanuni hizi ni pamoja na Dhamana ya Ardhi ambazo zilianza kutumika mwezi Agosti, 2005 na Sheria ya Kusajili Shughuli za Biashara ya mwaka 2006;

(ii) Kukamilisha uandaaji wa rasimu za Miswada kwa ajili ya sheria mbalimbali kama vile Miswada ya Kuthamanisha Ardhi; Uwakala wa Mali; Usalama Sehemu za Kazi; Fidia kwa Wafanyakazi; Kukuza Ajira na kutoa huduma za kukusanya takwimu; ambayo imekwisha wasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(iii) Kuoanisha na kuhuisha mfumo wa udhibiti wa leseni;

(iv) Kukamilisha upembuzi wa mahitaji ya uboreshaji wa masjala za *BRELA* ili kuwa na masijala za kisasa;

(v) Kuandaa mfumo wa kisheria na kitaasisi ili kulinda ubora, afya na usalama wa mazao ya kilimo na mazao ya asilia ili kwenda sambamba na matakwa ya soko la ndani na nje;

(vi) Kupitia Sera ya Maendeleo ya Kilimo ili kuendana na mahitaji ya kisasa;

(vii) Kufanya mapitio ya mfumo wa sheria za uendeshaji wa kesi za madai;

(viii) Kukamilisha ukarabati wa Jengo la Mahakama - Kitengo cha Biashara Kanda ya Ziwa (Mwanza);

(ix) Kufanya ziara ya mafunzo ya Maofisa wa Mahakama katika Mahakama za India;

(x) Kukamilisha mpango wa mafunzo ya kuwawezesha watendaji katika Sekta ya Umma kutoa huduma bora kwa Sekta Binafsi (kuachana na ukiritimba);

(xi) Kukamilisha maandalizi ya mfumo wa utoaji mafunzo ya tathmini yakinifu za faida na hasara za sera ya sheria na kutoa mafunzo kwa Maofisa wa Serikali na wadau toka Asasi zisizo za Kiserikali;

(xii) Kukamilisha maandalizi ya MKUMBITA Zanzibar; na

(xiii) Kuandaa mkakati wa kuendeleza Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuzingatia umuhimu wa Biashara Ndogo na za Kati katika harakati za kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Biashara Ndogo na za Kati na mafanikio mengi yalipatikana ambayo ni pamoja na: -

(i) Kuzinduliwa kwa Kamati ya Kitaifa ya kusimamia utekelezaji wa Sera ya Biashara Ndogo na za Kati;

(ii) Kuanzishwa kwa Mfuko wa Kuwezesha Kuhimili Ushindani *(SME Credit Facility - SCF),* wenye lengo la kuchangia kukuza biashara na uboreshaji wa bidhaa na huduma zinazouzwa nje ya nchi na zenye mwelekeo huo;

(iii) Kuanzishwa kwa mfuko wa dhamana wenye lengo la kutatua tatizo la kupata huduma za kifedha;

(iv) Kufanya maandalizi ya awali kwa ajili ya kuanzisha Mradi wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo Vijijini ifikapo mwaka 2007/2008;

(v) Kurekebishwa kwa taratibu za kupata leseni za biashara ikiwa ni pamoja na kuondoa ada ya leseni kwa biashara ambazo mzunguko wake haufikii shilingi milioni ishirini; na

(vi) Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia ilikamilisha maandalizi ya Mradi wa Biashara Ndogo na za Kati unaolenga kuwezesha ushindani na uwezo wa Sekta Binafsi kushiriki katika masoko ya ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa sera hii kwa kuanzisha na kuzindua rasmi Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi, kuandaa muundo wa Sekretarieti ya Baraza, kuandaa Mpango wa Utekelezaji kwa mwaka 2006/2007 na kuteua Katibu Mtendaji wa Sekretarieti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2005/2006, Serikali iliendelea kutekeleza Sera ya Idadi ya Watu kupitia Mradi wa Mipango ya Idadi ya Watu. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kuhuisha Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu, kuandaa Mpango wa Utekelezaji na kuhamasisha Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa Serikali na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ili masuala ya idadi ya watu yaendelee kupewa kipaumbele katika mipango ya maendeleo. Aidha, baadhi ya Wilaya ambazo Maofisa Mipango wake walikwisha kupatiwa mafunzo kuhusu kutengamanisha masuala ya idadi ya watu na maendeleo, zilifanyiwa tathmini. Kazi nyingine iliyofanyika ni tathmini ya Mtandao wa Taarifa ya Idadi ya Watu *(Population Information Network),* ambayo inatoa mwongozo wa namna ya kuboresha mtandao huo ili kuongeza upatikanaji wa taarifa kwa matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Ushauri wa Kitaalam, iliandaa Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma za Ushauri wa Kitaalam nchini iliyopitishwa mwaka 2004. Mpango huo unalenga katika kushughulikia matatizo yaliyoainishwa katika sera na kuiendeleza Sekta ya Ushauri wa Kitaalam nchini. Aidha, Sera hii pamoja na Mpango wa Utekelezaji vilizinduliwa rasmi mwezi Juni, 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, iliendelea na jukumu lake la kutoa Mwongozo wa Mpango na Bajeti. Mwaka 2006/2007, ukiwa ni mwaka wa pili wa utekelezaji wa MKUKUTA, Wizara iliwakutanisha wadau mbalimbali kufuatana na

maeneo ya MKUKUTA *(clusters)* na kujadiliana nao kuhusu ugawaji wa rasilimali na maeneo ya kuzingatiwa katika utekelezaji. Mafanikio makubwa yalionekana katika eneo la mazingira, ambapo wadau walikubaliana maeneo ya kushirikiana na hivyo kupunguza mahitaji ya bajeti kutoka shilingi bilioni 30 hadi bilioni 9.4 katika eneo la kudhibiti uharibifu wa vyanzo vya maji na ardhi oevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa, mwaka 2005/2006, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea: -

(i) Kutathmini na kubaini fursa za kuendeleza biashara ya nje pamoja na kufuatilia Maazimio ya Taasisi na Programu za Kimataifa ikiwa ni pamoja na *WTO, AGOA, EPA* na *EBA;*

(ii) Kuchambua na kubainisha fursa za kuchochea maendeleo ya kiuchumi kutokana na ushirikiano wa Kimataifa na Kikanda;

(iii) Kutathmini mwenendo wa uchumi duniani na kubaini ulinganifu wake na maendeleo ya uchumi wa Taifa;

(iv) Kuratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mpango wa Ushirikiano Mpya ili kuleta Maendeleo Barani Afrika *(NEPAD),* ikiwa ni pamoja na kuandaa Mpango wa Utekelezaji wa *African Peer Review Mechanism (APRM),* chini ya Mpango wa *NEPAD;* na

(v) Kuendeleza ushirikiano kati ya nchi zinazoendelea *(TCDC)*, kwa shabaha ya kuongeza kasi ya kuleta maendeleo katika nchi hizo kwa kutumia uzoefu uliopo kati ya nchi na nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia *(Millennium Development Goals - MDGs),* Tanzania iliteuliwa kuwa miongoni mwa nchi kumi za Kiafrika, kutekeleza Kijiji cha Mfano cha Milenia. Mradi wa Kijiji cha Mfano cha Milenia *(Millennium Village Project),* ulianzishwa kwa lengo la kufanya majaribio kuhusu utekelezaji wa Malengo ya Milenia. Kijiji cha Mbola kilichoko Mkoani Tabora, Wilaya ya Uyui, kilichaguliwa kwa kutumia vigezo vya Kijiji chenye msimu mmoja wa mvua na kinacholima mahindi kwenye ukanda wa miombo. Mradi wa Kijiji cha Milenia cha Mbola ulizinduliwa rasmi mwezi Mei, 2006 na Profesa Jeffrey Sachs, Mkurugenzi na Mshauri wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika masuala ya Milenia, chini ya uratibu wa *UNDP* na Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unatekelezwa kwa njia shirikishi, ambapo Umoja wa Mataifa unachangia asilimia 70 ya gharama zote na Serikali inachangia asilimia 20, ambapo wanakijiji wanachangia asilimia kumi. Kwa kuanzia, Mradi utazihusisha kaya 1,000 za Vijiji vya Mbola, Mpenge na Isila zenye wastani wa watu watano kila kaya, lengo likiwa ni kupanuka na kufikia kaya 3,000 kwa muda wa miaka mitano ijayo. Mradi utaanza na shughuli za afya na maji pamoja na kilimo, chini ya

usimamizi wa Wilaya na uratibu wa Mkoa. Mpaka sasa shughuli kubwa zilizofanyika ni kuajiri wafanyakazi pamoja na kutafuta eneo na vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutumia fursa hii kushukuru kwa heshima hii ambayo nchi yetu imepewa na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wa maeneo husika na wananchi kwa ujumla, kufanya kazi kwa bidii ili kufanikisha Mradi huu na hivyo kulinda heshima hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mafanikio makubwa yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya *TASAF,* Serikali imeendelea na utekelezaji wa shughuli za *TASAF* Awamu ya Pili. Mwaka 2005/2006, ulielekezwa katika uhamasishaji wa umma kuhusu Awamu ya Pili ya *TASAF* kupitia vipindi vya redio na televisheni, makala katika magazeti na vipeperushi. Miongozo mbalimbali ya utekelezaji wa Mradi katika ngazi za Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Miji, Vijiji, Kata/Shehia na Kamati za Miradi, iliandaliwa na kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na rahisi. Miongozo hiyo ni pamoja na ya usimamizi wa miradi, uhakiki wa eneo la mradi, uwezeshaji wa kuandaa miradi, kufanya tathmini ya uwajibikaji na ya maandalizi ya mradi wa jamii. Miongozo hii yote inalenga kurahisisha utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na *TASAF.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya utaratibu wa kufanya tathmini ya *TASAF* yameanza kwa kushirikiana na wadau katika Mfumo wa Ufuatialiaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania *(MKUKUTA Monitoring System).* Manunuzi ya vifaa kama vile magari, kompyuta na mashine za kutolea vivuli kwa ajili ya mradi yamefanyika na vifaa hivyo kusambazwa katika Halmashauri zote nchini. Pamoja na shughuli hizo, semina kuhusu Awamu ya Pili ya *TASAF* ziliendeshwa kwa wataalam na viongozi katika mamlaka zote za Miji na Wilaya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, kuanzia Desemba, 2005 na kukamilika mwezi Machi, 2006. Madhumuni ya semina hizo ni kujenga uelewa kuhusu dhana na taratibu za utekelezaji wa Awamu ya Pili ya *TASAF* kwa watendaji katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Miji. Semina hizo ziliwahusu pia Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Viongozi Wakuu wengine wa Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Jumla ya watendaji 1,400 na zaidi ya Wabunge na Wawakilishi 400, wamepata mafunzo hayo. Wataalam katika Halmashauri zote, wameendesha mafunzo kwenye maeneo yao na hivyo kuwawezesha wananchi wengi zaidi kupata ufahamu wa jinsi ya kuibua na kutekeleza miradi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilianzisha Mradi wa Kutoa Mikopo Midogo ikiwa ni hatua mojawapo ya kuendeleza jitihada za kupunguza umaskini wa kipato. Mradi kupitia Asasi za Kifedha, hutoa mikopo midogo kwa wananchi wenye vipato vidogo ili waitumie mikopo hiyo kufanyia biashara na hatimaye kujiongozea kipato. Kipato kikiongezeka ni rahisi kumudu mahitaji muhimu. Huduma hii ya mikopo ya *SELF* ipo katika Mikoa 14 ambayo ni Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Mtwara, Lindi, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mara, Mwanza, Iringa, Mbeya na Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi uliendelea kutoa elimu na uhamasishaji wa jamii, juu ya mbinu bora za kuweka akiba na kukopa ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo nafuu kwa ajili ya biashara ili kujiongezea kipato na kupunguza tatizo la ajira. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Mradi ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 608.5 na hivyo kufanya jumla ya mikopo iliyotolewa tangu Mradi uanze kufikia shilingi bilioni 6.243. Mikopo hii imewafikia walengwa wapatao 37,227, ambao kati yao wanawake ni asilimia 63.

Mheshimiwa Mwenyekiti, urejeshaji wa mikopo iliyotolewa kwa jumla ni mzuri, ambapo wastani wa urejeshaji ni asilimia 95. Vile vile, katika kipindi cha 2005/2006, Mradi uliendelea kutoa mafunzo kwa lengo la kuzijengea uwezo Asasi Shiriki ili ziweze kutoa mikopo na huduma nyingine kwa walengwa kwa ufanisi zaidi. Aidha, watendaji 308 walipatiwa mafunzo haya na hadi kufikia mwisho wa Machi, 2006, *SELF* imekwishatoa mafunzo kwa watendaji 1,402, wakiwemo Maofisa Mikopo, Mameneja wa Mikopo, Wahasibu na Wakurugenzi wa Bodi za Asasi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo *(SACCOS), CBOs* na *NGOs.* Mradi pia ulitoa mafunzo maalumu kwa viongozi wa *SACCOS* ili viweze kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *SELF* kupitia Asasi Shiriki, umegharimia mafunzo ya ujasiriamali kwa walengwa 2,820. Mradi ulifanya tathmini kwa lengo la kupata maoni ya walengwa ili kujua matatizo na mafanikio yaliyopatikana ili kuboresha shughuli za Mradi. Tathmini iliyofanyika imeonesha kuwa, Mradi umeanza kupata mafanikio kutokana na mikopo iliyotolewa. Miongoni mwa mafanikio hayo ni watu kuelewa umuhimu wa mikopo kama njia mojawapo ya kupambana na umaskini, Taasisi za Serikali kutoa ushirikiano katika kuhakikisha kuwa mikopo inawafikia walengwa na kuongezeka kwa Asasi zinazoshirikiana na Mradi katika eneo la Mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu na mingine inayosimamiwa na Serikali, inaendelea kuboreshwa ili kutoa masharti nafuu ya utoaji wa mikopo, kuwezesha wananchi wengi zaidi kufanya biashara mbalimbali kama vile kuongeza uzalishaji wa mazao, usindikaji bora wa vyakula, ufungashaji wa bidhaa na mbinu za kutafuta masoko. Mikakati ya kuwezesha wananchi, imepewa kipaumbele katika MKUKUTA, ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2005/2006, Programu ya Taifa ya Kuongeza Kipato, iliendelea na utekelezaji wa Mradi wa Chumvi huko Pemba, Mradi wa Mama Lishe Dar es Salaam na Miradi ya Ufugaji Nyuki Wilayani Rufiji na Dodoma Vijijini. Baadhi ya shughuli zilizofanyika ni pamoja na kuendelea kutoa mafunzo kwa wafugaji nyuki, kuhusu njia bora za kutunza na kurina asali, pamoja na kununua vifaa vya kisasa. Aidha, *NIGP* iliendelea kukarabati jengo la kuhifadhia chumvi lililoko Chake Chake, Pemba, pamoja na ununuzi wa mashine za mikono za kuzalishia chumvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2005/2006, Ofisi ya Taifa ya Takwimu iliendelea na majukumu ya kukusanya, kuchambua na kusambaza takwimu. Tafiti zifuatazo zilikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na: Uchambuzi wa takwimu za Sensa ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 2003; Shughuli za

Kiuchumi kwa kipindi cha mwaka 2003 – 2005 na Uzalishaji Mali Viwandani kwa kila robo mwaka. Pia, Utafiti na Uchambuzi wa Nguvu Kazi 2005/2006 *(Integrated Labour Force Survey)* na Uchambuzi wa Utafiti wa Ajira na Mapato kwa mwaka 2002/2003 uliendelea. Hali kadhalika, uchambuzi wa kina wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi 2002 uliendelea. Baadhi ya ripoti zilizotokana na Sensa ya Watu na Makazi zilizotayarishwa na kusambazwa katika kipindi hicho ni pamoja na:-

(i) Mchanganuo wa takwimu katika ngazi ya Kijiji zilizojumuisha mgawanyo wa Kijiji/Mtaa, kiumri, kijinsia, watoto yatima, kaya ambazo wakuu wake wa kaya ni watoto wenye umri chini ya miaka 17 na hali ya uraia;

(ii) Mchanganuo wa hali ya kiuchumi na kijamii katika ngazi ya Taifa;

(iii) Makadirio ya Idadi ya Watu katika ngazi ya Taifa katika kipindi cha mwaka 2003 hadi 2025; na

(iv) Mchanganuo wa vifo vya watoto wachanga chini ya mwaka mmoja na watoto chini ya miaka mitano, kwa Wilaya zote 129 za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Utafiti wa Afya ya Mama na Mtoto 2004/2005, uliendelea na ripoti ilikamilika na kusambazwa kwa wadau mbalimbali, sambamba na Ripoti ya Takwimu za Mazingira Tanzania. Uchambuzi na utayarishaji wa ramani kwa kutumia kompyuta *(Digitized Geographic Information System),* uliendelea ambapo ramani za Mkoa wa Pwani na Wilaya za Same na Mwanga katika Mkoa wa Kilimanjaro zilikamilika. Tafiti hizi, pamoja na nyinginezo, zitatoa vigezo vitakavyotumika kutathmini hali ya kijamii na kiuchumi katika kutekeleza malengo ya Kitaifa kama ilivyoainishwa kwenye MKUKUTA. Hali kadhalika, Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wapo katika hatua za mwisho za kuandaa Mkakati wa Kuboresha Ukusanyaji wa Takwimu nchini *(Tanzania Statistical Master Plan).* Vile vile, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imekuwa mstari wa mbele katika kuunganisha na kuzihakiki takwimu, pamoja na kuandaa kitabu ambacho kinatumika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC Facts and Figures).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2005/2006, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, imeendelea kuboresha Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Dodoma, pamoja na Chuo cha Takwimu cha Mashariki mwa Afrika ili viweze kutoa Wataalam wa Mipango na Takwimu wa kutosha. Vyuo hivyo vimeendelea kupanuliwa kwa kuongeza na kukarabati miundombinu yake, kuajiri wakufunzi na kupatiwa vitendea kazi ili kukidhi mahitaji ya vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, kiliendelea na awamu nyingine ya ujenzi wa bweni la wanafunzi, ambapo Awamu ya Pili imekamilika hivyo, kupata jumla ya vyumba 94 ambavyo vina uwezo wa kuchukua wanafunzi 282. Aidha, michoro ya majengo ya Maktaba na Taaluma ikiwa ni pamoja na

taratibu za kuwapata Makandarasi wa Ujenzi wa majengo hayo, zimekamilika. Kwa upande wa taaluma, jumla ya wanafunzi 87 walihudhuria Mafunzo ya Cheti, 156 Stashahada ya Juu katika Mipango ya Mazingira na 138 Stashahada ya Juu katika Mipango ya Mikoa, 44 Stashahada ya Uzamili katika Mipango ya Mikoa na 20 Stashahada ya Uzamili katika Mipango ya Mazingira. Jumla ya wanafunzi 203 walidahiliwa katika Mafunzo ya Shahada ya Kwanza katika fani mbalimbali kama ifuatavyo: 72 Mipango ya Maendeleo ya Mikoa, 69 Mipango na Usimamizi wa Mazingira na 62 Mipango ya Idadi ya Watu na Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yanayokikabili Chuo cha Takwimu cha Mashariki mwa Afrika, yanapatiwa ufumbuzi kwa awamu kulingana na uwezo wa bajeti ya Serikali. Katika mwaka 2005/2006, Chuo kilichimba kisima cha maji, hivyo kutatua tatizo la maji chuoni hapo. Ili kutatua tatizo la umeme, taratibu za kununua jenereta zinakamilishwa. Aidha, Wizara inafanya mawasiliano na Wizara za Miundombinu, Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, pamoja na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni katika kutatua tatizo la barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2005/2006, Chuo cha Takwimu cha Mashariki mwa Afrika, kiliendesha mafunzo katika ngazi ya Cheti na Stashahada ili kuboresha ukusanyaji, uchambuzi, utunzaji na matumizi ya takwimu. Katika mwaka huo, Chuo kilikuwa na jumla ya wanafunzi 57, kati ya hao sita ni kutoka Afrika ya Kusini, watatu Sudan, 37 Tanzania Bara na 11 Tanzania Zanzibar. Wanafunzi 19 kutoka Tanzania Bara walikuwa ni waajiriwa wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, waliofadhiliwa na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji katika Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Kukusanya na Kuchambua Takwimu za Kiutawala chini ya MKUKUTA. Chuo pia kiliendesha mafunzo mbalimbali ya muda mfupi kwa ajili ya waajiriwa 75 wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tovuti ya Taifa imeendelea kuboreshwa kwa kuongeza upatikanaji wa taarifa na kwa wakati. Tovuti imesaidia kwa kiasi kikubwa, kusambaza taarifa muhimu kwa wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa haraka na kwa usahihi zaidi. Katika mwaka 2005/2006, kazi ya kuhuisha na kupitia upya mfumo uliopo na taarifa mbalimbali iliendelea. Aidha, utengenezaji wa mfumo mpya na uingizaji wa taarifa kwenye mfumo huo unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kutumia njia mbalimbali, zikiwemo ukarabati wa majengo na ununuzi wa samani na vitendea kazi. Kazi ya ukarabati wa jengo la Wizara iliendelea, ambapo shughuli ya kuweka vifaa vya usalama kama vile, vifaa vya zima moto na kamera za usalama imekamilika. Hali kadhalika, ukarabati wa jengo la Ofisi ya Taifa ya Takwimu sehemu ya ghorofa ya kwanza unaendelea. Aidha, Wizara imewapeleka watumishi wake 17 kwenye mafunzo ya muda mrefu na watumishi 22 kwenye mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi. Ili kukidhi mahitaji ya muundo wa utumishi Serikalini, Wizara yangu imewapeleka watumishi tisa kwenye mafunzo ya Elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu pia itaendelea kuelimisha na kuhamasisha wananchi kuhusu MKUKUTA. Njia zitakazotumika ni pamoja na Vyombo vya Habari, vipeperushi, Midahalo ya Kitaifa, kuandaa mijadala ya kisekta na kuendesha mafunzo na semina kuhusu MKUKUTA kwa wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge. Aidha, Wizara itaandaa ripoti mbalimbali zinazohusu jitihada za Serikali katika kupambana na umaskini ikiwa ni pamoja na taarifa ya utekelezaji wa MKUKUTA *(MKUKUTA Implementation Progress Report)* na Taarifa ya Hali ya Umaskini *(Poverty Status Report).* Ripoti zote hizo zitasambazwa kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuwekwa kwenye Tovuti ya Mfumo wa Ufuatiliaji Hali ya Umaskini *(www.povertymonitoring.go.tz)* na Tovuti ya Taifa *(www.tanzania.go.tz).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Serikali itaweka mkazo katika kutekeleza Mfumo wa Kufuatilia Hali ya Umaskini nchini. Kupitia mfumo huu, kazi kuu zifuatazo zitafanyika: Savei ya Hali ya Matumizi na Kipato katika kaya binafsi. Savei hii itatupatia takwimu za hali halisi ya umaskini katika ngazi ya kaya. Savei kama hii ilifanyika mara ya mwisho mwaka 2000/2001. Savei nyingine itakayofanyika ni ya Hali ya Ajira na pia kufanya uchambuzi utakaotoa hali halisi ya maendeleo katika Sekta mbalimbali. Kazi nyingine itakayopewa kipaumbele ni kuandaa programu ya kutambua watu wenye hali tete na jinsi ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007,Wizara yangu itashirikiana na Sekta mbalimbali, kuainisha gharama zinazohitajika katika kutekeleza MKUKUTA. Hii itarahisisha majadiliano na wadau mbalimbali katika kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania, utaendelea kutekelezwa kwa kuendelea na ujenzi wa Eneo Maalumu la Uwekezaji lililopo Mabibo *(The Benjamin William Mkapa Special Economic Zone – BWM SEZ);* kuunda Mamlaka ya Kusimamia Maeneo Maalum ya Uwekezaji *(SEZs Authority)* na kuanza matayarisho ya ujenzi wa Kituo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT-SEZ)* katika eneo ambalo limetengwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Serikali itaendelea na juhudi za kuutangaza mpango huo, kwa kuchapisha nakala zaidi za vitabu na kuvisambaza kwenye Wizara, Mikoa, ofisi zinazowakilisha Mashirika ya Kimataifa nchini, Sekta Binafsi, pamoja na kwenye Balozi zetu zilizopo nchi za nje ili kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi husussan, kuwekeza kwenye *SEZs.* Katika kutangaza eneo maalum la kwanza nchini la uwekezaji raslimali linalojengwa Mabibo, ripoti na vipeperushi vitakamilishwa ili kuonesha fursa na vivutio vilivyoko kwenye eneo hilo na vitasambazwa ndani na nje ya nchi, kwa lengo la kuvutia wawekezaji kwa wingi hasa pale ujenzi wa miundombinu utakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea na kazi ya kuimarisha mazingira ya kufanyia biashara na uwekezaji, ikiwa ni pamoja na kuratibu utekelezaji wa mradi wa Biashara Ndogo na za Kati, MKUMBITA, Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, Sera ya Uwekezaji Rasilimali; kutayarisha Mkakati wa Kukuza Sekta Binafsi, kuhimiza uanzishaji wa mifumo itakayowezesha uendeshaji endelevu wa biashara ndogo na za kati, kuhimiza na kufuatilia kazi za

uboreshaji wa mazingira ya biashara ikiwemo mapitio ya sheria na kanuni za biashara ndogo na za kati, kufanya utafiti wa kubaini fursa za kukuza uchumi na kufanya utafiti wa kubaini Sekta zenye uwezo wa kuharakisha ukuaji wa uchumi kwa lengo la kuhimiza uwekezaji katika Sekta hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Kituo cha Uwekezaji Tanzania, kitaendelea na juhudi za kutoa huduma mbalimbali za uwekezaji kwa utaratibu wa *One Stop Centre.* Aidha, Kituo kitawahamasisha wawekezaji wa ndani na nje na pia kuwasaidia wawekezaji wadogo wadogo na wa kati *(SMEs),* ili waweze kuandaa miradi inayouzika kwa lengo la kupata mikopo kutoka kwenye mabenki. Kazi ya kutangaza miradi ya *SMEs* itaendelea kwa lengo la kuwatafutia wabia wa ndani na nje. Vile vile, Kituo kitafanya tafiti na kutoa taarifa za Sekta, Mikoa, maeneo na miradi mbalimbali inayohitaji uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo pia kitafungua Ofisi ya Kanda ya Kusini ili kusogeza karibu huduma kwa Mikoa ya Kusini. Kwa upande wa mawasiliano, Kituo kitaanza kutumia mfumo mpya wa *Workflow Management System,* kwa kutumia mtandao wa kompyuta ili kuboresha huduma kwa wawekezaji kwa kutoa taarifa mbalimbali katika muda mfupi. Aidha, Kituo kitaendesha semina za uwekezaji katika nchi za Saudi Arabia, Kuwait, Qatar, Nchi za Falme za Kiarabu *(UAE)* na Yemen. Hali kadhalika semina hizo zitatolewa katika baadhi ya Miji Mikuu ya Ulaya, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)*, nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC),* Nchi za Mashariki ya Mbali na Marekani. Aidha, mkazo upo katika kukamilisha mpango wa kuongeza kasi ya uwekezaji nchini unaofanywa kwa kushirikiana na Wataalamu wa Kampuni ya *A.T. Kearney* na Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC),* itaendelea kushughulikia urekebishaji wa Mashirika ya Huduma, miundombinu na Mashirika yaliyosalia ya kibiashara. Mashirika yaliyo katika hatua mbalimbali za urekebishaji ni pamoja na Shirika la Reli *(TRC),* Shirika la Bima la Taifa *(NIC),* Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA),* Shirika la Posta *(TPC)* na *Marine Services Company,* inayotoa huduma ya usafiri katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Tume pia itaendelea kuzijengea uwezo mamlaka mpya za udhibiti na kusimamia ushindani zilizoanzishwa ili ziweze kutekeleza majukumu yao kama ilivyoainishwa kwenye sheria za kuanzisha mamlaka hizo za udhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza litaendelea kuimarisha mashauriano kati ya Serikali na Sekta Binafsi nchini katika ngazi ya Kitaifa na ya Kimkoa kwa lengo la kuboresha mazingira ya uwekezaji na ya kufanyia biashara. Baraza litafungua Mabaraza ya Biashara ya Mikoa mingine saba, ambayo bado haina Mabaraza hayo. Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Singida, Rukwa, Mara, Tabora, Shinyanga na Lindi. Aidha, Baraza litasimamia uendeshaji wa Mabaraza ya Biashara ya Mikoa kwa madhumuni ya kuyawezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitaifa, Baraza linatarajia kufanya mikutano minne chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Mikutano hiyo ni Mkutano wa Nne wa Baraza *(4th Council Meeting),* Mkutano wa Wawekezaji wa Ndani

na miwili ya Wawekezaji toka Nje *(Investors' Round Table Meetings).* Baraza la Taifa pia litaendelea kushirikiana na Baraza la Biashara la Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kupitia kitengo chake cha *Better Regulation Unit (BRU),* itaendelea kuratibu MKUMBITA. Kazi zinazotarajiwa kufanywa ni pamoja na kuendelea kufanya maboresho ya Sheria na Kanuni za Ardhi; kuandaa na kutekeleza *Geographic Information System* ili kuanzisha masjala za ardhi nchini kote na kurahisisha upimaji wa ardhi. Kazi nyingine ni kutekeleza Sheria za Ardhi ya Vijiji kwa kupima maeneo ya kimila na kutoa hati; kurasimisha rasilimali katika maeneo yasiyopimwa; kuboresha usuluhishi wa migogoro ya ardhi kwa kujenga uwezo wa watendaji wa masuala ya ardhi; kukamilisha uandaaji wa Sheria ya Hifadhi za Jamii na Sera ya Mafunzo na Ufundi Stadi; kutengeneza Vitambulisho vya Taifa; kuandaa mfumo wa usuluhishi muafaka na mbadala wa migogoro ya kibiashara; kutekeleza uboreshaji wa masjala za *BRELA,* kuendelea kutoa mafunzo ya kuwawezesha watendaji katika Sekta ya Umma, kutoa huduma bora kwa Sekta Binafsi ili kuachana na ukiritimba na kutekeleza MKUMBITA Zanzibar katika maeneo yaliyoainishwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Aidha, Wizara itaendelea kutoa msukumo wa pekee na thabiti katika kuendeleza Sekta Binafsi kwa kuweka mazingira bora ya kufanyia biashara na uwezeshaji nchini na kukamilisha Mkakati wa Maendeleo ya Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kuratibu utekelezaji wa mipango mbalimbali chini ya Programu ya Uendelezaji wa Biashara Ndogo na za Kati. Mipango hiyo ambayo itaendelea kutekelezwa na Asasi mbalimbali zilizo chini na nje ya Wizara yangu ni pamoja na kujenga uwezo wa Sekta Binafsi kuongeza thamani na ubora wa bidhaa kwa kuzingatia matakwa ya soko la Kimataifa; kuweka mfumo wa kurahisisha mawasiliano kati ya viwanda vidogo na biashara ndogo; kuimarisha na kuendeleza mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa na takwimu za masoko kwa wajasiriamali; kuimarisha viwanda vidogo na biashara ndogo na kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa Kuendeleza Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Serikali itajenga uwezo wa Wizara na Baraza la Uwezeshaji ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Sera mbalimbali za kisekta na sheria, zitapitiwa upya ili kubaini kama zinaendana na Sera ya Uwezeshaji na kutoa mapendekezo ya maboresho kwa kadri itakavyoonekana inafaa. Serikali inatarajia kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi *(Mwananchi Empowerment Fund),* ambao utatumika kutoa dhamana ya mikopo kwa wananchi kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kiuchumi kupitia mabenki.

Aidha, daftari *(register),* la kuandikisha vikundi mbalimbali vya wananchi vinavyofanya shughuli za kiuchumi, litaanzishwa ili kuweza kufuatilia na kufanya tathmini ya hali ya maendeleo ya kiuchumi. Wizara pia itafanya utafiti ili kuainisha maeneo ambayo yanaweza kutoa matokeo ya haraka ya uwezeshaji ili yaweze kupewa kipaumbele. Serikali pia itaandaa na kufanya midahalo ya namna ya kujenga na kuendeleza kundi la kati kiuchumi *(middle class),* kwa lengo la kuongeza kasi ya ukuaji

wa uchumi nchini na kupanua nafasi za ajira na kuandaa utaratibu bora na wa uhakika wa kufikisha huduma za uwezeshaji na taarifa kwa wananchi kutoka ngazi ya Taifa hadi Kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Wizara itaratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Huduma za Ushauri wa Kitaalam kwa kukiwezesha Chama cha Washauri wa Kitaalamu Tanzania *(TACO)*, ambacho kwa kuanzia, kitakuwa Sekretarieti ya Baraza la Ushauri wa Kitaalam litakaloundwa hapo baadaye. Chama hicho kitajengewa uwezo ili kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Baadhi ya majukumu hayo ni pamoja na kupitia sheria zilizopo na kuzifanyia marekebisho kulingana na maelekezo ya sera na kuainisha mahitaji ya mafunzo kwa washauri wa kitaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea kukusanya na kuchambua takwimu za kiuchumi na kijamii. Aidha, Ofisi itaendelea kuchambua na kufanya tafiti mbalimbali zilizoainishwa, katika Mpango Kabambe wa Kufuatilia Hali ya Umaskini Nchini.

Uchambuzi wa takwimu za Sensa ya Kilimo na Mifugo, tafiti za Shughuli za Kiuchumi na Uzalishaji Mali Viwandani kwa kila robo mwaka, zitaendelea kutoa taarifa mbalimbali zitakazoimarisha mipango na mikakati kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. Ofisi pia, itaratibu uandaaji wa *Tanzania Statistical Master Plan,* utakaowahusisha wadau mbalimbali kama vile, Vitengo vya Takwimu vya Wizara na Asasi zote na watumiaji na wachambuzi wa takwimu katika Vyuo vya Elimu ya Juu. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea kukusanya takwimu za fahirisi ya bei, uzalishaji viwandani na zile za ukadiriaji wa Pato la Taifa. Kazi nyingine zitakazoendelea ni pamoja na utengaji na uingizaji wa maeneo ya kuhesabia watu kwenye kompyuta kama sehemu ya maandalizi ya sensa ya watu na makazi itakayofanyika mwaka 2012; kukusanya na kuchambua takwimu za mazingira na kutayarisha Taarifa za Hali ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii za Mikoa na Hali ya Uwekezaji *(Regional Socio-economic and Investment Profiles).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, tafiti mbalimbali ama zitafanyika au zitafanyiwa maandalizi ya awali kama sehemu ya kukidhi mahitaji ya MKUKUTA. Tafiti zitakazofanyika ni pamoja na: -

(i) Utafiti wa Ajira na Mapato *(Employment and Earnings Survey);*

(ii) Utafiti wa Watu wenye Uwezo wa Kufanya kazi, Ajira kwa Watoto na Matumizi ya Muda *(Integrated Labour Force Survey);*

(iii) Utafiti wa Biashara ya Ndani *(Distributive Trade Survey);* na

(iv) Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi *(Household Budget Survey).*

Tafiti zitakazofanyiwa maandalizi ya awali ni pamoja na Sensa ya Viwanda; Utafiti wa Hali ya VVU/UKIMWI; na Utafiti wa Hali ya Ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea na kazi ya kuratibu, kuboresha na kutayarisha muundo na mfumo wa kisasa unaoendana na wakati. Aidha, kazi ya kuhuisha taarifa mbalimbali zilizopo katika Tovuti ya Taifa itaendelea kulingana na mpango maalum wa kuhuisha taarifa hizo *(content updating plan).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea kuboresha Maktaba yake ili kuifanya iwe ya kisasa zaidi. Baada ya kufanya ukarabati, kununua samani na baadhi ya vitabu, Wizara itaendelea kununua vitabu vingine na majarida mbalimbali ili kukidhi matarajio ya watumiaji. Katika jitihada za kuboresha huduma za Maktaba ili ziwe za kisasa zaidi, Wizara ipo katika hatua za mwisho za kuandaa *on-line catalogue* ili watumiaji wa Maktaba waweze kupata taarifa za machapisho mbalimbali yaliyopo Maktaba kwa kutumia wavuti *(Internet).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, kazi ya kutengeneza Ruwaza ya Uchambuzi wa Uchumi Jumla *(Macro-Economic Modelling)* itaendelea. Madhumuni yake ni kuimarisha na kujenga uwezo wa kubainisha mwelekeo wa mwenendo wa uchumi na hivyo kuboresha utayarishaji wa sera za uchumi jumla na mfumo wa matumizi ya rasilimali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea kufanya utafiti wa shughuli za kijamii na kiuchumi nchini kwa lengo la kuainisha viashiria vitakavyotumika katika kuchambua na kubainisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi yanayotokana na utekelezaji wa programu na mikakati mbalimbali ya kufikia azma ya malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na MKUKUTA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, UKIMWI bado ni janga linaloendelea kuangamiza nguvukazi ya Taifa. Wizara yangu pamoja na Asasi zake, inaungana na Wizara nyingine pamoja na Asasi mbalimbali katika jitihada za kupunguza na hatimaye kutokomeza kabisa maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI sehemu za kazi. Katika mwaka 2006/2007, mkazo zaidi utawekwa katika kuendeleza mikakati iliyopo ya kuwasaidia wale wote watakaokubali kupima afya zao kwa hiari na kugundulika kuwa na virusi vya UKIMWI. Aidha, semina kuhusu janga la UKIMWI kwa wafanyakazi na familia zao, pamoja na wanafunzi walioko katika vyuo ambavyo vipo chini ya Wizara hii, zitaendelea kutolewa. Hali kadhalika Wizara inatarajia kufanya tathmini ya athari za UKIMWI katika uchumi, kutangaza ripoti ya utafiti ya hali ya UKIMWI na Mkakati wa kupambana na UKIMWI katika Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa wafanyakazi walio chini ya Wizara pamoja na kuandaa na kusambaza taarifa kuhusu masuala ya UKIMWI kwa kutumia vipeperushi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali, kupitia Kamati ya Taifa ya Utandawazi, itaendelea kutekeleza Mkakati wa Mapendekezo ya Taarifa ya Utandawazi Wenye Haki. Masuala yatakayotekelezwa ni pamoja na kuendelea kuhamasisha wananchi kuhusu

utandawazi wenye haki ili waweze kubaini vikwazo na fursa zilizoko katika uzalishaji wa kishindani kwa Kisekta, Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Chuo cha Takwimu cha Mashariki mwa Afrika, kitaendelea kutoa mafunzo ya cheti na stashahada kwa watumishi mbalimbali ikiwa ni pamoja na waajiriwa wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Chuo kitaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi ya takwimu kulingana na mahitaji ya wadau na kusaidia kwenye tafiti za kitakwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Dodoma, kitaendelea na upanuzi na uboreshaji wa huduma zake ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa jengo la maktaba, lenye uwezo wa kuhudumia watumiaji 600 kwa wakati mmoja; kuendeleza ujenzi wa jengo la taaluma; kuanza ujenzi wa jengo la ukumbi mkubwa kwa matumizi mbalimbali *(Multipurpose Hall),* lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,500 kwa wakati mmoja na ujenzi wa uzio, kuzunguka chuo. Aidha, Chuo kitaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi, kufanya utafiti na kutoa ushauri na uelekezi kwa wadau wa maendeleo hasa katika ngazi za Vitongoji, Vijiji na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa Kitaifa kuhusu hali ya wataalam ulifanyika kwa mara ya mwisho hapa nchini mwaka 1992, hivyo kwa sasa idadi halisi ya wataalam wa fani na ngazi mbalimbali waliopo nchini haijulikani. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Wizara itafanya utafiti wa Kitaifa ili kujua idadi ya wataalam wa ngazi ya juu na ya kati waliopo nchini na upungufu wa wataalam hao katika fani mbalimbali. Matokeo ya utafiti huo yatakuwa ndiyo msingi wa kufanya makadirio ya mahitaji ya wataalam kwa miaka ijayo. Aidha, matokeo hayo yatasaidia kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Rasilimali Watu ikiwa ni pamoja na kuzishauri Taasisi za Elimu ya Juu kuhusu fani zinazotakiwa kufundishwa na zinazohitajika katika soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kuzipatia ofisi huduma muhimu kama vile maji, umeme, simu, vitendea kazi na mahitaji mengine ya kiofisi. Wizara pia itashughulikia ajira mpya na mbadala na kutoa motisha kwa watumishi ili kuongeza tija katika shughuli za kila siku za Wizara. Kazi nyingine ni kufanya matengenezo ya mitambo na vifaa na ukarabati wa ofisi; kuboresha mazingira ya kufanyia kazi; kutoa elimu ya utawala bora kwa watumishi, na kuwawezesha wafanyakazi kushiriki kwenye michezo mbalimbali ili kujenga afya zao na pia kupata burudani. Pia, juhudi zitaendelea kufanyika kuongeza nafasi za ofisi ili ziweze kukidhi mahitaji halisi kwa kuzingatia ongezeko la watumishi kutokana na kupanuka kwa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itafanya tathmini ili kujua idadi na sifa za Wachumi, Watakwimu na Maofisa Mipango wote ili kubaini mahitaji ya kitaaluma. Matokeo ya tathmini hiyo, yatasaidia katika kutayarisha mkakati wa muda mfupi na mrefu wa kuwaendeleza watumishi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea kutathmini na kubaini fursa za kuendeleza biashara ya nje pamoja na kufuatilia fursa,

Maazimio na Mikataba ya Kimataifa, ikiwa ni pamoja na *WTO, AGOA* na *EU/ACP*; kuchambua na kubainisha fursa za kuchochea maendeleo ya kiuchumi kutokana na ushirikiano wa Kimataifa na Kikanda; kutathmini mwenendo wa uchumi duniani na kubaini ulinganifu wake na maendeleo ya uchumi wa Taifa na kuandaa na kushiriki katika Mikutano ya Kimataifa ya Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi na nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kuratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mpango Mpya wa Ushirikiano ili kuleta Maendeleo Barani Afrika *(NEPAD)* na hasa kuanza utekelezaji wa Mpango wa *African Peer Review Mechanism (APRM),* pamoja na kushiriki katika Mkutano wa Tatu wa Kimataifa wa Tokyo kuhusu Maendeleo ya Afrika *(TICAD III)* na Mpango wa Maendeleo ya Nchi Maskini zaidi Duniani.

Wizara pia itaratibu Ushirikiano wa Kiufundi kati ya Tanzania na nchi zinazoendelea *(TCDC),* majadiliano ya mikataba ya kukuza na kulinda rasilimali kati ya Serikali ya Tanzania na nchi nyingine kwa lengo la kuendeleza uwekezaji rasilimali na kutathmini matumizi ya misaada kwa lengo la kuhakikisha kuwa inakuwa kichocheo cha maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya *TASAF* Awamu ya Pili itatekelezwa katika Wilaya zote za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Katika mwaka 2006/2007, *TASAF* itajielekeza katika kujenga uwezo na uelewa wa wananchi kuhusu suala zima la utekelezaji wa Miradi kwa lengo la kuimarisha dhana ya umiliki wa jamii ili itambue kuwa miradi hiyo ni mali yao na kwa ajili ya maendeleo yao na iwe endelevu. Ili kufanikisha azma hiyo, mikakati inaandaliwa ya kuwafikia wananchi ili kutoa mafunzo zaidi kuhusu taratibu za utekelezaji wa miradi itakayokuwa inafadhiliwa na *TASAF*. Aidha, *TASAF* inatarajia kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi itakayoibuliwa na wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Programu ya Taifa ya Kuongeza Kipato *(NIGP),* itaendelea kukamilisha miradi inayoendelea pamoja na kutekeleza miradi mipya. *NIGP* imepanga kuendelea na ukamilishaji wa shughuli za miradi minne, inayolenga katika kuongeza kipato kwa wananchi. Shughuli zitakazofanyika ni pamoja na kuimarisha jumuiya za wafugaji nyuki na kuwapatia vifaa bora vya kuzalishia asali na nta, pamoja na kutoa mafunzo ya ufugaji bora wa nyuki katika Mikoa ya Pwani na Dodoma.

Aidha, *NIGP* itaendelea na uboreshaji wa mashamba ya chumvi Chake Chake, Pemba na kukamilisha ukarabati wa ghala la kuhifadhia chumvi, pamoja na kukamilisha uwekaji wa mashine za kuzalishia chumvi. Vile vile, *NIGP* itakamilisha utoaji mafunzo kwa Mamalishe wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kupitia jumuiya yao iitwayo Umoja wa Mamalishe Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Mradi wa *SELF* utaendelea na shughuli za uhamasishaji na utoaji wa elimu kwa umma kupitia njia mbalimbali kama vile, Kipindi cha Redio "KOPA UJIENDELEZE", kinachorushwa hewani kupitia Redio Tanzania Dar es Salaam, Sauti ya Tanzania Zanzibar na *Radio Free Africa.* Aidha, vipindi maalum vya Televisheni, warsha za uhamasishaji kwa Madiwani, wadau na

machapisho mbalimbali vitatolewa. Mikakati ya uhamasishaji wa jamii italenga kuwepo kwa huduma ya mikopo kwa wajasiriamali wadogo ili walengwa waweze kunufaika na mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SELF* itaendelea kuzijengea uwezo Asasi za Kifedha, pamoja na wajasiriamali wadogo na kutoa mikopo. Katika utoaji mikopo, kipaumbele kitawekwa kwenye Asasi zinazotimiza masharti ya mikopo hiyo. Aidha, urejeshwaji wa mikopo iliyotolewa na itakayotolewa, utaendelea kuimarishwa ili huduma zitolewazo na *SELF* ziweze kuwa endelevu na hivyo, kuwawezesha wananchi wengi zaidi waweze kukopa na kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu imeazimia kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Mpango wa Bajeti. Watekelezaji watatakiwa kutoa taarifa za utekelezaji kila robo mwaka na taarifa hizi zitapitiwa na Kamati Maalum ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Malengo *(Monitoring and Evaluation Team),* ambayo itatoa mapendekezo yake kuhusu mwenendo wa utekelezaji na bajeti kila robo mwaka na kuchukua hatua za kurekebisha mara kasoro zitakapojitokeza ili bajeti na mipango itekelezwe kufuatana na miongozo inayotolewa. Aidha, Kamati hii maalum itapatiwa mafunzo ya muda mfupi ya namna ya kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, maandalizi ya awali ya kufanya marekebisho ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo yatafanyika pamoja na ukaguzi wa miradi. Lengo litakuwa ni kukamilisha marekebisho hayo na kuanza kutumika kwa mfumo huo katika ngazi zote za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Hali ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii ya Mikoa na Wilaya, mradi huu una malengo makuu mawili; kukusanya takwimu kwa ajili ya kutayarisha vitabu vya Hali ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii katika Mikoa 14 ikiwa ni pamoja na kuanzisha uandishi wa Hali ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii katika Wilaya 20 kwa kuanzia. Utekelezaji wa Mradi huu utasadia wawekezaji kupata taarifa sahihi na hivyo kushawishi uwekezaji zaidi katika Mikoa na Wilaya husika. Lengo la pili ni kuandaa Programu ya Kitaifa inayoelekeza maeneo muhimu ya uwekezaji wa mitaji ya umma na ya binafsi kwenye Sekta mbalimbali na Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuishauri Serikali katika masuala ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa jumla. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, juhudi zitaelekezwa zaidi katika kutekeleza malengo yaliyowekwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Malengo ya Mpango wa Muda wa Kati ya Wizara ni kuhimiza ukuaji endelevu na wa kasi wa uchumi wenye manufaa kwa wote, pamoja na kuboresha ustawi wa jamii ya Watanzania. Katika kutimiza azma hiyo, Wizara itaongozwa na Mpango Mkakati ambao umebainisha wazi Dira, Dhamira, Malengo, pamoja na Mikakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2006/2007, Wizara itaelekeza nguvu zake katika maeneo ya kipaumbele yafuatayo: -

(i) Kuhimiza, kufuatilia na kuratibu masuala ya kukuza uchumi na kuondoa umasikini;

(ii) Kutoa taarifa za kiuchumi na kijamii zilizochanganuliwa juu ya masuala ya maendeleo ili zitumike katika kutoa maamuzi sahihi ya kisera;

(iii) Kuendeleza na kuimarisha mtandao wa taarifa za kiuchumi na kijamii na kuongeza ubora na upatikanaji wa taarifa kwa wakati kwenye Tovuti ya Taifa;

(iv) Kuwapatia watumishi mafunzo ili kuinua uwezo wao katika kuchambua na kuandaa sera pamoja na kufanya tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya kiuchumi na kijamii, kutathmini mwenendo wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kujenga uwezo wa kuendesha mazungumzo, majadiliano na washirika wetu wa maendeleo *(negotiation skills);*

(v) Kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni utunzaji wa mazingira, usawa wa kijinsia, mapambano dhidi ya janga la VVU/UKIMWI na Utawala Bora katika mipango, programu na mikakati ya maendeleo;

(vi) Kukusanya, kuchambua na kusambaza takwimu na taarifa za uchumi jumla kwa ajili ya sera na mipango;

(vii) Kupitia mfumo wa kusimamia na kutathmini viashiria vikuu vya kiuchumi na kijamii;

(viii) Kufanya tafiti mbalimbali za kiuchumi na kijamii; na

(ix) Kuongeza fursa za ajira kwa kuhimiza na kuongeza uwekezaji katika Sekta za Uzalishaji, miundombinu ya kiuchumi na huduma za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha mapendekezo ya bajeti ya Sh.71,930,220,300/= kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, pamoja na Asasi zilizo chini yake kwa mwaka 2006/2007 kwa mchanganuo ufuatao: -

(i) Bajeti ya Maendeleo ni Sh.49,556,908,300/=, ambazo kati ya hizo Sh.12,188,997,000/= ni fedha za ndani na Sh.37,367,911,300/= ni fedha za nje.

(ii) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida Sh.22,373,312,000/=, kati ya fedha hizo, Sh.4,609,312,000/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh.17,764,000,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ADAM K. A. MALIMA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 81 (1) cha Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba sasa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kwa mwaka wa fedha 2005/2006, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijafanya hivyo, naomba nitumie fursa hii, kukipongeza Chama cha Mapinduzi, kwa kukamilisha mchakato wa kupata Mwenyekiti, pamoja na safu nzima ya Uongozi ya Chama cha Mapinduzi. Katika mchakato huo, nadhani nitaeleweka nikipendekeza Bunge lako, liwapongeze wote waliopata nyadhifa mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 29 Mei, 2006, Kamati yangu ilikutana na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma H. Ngasongwa, pamoja na Watendaji Wakuu wa Wizara kutoka idara mbalimbali za Wizara. Kamati yangu ilipata fursa ya kupitia, kuchambua na kujadili taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka 2005/2006 na taarifa ya Shabaha na Malengo ya Wizara hiyo kama ilivyo kwenye makadirio ya matumizi kwa mwaka 2006/2007. Kamati inampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wasaidizi wao wote, kwa kazi nzuri sana na za kuridhisha walizofanya kwa kipindi chote cha mwaka 2005 na matayarisho ya bajeti ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kujadili taarifa hizo, Kamati ilipata fursa ya kuzifahamu Idara mbalimbali za Wizara, Mashirika na Asasi mbalimbali, pamoja na majukumu yake ya kusimamia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, pamoja na Sera na Mikakati ya Kupambana na Umaskini *(Poverty Reduction Strategy)* na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

Kamati imetaarifiwa kwamba, katika kufanikisha majukumu yake katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, ilitengewa jumla ya shilingi 13,761,069,681/= kwa matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,729,543,636/= zilitengwa kwa ajili ya mishahara na shilingi 11,031,526,045/= kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2005/2006, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, ilitengewa kiasi cha shilingi 40,404,626,206/= kwa matumizi ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 5,743,800,000/= zilikuwa fedha za ndani na shilingi 34,660,826,206/= zilikuwa fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imepokea taarifa kwamba, katika kuandaa Bajeti ya mwaka 2006/2007, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, imezingatia mabadiliko ya muundo wa Serikali, ambayo yameongeza majukumu ya Wizara na hivyo kuwepo umuhimu wa kupitia upya malengo, mikakati na kazi zilizo chini ya Wizara. Aidha, katika kutekeleza mpango wa bajeti, Kamati imeelezwa kwamba, Wizara

imezingatia pia malengo ya Ilani ya Uchaguzi na maelezo ya mwongozo ya mpango wa bajeti kwa kipindi cha 2006/2007 hadi 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati imeelezwa kuwa, Wizara itaendelea kuchambua mwenendo wa vigezo na viashiria vya uchumi jumla, kuratibu maandalizi ya hali ya uchumi na maendeleo ya jamii, kuandaa na kufuatilia utekelezaji wa sera za jumla za uchumi na maendeleo ya jamii na kuhamasisha utekelezaji wa malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2000/2005, pamoja na kuchambua na kufuatilia mwenendo wa viashiria na vigezo katika mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini (MKUKUTA).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati imeridhika kwamba, Wizara itaendelea kutathmini na kubaini fursa za kuendeleza biashara ya pamoja na kufuatilia maazimio ya taasisi ya Programu za Kimataifa kama *WTO, AGOA* na kadhalika. Pamoja na kuratibu ushiriki wa Tanzania kwenye mipango mipya ili kuleta maendeleo Barani Afrika kama *NEPAD* na hasa pia kuanzisha utekelezaji wa mpango wa *Africa Peer Review Mechanism*, kushiriki mkutano wa tatu wa Kimataifa wa Tokyo kule Tayca 3 wa Maendeleo ya Afrika na mpango wa maendeleo ya nchi maskini zaidi duniani. Pia Kamati imeridhika kwamba, wanaendelea kutathmini matumizi ya misaada kwa lengo la kuhakikisha kuwa, inakuwa kichocheo cha maendeleo endelevu na kuratibu utekelezaji wa *Tanzania Mini Tiger Plan* 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imepokea Taarifa ya Wizara kwamba, itaendelea kupanua uwigo wa kuainisha masuala ya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo, kuandaa mpango wa utekelezaji wa mkataba wa kuendeleza rasilimali watu, ambayo inaendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo, pamoja na kuandaa mikakati ya kukuza ajira na kuendeleza ajira binafsi, kukamilisha kazi ya kuandaa vigezo vya kitaalam vya kupima mafanikio ya utoaji wa huduma za jamii kwa wananchi katika ngazi za Wilaya, pamoja na kuanzisha mfumo wa utaratibu na usimamizi wa masuala na ufahamu wa utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imepokea taarifa kwamba, katika mwaka 2006/2007, Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma, itaendelea kushughulikia urekebishaji wa mashirika ya huduma na miundombinu na mashirika yaliyosalia ya kibiashara. Mashirika yaliyokuwa katika hatua mbalimbali za urekebishaji ni pamoja na Shirika la Reli, vitengo vilivyosalia vya kibishara vya Mamlaka ya Bandari *(THA)*, Shirika la Bima la Taifa, Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA)*, Shirika la Posta na *Marine Services Company* inayotoa huduma ya usafiri katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhika kwamba, Serikali itaendelea kuimarisha Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini na Chuo cha Takwimu cha Mashariki mwa Afrika. Utekelezaji wa malengo haya, utatoa dira nzuri katika maandalizi bora zaidi ya watalaam wa fani hizi ambao ni muhimu sana kwa taifa letu na utekelezaji wa malengo ya uchumi na ya kijamii ya Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Kamati imetathmini miongoni mwa majukumu makubwa ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

- Kuandaa mipango ya maendeleo;

- Kuandaa miongozo ya bajeti pamoja na taarifa mbalimbali za hali uchumi na jamii;

- Kusimamia na kuratibu mikakati; mipango na *program* yote ya Kitaifa ya kuondoa umaskini, ikiongozwa na mpango wa MKUKUTA na kuoanisha utekelezaji huu na mikakati mingine katika ngazi ya Taifa, Kimkoa na Wilaya, ambao mafanikio ya utekelezaji wa mipango hiyo yana faida za moja kwa moja kwenye Mipango Mikuu ya Kitaifa;

- Kuboresha na kuweka mazingira bora katika utendaji wa kazi na upatikanaji wa nyenzo ili kuwawezesha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza Tanzania na kukua kwa sekta binafsi;

- Kuishauri Serikali katika masuala ya uchumi na kusimamia uendeshaji wa uchumi wa nchi *(Economic Management);* na
- Kukusanya na kuandaa taarifa na kutawanya takwimu za Kitaifa kwa wadau wote wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majukumu ambayo yametajwa hapo awali, Kamati inayo maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Majukumu ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ni makubwa sana. Kama ingekuwa tuna tunalinganisha na kiwiliwili cha mwanadamu, Wizara ya Fedha ingekuwa ni moyo na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ingekuwa ndiyo ubongo wa Serikali. Lakini malengo makuu ya Ilani ya Uchaguzi na Serikali ya Awamu ya Nne na makubaliano ambayo Wizara hii imeingia na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alipokwenda kuitembelea Wizara hiyo, yanaifanya Wizara hii kuwa sawa na kitengo cha kazi kisicholala. Ili Serikali ifikie theluthi ya malengo ya kiuchumi, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, ni lazima itambue kwamba, utekelezaji wa majukumu yao, unataka wao ndiyo wawe mfano mkuu wa ari mpya na kasi mpya Serikalini. *(Makofi)*

Mabadiliko ya kichumi yanayotokea kila siku, yana athari za kiuchumi, kijamii na hata kisiasa na ndiyo maana Kamati inahimiza ufuatiliaji wa Serikali wa mwenendo wa kiuchumi kwa namna ambayo inawezesha uchumi wa Tanzania kuhimili mabadiliko katika thamani za fedha za kigeni *(foreign exchange fluctuations effect)* na athari zake za haraka kwa biashara za nje, mienendo ya bei za bidhaa kama mafuta ya *petrol* na athari zake kwa mfuko wa bei, bei kwenye masoko ya dunia, bidhaa zetu kuu za biashara kama kahawa, pamba, korosho chai, ili Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji au kitengo

husika, kinachotathmini sera ya uchumi, kitumie nafasi yake hiyo ili kutoa mwongozo kwa Mtanzania wa kawaida, ambaye anatakiwa aongozwe kuhusu namna na mazingira ya kufanya biashara katika uchumi unaobadilika kila saa.

Dhana nzima ya uwezeshaji na utekelezaji wake ambao ndiyo msingi mkuu wa mafanikio yanayotarajiwa ya kiuchumi na ya kijamii ya Mtanzania, yanataka yapate majibu katika Wizara hii. Maendeleo ya wananchi walio wengi, msingi wake mkubwa ni kilimo, viwanda vidogo na vikubwa. Katika sekta hizi mbili, ndizo zinazotegemewa kwa kiwango kikubwa katika kuchangia na kukuza Pato la Taifa kwa manufaa ya Watanzania wote. Sekta hizi bado hazijaendelezwa kwa kiwango cha kuzifanya kuwa mihimili mikuu kwa kujenga uchumi ulio imara. Mathalani sekta ya viwanda, inachangia hadi hivi sasa asilimia 9.5 katika Pato la Taifa na sekta ya kilimo inayobeba zaidi ya asilimia 80, inachangia kwa asilimia 5.7 ya Pato la Taifa. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutekeleza azma yake ya kuanzisha Benki ya Kuendeleza Kilimo na Mabenki ya Kuendeleza Viwanda. Serikali ikamilishe utaratibu wa kuipatia *Tanzania Investment Bank* mtaji wa kutosha kwa lengo la kuijengea uwezo wa kiutendaji. Aidha, kutoka na umuhimu wa ufahamu wa dhana ya uwezeshaji kwa Mtanzania wa kawaida, Kamati inaishauri Serikali kuanza mikakati ya makusudi ya kuongeza ufahamu wa uwezeshaji hasa kwa kuwa kuna baadhi wanaamini kwamba, uwezeshaji ni msaada na kwamba fedha au rasilimali hizi si za kurejeshwa. Kamati inasisitiza umuhimu wa suala hili ili wananchi wawe wamejiandaa ipasavyo wakati utekelezaji wa uwezeshaji katika ngazi mbalimbali unaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na hili pia Kamati inasisitiza umuhimu wa ushirikishwaji wa sekta binafsi, Watanzania wa nafasi zote za kiuchumi; wenye vipato vya juu na vipato vya chini, katika *public private partnerships (BPP).* Kamati inaishauri Serikali kuimarisha kitengo cha kutathmini mwenendo wa kichumi sanjari na kuboresha elimu ya uraia kwa Watanzania ili wote tutambue nafasi yetu na uwajibikaji wetu katika kufikia malengo ya uzalishaji, ufanisi, udhibiti na usimamizi wa rasilimali na mali. Ni vyema ikafahamika kwa uwazi kabisa kwamba, jukumu la maendeleo siyo la Serikali peke yake, kila mmoja wetu anawajibika katika kufikia malengo ya maisha ya bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua kubwa zilizofikiwa katika ujenzi wa barabara zetu hapa nchini. Pamoja na mafanikio haya mazuri, Kamati inaishauri Wizara kufanya tathmini ya kina ya mchango wa kiuchumi na manufaa pana *(broad benefits),* yanayotiririka kwa wananchi wa maeneo husika, kwa kukamilisha barabara kuu zinazounganisha Tanzania. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na wadau mbalimbali kuendeleza mawazo na mipango mipya na kuishauri Serikali jinsi ya kuunganisha barabara kuu kati ya Mikoa hususan barabara ya Dodoma - Iringa, Dodoma - Arusha, Dodoma - Manyoni, Itigi, Tabora, Kigoma, Tunduma, Sumbawanga, Mpanda, Kibondo, Mtwara, Tunduru, Songea, mpaka *Mbamba Bay* na barabara ianziayo Dar es Salaam mpaka Mbagala kupitia Mkuranga, Kibiti, Lindi na Mtwara. *(Makofi)*

Kamati imepokea taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa zoezi la ubinafsishaji wa yaliyokuwa mashirika ya umma kuanzia Julai, 2005 hadi Machi, 2006, mashirika yaliendelea kubinafsishwa na kufikia jumla ya mashirika yaliyobinafishwa kuwa 322 na mali zilizouzwa 647 tangu utekelezaji wa sera hii uanze, miaka 23 iliyopita.

Ni maoni ya Kamati kwamba, zoezi hili lingefanywa kwa umakini zaidi, Serikali ingepata mapato mengi zaidi kwa uuzaji wa mashirika hayo, ambayo mengine yameuzwa kwa haraka na kwa bei ya chini kuliko thamani stahili. Kamati inaishauri Serikali, kuzingatia mafunzo yote yaliyokwisha patikana katika ubinafsishaji wa mashirika makubwa yaliyopita. Wakati wa kukamilisha ubinafsishaji wa Shirika la Bima la *(NIC)*, Shirika la Posta *(TPC)*, *Marine Services Limited* na mengine. Aidha, Kamati inapendekeza kwamba, matatizo yanayoikabili *ATCL* na yale ya mikataba ya uongozi wa *TANESCO,* yapate ufumbuzi wa haraka kwa kuwa ni mashirika yenye umuhimu kwa taifa letu na kudhoofika kwa mashirika haya kwa sababu yoyote ile, kunaleta sura mbaya na hasara za kiuchumi kwa taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu urekebishaji wa Shirika la Reli Tanzania, mkakati wa Serikali ni ukodishaji wa miundombinu na huduma za reli katika mtandao wa *Tanzania Railways Corporation,* kwa mwendeshaji binafsi kwa miaka 25 kama ilivyoelezwa na Serikali. Kati ya wazabuni watatu waliowakilisha zabuni zao, zabuni iliyowasilishwa na kampuni ya *RITES* ya India ndiyo iliyoshinda. Lakini kutokana na unyeti wa hali ya juu wa huduma ya reli hivi sasa, hasa kwa kuzingatia kuwa ukamilishaji wa barabara kati ya Dodoma, Manyoni, Itigi na Tabora bado unasuasua, Kamati ina wasiwasi katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, muda wa ukodishaji wa miaka 25 ni mrefu mno, endapo kampuni hiyo itashindwa kutekeleza majukumu yaliyokubalika katika mkataba. Kamati inataka ufafanuzi kwamba, kampuni hiyo itawekeza kwa kiasi gain, *investment structure* na katika maeneo yapi ili kuhakikisha kuwa wanatukabidhi Shirika la Reli katika hali nzuri ya kibiashara, mkataba utakapomalizika. *(Makofi)*

Pili, ni makubaliano gani yaliyofikiwa na kampuni hiyo kuhusu uboreshaji wa viwango vya huduma ya reli kwa usafirishaji wa abiria na mizigo, hususan ni muda gani wa ukodishaji ambapo mabadiliko ya huduma hizi yataanza kuonekana? Watalaam na wafanyakazi wa Kitanzania wanaoendesha shirika hilo hivi sasa, kuna utaratibu gani wa kuwaendeleza *(Human Resource Development),* ili baada ya mkataba kumalizika, Watanzania waweze kuendesha shirika hilo? *(Makofi)*

Tatu, wajibu wa Serikali katika kusimamia na kuhakikisha kuwa mkataba huo unatekelezwa kwa mujibu wa makubaliano, ni vipengele gani ambavyo vipo, vinavyofanya Serikali kujizatiti katika hilo ili historia ya *City Water, ATCL* na mashirika mengine, tuliyopata nayo matatizo, yasijirudie katika mkataba huu wa ukodishaji.

Kwa kuzingatia masuala hayo hapo juu, Kamati inashauri Serikali iridhie kwamba, mkataba wa ukodishaji wa *TRC* uwasilishwe kwenye Kamati hii ya Fedha na Uchumi, kama Kamati husika na *PSRC*, kabla mkataba huo haujaanza kutekelezwa ili

Kamati iweze kuupitia na kuuridhia kama sehemu ya wajibu wake wa usimamizi na ushauri kwa Serikali kwa niaba ya wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Kamati inashauri ifanyike tathimini ya haraka kuhusu Mashirika ya Umma, ambayo hayajabinafsishwa na ambayo yanaendelea kuwa mzigo kwa taifa, kwa kuendelea kuwepo wafanyakazi wakati mashirika hayo hayafanyi kazi. Utaratibu huo utaifanya Serikali ije kuwalipa *Terminal Benefits* kubwa, bila sababu hapo mwishoni. Serikali ichukue hatua ya kukamilisha zoezi la kubinafsisha mashirika hayo. Katika Mkutano wa Bunge wa mwezi Februari, 2006, Bunge lilipitisha Muswada wa Sheria ya Kuweka Utaratibu utakaosimamia uanzishaji na usimamizi wa maeneo maalum ya uwekezaji wa rasilimali *(Special Economic Zones)*. Kamati inapendekeza kwamba, Mamlaka za *SEZ* na *EPZ,* ambazo sheria zake tayari zimepitishwa na Bunge hili zianze kazi.

Serikali itenge maeneo makubwa na ya kutosha kwa ajili ya programu ya *SEZ* na *EPZ*. Eneo kama la *SEZ* Ubungo ni dogo likilinganishwa na mtaji mkubwa na malengo yaliyowekwa kwa ajili ya miundombinu, maji, umeme, barabara mawasiliano na kadhalika. Kamati ingependa kujua, Serikali katika mwaka wa fedha 2006/2007, imetenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu wa *SEZ*? Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya mara moja ili kubaini uwezo wa rasilimali zetu za kuchangia na kukuza Pato la Taifa. Katika rasilimali hizo ni pamoja na mkaa wa mawe Mchuchuma, chuma cha Liganga, *gas* yaani *natural gas* ya *Mnazi Bay* na Songosongo kwa miradi mikubwa na pia kwa miradi midogo, uzalishaji wa bidhaa zisizo asilia kama asali, viungo, mboga mboga, nyama na bidhaa nyingine ambazo zina masoko ya nje. Ili kubaini kwamba ni maeneo gani ambayo yakifanyiwa mkazo wa haraka kwa kuelekeza nguvu za fikra, usimamizi na uwezo wa kiuchumi, Watanzania watajikwamua kiuchumi haraka zaidi.

Kamati inapenda kutenga maoni yake maalum kwa Mradi wa Chuma cha Liganga, ambao una nafasi ya kipekee ya kunyanyua uchumi wa Tanzania. Lakini Wizara husika hazijawasilisha mpango au mkakati wa uhakika wa ni nani na ni lini utekelezaji wa Mradi huu utaanza, pamoja na kwamba utekelezaji wake umetajwa katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005.

Kamati inaishauri Serikali, kuzingatia mafunzo yote yaliyokwisha patikana katika ubinafsishaji wa mashirika makubwa yaliyopita, wakati wa kukamilisha ubinafsishaji wa Shirika la Bima la Taifa *(NIC)*, Shirika la Posta *(TPC), Marine Services Limited* na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhia taarifa ya kwamba, Wizara itaboresha mfumo wa ufuatiliaji wa malengo ya kiuchumi yaliyowekwa na Serikali. Chini ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kuna Mabaraza, Programu na Idara zinazosimamia kwa ujumla malengo mbalimbali ya Wizara hii. Mfano Baraza la Taifa la Biashara, Mpango wa Kuboresha Mazingira, MKUMBITA, programu ya kuendeleza biashara ndogo, programu ya taifa ya kuongeza kipato, mradi wa mikopo midogo midogo, ambayo inaoanishwa na Sera ya Taifa ya Uwezeshaji kama tulivyoambiwa, Sera ya Taifa ya Idadi ya watu, Sera ya Taifa ya Huduma za Ushauri na

kadhalika. Ni maoni ya Kamati kuwa, katika usimamizi wa Mabaraza, Program*u* na Sera, kuna watalaam waliopewa dhamana kubwa na hivyo pamoja na uzuri wa malengo hayo, Kamati inashauri kwamba, ni wakati sasa tutaanza kuomba maelezo ya michango kwa uchumi wetu na maendeleo ya Watanzania yanayotokana na utekelezaji na kuwepo kwa mikakati yote hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha utekelezaji wa kazi za Wizara na asasi zilizo chini yake, Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, anaomba Bunge lako Tukufu, kuidhinisha matumizi ya jumla ya shilingi 71,930,200,300/= kama ifuatavyo: Matumizi ya kawaida shilingi 22,373,312,000/= na Miradi ya Maendeleo shilingi 49,556,908,300/=. Kamati inaomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe maombi haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii sasa, niwapongeze kwa dhati kabisa, Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa michango, maoni na kwa kufanya kazi zote za Kamati hii, bila kuchoka. Naomba niwatambue Wajumbe hao kwa majina yao mbele ya Bunge lako Tukufu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mwenyekiti na Mheshimiwa Adam K. Malima, Makamu Mwenyekiti. Wajumbe ni Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Omar Sheha Mussa, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Dr. Omar M. Nibuka, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba kumshukuru Spika, Naibu Spika, kwa pamoja, kwa kutupatia miongozo mbalimbali wakati Kamati inatekeleza majukumu yake. Aidha, pia napenda kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka na Sekretarieti ya Ofisi ya Bunge, hususan Makatibu wa Kamati yetu, Ndugu Anselm Mrema na Ndugu Helen Mbeba, kwa kuipa Kamati uwezo na nyenzo zote muhimu katika kufanikisha kazi za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia familia na ndugu wenye mapenzi makubwa. Naomba nimshukuru mke wangu Zinduna na watoto wangu Ali, Abdallah, Amin na Mariam; wadogo zangu na wazazi wangu, ambao ndiyo wamekuwa ngao ya maisha yangu yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru Wabunge wenzangu wote, kwa wema wao, ukarimu wao na mapenzi yao kwangu, ikizingatiwa kwamba, ushirikiano wetu humu ndani ndiyo msingi mkuu wa mafanikio yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa nafasi maalum, niwashukuru Wabunge Waandamizi, wazee wetu, mama zangu akina Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi na Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi na wazee wangu Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa John S. Malecela, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mzee William H. Shellukindo, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Athumani S. Janguo, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Phares K. Kabuye, Mheshimiwa Gideon A. Cheyo na wengine. Nadiriki kusema, kuwepo kwenu humu ndani, ndiyo kunalipa hekima, heshima na uwezo mkubwa wa Bunge hili na kulifanya Bunge hili kuwa Bunge bora Afrika na labda Dunia nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru kaka yangu, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, kwa kutenga muda kila mara, kunipatia vineno vya ushauri na mwongozo wa kaka kwa mdogo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitambue mchango na nimshukuru Mwenyezi Mungu na nimwombee na *Maofila* na nimshukuru kwa mwongozo wake wote, maisha yangu yote, Marehemu Mzee wangu, Profesa Kighoma Ali Malima, kwa kunivumilia katika miaka ya utoto wangu, baadhi ya utundu na utukutu. Mwongozo wake kwa kunigonga kichwa hapa leo, nchi yangu na chama changu na Bunge hili limenipa heshima na kusimama mbele yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, napenda kutamka kwamba, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wa Kambi ya Upinzani, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kwa mwaka wa fedha 2006/2007. Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniweka salama na kuwa hapa kwa mara nyingine tena, kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kwa mwaka wa fedha 2006/2007, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu 45(3)(b)(c) na 81(1), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutoa salamu zangu za kuutakia kila mafanikio mema, Mkutano Mkuu Maalumu wa Chama Changu cha Demokrasia na Maendeleo *(CHADEMA),* ambao utafanyika kesho na keshokutwa katika hali ya kuhakikisha kwamba, tunafanya marekebisho makubwa ya kukiimarisha chama chetu ili kuweza kuimarisha demokrasia katika nchi yetu.

Pia, napenda nichukue nafasi hii, kwa kuwa kesho itabidi niende kuhudhuria Mkutano huu, niwataarifu rasmi Wabunge wenzangu kwamba, kufuatia kutangazwa kwa nafasi za uongozi katika *CPA,* nimeomba kugombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti. Ninaamini kabisa kwamba, kufuatia *spirit* ambayo tumeionesha ya Umoja wa Kitaifa, ambayo tumeidhihirisha kwa dunia leo asubuhi, mtakapoteua Mwenyekiti kutoka Chama Tawala, Makamu Mwenyekiti atakuwa Chama cha Upinzani. Naomba wote kwa dhati kabisa, bila kujali itikadi za vyama vyetu, muweze kunipa kura niwe Makamu Mwenyekiti, nimsaidie Mwenyekiti atakayechaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo Cha Uwekezaji Vitega Uchumi *(TIC)* ni asasi muhimu katika juhudi za kukuza uchumi wa nchi yetu. Asasi hii imejitahidi kufanya kazi katika mazingira magumu, lakini imepata mafanikio ya kujivunia katika kuongeza wawekezaji katika nchi yetu. Hata hivyo, juhudi zinapaswa kufanyika zaidi kuhakikisha kuwa, uwekezaji nchini unafaidisha wananchi na rasilimali za nchi yetu zinalindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua malalamiko ya wananchi, kuhusu baadhi ya wawekezaji kunyanyasa wananchi ambao wamewaajiri katika maeneo mbalimbali. Kwa kweli kama Taifa, ni lazima kuhakikisha kuwa, hatuachi wananchi wetu wakinyanyaswa kwa kisingizio cha kuwekeza katika nchi yetu. Lawama hizi kutoka kwa wananchi ni nyingi sana na uwezo wa *TIC* kufanya ufuatiliaji dhidi ya hawa wawekezaji kwa kweli bado ni mdogo.

Kambi ya Upinzani inashauri Serikali kujenga uwezo wa *TIC* kufuatilia wawekezaji na hasa wawekezaji wageni ili kutambua mapema malalamiko haya ya Watanzania dhidi ya unyanyasaji na kuweza kuyachukulia hatua zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kuvutia wawekezaji ni kazi kubwa na nyeti mno. Sisi kama Taifa bado hatujaweka mikakati mahususi ya kuvutia wawekezaji wengi zaidi kutoka nchi mbali mbali duniani. Kwa mfano bado Balozi zetu katika Mataifa mbalimbali hazijapalekewa wafanyakazi wataalamu wa biashara na masuala ya uwekezaji. Imefikia wakati sasa kuanza kutekeleza Sera ya Diplomasia ya kiuchumi kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapendekeza yafuatayo ili kuboresha uwekezaji nchini kutoka Mataifa makubwa. *(Makofi)*

(i) Kuweka maafisa wa masuala ya biashara na uwekezaji katika Balozi zetu zote zenye *potential* ya wawekezaji. Maafisa wapate mafunzo maalumu ya utangazaji wa fursa za uwekezaji zilizopo nchini na vile vile kutoa taarifa nchini juu ya fursa za biashara zilizoko huko.

(ii) Kwa nchi kubwa kama Marekani, Uingereza, China, India na Ujerumani, Serikali iangalie uwezekano wa kufungua vituo vya biashara na uwekezaji katika mikoa muhimu ya nchi hizo na baadae pia vituo hivyo kufanya kazi kama *consulates* zetu. Mfano dhahiri ni umuhimu wa kufungua Kituo cha Biashara na Uwekezaji katika Jimbo la Califonia nchini Marekani na Munich nchini Ujerumani ili kuweza kuitangaza nchi yetu kwa wepesi zaidi.

(iii) Kuna nchi ambazo ni wawekezaji wazuri nchini kwetu kama Uholanzi lakini nchi yetu haina Ubalozi Uholanzi. Nashauri maeneo kama haya tufungue vituo vya biashara haraka iwezekanavyo ili kuweza kushindana vizuri katika kutafuta wawekezaji na nchi ya Uganda ni mfano wa nchi za Kiafrika ambayo imefanya hivyo kwa maeneo ambayo hawana Balozi.

(iv) Nchi nyingine za Afrika zimeanza juhudi maalumu kuwapata Waafrika walioko nje *(African Diaspora)* waweze kuwekeza katika nchi zao. Kwa mfano nchi ya Ghana imeunda Wizara maalumu kwa ajili hii *(Ministry of Tourism and African Diaspora*). Ni vema sasa *TIC* nayo kwa msaada kutoka Serikalini iangalie ni jinsi gani ya kuweza kuhakikisha kwamba tunapata wawekezaji hawa wa Afrika waliozagaa katika nchi mbalimbali duniani ili waweze kuja kuwekeza katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kampuni ya Bia Tanzania inatumia jumla ya dola za Marekani milioni mbili kutangaza kinywaji chake cha *RedBull* peke yake, *TIC* inatengewa jumla ya dola milioni moja na laki nne tu kwa lengo la kuitangaza nchi kwa shughuli zake zote. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa kujitangaza nchi ni jambo la msingi na kwa kweli tunaomba *TIC* ipewe uwezo zaidi, ipatiwe fedha zaidi ili iweze kuitangaza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Uwekezaji nchini inaonesha kuwa bado uwekezaji nchini umejikita katika mikoa michache. Kuna mikoa haina wawekezaji kabisa kwa mujibu wa ripoti ya *TIC* ya mwaka 2004. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuweka sawa mazingira bora ya uwekezaji katika mikoa hiyo iliyo pembezoni *(marginalised region)* ili nayo pia ifaidike na juhudi za *TIC* na tunaposema mikoa iliyo pembezoni hatuna maana ya mikoa iliyoko pembeni, kwa sababu pembezoni na pembeni ni vitu viwili tofauti, mfano Mkoa wa Pwani hauko pembeni lakini uko pembezoni kwa *marginalised* kwa sababu kila uwekezaji unaofanywa unafanywa Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani ukasahaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kasi ya kufungua vituo vya uwekezaji vya Kanda iongezeke ili kutoa huduma bora za uwekezaji nchini. Kambi ya Upinzani

inaishauri Serikali iweke mazingira ya watu binafsi kuanzisha vituo vya uwekezaji yaani *Investment Promotion Agencies* za *private sector* ili ziweze kusaidiana na *TIC* katika kuhakikisha kwamba tunaitangaza nchi yetu ndani na nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa katika eneo hili ni suala zima la Sera yetu ya uwekezaji ya mwaka 1996. Sera hii kwa kweli ni ya muda mrefu na tunadhani kwamba imepitwa na wakati. Mazingira ya mwaka 1990 yamebadilika sana kuliganisha na mazingira ya mwaka 2006. Tumekuwa tukiona ukwepaji mkubwa wa kodi kutoka kwa wawekezaji wakubwa. Tumekuwa tukishuhudia biashara zikibadilishwa majina kutoka jina moja na mtu mmoja na kuwa jina lingeni na mtu mwingine na kuiletea nchi hasara. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inapendekeza kwa Serikali hususan *TIC* kufanya mapitio ya Sera ya Uwekezaji Tanzania na pia sheria ya uwekezaji ili iendane sambamba na mabadiliko yanayoelekea kufanywa sasa katika sekta nyingine, mfano Sekta ya Madini. Sheria hiyo iwe nguzo ya kulinda rasilimali za nchi yetu badala kuwa chanzo cha wizi na uporaji wa maliasili ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua ya kuwa lengo kubwa la kubinafsisha Mashirika ya Umma katika programu inayoendeshwa na *The Presidential Parastatal Sector Reform Commission (PSRC)* iliyoanzishwa chini ya *The Public Corporations Act,* ya mwaka 1992 iliyorekebishwa mwaka 1993 na 1999, ilikuwa ni kuleta ufanisi zaidi katika uzalishaji na vile vile kupanua uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake ya Bajeti ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Waziri ameliarifu Bunge lako Tukufu kuwa *PSRC* sasa imebaki na Mashirika machache ya kubinafsisha, miongoni mwa Mashirika haya ni Shirika la Bima na Shirika la Reli Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu wakati natoa maoni ya Kambi ya Upinzani katika Wizara hii ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji mwezi Juni, 2006 nilizungumzia kuhusiana na malalamiko ya wananchi kuhusiana na ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma. Kwa umaalumu wake niligusia kuhusu mali za Shirika la Ndege Tanzania zilizozagaa miji kadhaa duniani. Mali hizi ni kama vile nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *ATC Holdings* lililoundwa kumiliki mali hizi bado halijaweza kukamilisha umiliki wa nyumba hizi katika nchi kama Afrika Kusini na Zimbabwe. Muda unavyozidi kuyoyoma, Taifa laweza kupoteza nyumba hizi. Kwa hiyo, tunaomba kupitia *PSRC* juhudi ziongezwe ili *ATC Holdings* iweze kupata umiliki wa nyumba zetu hizi zilizoko katika nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji amelitaarifu Bunge kuwa baada ya kubinafsisha *TRC* litaundwa Shirika linaloitwa *Reli Assets Holding Company (RAHCO)* ili kushughulikia uuzaji wa mali zisizo za msingi za iliyokuwa *TRC* ya Umma. Huu ndio umekuwa utaratibu wa ubinafsishaji na wala hatutaki kupingana nao. Tunachoomba tu ni umiliki wa kampuni hii usiwe na makosa kama yale ya umiliki wa Kampuni ya Simu 2000 ambayo ilileta

malalamiko mengi na inasemakana kuwa sasa Kampuni hii ni mali ya watu wachache. Hata hivyo, baada ya muda sasa *TTCL* imerudi kumilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja baada ya wawekezaji kujitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge kuhusu mali zilizokuwa chini yake itakuwaje baada ya kuwa *TTCL* imerudi kuwa mali ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunajua kuwa *TRC* inakodishwa na wala haiuzwi. Hata kama ukodishwaji ni wa muda mrefu sawa na kuuza tu! Sasa kama tunakodisha *TRC* ni kwa nini tunauza mali zake zinazoitwa zisizo za msingi? Kambi ya Upinzani inaomba kupatiwa majibu katika suala hili.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kubinafsisha Shirika la Bima la Taifa *(NIC)* kuna masuala kadhaa ambayo sasa kama Watanzania wazalendo tunaona Mheshimiwa Waziri anatakiwa kuwaeleza Watanzania ni jinsi gani *PSRC* imefikia uamuzi wa kuuza na tathmini ya mali zake kama majengo ya Kitega Uchumi, *Life House* na mengineyo mengi na vile vile majengo haya yamethaminiwa kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini taarifa ya Idara ya Usimamizi ya masuala ya Bima nchini, inaonyesha kuwa *NIC* ndiyo inayoongoza kuwa na soko kubwa yaani *market share* kubwa kulinganisha na makampuni yote ya Bima hapa nchini hivi sasa na kwa kweli haipo katika hali ambayo ni mbaya sana ya kuweza kufilisiwa. Kwa hiyo, ilikuwa na hili nalo tupate maelezo kuhusu uamuzi huu wa kubinafsisha Shirika la Bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kabisa katika kubinafsisha Mashirika kama hili mbali na vigezo vingine lakini bado uzalendo unatakiwa kupewa kipaumbele. Hivyo kama kweli *NIC* ilikuwa na matatizo ya kifedha ni kwa nini Serikali isiuze baadhi ya majengo yake ili kuliongezea mtaji?

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iweke wazi kuhusu kauli ya Mtendaji Mkuu wa Shirika hilo kuwa *NIC* bado ina uwezo wa kujiendesha kibiashara na kiushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa ambayo ipo inaonyesha kuwa mwekezaji wa Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa badala ya kuiingizia Serikali fedha yeye anaihujumu Serikali. Hii inatokana na ukweli kwamba Serikali ilisitisha *withholding tax* lakini Mtibwa bado inaendelea kuwakata wakulima kodi hiyo na mbaya zaidi mwekezaji huyu anashindwa kuiwasilisha katika mamlaka husika na anaiweka katika Benki. Aidha, Kiwanda kinashindwa kuwalipa wafanyakazi mishahara yao na marupurupu yao kwa takriban miezi mitatu japokuwa fedha zipo.

Mheshimiwa mwenyekiti, hapa tunaitaka Serikali itoe tamko kama fedha hizo zinawekwa benki riba inayopatikana inakuwa ni ya nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko kutoka kwa *Mtibwa Outgrowers Association* yaani Chama cha Wakulima wa Miwa wa Nje Mtibwa kuhusiana na mmiliki wa Kampuni ya Mtibwa *(Mtibwa Sugar)* kuwa katika misimu ya kilimo toka mwaka 2004/2005 hadi 2005/2006 kiwanda kwa makusudi kilikataa kununua miwa ya wakulima wakati miwa ikiwa tayari imekatwa na kusababisha kuharibika. Aidha, kuna malalamiko mengi ya wafanyakazi kutokulipwa stahili zao za kisheria zilizoainishwa katika mikataba ya kazi. Mfano, michango yao ya *NSSF* na *PPF. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya kawaida jambo hili ni hujuma ya makusudi kwa Serikali na wahusika. Wananchi hao inasemekana walipoteza takribani shilingi 1,186,436,522/=. Kwa mzunguko wa uchumi katika Wilaya na mkoa mzima wa Morogoro unatokana na juhudi za wakulima wanazozifanya na lengo zima la kubinafsisha ni kukuza kipato miongoni mwa jamii husika. Kukataa kununua mazao hayo kwa makusudi ni hujuma kwa wafanyakazi hawa na wakulima hao wanyonge. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili ni nini hatma ya fedha za wakulima hawa zilizopotea? *(Makofi)*

Aidha tunaitaka Serikali iwaeleze wananchi wa Mtibwa ni kwani mmiliki huyo anamiliki 100% ya kiwanda hicho, je, maslahi ya Serikali yanaangaliwa na nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sababu kubwa iliyokuwa inatolewa na Serikali kuhusu kubinafsisha Mashirika ya Umma ilikuwa ni kuongeza ajira na kuongeza pato la nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, jedwali namba mbili inaonyesha kuwa kati ya mwaka 1995 na mwaka 2005 kipindi cha miaka kumi, ajira za nchi zimepotea kutoka ajira 126,052 na mwaka 2005 kwa watu waliokuwa wameajiriwa kwenye viwanda hadi kufikia ajira 88,713 kwa watu waliokuwa wameajiriwa kwenye viwanda. Kwa hiyo, inaonekana toka tumeanza juhudi za kubinafsisha viwanda ajira za Watanzania zimeporomoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu hizo Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania ni kweli uuzaji wa viwanda vyetu umeongeza ajira au umezidi kuwafanya Watanzania wasiwe ana ajira? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaitaka Serikali ieleze ni kwa nini kumekuwa na punguzo kubwa kiasi hicho la ajira katika sekta hii? Naishauri Serikali katika utafiti wa ajira na mapato ambao unaelekea kufanywa na Ofisi ya Takwimu ya Taifa pia tuangalie athari ya ubinafsishaji ya ajira rasmi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkanganyiko huu wa hoja zinazotolewa na Serikali pindi inapotaka kuhalalisha uuzwaji wa mali ya umma unakuwa ni sugu sasa. Hivyo basi tunaitaka Serikali iwaeleze Watanzania kuwa Sera hii iliyokuwa inashabikiwa kwa nguvu

zote na ilikuwa inaelekea kuwaongezea umaskini wananchi kwa sababu wanapoteza ajira zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jedwali hilo hilo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, imeonyesha pia mchango wa sekta ya viwanda katika mauzo ya nje ya bidhaa zisizo asilia *(none traditional products)* toka mwaka 1995 ilikuwa ni 36.5% na mwaka 2005 yalikuwa ni 13.1%. Hili ni punguzo la zaidi ya asilimia 300. Kwa hiyo, tunataka tuangalie ni vipi ubinafsishaji umepelekea uzalishaji na uuzaji wa bidhaa za kiwanda nje kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iweze kutoa maelezo ili kuweza kufafanua mambo haya ambayo nimeyaeleza.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Taifa ya Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ni sera muafaka kabisa katika kuwafanya Watanzania wamiliki uchumi wao. Hata hivyo, tunaishauri Serikali iharakishe kuanza kazi kwa Baraza la Uwezeshaji ili mipango yote ya uwezeshaji wa wananchi ipitie katika Baraza hilo haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishauri Serikali kabla ya kuanza kutoa pesa zile za mikoa shilingi milioni 500 kama zilivyoonyeshwa katika hotuba ya Waziri Mkuu, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji izielekeze Sekretarieti za Mikoa kuhusu ni Sekta zipi ambazo zinaweza zikapelekea umaskini kupungua katika mikoa mbalimbali. Kwa sababu mikoa yetu ina sekta za kiuchumi tofauti tofauti. Kwa hiyo, kila Mkoa tuweze kuangalia zile *drivers of growth* ni zipi ili katika kutoa hizo pesa kwa wananchi tuweze kuzi-*target* katika *drivers of growth* ili waweze kuongeza ajira na kupunguza umaskini wa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunapongeza mradi wa kutengeneza *regional profiles* na ni mradi wa muhimu sana na tunaomba uharakishwe na vile vile tuongeze idadi ya Wilaya ambazo zinatakiwa kufanyiwa *profile* zao ili tuweze kutumia hizo *profile* kwa ajili ya kuuza fursa za uwekezaji katika Wilaya hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa *Mini-Tiger Plan 2020* ni mpango maalum wa kuharakisha maendeleo nchini ni mzuri sana. Hata hivyo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Toleo la mwaka 2005, Ibara 63(3)(c) inataka mipango yote ya muda mrefu au muda mfupi ya nchi iletwe katika Bunge na pia kutunga sheria ya utekelezaji wa mipango hiyo. Mpango wa *Mini-Tiger Plan* kwa kumbukumbu zetu haujawahi kuletwa Bungeni wala kujadiliwa katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuuleta Muswada wa mpango huu Bungeni ili kutimiza matakwa ya Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ilitunga utaratibu wa *Build, Operate and Transfer( BOT)* katika ujenzi wa miundombinu ya nchi. Lakini toka utaratibu huu utungwe mpaka sasa hakuna mradi hata mmoja ambao umekwishafanyika kutokana na mpango huu wa *Build, Operate and Transfer*. Aidha,

sheria inayoendana na sera hii bado haijatungwa na sasa ni takribani miaka mitano toka utaratibu huu uanzishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi sababu hiyo inamfanya hata yule mwenye nia ya kuwekeza katika utaratibu huu kushindwa kutokana na kutokuwa na kitengo cha kushughulikia mpango huu. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo rasmi kuhusiana na utaratibu mzima wa wa *Build, Operate and Trasfer. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu MKURABITA, kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania kufuatia mabadiliko ya mwaka 2005 Katiba inasema kuwa ni marufuku kunyang'anya mali ya mwananchi kwa njia ya kutaifisha au vinginevyo kwa mujibu wa Sheria na bila kulipa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nilikuwa napenda tena kutahadharisha Serikali kwamba tunapokuwa tunatoa kauli kwa ajili ya kunyang'anya mali za wananchi tuweze kuhakikisha kwamba mwaka jana Bunge lilifanya mabadiliko ya Katiba na kupitisha kifungu kinachoonyesha kwamba ni marufuku kabisa kunyang'anya wananchi mali zao bila kuwalipa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Tanzania Economic Intelligence Unit.* Wizara hii ndiyo yenye dhamana kuu ya kuhakikisha kuwa kile kinachowekezwa au kubinafsishwa kinakuwa na mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi kwa ujumla. Kama kumbukumbu zetu zitakuwa ni nzuri.

Kambi ya Upinzani katika moja ya hotuba zake miaka ya nyuma iliwahi kuishauri Serikali kuanzisha kitengo cha ujasusi wa kiuchumi yaani *Tanzania Economic Intelligence Unit* ili kuweza kufanya kazi ya uteligensia kwa fursa za kiuchumi kwa ajili ya nchi yetu. Tunapenda kurudia wazo hili na Wizara ilichukue ili kuweza kuangalia uwezekano wa kuwa na Kitengo cha Ujasusi wa Kiuchumi kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa kitengo hicho itakuwa ni jukumu kubwa la kufanya uchunguzi kwa manufaa ya Taifa, ni jinsi gani makampuni yanafanya biashara zao kwa ujumla, masoko yao na masoko ya malighafi zao kwa mfano ulio hai ni kwa nini bei, kwa mfano kama sukari kutoka sehemu mbalimbali inakuwa na bei tofauti na bei ambayo ipo nchini. Kwa hiyo, tulikuwa tunapenda Serikali ijaribu kuliangalia wazo hili na kuweza kuunda Kitengo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa kuanza mchakato wa kutunga sera wa ushauri wa kitaalam. Vijana wetu wa Kitanzania na Watanzania kwa ujumla wa ndani wanapoteza pesa nyingi sana kwa sababu ya kutokuwa na sera hii. Washauri wa kitaalam wengi kutoka nje ndio ambao wanafanya shughuli mbalimbali kufuatana na masharti ambayo tunapewa na wafadhili. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Serikali iharakishe kuwepo kwa sera hii ili baadaye washauri wetu wa kitaalam wa ndani

waweze kufaidika na kazi ambazo zinapatikana ndani ya nchi yetu badala ya kuwapa kazi hizo wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa napenda kuwatia moyo watumishi wote wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kuanzia kwa Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na wafanyakazi wengine wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Katika machache hayo niliyoyasema natumai Serikali itaweza kujibu hoja ambazo tumezitoa na kwa kweli kwa sababu hotuba ya Mheshimiwa Waziri imejaribu kuelezea mambo mengi sana ya kimsingi isipokuwa haya mambo ambayo tumeomba watoe maelezo zaidi, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani Bungeni tunaweza kuwaunga mkono Wizara ili iweze kufanya kazi nzuri ya kuweza kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi yetu unakomaa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea maoni ya Kambi ya Upinzani yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Kabwe Zitto, sasa tunao wachangiaji kadhaa na tutaanza mara moja uchangiaji kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Lakini zoezi hili litatupeleka pia mpaka siku ya Jumatatu na hatutamaliza hoja hii siku ya leo. *(Makofi)*

Sasa ningependa niwasome wachangiaji wote kusudi kama kuna mchangiaji ambaye hayuko huku ndani aweze kuja na kujiandaa na tumewapanga kulingana na jinsi walivyoweza kuchangia ndani ya Bunge. Kwa hiyo, wale ambao wamechangia mara chache wataanza na wale waliochangia mara nyingi watafuatia.

Sasa tutaanza na Mheshimiwa Devota Likokola, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Godrey Zambi, Mheshimiwa Raynald Mrope na Mheshimiwa Peter Serukamba, kama muda wetu utatutosha mpaka siku hiyo ya Jumatatu kadri ya mpango wa ratiba ya kazi ya Jumatatu. *(Makofi)*

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii nikiwa kama mchangiaji wa kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba hii vizuri na kutupatia maeneo ambayo Wizara yetu ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, inapenda kuyafanyia kazi katika kipindi cha mwaka 2006/2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Lakini pia nitachangia katika maeneo matatu na nitachangia katika maeneo yafuatayo:-

Moja, nitachangia katika eneo muhimu la uwekezaji yaani *SEZ,* ntachangia katika eneo la uwezeshaji wa wananchi na nitachangia katika eneo la uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza na *SEZ.* Napenda kuipongeza Serikali kwa wazo lake kubwa la kuanzisha maeneo muhimu ya uwekezaji. Ninaamini ya kwamba maeneo haya yatasaidia sana katika kujenga uchumi wa nchi yetu na hatimaye nchi yetu itaweza kuendelea kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya *SEZ* yatatusaidia sana katika kuongeza Pato la Taifa lakini vile vile yatatusaidia katika kukuza ajira. Maeneo haya yatatusaidia sana katika kuongeza fedha za kigeni na vile vile tunaweza tukapata teknolojia kutokana na maeneo haya kulingana na wawekezaji ambao watakuja na wataanzisha uwekezaji katika maeneo haya na hali kadhalika itawasaidia wazalendo kupata teknolojia ambazo ni za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuendeleza mchakato huu wa kuanzisha maeneo ya *SEZ* naishauri Serikali tumeanza na suala zima la *EPZ* lakini bado Serikali haikuweza kupata pesa za kutosha. Kama kweli tunataka kuendelea na mchakato wa *SEZ* basi Serikali itenge pesa za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo haya yanapenda sana ushirikishwaji wa sekta binafsi, hatuwezi kuendeleza *SEZ* iwapo Serikali peke yake itaendelea na mchakato huu. Napenda kuanzia sasa hivi tangu ambapo wataalam wetu wanaenda kujifunza katika maeneo mbalimbali ya uwekezaji wanaenda kufanya stadi mbalimbali, wanafanya mipango mbalimbali ni vizuri Serikali ikashirikisha sekta binafsi. Ninaamini ya kwamba kama Serikali itashirikisha sekta binafsi maana yake wananchi wa Tanzania na wazalendo wataweza kushiriki katika mchakato huu na vile vile wataweza kuiendeleza sana nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuzungumzia maeneo ambayo yataanzishwa eneo muhimu la uwekezaji yaani *SEZ* iangaliwe kwa kina. Tumekuwa na utaratibu wa kuanzisha vitu vyote katika jiji la Dar es Salaam na Morogoro. Katika kipindi hiki cha Awamu ya Nne naiomba Serikali iangalie mikoa mingine kama vile Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma Mheshimiwa Mwenyekiti, unazalisha mazao mengi ya nafaka na wananchi wa Mkoa wa Ruvuma wanapenda mazao yale yasindikwe na yaweze kupunguzwa thamani katika eneo lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika maeneo ya *SEZ* Mkoa wa Ruvuma ufikiriwe. Kwa sababu Mkoa wa Ruvuma una kila aina ya fursa, tuna barabara nzuri Mkoa wa Ruvuma, tuna kiwanja cha ndege kizuri, kwa hivyo sioni tatizo kwa nini *SEZ* isianzishwe katika Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Ruvuma wamechoka walikuwa wanazalisha tumbaku lakini inaenda kusindikwa Morogoro. Kwa nini isisindikwe hapo hapo Songea? Wanazalisha mahindi na wanazalisha maharage. Lakini usindikaji wote unaenda ufanyika katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwapa moyo na kuwaongezea uzalishaji wakulima wa Mkoa wa Ruvuma, nashauri viwanda vya usindikaji wa mazao ya nafaka zijengwe Mkoa wa Ruvuma na tafadhali Mheshimiwa Waziri na Wizara hii isaidie sana kuvutia wawekezaji katika Mkoa wa Ruvuma*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie katika suala zima la uwezeshwaji wa wananchi. Kama ambavyo Kamati imeshauri bado dhana hii ni ngumu sana kwa wananchi bado haijaeleweka. Naomba kwa dhati kabisa Wizara ifanye semina za makusudi katika maeneo yote ya Tanzania ili wananchi waelewe wazi uwezeshwaji huu ni wa aina gani. Lakini vile vile ninaomba niseme kwamba mimi ninaamini Tanzania itaendelea tu kama Watanzania wenyewe watawezeshwa na Watanzania wakiwezeshwa watakuwa na uwezo mkubwa wa kuzalisha mali. Maendeleo tunayoyataka ni ya Watanzania kwa hiyo, ni vizuri sana katika kuwawezesha Watanzania watajenga uwezo na watajenga kujiamini katika kuzalisha mali na hatimaye nchi yetu itaweza kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaelewa vizuri katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijaona akizungumzia ni namna gani ya uwezeshwaji wa wananchi. Ile hotuba inasema kwamba Wizara inatarajia kuanzisha mfuko wa kuwawesha wananchi, wakati ambapo tumeambiwa awamu hii ni ya *speed.* Tumeambiwa awamu hii ni ya kasi, bado Wizara ndiyo kwanza inatarajia kuanzisha mfuko.

Naomba mfuko huo uanzishwe mara moja ili Watanzania wawezeshwe na waweze kuendelea na uzalishaji lakini vile vile tumeona kwamba bado kuna maneno kama vile kuandaa mpango wa kuwawezesha lakini vile vile tumeona Waziri Mkuu ameshatoa pesa za kuwawezesha kwa hiyo, katika hilo naomba Mheshimiwa Waziri atuweke wazi ili Watanzania tutakapotoka hapa tuwe na maneno ya kuwaeleza wananchi wetu kwamba Serikali itawawezesha kwa namna moja, mbili, tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwawezesha wananchi, naipongeza Wizara, imeweka taasisi mbalimbali kama vile *SELF* lakini naomba kutoa masikitiko yangu kwamba malengo yaliyowekwa na *SELF* katika Mkoa wa Ruvuma kwamba utatoa

mikopo ya shilingi milioni 800 kwa kweli hayajaweza kufikiwa wananchi wa Ruvuma pamoja na Serikali yao kuwapenda na kuwatengea fungu hilo la fedha lakini *SELF* haijaweza kupeleka pesa hizo zote. Nani alaumiwe siwezi kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama *SELF* iliweka malengo na wananchi hawajaweza kuzikopa zile pesa zote kwa hivyo naomba *SELF* iweke mkakati maalum wa kwenda kuangalia viwango gani vya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma wanavihitaji ili waweze kupata mikopo hiyo. Ni jambo la kushangaza sana kama Serikali imewapenda wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kuwatengenea shilingi milioni 800 *SELF* iwakopeshe shilingi milioni 55 tu kwa kweli inasikitisha.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini ya kwamba wananchi wengi wa Mkoa wa Ruvuma wanahitaji hiyo mikopo pengine kuna tatizo la uelewa taratibu gani zitumike, basi naiomba *SELF* ikishirikiana na Mkoa wa Ruvuma ili wananchi waweze kunufaika na fedha ambazo Serikali imewapangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala zima la uwekezaji. Suala la uwekezaji katika nchi yetu ninaipongeza sana *TIC* kwa kazi nzuri iliyofanya. Na kweli katika maeneo mbalimbali hususan Kaskazini mwa Tanzania kazi ya *TIC* inaonekana vizuri zaidi.

Naomba kusema kwamba Mikoa ya Kusini kazi ya *TIC* bado haina *impact* kubwa. Naiomba Serikali iangalie mikoa ya Kusini na katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema ya kwamba sasa hivi *TIC* itafungua Ofisi katika Kanda ya Kusini. Ninapongeza sana katika hilo na naomba niseme Mkoa wa Ruvuma katika mikoa ya Kusini tukiambiwa mikoa ya Kusini tunaambiwa sisi tuko Nyanda za Juu Kusini, kwa hiyo, hakuna Ofisi inayofunguliwa pale. Tukiambiwa tuko Nyanda za Juu za Kusini tunaambiwa sisi tuko Kusini Lindi na Mtwara. Kwa hiyo, hakuna, sisi tunayumba tu. Lakini kwa vile Mheshimiwa Waziri amesema Ofisi itafunguliwa Mikoa ya Kusini, naomba sasa wauangalie huo Mkoa wa Ruvuma ambao kwa muda mrefu umekuwa ukiyumbayumba na vitu vingi vya kikanda vimekuwa havipo katika Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, atueleze kidogo, angalau mipango gani Serikali imeweka kwa yale matamko ambayo Mheshimiwa Rais alitoa kuhusiana na mkoa wa Rukwa, Tabora, Lindi, Mtwara, Kigoma na Ruvuma. Mikoa hii tumeambiwa wazi haijaendelezwa na nategemea kwamba kwa vile Wizara hii ni Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji angalau kwa kidogo ingeweze kutupa sasa matumaini ili wananchi wa mikoa hiyo wajue Serikali ina mipango moja, mbili, tatu ya kuiendeleza mikoa hii. Lakini mpaka mwisho wa *speech* ya Mheshimiwa Waziri sijasikia mpango gani umewekwa kwa ajili ya mikoa hii sita ambayo Mheshimiwa Waziri amezitamka wazi, kwamba haijaendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa pongezi za dhati, kwa wenzetu wa MKURABITA na vilevile wa *BRELA*. Wenzetu wa MKURABITA wamejitahidi sana na ninawashukuru sana kwa safari ambayo waliifanya rasmi katika Wilaya ya Songea, ili

kuangalia namna gani wataweza kurasilimisha biashara za wanyonge katika Wilaya yetu ya Songea. Katika hilo ninawapongeza sana watu wa MKURABITA, lakini vile vile nawapongeza watu wa *BRELA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda sana kuipongeza Wizara hii na nachukua nafasi hii kuwapongeza sana wataalam wa Wizara hii katika kufanya kazi zao kwa umahiri mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi katika vikao vyetu vya Kamati tumekuwa tukipata ripoti zilizokamilika vizuri na zinazoeleweka vizuri. Kwa hivyo, kwa heshima na taadhima napenda kuunga hoja mkono, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukru sana Mheshimiwa Devota Likokola, kwa kuniwakilisha hata mimi Mwenyekiti wako kule Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ingawa sikuwa nimejiandaa vizuri kwa sababu asubuhi sikutajwa, lakini nashukuru kwa fursa hiyo ya upendeleo nitaitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niwapongeze Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Salome Mbatia, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara kwa kuandaa na hatimaye kuwasilisha hoja ambayo sasa hivi tunaijadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili naomba pia kutumia fursa hii kuwashukuru wanawake wa mkoa wa Manyara kwa imani yao kubwa kwangu kwa sababu ni mara chache sana nimesimama hapa katika Bunge lako Tukufu. Nawapa shukrani zangu za dhati kwa kunichagua kwa kura nyingi na kuwahakikishia kwamba sitaawaangusha, nitajitahidi kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia kuwatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utakuwa mfupi na nitachangia maeneo matatu kama ifuatavyo.

Kwanza nikianza katika suala lazima la uchumi, Wizara hii ndio Wizara ambayo inaweka mipango na mikakati yote ya uchumi wa nchi yetu, kwa hivyo, mikakati itakapokuwa mizuri na bora nadhani ndio tegemeo la nchi katika uchumi kwa ujumla. Kwa hivyo, hatuna budi kuitupia macho kwa umakini sana kwa sababu uchumi wetu sasa hivi unategemea kilimo, na nadhani uchumi wa nchi yoyote unapotegemea kilimo, ni kigezo tosha kuonyesha kwamba nchi hiyo ni maskini. Hakuna nchi iliyoendelea duniani ambayo uchumi wake unategemea kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wakati mmoja Marehemu Baba wa Taifa alizungumzia kwamba wakati nchi zinazoendelea zinapotembea, hatuna budi sisi tukimbie. Kwa hivyo, nadhani ni wakati muafaka kwa Wizara hii kuifikiria na kutafakari suala hili na kuipa kipaumbele katika utekelezaji, sielewi kwa nini ni wakati mrefu

nimesikia ni muda mrefu sana umepita, napata kusikia kwamba tunapaswa kukimbia wakati wenzetu, hususan nchi zinazoendelea zinatembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi Watanzania, nadhani ni wakati muafaka kufikiria kwamba uchumi wetu hatuna budi kuibadili na mimi kwa mawazo yangu Mwenyekiti, nafikiria kwamba tutakapobadili mfumo wa uchumi, hususan tukategemea viwanda zaidi na biashara na masoko tunaweza tukabadilisha mfumo wetu wa uchumi na hatimaye kufikia azma ya kukimbia wakati wenzetu wanatembea. Kwa sababu wakulima wetu wa Tanzania wanajua kilimo bora, sasa hivi mkulima utakapomuuliza kwamba *spacing* ya mahindi kwa mfano ama maharage, kutoka mche hadi mche na kutoka mstari hadi mstari, ni kilometa ngapi, atakwambia kwa kirahisi kabisa tena kwa ubora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kusisitiza kilimo kwa wakulima ni jambo dogo sana, wakulima wetu tutaupa msisitizo na msukumo mkubwa kama tutawahakikishia soko la mazao watakayozalisha kwa ziada. Wakulima watakapopewa soko la uhakika bila kubabaishwa na kuambiwa wasubiri kwa muda wa miezi sita au mwaka mmoja, baada ya kuuza mazao yao watalima na kuzalisha ziada tena kwa ubora unaotegemewa. Kwa hivyo, mimi nadhani tuanze kufikiria kwamba uchumi wetu badala ya kutegemea kilimo tutegemee zaidi viwanda, biashara na masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wetu hauna budi uende katika ubora wa kutumia sayansi na teknolojia, kama kweli tunataka kutokana na lindi la umaskini, kwa sababu mimi naamini kwamba MKUKUTA peke yake hautatufikisha mbali sana. Mimi nadhani ni wakati muafaka tukabuni mbinu mbalimbali za kuweza kuboresha uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nataka kuchangia ni suala zima la mipango, nadhani, suala zima la utandawazi si suala la hiari la nchi, ni suala la hali halisi, hatuna budi kupanga uchumi wetu wa masuala yote ya maendeleo kuzingatia utandawazi kwa dunia ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi navyoona hatuna *option* ya utandawazi kwa sababu ni hali halisi na kwa hivyo tuanzishe mfumo wa kuzalisha bidhaa bora zaidi, ili tuweze kushindana katika soko la dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni lauwezeshaji la kiuchumi sasa nijikite katika mkoa wangu wa Manyara, Mkoa wa Manyara ni mkoa mpya uligawanyika toka Mkoa wa Arusha hivi karibuni, lakini mkoa huu una ardhi yenye rutuba na hali nzuri ya hewa ambayo inaweza ikazalisha mazao mengi ya kila aina.

Kwa hiyo, hauna tatizo na kuzalisha mazao ya kilimo, lakini kinachosikitisha ni kwamba katika nchi nzima ya Tanzania mkoa huu una makabila yaliyo maskini kuliko makabila mengine yote Tanzania. Baadhi ya makabila ya mkoa huu bado wanategemea matunda na bado wanategemea kuwinda wanyama wadogo wadogo na bado wanavaa ngozi kama vazi rasmi ama vazi la kudumu. Kwa hivyo vigezo vitatu vinadhihirisha

kwamba kwa kweli tuna makabila ambayo wapo katika hali ya umaskini uliokithiri. *(Makofi)*

Naomba kwa heshima na taadhima, Wizara itenge fungu maalum kuwapa wananchi wa Manyara, elimu ya kuwahamasisha kubadilika na hali duni ya kimaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikitisha pia ni kuona kwamba mkoa huu katika taarifa hii ya bajeti imeachwa pembeni. Ukurasa wa 34 wa kijitabu cha hotuba ya Waziri umeorodheshwa mikoa 14 inayolengwa na mradi wa mikopo midogo midogo ya *SELF* ikiwepo mkoa wa Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mbeya, Mwanza na kadhalika. Mikoa ambayo mimi naiona kwamba imepiga hatua kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikoa hii iliyoorodheshwa wanalengwa, nina hakika na mabilioni ya fedha zinazotolewa na taasisi za fedha kama *PRIDE, FINCA* na taasisi zingine za fedha na taasisi kama hizo, hazijafika hata moja mkoani Manyara, sasa nashangaa taasisi hii ambayo ni ya Serikali haijaweza kufika hata katika Wilaya moja ya mkoa wa Manyara. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali pia iweze kutupia macho mkoa huu, pengine si makusudi kwa sababu mkoa huu ulikuwa pamoja na mkoa wa Arusha, lakini basi yale yote ambayo yamepangwa kwa ajili ya mkoa wa Manyara, yasimezwe na mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kwa mradi wa *SELF* tu bali miradi mingine ya Serikali iweze kufikishwa, ili wananchi pia wa mkoa wa Manyara waweze kunufaika na fursa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ombi maalum pia kabisa kwa Wizara hii ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, iupe kipaumbele na upendeleo wa makusudi mkoa wa Manyara, ili wananchi wa mkoa huu wafaidi matunda ya Serikali ya kuwezeshwa kiuchumi na kuzingatia uchumi ambao unaelekea katika misingi ya sayansi na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kama nilivyosema nitaongea kwa kifupi, naomba kuunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, naomba tu niweke kumbukumbu vizuri, Mheshimiwa Martha Umbulla, fursa hii haikuwa ya kukupendelea, ilikuwa ni haki yako kwa sababu ulitoa taarifa ya kuomba kuchangia na jina lako halikutokea na umechangia mara moja tu Bungeni na ndio maana tumekupa nafasi ya kuchangia na sio upendeleo. *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kuleta taarifa na hoja nzuri sana ambayo nadhani imeandikwa kiutaalam. Mimi nataka niwapongeze wa Wizara yote, akiwepo Katibu Mkuu, Dr. Enos Bukuku na watumishi wote wa Wizara ambao kwa kweli nafahamu wamefanya kazi yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nataka nitumie nafasi hii kuwashukuru wenzetu hasa Kamati ya Fedha na Uchumi ambayo taarifa yake imesomwa na ndugu yetu Mheshimiaw Adam Malima, kwa ufasaha wa hali ya juu sana na mimi namshukuru kwa sababu katika majumlisho yake, amejaribu kuwazungumzia baadhi ya viongozi wa zamani katika Bunge hili, akisema wamekuwa wakisaidiana na ushahidi umeouonyesha ya kwamba yeye mwenyewe amepewa nafasi na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, ili aanze kupata uzoefu sasa wa namna ya kukaa humo ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na uzoefu mzuri sana, najua viongozi wenzangu watakubaliana nami, nimeona Mheshimiwa Mohamed Missanga, huwa anaitoa nafasi, hata ukimkuta Mheshimiwa William Shellukindo huwa anawapa nafasi vijana, mama Anna Abdallah, huwapa nafasi, Mheshimiwa Gideon Cheyo, anawapa nafasi, hivyo kwa kweli uongozi unathamini sana kuwepo vijana katika Bunge hili. Ndio maana tunawasaidia kuwafundisha mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nataka nimpongeze ndugu yetu upande wa upinzani, Mheshimiwa Kabwe Zitto, ametoa taarifa yake ambayo ni nzuri, ni vizuri ikachambuliwa na yale ambayo yamo ndani ya uwezo wetu tuyape maelezo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa na mambo mawili muhimu sana, kwanza nataka nimthibitishie Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa ya kwamba naunga mkono hoja yake mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliunga mkono kwa sababu mambo mawili, ya kwanza, kati ya Wizara ambayo imeandaa makabrasha mengi yanayozungumzia mbinu za kufufua uchumi na kuendeleza nchi yetu ni Wizara yako ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na makabrasha tuliyonayo, tungekuwa na uwezo wa kuyasoma na kuyatafsiri inavyotakiwa, nchi hii ingekuwa mbali, tatizo hatuna wataalam ambao wanafika mpaka kule vijijini, ambao wanaweza angalau kutafsiri kwa maneno kwa vitendo, hotuba na makabrusha mengi ambayo tumekwisha yaandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa sasa ni chuo chetu cha mipango kifanye kazi hiyo ya kwa kuwaelimisha vijana wenzetu mpaka vijijini, tupate maafisa mipango watakaopelekwa mpaka vijijini. Ndio kazi mojawapo Mheshimiwa Waziri tungeomba kweli msaidie chuo cha mipango kifanye kazi yake. Haya makabrasha yatabaki mwenye mashelfu, hakuna atakayeyaangalia, yatatumika na watu wengine, wataendelea kutumia utaalam tuliokuwa nao. Tuwasaidie vijana waelewe nini kinatakiwa kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kusema hayo, kuna mtaalam mmoja wa Afrika anaita Dr. Norman aliwahi kusema hivi: "Kutekeleza sera za chama kilichoshinda uchaguzi, si hiari ya mtu au taasisi au chama kingine chochote, bali niwajibu wa kila mtu," mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alilisema hilo kwa sababu anaona kuna upinzani wa kuvuta *(Tag of war)*. Unapovuta *tag of war,* kuna wengine wanavuta upande huu mwingine upande huu. Lakini unapozungumzia chama kinapotoa maagizo na maelekezo, sasa hiyo kazi ni wote, hata wenzio wote wa upande wa vyama vya upinzani

wanawajibika kusimamia na kuhakikisha wanafanikiwa ili angalau sera za Chama cha Mapinduzi kinaendelea. Sasa tatizo letu kubwa katika nchi hii, ni tatizo la kilimo chetu ambacho nitakieleza kwa ufupi.

Kwanza ukiangalia bei ambayo mkulima wetu anapewa ambayo imeachwa kwenye soko, wanaita nguvu za soko, nilifundishwa na mtaalam mmoja Marekani akasema na Wamarekani mnawafahamu akasema hivi: "Nguvu za soko zinafaa pale tu nchi inapokuwa na uchumi mbadala. Kama nchi ina viwanda vingi na haitegemei kilimo, hivyo kilimo sio jambo muhimu, kwetu sisi asilimia ya Watanzania wanategemea kilimo. Ukichukua madini, viwanda, maliasili, bado vinachukua nafasi ndogo sana ya jamii maana yake ni kwamba umaskini wetu ukiuangalia utaanza kuaangalia kutoka kwa wakulima ambao ni asilimia 80," mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba kilimo kikiteterekea kidogo ujue ni maafa ya Taifa, hivyo kweli sisi kilimo chetu bado kiko katika hali hiyo, nataka kuzungumza. Marekani kabla ya vita kuu ya pili, walikuwa wanategemea chakula chao kutoka Canada, lakini walifikia mahali fulani wakasema kuanzia sasa kufa na kupona hatutaki tena kuagiza chakula kutoka Canada na Marekani, sasa wana chakula cha kutosha, waliweka mikakati yao na wakahakikisha wana chakula cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, China na yenyewe katika *cultural revolution* wakaanzisha kitu kinaitwa mapinduzi katika kilimo. Walipoamua katika miaka ya 1979 mpaka karibuni 1989 wakasema lazima tuhakikishe tunalisha watu wetu na pia tupate ziada ya kuuza nje, wakafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malaysia pia Rais wao mwaka 1981, akasema miaka kumi yangu ya uongozi nitahakikisha ya kwamba naingia ulimwengu wa pili, niko ulimwengu wa tatu, nataka kuingia ulimwengu wa pili na kweli mpaka sasa Malaysia wako mbali sana. Lakini ni uamuzi tu Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ameamua kwa dhati ya kwamba anataka kuondokana na umaskini tulionao, ili Watanzania waishi maisha bora, hivyo kazi iliyopo ni yetu sisi Watanzania. Kazi iliyopo ni sisi Watanzania kumsaidia Rais azma aliyokuwa nayo itekelezwe, nini tufanye sasa ndio nataka nije katika *agenda* inayohusika. *(Makofi)*

La kwanza tuachane kwanza na mazoea tuliyokuwa nayo, unajua mazoea yana taabu na waimbaji fulani waliwahi kuimba wimbo kidogo. Bei ya mazao isipoangaliwa wakulima hawatapa motisha ya kuzalisha, mahindi bei yake namshukuru msemaji aliyemaliza sasa hivi, Mheshimiaw Devota Likokola, amezungumzia kwa uchungu sana kuhusiana na mikoa ambayo inazalisha mahindi. Bei ya mazo isipopanda itakuwa ni tatizo kwa wakulima wetu hawatakubali kuendelea kuzalisha, watatoa chakula kidogo tu kwa ajili ya matumizi yao. Lakini ukipandisha bei tu mkulima utashangaa atakavyolima, nalisema hilo kwa sababu mwaka 2004/2005, tulipokuwa na njaa katika nchi hii *SGR* yetu ambayo ni hifadhi ya chakula, ilikuwa na tani 71,000 katika maghala yake yote. Lakini mwaka uliofuata, chakula kilikuwa hakitoshi ikabidi tuagize tani 42,000 kutoka nje nchi na Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ambayo tulikuwa tunanunua chakula kwa mkulima, ilikuwa ni shilingi 12,000 kwa kilo 100, shilingi 2,012, ambayo ni sawa na gunia moja, kwa Watanzania, tulikuwa tunanunua kwa wakulima kwa kutumia *SGR*. Lakini tulipotaka kuagiza chakula kutoka nje, ikabidi tununue kwa shilingi 32,000 kwa gunia lile lile, hata wanapozungumza ati ni rahisi kuagiza chakula kutoka nje, kulika kuagiza kutoka Sumbawanga, mimi sikubaliani nao hata kidogo. Sumbawanga kama unaweza kupata kwa shilingi 12,000 na nje ukapata kwa shilingi 34,000 kwa gunia hilo hilo, wapi rahisi, ndio maana nataka Mheshimiwa Waziri muangalie katika mipango suala la kilimo na bei, liangaliwe upya, ili tuwe na uhakika ya kwamba tunaweza kufanikiwa. La pili ni suala la mbolea, kilimo ni mbolea, kilimo ni maji, kilimo ni mbegu, unaweza kulima ukikosa mbolea, matokea yake utayapata wakati huo huo. Tena matokeo unayoona yakiwa bado shambani, nini kinajaribu kufanyika, mwaka jana nitatoa mfano, mimi nilikuwa nimemshauri kampuni moja iagize mbolea kutoka nje baada ya kuona bei ya mbolea ambayo tunauzia hasa *Urea* ni kubwa sana nikashauri hiyo kampuni, agiza mbolea kutoka nje.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichogudua ni mambo makubwa matatu, la kwanza kumbe ukiagiza mbolea kidogo, bei yake inakuwa ni kubwa sana na nitatoa sababu zake, ukiagiza nyingi kwa wakati mmoja bei yake ni ndogo sana, nini kinafanyika hapa, wakulima wanategemea hao wanaowaagiza tani 2000, tani 1000 kote humo mmoja. Ndio maana nataka niingie katika kipindi ambacho ni vizuri tukakizingatia hasa cha uwezeshaji, nina takwimu zifuatazo, Ukiaagiza tani 300,000 mpaka 500,000, na kwa taarifa yako nchi hii kwa mbolea ya *Urea,* nachukua mfano *Urea,* tunahitaji wastani wa tani 100,000 kwa nchi yetu. Ukichukua mfano wa tani 100,000 ambazo zinahitaji sasa tuangalie bei inayouzwa katika masoko ya dunia na hasa Ujerumani, ukichukua 300,000 mpaka 500,000 utapata kwa bei ya dola 80 kwa tani ambayo ni sawa na shilingi 6,300 kwa mfuko wa kilo 50 ambao ndio mifuko yetu. Ukiagiza tani 100,000 mpaka 150,000 utapata kwa bei ya dola 110, ambayo ni sawa na shilingi 6,930 kwa mfuko. Ukiagiza tani 10,000 mpaka 100,000 utapata dola 125 kwa tani ambayo ni sawa na 7,875 kwa mfuko, bei ya hapa Dar es Salaam, sio nimechanganya na gharama zote, kwa mfuko utapata kwa shilingi 7,875. Ukiagiza tani 100 bei inapanda itakuwa shilingi 17,514 kwa mfuko wa kilo 50, maana yake nini ukitaka tufanikiwe bila kujali hata ruzuku, ambayo tunaitoa ambayo wakati mwingine mimi sikufichi ruzuku ilitolewa lakini wengi hatukuona faida yake, kwa sababu ilipotea, bei zikarudi zilezile, sijui kuna mbinu gani ambayo zinafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia utaratibu ukitumia wa kuagiza tani 100,000 ambao ndio *minimum,* zinazohitajika kwa nchi nzima, utaipata mbolea kwa hapa Dar es Salaam, shilingi 6,930, ongeza hata shilingi 3,000 kwa gharama za kusafirisha ikishafika mkoani inafika 10,000, mbolea ambayo tunaipata pamoja na ruzuku ni shilingi 14,000, 4,000 ume-*save* tena bila ruzuku. Nalisema hilo kwa sababu lazima tuangalie. Tumewaachia wafanyabiashara wachache mmoja, mmoja analeta tani 1,000 huyu 2,000 ndio tumefikia, kwa nini msituwezeshe akina Kimiti na gharama yake yote nimefanya. Uniwezesha mimi kunipa bilioni 2 na milioni 200, ruzuku yote na mbolea na nini ni bilioni 20 imetamkwa hapa, nipe bilioni 2 tu nikuletee mbolea, na nitauza shilingi 10,000 kwa mfuko bila hata ruzuku. *(Makofi)*

Sasa ni utaratibu tu wa kuwaandaa wananchi kuwawezesha ndio tunarudi kwenye kuwezesha, ili tuone hawa tulionao tunaweza kuwasaidia vipi, tunaagiza kontena moja linainga hapa linamwaga mbolea umemaliza ugomvi, lakini ukimwacha mmoja mmoja na kuna-*syndicate* kubwa sana ya mbolea, utapata matatizo, watakuuzia bei wanayotaka. Lakini nikasema nini tatizo, ni usambazaji, sitatizo, kuna ma-*stockist* mawakala nchi hii, wako 639, wako wamesambaa mahali kemkem. Pia tunaweza kutumia *SACCOS,* ukiwaambia kila mmoja aje achukue tani 50, hata wiki haifiki watamaliza, mradi bei yako iwe chini, nilidhani vizuri tukajiandaa, kwa sababu hali hiyo ikiendelea, tunaweza kuzani wakulima wetu hawatekelezi majumu yao, na bei itaendelea kuwa ni kubwa, tutashindwa kutekeleza majukumu yetu. Lingine naomba sana suala la sera ya idadi ya watu, sasa pamoja na kwamba imekamilika, sasa tuandae Tume ambayo itashughulikia suala zima. Hiyo Tume ndio itasimamia mambo yote haya na mimi ninaimani kabisa Mheshimiwa Waziri ukiandaa Tume kuna wataalam wengi sana watakusaidia kufanya kazi yako vizuri na mipango itakwenda ili angalau uchumi uendane na idadi ya watu na mipango tunayoipanga kwa ajili ya watu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala ambalo wanasema ya kwamba ni kuratibu shughuli zote ya mashirika ambayo yamebinafishwa, mimi naomba sana, hii ni kazi kubwa tungeomba Wizara yako iendelee kuratibu haya malalamiko yaliyozungumzwa, juu ya wakulima wa miwa, juu ya viwanda, wafanyakazi katika viwanda, Serikali ina jukumu sana kujaribu kuratibu, ili tuone tunafanya nini kupunguza baadhi ya kero. Maana yake baadaye yataturudia sisi wananchi wataanza kutulaamu ya kwamba umebinafsisha, lakini hakuna lolote, mambo hayaendi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu kidogo kwenye hoja hii ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Awali ya yote kabisa naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kwa hotuba yake nzuri ambayo inaeleweka, napenda kuwapongeza na kuwashukuru wasaidizi wake, Naibu Waziri na Katibu Mkuu walivyomsaidia kwa ufanisi, tukijua kwamba amehamia tu muda si mrefu kwenye Wizara hiyo, lakini yeye kama mchumi tena mchumi wa mambo ya kilimo, nadhani atatusaidia sana kama tulivyosaidiwa na mwenzake aliyemtangulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitakuwa na mchango katika maeneo machache tu, la kwanza kabisa katika ukurasa ule wa 55 kifungu 52 inayohusu ubinafsishaji. Napenda sana kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya kubinafsisha mashirika ya umma na kupunguza mzigo wa Serikali ni kazi nzuri sana imefanyika, ni kazi kubwa. Lakini vile vile nadhani kuna masomo tumejifunza hapo, kwa hiyo, tunategemea kwamba mashirika yaliyobaki, ubinafsishaji wake hautakuwa na matatizo kama ulivyo kwenye mashirika ambayo yametangulia. *(Makofi)*

Kwa mfano katika mashirika yaliyobinafsishwa kumetokea dosari mbalimbali, kuna baadhi ya wawekezaji waliouziwa viwanda wamevifunga havifanyi kazi kwa mfano viwanda vya ngozi, magunia na mbao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengine kwa mfano kwenye ubinafsishaji wa mashamba hasa ya mkonge mikataba imekiukwa, kwa mfano kuna mwekezaji mmoja amebinafsishiwa mashamba kumi lakini ameendeleza shamba moja tu hivi kweli tumtazame tu akae hivyo? Kwa sababu kuna mkataba pale na hiyo mali ipo pale hata kama ametoa fedha zake lakini mali ile tunaihitaji sisi ya mkonge nadhani hapo kuna kitu cha kutazama.

Lingine lililojitokeza ni kwamba kuna matatizo mengi yamejitokeza kwenye baadhi ya mashirika yaliyobinafsishwa ya wafanyakazi kutolipwa mishahara yao kisheria, maslahi yao kutochangiwa kwa mfano kwenye mifuko hii ya hifadhi ya jamii. Sasa mimi napendekeza kwamba kama Sheria iliyounda *PSRC* haina meno ya kutosha basi irudishwe hapa Bungeni tuirekebishe tuondoe hayo matatizo kuliko kila wakati kusikiliza hayo malalamiko na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipoangalia nchi hii kwa kweli itakuwa ni mahali kwa mtu yeyote anaweza kuja na hela zake tukampa kitu tu akakaa akafanya vile anavyotaka na sisi hatufanyi chochote, hebu tazama hii Sheria kama ina mapungufu kwa kweli tuirekebishe vinginevyo inatutia kinyaa kila ukifika unalalamikiwa na wananchi, wafanyakazi kwamba mambo hayaendi vizuri na Sheria ipo. Sasa thamana kwa kweli tuliyoitoa pale kwa mfano kwenye ardhi si kwamba mtu tu achukue tu hicho kitu, nadhani Serikali pale haikutaka fedha tu bali ilitaka mtu huyu alipe fedha lakini afanye shughuli ile iliyokuwa inafanywa pale iendelezwe kwa ajili ya uchumi wetu. Kuna ajira nyingi zimepotea kwa namna hiyo ijapokuwa zimeongezeka, sasa ningeshauri Wizara kwa kweli kama kuna utafiti wa kufanya au kuna Kamati ya kufanya ya kiutendaji iundwe ili iweze kutafiti ni njia gani au Sheria hizi zina upungufu gani ili tusikae tunalalamika tu kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajiandaa kurekebisha Shirika la Reli, Posta na hata Bima lakini mimi napenda kuishauri Serikali kabisa kwamba kwenye suala la Reli tusilete mchezo. Reli katika nchi yoyote kwa kweli ni miundombinu mkubwa sana na muhimu sana na ambao unachukua watu wengi sana, sasa mimi nadhani badala ya kuondoa nguvu za Serikali kwenye Reli tungezipeleka hizo kwenye miundombinu hii ili uchumi uweze kuibuka kuliko kufanya kitu chochote kile.

Kwa mfano mtu atakayekuja anataka kuja kufanyabiashara tu hapendi hasara, sasa tuangalie tusije tukapoteza muda tukadhani tutasaidiwa kumbe tunacheleweshwa, tunahitaji kwa kweli usafiri wa reli hapa nchini ndiyo ambao utatukomboa, hatuwezi kutegemea malori kwani malori hayatatupeleka mahali popote, malori ni ya kubeba mizigo michache tu kwa mfano sasa hivi malori yanaleta mizigo mpaka Dodoma hapa kupeleka Mikoa ya Magharibi, muda ni mrefu sana unaotumiwa hapa na uwezo ni mdogo sana.

Mimi napenda kuishauri Serikali kabisa kwenye reli kwa kweli kama kuna tatizo tuletewe mpango maalum wa kuibua reli na tuifungue reli hii ya Kati mpaka Kigoma na Mwanza, tuifungue reli ya kutoka Ruvu kwenda Tanga mpaka Moshi na Arusha halafu kwenda Musoma. Reli ya Musoma inakuwa kitendawili hebu tuangalie hata katika mipango angalau ionekane hata kama ni kuwekea token fedha za kuonyesha kwamba tuna nia safi basi *token fund* ingewekwa hapo ili isipotee ili Serikali inayokuja ijue kuna kazi hiyo ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la kutegemea wawekezaji kutoka nje linaweza kutuletea matatizo kwa mfano tukiangalia *National Insurance Cooperation* au *Company*. Bima ni jambo la Kimataifa sasa tusije tukaondoa ushiriki wa wananchi wa Tanzania tukawakabidhi ma-*art nationals branches* za ma-*art nationals,* Mashirika Tanzu ya Mashirika makubwa na sisi tukajiondoa hebu tuitazame vizuri *National Insurance* ina matatizo gani? Hatuwezi sisi wenyewe hizi hisa zetu tukaziuza hapa nchini ikabaki bado ni ya kwetu, tusije tukafanya makosa kama tulivyofanya kwa *NDC. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NDC* iko mbali, sasa tunategemea *National Microfinance* na nadhani Serikali itakumbuka jinsi tulivyohangaika nayo kwa wiki nzima hatukubaliani nayo mpaka sasa hivi Serikali sasa inapata gawio. Ni kazi nzuri hiyo mimi naomba sana tuwe waangalifu tusije tukaikabidhi nchi hii kwa watu wachache tena watu wenyewe wageni watakuja watachukua fedha wakiona mambo yanazidi kuwa magumu basi wataondoka. Jamani tuwe waangalifu *National Insurance* ni hako Kashirika hako hatutaki Serikali iwekeze huko, lakini hisa za wananchi zinaweza kupelekwa huko katengenezwe twende huko kuliko kuwakabidhi hao hao ambao kwa sasa kila kitu itabidi tuwategemee huko nje. Nadhani siyo jambo zuri hilo yaani *National Insurance* haina tofauti na Mabenki hayo tukiwakabidhi basi mambo yote wataamua wao na sisi hapa tutakuwa ni wasikilizaji tu, *National Insurance* napenda kuizungumzia kwa sababu tuna uzoefu kwenye *National Bank of Commerce. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kabisa kwa uzalendo wangu naiomba Serikali tuwe waangalifu sana kwenye ubinafsishaji wa *assets* au mali za Serikali ambazo zina uhusiano na ardhi. Pamoja na uwekezaji kwenye ardhi tuwe waangalifu sana tutakuja kufika mahali tutakuwa na matatizo makubwa sana kwa sababu sasa hivi hapa Tanzania sisi hatuna wafanyabiashara wakubwa ni wachache sana, sasa kama tutataka tupate wawekezaji kutoka nje bila kuimarisha walioko nje bila kuwaimarisha walioko nje kuwawezesha wakaweza wao kwenye ardhi tunaweza kujikuta tuko katika hali ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zimbabwe iko katika matatizo na wote tunayasikia, *South Africa* pengine wengine hatuelewi ardhi kubwa kule imeshikwa na wachache nadhani asilimia karibu 80, wananchi wale waliojitawala sasa hivi wanahangaika kupata ardhi kwa hiyo Serikali inabembeleza wenye ardhi kubwa wawagawie hawa wadogo nao wenye ardhi wanazungumza wanasema tutakubaliana kati ya ninayeuza mimi na anayenunua yaani *willing buyer* na *willing seller*. Kwa hiyo, Serikali hapo imeingia

mkenge na Serikali itabidi iombe sasa yaani kuomba ardhi yako kwa mtu ambaye umembinafsisha bila kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatuko wenyewe, suala la kujenga uchumi unajitegemea kwa kweli unahitaji maamuzi mazito ambayo haiondoi Serikali hata kidogo. Ni lazima Serikali kwa njia yoyote ile hata kama ni kwa *regulations* kwa kudhibiti lazima iwepo hata pengine kuingia wakati mwingine unasema nitaendesha mimi mwenyewe mpaka wakati wewe utakapokuwa tayari maana yake siwezi kukubali kazi hii iharibike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma gazeti linaloitwa *News Week* la Jumatatu tarehe 07 Agosti, 2006 na kulikuwa na mahojiano ya Makamu wa Rais wa nchi ya Bolivia nchi ambayo inaendelea kama ya kwetu. Makamu wa Rais huyo anaitwa Arvadro Gashia Lenela amesema hivi nitasoma kwa kiingereza hapo kama walivyoandika nisije nikachafua mwelekeo wa hoja yenyewe: *"Capitalism will continue, the market will continue, Foreign Investment will continue but in a country like ours with an especially large Rural Sector, Strong Indigenous Culture, an absence of a large design Sector then we sometimes need the State to step in."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hiyo na ninaunga hoja mkono. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo na hasa kwa hiyo nukuu yako ya leo, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga na Mheshimiwa Job Yustino Ndugai ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kinipa nafasi ya kuchangia jioni hii ili niweze na mimi kutoa mchango wangu kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukushukuru wewe sasa nimpongeze sana Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa, Waziri kwa kazi nzuri ambayoanaifanya kwenye Wizara hii na hata huko alikokuwa. Nimshukuru na pia nimpongeze sana Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Naibu Waziri wake kwa umahiri wake na kwa *seriousness* yake katika kufanya kazi yake vizuri katika Wizara hii. Lakini kama alivyosema mwenzangu pamoja na Katibu Mkuu Ndugu Dr. Bukuku, wote hawa kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na timu nzuri ambayo imepangwa, sisi watu wa mpira kama ingekuwa ni timu ya mpira basi imepangwa vizuri, *list* yote imeenea, kazi iliyobaki ni kufunga magoli basi naomba mtufungie magoli mazuri katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nizungumzie zaidi habari ya ubinafsishaji. Kwanza nianze pale kwenye ukurasa wa 52 Kifungu namba 55 Mheshimiwa Waziri anazungumzia ubinafsishaji wa mashirika kadhaa pamoja na *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anayesahau fadhila si muungwana. Wenzetu wa Serikali ya China imefanya kazi nzuri sana, imetusaidia sana katika kutusaidia juu ya ujenzi wa reli ya *TAZARA* na uendeshaji wa reli hiyo ya *TAZARA,* hilo halina ubishi na sisi kama waungwana tuna kila sababu ya kuwashukuru na kuwapongeza wenzetu wa Serikali ya China kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutujengea na hatimaye kutusaidia ili reli hii iendelee ku-*operate* mpaka hii leo. *(Makofi)*

Mimi nina hakika kama si China tusingezungumza *TAZARA* sasa hivi huo ndiyo ukweli. Kwa sababu Tanzania kama Tanzania tumeshindwa kulipa majukumu yetu na wenzetu wa Zambia vile vile hawajalipa zile ambazo wanastahili kulipa. Mtu anayenunua vichwa, mabehewa na kadhalika ni Mchina ndiye anayeleta sisi aah, hatulipi kazi yetu kutumia tu. Kwa hiyo, ni lazima tumshukuru na tuwapongeze wenzetu wa China kwa ujenzi na kwa uendeshaji wa reli ya *TAZARA*.

Sasa ninapoona mahali kwamba inadaiwa sasa kwa maana kwamba hii reli inabinafsishwa napata mshtuko na wasiwasi ni kiasi gani tumewasiliana na wenzetu Wachina na kufika mahali na kuona kwamba hii reli ibinafsishwe. Tumewahusisha kiasi gani? Wamekubali? Wameridhika? Au ni ulofa wetu sisi ambao tumekosa ku-*inject* kile ambacho tunatakiwa ku-*inject* sisi na wenzetu wa Zambia ndiyo tukafika mahali sasa tunaanza kuwalazimisha wale ili tuibinafsishe hii reli kwa sababu tunakwepa kutimiza majukumu yetu ya makubaliano ambayo tulikuwa tumekubaliana ya kuilea hii *TAZARA*.

Ombi langu nataka kujua hapa Serikali ya China imehusishwa kiasi gani na je, wamekubali kwamba reli hii ibinafsishwe? Vinginevyo mimi ni mtu wa mwisho kabisa kusema kwamba *TAZARA* ibinafsishwe kwa sababu ya wenzetu wa China wamefanya kazi nzuri sana katika kutujengea na baadaye katika kuilea reli hii. Nitapenda kupata maelezo je, Serikali ya China wanasemaje juu ya ubinafsishaji wa reli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamisha ubinafsishaji katika Mamlaka ya Bandari katika vile vitengo vingine ambavyo havijabinafsishwa, amesimamisha, si kitu kidogo hicho inataka moyo na ujasiri, hayakufanyika lakini sasa yamefanyika kwani,hayawi hayawi sasa yamekuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kusimamisha baadhi ya vitengo ambavyo vilikuwa vinangojea kubinafsishwa kwa ujasiri kwa sababu mengi tulisema jamani hivi kweli ni lazima watu wote wafe siku moja? Si kila mtu na siku yake? Basi maadam tumekubaliana kisera kwamba ubinafsishaji ni sera nzuri lazima tubinafsishe kila kitu? Si maeneo mengine tunaweza tukayaacha tu?

Sasa Mheshimiwa Rais ametupa mfano hapa kama limewezekana la Bandari, mimi nina hakika na hayo mengine yanawezekana kwa mfano la *TANESCO* linawezekana na mengine mengi, njia ni hii tumeonyeshwa na Mheshimiwa Rais. Nampongeza sana kwa hilo aliloliamua la kusimamisha ubinafsishaji wa baadhi ya vile vitengo ambavyo vilibaki kule Bandarini ukiacha ile *Container Terminal (TICTS)* kwa jina maarufu ambalo tumelizoea limeshabinafsishwa na *report* tumepewa hapa Ndugu

zetu ta *TICTS* wameendelea kufanya vizuri na hivi karibuni wamepewa eneo kubwa zaidi ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo basi nataka niamini kwamba sasa Mamlaka ya Bandari siyo *specified* tena au *TPA* siyo *specified* watakuwa *dispecified* na kwa maana hiyo sasa wataachiwa wafanye mambo yao kwa mujibu wa taratibu na sheria ile ambayo ilianzisha *TPA*. Vile vikwazo vya urasimu na ujanjaujanja wa *PSRC* na kadhalika vile havipo tena, maadam wametanzuliwa hebu waachieni wafanye kazi ili tuweze kuwapima juu ya matokeo ambayo wanaweza wakayaleta baada ya hapo. Tuachane na hayo mambo mengine sasa tuwape nafasi wapewe ushirikiano na pia wapewe kila aina ya msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano watahitaji ku-*invest* katika vifaa kwa ajili ya *General Cargo,* kwa utaratibu wa zamani inaweza kuchukua miaka kabla ya kupata vifaa kwa ajili ya *General Cargo* na hilo ni jambo la haraka ili waweze kufanya kazi vizuri ni lazima wapate *equipments* kwa ajili ya *General Cargo* kwa maana ya kwamba vile vitengo vingine ambavyo sasa havitabinafsishwa ambavyo vilikuwa vibinafsishwe kwa sababu hakuna mtu mwingine atakayekuja kununua ni wao ndiyo itabidi wanunue. Sasa kwa utaratibu wa Serikali wa kawaida wa urasimu na kadhalika inaweza ikachukua muda mrefu, ombi langu hapa kwa Serikali kwa ujumla ni kwamba wapewe kila msaada urasimu uondolewe ili waweze kufanya kazi yao kama inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nichangie ni suala la Posta. Katika ukurasa wa 53 Mheshimiwa Waziri pale anaeleza kwamba miongoni mwa mashirika ambayo yatabinafsishwa ni pamoja na Shirika la Posta. Suala la Posta limechukua muda mrefu sana hivi kuna tatizo gani? Mbona kuna vitu vingine vinaamuliwa siku mbili au tatu na vinakamilika? Tatizo liko wapi? Kila siku tunazungumza habari ya Posta tu huyu Posta amekuwa yatima, hana mtaji hakupewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria inasema Waziri wa Fedha na wa Mawasiliano wakae kwa Mujibu wa Sheria Namba 19 iliyowaunda wapewe mtaji toka mwaka 1992 mpaka leo hawajakaa hawa Mawaziri utafikiri mmoja anakaa Mbinguni na mmoja anakaa ardhini. Hawajakaa hata siku moja waka-*determine* huo mtaji lakini shirika lile linatakiwa lifanye kazi je litafanya kazi namna gani? Kila siku tunazungumza kwenye vikao vya Kamati na tunaleta *recommendations* humu ndani lakini hakuna kinachofanyika, kuna nini? Kulikoni? Mbona mambo mengine yanaamuliwa haraka haraka? Tathmini Serikali imeshafanya juu ya mikopo, madeni yale yaliyorithi, juu ya *pension* za watumishi wale wa *East African Community* sasa kuna tatizo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba Serikali iko hapa yote niwaombe sana kwamba suala Posta likamilike isije ikafa kwa sababu kwa kweli kama si umahiri wa viongozi wa Shirika la Posta hii Posta ingekuwa imekufa lakini kwa sababu ni wajanja, watundu, wanafanya kazi vizuri, wanakuwa *innovative* wanaangalia maeneo mengine, wanafanya kazi bila mtaji, wanafanya kazi bila mikopo hebu waamulieni *cabinet* mnakaa kila siku na hata leo mlikuwa na *cabinet,* juzi pia mlikuwa na *cabinet*

khaa! Mnazunguza nini kama la Posta hamlizungumzi basi? Mnazungumza mambo gani mengine ya *interest* bwana? Na hili la Posta linatakiwa lizungumwe na *cabinet* zungumzeni basi kama mnavyozungumza mambo mengine au hapa hakuna jambo ambalo linawafaa katika Posta yanawafaa mambo mengine peke yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzangu amesema habari ya *TRC,* na mimi nataka nirudie kwamba *TRC* ni Shirika muhimu, Shirika la Reli ni Siasa kwa Tanzania. Rafiki zangu wa kutoka Mwanza na Kigoma wanajua zaidi kuliko mimi kwamba *TRC* ni muhimu na ni siasa. Ukitaka rafiki zangu humu wakose kula wa kutoka Mwanza, Tabora, Kigoma na Buruga habari ya usafiri wa *TRC,* kwa hiyo, ubinafsishaji wa *TRC* kama alivyosema Mheshimiwa William Shellukindo, kwa kweli ni lazima uwe makini, ufanye kimakini na uepuke matatizo na mapungufu yale yaliyofanywa katika mikataba ile ambayo imepita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba iliyopita kumekuwa na matatizo mengi sana, sasa mimi naomba yale yaliyokuwa yamepita kule nyuma yasirudiwe inawezekana ndiyo tulikuwa tunaanza ubinafsishaji tusilaumiane sana. Lakini sasa tumejifunza kwamba kufanya kosa siyo kosa, lakini kuridia kosa ndiyo kosa, sasa maadamu tumejifunza tusirudie naomba sasa liangaliwe hiyo *rights* ambayo inasemekana atapewa hiyo kampuni lazima aangalie hatuna mabehewa na yeye anasema atatupa huu mkataba ni lazima ujulikane kama atatupa, hatuna *engine* amesema atatupa huo mkataba lazima useme kama tutapata *engine,* hatuna mataruma ya reli ni lazima tupewe tena za kisasa paundi 120 siyo 60 na 80 hizi za kisasa ni lazima na sisi tuende na paundi 120. Halafu ajue ziko reli nyingine za mfano Singida hizi hazifanyi biashara ni *Public Service Obligation* lazima ajue, Reli ya rafiki yangu Mheshimiwa Said Amour Arfi kule Mpanda lazima ajue katika mkataba huo vitu kama hivyo ni vizuri vikajieleza wazi ili kusudi basi pasije pakawa pana matatizo hapo baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu tumejifunza katika mikataba iliyopita chukua Mkataba wa *TTCL, ATCL, CADCO* mtu analipa dola 1,000 kwa mwaka mpaka leo, aibu. Hebu Uwanja ule wa Kilimanjaro dola 1,000 mpaka leo, haifai lakini ndiyo analipa sasa tukisema tuleteeni mikataba tuone hapa mnakuwa wakali. Ungekuja hapa mkataba sisi tungelibali dola 1,000 haiwezekani tusingekubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chukua *TTCL* kwanza ilikuwa makosa kuhusisha makosa ulipaji wa dola 60,000 na mahesabu *Audit and Accounts* makosa kwa sababu yule mwekezaji alipewa nafasi ya kufanua *due delegantes* akaifanya akaridhika akasema hili Shirika linanifaa akaja pale. *(Makofi)*

Sasa leo anaambiwa alipe 120 anasema hapana natanguliza kwanza cha mbele 60 na 60 nitalipa baadaye mpaka mtakaponiambia hesabu zenu ni safi, hiyo peke yake *it was wrong* na ndiyo maana mpaka leo zile pesa hatukuzipata Mkataba ule vile vile alikuwa analipa kila 3.5 ya mapato yote ya *TTCL* na 3.5 ya mapato *Celtel* lakini aliyekuwa analipa alikuwa analipa *TTCL Celtel* halipi chochote ingawa *development equipments* na kadhalika za *Celtel* anagharamia *TTCL.* Mambo mengine yanashangaza lakini nasema leteni mikataba tuone mnaficha nini tunataka tuangalie, haya si ndiyo mambo tunayotaka

tuyaone? Unakuta Mkataba wa *IPTL* mapato yote ya *IPTL* yaende kwanza Afrika Kusini yote kila kitu walichonunua hapa kwa *code* yao 083 lazima yaende Afrika Kusini yote na matumizi anatumia yeye anavyoona inafaa halafu anawaletea taarifa kwamba jamani nimetumia hizi na ninawadai kiasi kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimia Mwenyekiti, katika ndege hakuna kitu muhimu kama *Traffic Lights,* wewe inakuwaje huyu *South Africa* na *Air Ways partner* wako anachukua *route* zako wewe anakuwaje *partner* wako wakati anachukua *route* zako? Alipoona *route* ya kutoka Johannesburg ya kwenda Zanzibar ni ya muhimu akaleta visa akaichukua yeye sasa hivi *ATCL* haiende Zanzibar kutoka Johannesburg wanakwenda wao *South African Airways* ndiyo wanatoka Johannesburg wanakwenda Zanzaibar, Mkataba huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi zote za Harare, Lusaka, Nairobi na Dubai zimefungwa lakini yeye anatumia ofisi zake, pale penye ofisi ya *Air Tanzania* yeye hataki kutumia ofisi za Tanzania anatumia Ofisi yake *partner* wa namna gani huyo? Mkataba wa namna huo? Sasa yote hayo ndugu zangu tukisema mnasema ooh, sisi tunafanyaje. Leteni mikataba tuone, leteni tuone na tukiona kabisa mimi ninahakika tunaweza tukawasaidia kutatua baadhi ya matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba kwa sababu tumeumwa na nyoka kila tukiguswa na jani tunaruka. *(Makofi)*

Mheshimiaw Mwenyekiti, kwa hiyo, tunasema katika kubinafsisha Shirika la Reli tunaomba sana suala la Mkataba huu uangaliwe vizuri kama katika Bunge mnaona ni tatizo leteni kwenye Kamati tutaangalia kwenye Kamati na msilete Mkataba wote lete basi angalau sema bwana mpaka sasa tumefikia mahali fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mkija mkafunga mikataba kama hiyo tunayoizungumzia kama ya kina *ATCL* ya kupeleka mapato yetu *South Africa,* ya kupeleka kila kitu *South Africa* tulikuwa na kitengo chetu cha Uhandisi kimekufa wenzetu wameua katisa sasa hivi pale *ATCL* ukienda hakuna kitu kinaitwa *schedule time table* kwani leo wanavuruga, kesho wanavuruga nia yake ni kuua *image* kabisa.

Sasa hivi hakuna mtu wala *image* ya *ATCL,* hakuna mtu anatoka Ufaransa a-*book* ndege yake Ufaransa ili aje huku apande *ATCL* haina *image* imeharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kwamba Serikali ipo hapa, ndoa inakufa hiyo, vipi wenzetu wanaendelea kutawala na wakati ndoa inakufa? Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI :** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu na nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa, kwa hotuba nzuri aliyokuwa ameiandaa na pia nimpongeze msaidizi wake Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii mpya ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nianzie alipomalizia Mheshimiwa Mohamed Missanga, kwa aliyoyasema na kama ni kweli aliyoyasema ambayo sipendi kuamini

kwamba siyo ya kweli kwa sababu ni Mbunge tunayemheshimu sana na ni Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Miundombinu. Napenda niseme hapa mwanzo kwamba basi Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, una kazi ya kufanya hebu anzia hapo alipomalizia Mheshimiwa Mohamed Missanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo Wizara inayoshughulikia uchumi wetu, ndiyo yenye jukumu la kubuni sera. Wizara hii ndiyo yenye shughuli ya kubainisha fursa za uwekezaji katika nchi yetu, inashughulikia masuala ya kuendeleza rasilimali watu hata programu za kuongeza ajira zinategemewa zianzie kwenye Wizara hii. Sera za Maendeleo Vijijini zinategemewa kutoka kwenye Wizara hii, masuala yote ya takwimu na masuala ya kuondoa umaskini ambayo siku za nyuma yalikuwa Ofisi ya Makamu wa Rais lakini pia yamehamishiwa huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu hayo ni makubwa, mazito tunatumaini kwamba wenzetu hamtatuangusha maana ukishakosea katika *level* ya sera kutoka kule mwanzo tayari tunaofuata wengine wote tutatetereka, naamini mtajipanga vizuri ili muweze kukidhi matumaini na matarajio ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa suala la shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa ambalo tulikuwa tukiliongelea hapa Bungeni ambazo kwa taarifa tulizozipata jana zimeongezeka mara mbili maradufu kwamba sasa ni wastani wa shilingi bilioni moja kwa kila mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dalili ya nia njema kabisa kutoka upande wa Serikali kwa wananchi wake, hii ilikuwa ni ahadi ya Chama cha Mapinduzi na ahadi ya mgombea wetu wa Urais ambayo sasa inaelekea kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunaendelea kukumbusha kwa mipango itakayopangwa kwamba bado msisitizo na mlengo wetu uwe ni wananchi walio na hali ya chini, tuwasaidie hao ambao hali yao haiwaruhusu kuweza kuingia katika Benki yoyote na kumwuona Meneja wa Benki tuanze na hao kwanza na wengine wenye nafuu kidogo watafuata baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwasaidie wanaojishughulisha na biashara ndogo ndogo, tuwasaidie wanaojishughulisha na kilimo kidogo cha kawaida, wanaojishughulisha na ufugaji mdogo waweze kusogea ili waweze kupambana na umaskini. Takwimu zote zinaonyesha kwamba umaskini ni mkubwa zaidi vijijini kuliko mijini, matarajio yangu ni kwamba fedha hizi kwa sehemu kubwa zitaelekea kusaidia wananchi wa vijijini.

Nashauri kwamba wananchi wa vijijini na hasa akinamama watakaotaka kukopeshwa fedha hizi waruhusiwe kukopa fedha kiwango cha kuweza kununua ng'ombe wa maziwa wa kuweza kumfuga. Tukianzia hapo tutakwenda vizuri zaidi kuliko mikopo ya shilingi 50,000/= na shilingi 30,000/= haitatusaidia sana kwa maana ya vijijini. Mikopo ya aina ya *PRIDE,* unachukua fedha Ijumaa leo, Ijumaa ya wiki ijayo uanze kurejesha, hapana, ipangwe vizuri. Ukikopa fedha za kununua ng'ombe leo,

huwezi wiki ijayo Ijumaa ukaweza kurejesha hizo fedha, huyo ng'ombe ameshaanza kubeba mimba lini, amezaa ndama lini, umeshaanza kumkamua maziwa lini? Pawe na utaratibu mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile vijijini watakaotaka kukopa kwa ajili ya kununua wanyama kazi, ili tuweze kufanya mapinduzi makubwa ya kilimo hasa katika maeneo kama haya ya kwetu ya Dodoma na Mikoa mingine ambayo ardhi yake siyo ngumu sana. Wanaotaka kukopa fedha kwa ajili ya kununulia majembe ya plau, wanaotaka kukopa kwa ajili ya kilimo cha bustani kwa kununua pampu zinazoitwa Manemeka zipewe kipaumbele, ziwe katika maeneo hayo na hii itawezekana kupitia *SACCOS* kwa masharti nafuu sio tu asilimia ya kurudisha, lakini ni unafuu vile vile wa subira ya kuanza lini waanze kurejeshea hizo fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisogee mbele kidogo. Tulielezwa habari ya *TASAF* kwenda nchi nzima na *TASAF* kwa kiwango kingine wanafanya kazi kwa karibu sana na Wizara hii ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Semina zimeshafanywa katika Wilaya, magari yameshapelekwa, mafunzo mbalimbali yamekwishatolewa, miradi katika sehemu nyingi imeshachanganuliwa na imeshawasilishwa, lakini fedha ziko wapi?

Sasa ni vizuri haya mambo yakaenda vizuri kwa wakati. Kwa sehemu nyingi za nchi yetu hivi sasa ni kiangazi ambapo wananchi wengi wanaweza wakafanya miradi ya maendeleo. Utakapopeleka fedha hizo mwezi Januari na Februari mwaka kesho wananchi wanashughulika na mashamba yao, wakati huo ndiyo unapeleka fedha ya *TASAF* ya kujenga Zahanati au ya kujenga shule watagawanya muda vipi, kati ya kushughulikia shughuli zao za kiuchumi za kilimo na shughuli za jumla za maendeleo ya kijiji. Nilidhani huu ndiyo wakati muafaka kabisa wa kupeleka fedha za *TASAF*. Kwa hiyo, nasisitiza kwamba jambo lipewe kipaumbele kinachostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika Bunge hili tuliahidiwa fedha za *MMES* kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari kila Kata na wakati huu ndiyo wakati wa kujenga hizo Shule za Sekondari. Lakini mpaka sasa hivi ninavyoongea angalau kwa Wilaya yangu na Mkoa wangu wa Dodoma nina hakika hata senti moja ya *MMES* haijapelekwa. Sasa mnataka mpeleke fedha hizo lini? Ndiyo mipango hiyo Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa. Mpango ili uwe Mpango, uwe na maana lazima upangwe kwa wakati na utekelezaji wake uendane na hali halisi ya maisha na mzunguko wa maisha ya watu. Ukipeleka fedha hizo mwezi Februari mwakani, nani akajenge Shule ya Sekondari badala ya kwenda kupalilia shamba lake na tulisema hapa kwamba fedha zipitishiwe kwenye Halmashauri. Lakini mpaka sasa hivi hatujajibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ule mkondo ambao zilikuwa zinapitia kwa ma-*headmaster* una matatizo makubwa sana. Kwa hiyo, tungeomba fedha kama hizi za maendeleo zinazosubiriwa kwa hamu, wananchi wameshachanga, wanajitahidi sasa hivi wanajenga shule za sekondari zao, lakini mkono wa Serikali unakuwa ngumu wakati ni ahadi tu, ni ngumu kweli. Tunafikia sasa hivi karibu miezi tisa kama sio mwaka hela ya *MMES* haijaonekana popote pale wakati ahadi ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusisitiza kabisa kwamba fedha hizi kama zipo kweli basi zitoke, zipelekwe huko tujenge Shule za Sekondari, hizo fedha zikipelekwa mwezi Desemba mwaka huu wakati watoto wanaanza *form one* mwezi Januari,mwakani, haiwezekani kabisa. Kwa hiyo, zipelekwa fedha mwezi huu Agosti, zimechelewa sana mwezi Septemba, tuwe na miezi miwili, mitatu ya kufanya maandalizi kwa ajili ya vijana wanaoingia *form one* mwakani. Kwa mfano, kwa Wilaya yangu ya Kongwa, mwaka jana sisi tuliweza kufikia asilimia 100 ya kupeleka wanafunzi Shule za Sekondari, lakini wanafunzi wote waliokuwa wamefaulu ni 1,600 na kitu kidogo na tuliweza kuwapeleka wote. Wanafunzi 1,600 walikwenda Shule za Sekondari mwaka jana, lakini mwaka huu watakaofanya mtihani wa Darasa la Saba ni wanafunzi 4,500, tunategemea angalau elfu tatu na kitu waende Shule za Sekondari, maana yake ni mara mbili sasa ya wanafunzi 1600. Ni lengo ambalo ni asilimia 200 ya kupeleka watoto Shule za Sekondari. Kwa hiyo, tunayo kazi kweli ya kujenga Shule za Sekondari na tunahangaika kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema hizo fedha kama zipo zipelekwe jamani. Huwezi kuondoa umaskini bila kusomesha watoto, hicho ndicho kipaumbele cha kwanza na hii ni mara yangu kama ya nne hivi kusema hapa Bungeni jinsi nisivyokuwa na imani na Mpango mzima wa *MMES,* haukupangwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara nendeni pangueni hii *MMES,* Maofisa walioko pangueni, wapangwe Maofisa wengine wazuri zaidi ni mpango mzuri kweli wa ukombozi lakini hauendi na kama nyie mnaona unaenda, sisi wenzenu tulioko huko tunaona hauendi, mjitahidi mfanye sote tuuone kwamba mpango huu kweli unaenda na una nia njema kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri, amezungumzia programu ya Taifa ya kuongeza kipato *NIP.* Hii programu imekuwepo kwa miaka mingi. Lakini una mradi wa chumvi Pemba, Mama Lishe Dar es Salaam tena katika baadhi ya sehemu, ufugaji wa Nyuki Rufiji na Dodoma Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mradi unaitwa Programu ya Taifa ya Kuongeza Kipato. Chumvi Pemba, Mama Lishe Dar es Salaam, Ufugaji wa Nyuki Rufiji na Dodoma Vijiji. Sasa Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa japo sijasoma ile *mentally planning*, lakini kweli jamani hii ifike mahali hebu tuangalie tukiita jina Programu ya Taifa ifanane na jina lenyewe, vinginevyo tutachelewa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *SELF* vile vile uko kwenye Wizara yako Mheshimiwa Waziri na uko katika Mikoa 14, *SELF* sijui mwaka wa ngapi iko katika Mikoa 14. Tulipiga kelele *TASAF* iende nchi nzima. Sasa tunashukuru imeenda nchi mzima. *SELF* kila siku na bado mpaka leo ametusomea hapa iko katika Mikoa 14, inasubiri nini *SELF* kwenda katika nchi mzima. *SELF* iende katika nchi nzima. Wananchi wanahitaji kwenda mbele kwa kasi mpya. Kwa hiyo, ni matarajio yetu kwa bajeti ya mwakani itakuja na mipango iliyo bora zaidi ya *NIP* na *SELF.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho, nizungumzie habari ya uwezeshaji ambao tunautegemea sana kutoka Wizara hii. Kuhusu uwezeshaji na ametwambia hapa kwamba wanakusudia kuanzisha kitu kinaitwa *Mwananchi Empowerment Fund* iwasaidie wananchi kutoa dhamana ya mikopo, naunga mkono sana jambo hili. Ni matarajio yangu kwamba mwakani atakuja na mipango vizuri inayoeleweka. Kwa mfano, katika Sekta ya Wanyamapori, tuna maeneo mengi ambayo yanatupatia fedha nyingi, tuna samaki tumezungumza asubuhi hapa, tuna dhahabu na mambo mengine, lakini iko Sekta inaitwa ya Wanyamapori ambayo na yenyewe ni eneo ambalo lina fedha nyingi sana za kigeni na ni nzuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanyama hawa tunao kwenye Hifadhi zetu tena kwa wingi kuliko nchi yeyote Afrika. Vyuo vya Taaluma hiyo tunavyo katika nchi yetu na sisi ndiyo wahifadhi wa rasilimali hiyo. Lakini kuvuna tu hatuwezi, ni kama una shamba lako la mahindi, unaweza kupalilia, unaweza kupanda na unaweza kufanya nini, lakini kuvuna huwezi. Wanakuja wazungu kupitia makampuni yanayoitwa ya Uwindaji wa Kitalii, Makampuni haya yanadharau kweli kweli, tumeishakutana na baadhi yao wanasema nyinyi watu hamwezi kabisa. Hii ni *lucrative business* inahitaji *capital* kubwa *not less than three hundred million*, inataka watu wanaoaminiki, ninyi hamuaminiki na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli angalia hata masharti ili uingie katika biashara hii, unachohitaji ni kitalu. Kama mimi ni mtaalam wa masuala hayo, lakini siwezi kuingia katika eneo hilo ninahitaji kitalu, ili upate kitalu au mtu mwingine yeyote wa aina hiyo anatakiwa kwanza awe na *Land-cruiser* mbili mpya, awe na akaunti benki iliyo na fedha zisizopungua milioni 50, awe na mahema na mambo mengine, mlolongo mrefu, wangapi wataweza kuingia kwenye biashara kama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kupeleka watalii kwenye *National Parks* na Mbuga zetu nyingine, ukaanzishe *Tour Company,* unatakiwa uwe na magari angalau manne au matano mapya, hapa Waheshimiwa Wabunge tunahangaika na gari moja karibu tung'oane macho hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa katika uwezeshaji ndiyo maeneo hayo tunaomba muyaangalie. Katika kuwawezesha Watanzania nao waweze kuingia kuvuna tu wanyamapori wale na kufaidika nao. Hata kama huvuni, hii ya kupeleka watalii Mbugani wanaenda wanaangalia tu, wanawachukulia kwenye *binoculars* wala huvuni, humgusi wala hufanyi nini. Basi tuweke taratibu ambazo zitawasaidia wananchi wetu waweze kuingia katika biashara kama hizo waweze kunufaika na rasilimali tulizonazo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, isije ikanililia kengele ya pili. Naomba kuuunga mkono hoja iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Job Ndugai, nakushukuru sana kwa mchango wako haijapata kutokea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba niseme matangazo machache. Tangazo la kwanza, linatoka kwa Mheshimiwa William Shellukindo Mratibu wa Zoezi la Kulega Shabaha, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge waliojiandikisha kwa ajili ya kwenda kwenye zoezi la kulenga shabaha tarehe 12 Agosti, 2006 kwamba zoezi hilo sasa litafanyika tarehe 13 Agosti, 2006, usafiri utakuwepo Bungeni saa 2.00 asubuhi, kwa hiyo, si tarehe 12 Agosti, 2006, zoezi hilo litafanyika tarehe 13 Agosti, 2006. *(Makofi)*

Tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, na yeye anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo tarehe 12 Agosti, 2006 mara baada ya semina chumba namba 219 ghorofa ya pili. *(Makofi)*

Nimeagizwa na Katibu wa Kamati ya Wabunge wa CCM niwatangazie kwamba tafadhali Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi Jumatatu tarehe 14 Agosti, 2006 saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Wabunge wote wa Kamati ya Wabunge wa CCM. Lakini kikao hicho hakitakuwa kikao cha uchaguzi kama tulivyokubaliana. Lakini kinahusu *agenda* ile nyingine muhimu inayofahamika kwetu wote ndiyo itayojadiliwa siku hiyo.

Kwa hiyo, hilo ni tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. Kamati ya Wabunge wa CCM. *(Makofi)*

Nimeagizwa na Mheshimiwa Iddi Azzan, Mbunge wa Kinondoni niwakumbushe wale wachezaji wote mahiri wa timu za *Bunge Netball* na *Football* kwamba mchezo ule ule wa kasi na viwango vya hali ya juu utafanyika tena siku ya kesho katika Uwanja wa Jamhuri na mechi hizo zitakuwa kati ya timu hizo mbili za Bunge, lakini zitapambana na viongozi wa madhehebu ya dini hapa Dodoma. Kwa hali hiyo, tunaomba ile Kamati ya ufundi ya timu za Bunge ikiongozwa na Mheshimiwa Janeth Massaburi kama yupo iendelee kujiandaa kwa ajili ya ushindi wa pambano hilo la kesho hapo Uwanja wa Jamhuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu waliobaki ni Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Raynald Mrope na Mheshimiwa Peter Serukamba na kama nilivyosema mjadala huu tutaendelea nao siku ya Jumatatu kwa kuzingatia utaratibu utakaokuwa umepangwa. Baada ya kusema hayo, naomba kuahirisha Bunge mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 14 Agosti, 2006 saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.43 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu, Tarehe 14 Agosti, 2006 saa tatu asubuhi)*